# PARAKLITIKI

## WIMBO YA UFUFUO YA BWANA WETU YESU KRISTU




**CENTRE DE LA MISSION ORTHODOXE**
**KOLWEZI KONGO**
**2001**

# KIPANDE CHA SAUTI YA KWANZA

## MUPOSHO MANGARIBI

## ESPERINOS MKUBWA

***Maelezo:*** *Kisha ya Zaburi Proimiakos (Zaburi 104), na ya Kathisma ya Kwanza, hile wakati ya* «Bwana nimekuita», *tunaweka shairi kumi na tunaanza wimbo ya Ufufuo saba (7) na wimbo ya Mtakatifu ya hii siku tatu (3), ao ine za Ufufuo ya Kristu na sita wimbo ya Mtakatifu, kama eko mkubwa*.

**Wimbo ya Ufufuo ya Bwana Yesu Kristu**

Pokea, ee Bwana Mtakatifu, maombi zetu za mangaribi, na utupatie maondoleo ya zambi zetu; kwa maana ni wewe peke uliyeonyesha ku ulimwengu Ufufuo.

Mataifa, tembeyeni pembeni ya Sayuni na mumuzunguke, na mumutukuze ndani yake Yeye aliyefufuka katika wafu; kwa maana huyu ni Mungu wetu, aliyetukomboa ku maovu yetu.

Kujeni mataifa, tumusifu, na tumwabudu Kristu, tutukuze Ufufuo wake katika wafu; kwa maana huyu ni Mungu wetu, aliyekomboa dunia katika udanganyifu wa adui.

Mufurahi, ee ninyi mbingu, mupige baragumu ee ninyi misingi ya dunia, mupaze sauti ya furaha ee ninyi milima; kwa sababu angalieni Emmanueli alipigiliwa zambi zetu Msalabani, na mwenye kuleta uzima, aliuwa lufu, na kufufua Adamu, kwa kuwa yeye ni mpedna-wanadamu.

Yeye alipenda kwa mwili wake kusulubiwa kwa ajili yetu, aliteswa na alizikwa, na alifufuka katika wafu, tumwimbie na tumwombe, ee Kristu, sabitisha Kanisa yako mu imani ya Orthodoksi, leta amani ku uzima wetu, kwa kuwa Yeye ni mpenda-wanadamu.

Ku Kaburi yako yenyi kuleta uzima, tunasimama sisi wasiyostahili, tunatolea sifa yetu ku rehema Yako isiyo ya kusemwa, ee Kristu Mungu wetu; kwa sababu uliitika Msalaba, na lufu wewe msiye zambi, juu ya kuleta ku ulimwengu ufufuo, kwa kuwa yeye ni mpenda-wanadamu.

Neno la milele, pamoja na Baba wasipo mwanzo, alitoka, mu tumbo la Bikira asiye wakusemwa, na Msalaba na lufu juu yetu kwa mapendo yake alipokea kabisa, na alifufuka mu utukufu, tumusifu na tumwombe: Bwana mpaji wa uzima, utukufu kwako, Mwokozi wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba...

Elezo*: Tunaimba toka Mineon, kama eko Mtakatifu mkubwa.*

Sasa na siku zote. . THEOTOKION

*Sauti ya kwanza.*

Utukufu wa ulimwengu, uliyopandwa kwa watu, na ulizaa Bwana, mlango wa mbinguni, tumusifu Bikira Maria, wimbo wa wasiyo mwili, na pambo ya waaminifu; kwa sababu Yeye alikuwa mbingu, na Hekalu la umungu; yeye alipomoa ukuta ya adui, alibadilisha kwa amani, na alifungua ufalme. Basi pakuwa na hii, nanga ya imani, tuiko na mlinzi, Bwana aliyezaliwa

Kwake. Kwa hivi kuwa na moyo, kwa na moyo taifa la Mungu; kwa sababu Yeye anagobanisha adui sawa mwenyezi.

*Maelezo: Kisha ya Kuingia na ya Mwangaza Upole tunaimba Prokimenon ya hi siku:*

**PROKIMENON.**

*Sauti ya sita.*

Bwana anatawala, amevikwa utukufu.
*Shairi:* Bwana anavaa uwezo na unamuzunguka.
Bwana anatawala, amevikwa utukufu.
*Shairi:* Kwa sababu ulikaza ulimwengu, ambao hautatikisika.
Bwana anatawala, amevikwa utukufu.

*Maelezo: Kisha atasema Maombi Ekteni. Kisha:* Ee Bwana utujalie mangaribi hii...
Kisha: Tumalize ombi letu...*Kisha waimbaji wataimba Apostikha.*

**APOSTIKHA**

Kwa mateso yako, ee Kristu, ulituopoa ku tamaa mbaya, kwa Ufufuo Wako unatukomboa ku uharibifu, Utukufu Kwako, ee Bwana.

*Shairi:* Bwana anatawala, amevikwa utukufu. Bwana anavaa uwezo na unamuzunguka.

Kiumbe kishangilie, mbingu ifurahiwe, mataifa ipige mikono kwa furaha; kwa maana Kristu Mwokozi wetu, alipigiliya zambi zetu Msalabani, na aliuwa mauti, alitupatia uzima, alifufua Adamu mwenye kuanguka na uzao wake wote, kwa kuwa yeye ni mpenda-wanadamu.

*Shairi:* Kwa sababu ulikaza ulimwengu, ambao hautatikisika.

Japo uko Mfalme wa mbingu na inchi, ee Msiye sikilika, ulisulubishwa kwa kutaka kwako, kwa ajili ya kupenda wanadamu; wakati Hadeze ilikukuta kule chini ilipata uchungu, na wakati mioyo za wenye haki zilikupokea, zilishangilia; na wakati Adamu alikuona, ee Muumba, kuzimuni, alifufuka. Ajabu gani! Ginsi gani uzima wa wote ulionja kufa? Lakini ilifanyika kama alivyopenda kwa kwangaza dunia, inayopaza sauti na kusema: Ee Bwana, wewe uliyefufuka katika wafu, utukufu kwako.

*Shairi*: Ku makao yao kunafaa utakatifu, Bwana, juu ya urefu wa masiku.

Wanawake wabebaji manukato wakati walileta manukato, kwa maombolezo na walijiharikisha kaburini yako na kuishika; lakini hawakupate mwili wako usiyo na doa, na walisikia kwa Malaika muujiza mupya na wa ajabu, wakasema kwa Mitume; Bwana amefufuka na alileta rehema kubwa ku ulimwengu.

Utukufu kwa Baba...

Elezo*: Tunaimba toka Mineon, kama eko Mtakatifu mkubwa. Kama hakuna, tunaimba Utukufu..Sasa...Theotokion.*

Sasa na siku zote. . THEOTOKION

*Sauti ya kwanza.*

Tazama neno la Isaya linatimizwa; kwa sababu ulikuwa Bikira na ulizaa, na kisha kuzaa, ulibaki sawa mbele ya kuzaa; maana huyu aliyezaliwa alikuwa Mungu, kwa hii hali ya watu ilifanya mambo mapya. Lakini, ee Mzazi-Mungu, usitoangalie maombi ya watumishi wako, yanayotolewa katika hekalu lako; lakini sawa ulimuchukuwa mwenyi huruma mikononi mwako, uwasamehe watumishi wako, utuombee kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

### APOLITIKION YA UFUFUO

*Sauti ya kwanza.*

Wakati jiwe lilitiliwa muhuri na wayuda, na wakati Waaskari walichunga mwili wako usiyo doa, ulifufuka siku ya tatu, ee Mwokozi, uliupatia ulimwengu uzima. Kwa hii ezi mbingu ilipaza sauti kwa wewe mpaji wa uzima; utukufu kwa ufufuo wako, ee Kristu. Utukufu kwa ufalme wako, utukufu kwa shuruli yako ya ulimwengu, wewe peke Mpenda-wanadamu.

### THEOTOKION

Wakati Gabrieli alisema kwako Bikira, Salamu, kwa sauti; Rabi wa wote alichukua mwili, ndani yako safina takatifu, sawa mwenye haki Daudi alivyosema. Ulionekana kuwa munene sana kuliko mbingu, kwa sababu ulichukuwa Muumba wako. Utukufu kwa yule alikaa ndani yako; utukufu kwa huyu alitoka kwako; utukufu kwa huyu alitupatia uhuru juu ya uzazi wako.

## MU JUMA ASUBUI KATIKA SAUTI YA KWANZA

*Maelezo: Kisha Eksapsalme tunaimba: «*Bwana ndiwe...» Apolitikiona ya Ufufuo *(mara mbili), na kisha Theotokion. Padri atasema Ekteni Kidogo na waimbaji wataimba:*

### KATHISMA YA KWANZA

*Sauti ya kwanza*

Ewe Mwokozi, maaskari waliyolinda Kaburi yako wakaangushwa chini kwa uugaro wa Malaika aliyeonekana sababu ya kuwatangazia wanawake Ufufuo wako Takatifu; nawe mwenye kutuokoa ku mauti, tunakutuuza na tunasujudu mbele yako, mfufuliwa kaburini na Mungu wetu mmoja.

Utukufu kwa Baba...

Ewe Mungu wa mapendo, ulipigiliwa Msalabani kwa mapenzi yako, ukawekwa Kaburini kama mufu, ee chemchem ya uzima, kwa lufu yako, ee Mwenyezi, ulivunja nguvu ya mauti, wachungaji wa Hadeze wakatetemeka mbele yako; na wale waliyolala tangu milele katika mauti, ewe peke yako mpenda-wanadamu, ukawafufua pamoja nawe.

Sasa na siku zote...THEOTOKION.

Sisi wote tunaokimbilia ku wema tunakutambua kuwa Mzazi-Mungu, umekaa Bikira hata kisha kuzaa, kwani unawasaidia wenye zambi; katika wewe, ewe Bikira Safi kamili, tunapata wokovu katika hatari.

### KATHISMA YA MBILI

*Tu lithu sfragisthentos. Sauti ya kwanza*

Wanawake walikuja asubui mapema kaburini, Malaika akawatokea na wakashikwa na woga; uzima ukangaa kaburini, muujiza uliyowaogopesha, na wakaenda kuwatangazia Wafuasi ufufuo wa Bwana: Katika uwezo wake kubwa, Kristu amenyanganya Hadeze na kufufua wafu wote toka uvumbi wa kaburi; akafukuza woga wa huruma kwa uwezo wa Msalaba.

Utukufu kwa Baba...

Ewe Bwana msiyekufa, Uzima wa wote, ulipopigiliwa Msalabani na kuhesabiwa kati ya wafu, ukafufuka siku ya tatu, ewe Mwokozi, sababu ya kumfufua Adamu ku uvumbi wa Kaburi, na Majeshi ya mbinguni yanapaza kwako sauti, ewe chemchem ya uzima: Utukufu ku mateso yako kimungu, ee Kristu, utukufu ku ufufuo wako, utukufu ku mapenzi yako, ewe peke yako mpenda-wanadamu.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION.**

Ewe Maria makao bora ya Bwana, utuamushe kuzimuni huko tulikoangukia, utuopoe ku mkato wa ajabu wa matumaini, ku makosa yetu na ku sikitiko yote, ndiwe makimbilio ya wenye zambi, msaada, ulinzi na wokovu wa watumishi wako.

Maelezo: *Sasa tunaimba Evlogitaria ya Ufufuo ya Kristu. Kisha Ipakoi:*

### IPAKOI

Toba ya Munyanganyi ikashurtisha Paradizo, maombolezo ya Wabebaji manukato ya kutangaza furaha: Ee Kristu Mungu wetu, ulifufuka kwa kuleta ku dunia neema kubwa.

Maelezo: *Shemasi ao padri atasema Ekteni Kidogo na waimbaji wanaimba Anavathmi:*

## ANAVATHMI

### ANTIFONON YA KWANZA

Bwana, katika huzuni yangu sikiliza mwito wangu, napaza sauti kwako.

Kwa wao wenye kuishi jangwani kunaongezeka daima mapendo ya umungu yenye kuwa mbali na dunia hii ya bure.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote...

Heshima na utukufu kwa Roho Mtakatifu, kwa Baba na kwa Mwana; na tuimbe utukufu wa Utatu Mtakatifu.

### ANTIFONON YA MBILI

Ee Mungu wangu, ulinipandisha juu ya mulima wa amri yako: Unipe mwangaza wa fazila ili nikuimbe.

Ee Neno, kuume kwako kunanisaidia, unichunge, unilinde ili moto wa zambi usiniunguze.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote...

Katika Roho Mtakatifu kiumbe yote inakuwa mupya inarudi ku hali yake ya kwanza; kwani ana nguvu ileile kama Baba na Mwana.

### ANTIFONON YA TATU

Wakati waliponiambia: Tuendeni viwanjani mwa Bwana, roho yangu ikafurahiwa na moyo wangu ukajazwa na furaha.

Nyumba ya Daudi inaonyesha woga kubwa: Vitu vya ufalme vimewekwa, na huko kutahukumiwa kila taifa na kila lugha ya dunia.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote...

Heshima, usujudu, utukufu na uwezo kwa Roho Mtakatifu, kwa Baba na kwa Mwana. Kwani Utatu Mtakatifu ni Moja, lakini muna watu Tatu.

### PROKIMENON

Bwana anasema: Sasa nitasimama, nataka kusabitisha wokovu na kuulinda milele.

*Shairi*: Maneno ya Bwana ni sawa na ya kweli.

Bwana anasema: Sasa nitasimama, nataka kusabitisha wokovu na kuulinda milele.*(mara mbili).*

Maelezo: *Kisha waimbaji wataimba ao watasoma Kanuni ya ufufuo ya Bwana Yesu Kristu.*

**WIMBO YA KWANZA**

*Sauti ya kwanza.*

**IRMOS:** Ee Bwana msiyekufa, mukono wako wa kuume, wenyi ushindi, nzuri kwa nguvu yake, umejifunika utukufu sababu ya uwezo wako, uliponda maadui wakati uliwafungulia wana wa Israeli njia mupya chini ya bahari.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Wewe ambaye ku mwanzo mikono yako takatifu iliniumba na matope ya udongo, ulipanua pia mikono Msalabani sababu ya kuita ku udongo hii mwili wa mauti uliyopata wewe mwenyewe kwa Bikira sababu ya kuupatia umilele.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Huyu ambaye kwa pumuzi yake ya umungu aliumba roho yangu siku ya kwanza, alitoa roho yake ku lufu na akafa kwa kuniokoa; alipovunja minyororo ya Hadeze, akanifufua pamoja naye sababu ya kunipa utukufu wa milele.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Chemchem ya neema, salamu, mungazi takatifu tena mulango wa mbinguni, salamu, kinara cha zahabu, chombo ambamo manna ililindwa, mulima haramu uliyezaa Kristu kwa ajili ya dunia, hii chemchem ya uzima.

**IRMOS INGINE:** Kristu anazaliwa, mumutukuze, Kristu toka mbinguni, mumupokelee, Kristu duniani, mupandwe. Mwimbie Bwana, ninyi inchi, na kwa furaha mumusifu, mataifa, kwani Yeye ameshinda kwa utukufu.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Kristu aliyejifanya mutu amenifanya kuwa Mungu, Kristu amenitukuza alipojishusha, Kristu chemchem ya uzima ananiopoa alipoteswa mwilini; tena naimba, kwa shukrani: Kwani amevaa utukufu.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Kristu ameniinua, musulubiwa, Kristu aliyekufa amenifufua; Kristu amenipa uzima; kwa furaha ninapopiga mikono namuimbia Mwokozi wimbo wa ushindi: Kwani amevaa utukufu.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Ni Mungu mwenyewe uliyechukua tumboni mwako, ni Kristu uliyezaa katika ubikira wako, ee Bikira; ee Mtakatifu kamili, alipata mwili tumboni mwako, Mwana wa pekee tunayetambua umoja wa mutu katika hali mbili: Kwani amevaa utukufu.

**KANUNI YA MZAZI MUNGU**

*Su i tropeukhos.*

Mtakatifu Kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Wimbo gani wenyi kukustahili wewe uzaifu wetu unaweza kukutolea? Ni paka wimbo wa furaha Gabrieli alitunulia: Salamu, Mzazi-Mungu, Bikira na Mama msiyeolewa.

Utukufu kwa Baba...

Kwa Mama Bikira daima wa Mfalme mkubwa wa majeshi ya mbinguni, sisi waaminifu na moyo safi tunaimba kiroho: Salamu, Mzazi-Mungu, Bikira na Mama msiyeolewa.

Sasa na siku zote...

Isiyoweza kufumbuliwa na bahari ya kuzaa kwako kusiyoweza kusikilika; na imani isiyo ya kusita tunakuambia kweli: Salamu, Mzazi-Mungu, Bikira na Maria msiyeolewa.

## WIMBO YA TATU

**IRMOS:** Wewe peke yako mwenye kujua uzaifu ya ubinadamu, ulipofanana nao katika rehema yako, univike nguvu ya juu mbinguni ili niimbe mbele yako: Takatifu ni hekalu kiroho ya utukufu wako takatifu, ee Bwana mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Kisha kuanguka kwangu, ee Mungu mwema, ikanihurumia, ukashuka mpaka kwangu wakati uliniinua kwa usulubisho wako, ili niweze kuimba: Mtakatifu ni Bwana wa utukufu usiyoweza kufananishwa kwa wema wake.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Ee Kristu, ndiwe uzima wa kweli, ilivaa hali yangu ya kuharibika, kama Mungu mwenyi huruma; uliposhuka katika ivumbi wa mauti na ulipoharibu mauti ukafufua wafu siku ya tatu, ukawavika umilele.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Ee Bikira, tumboni mwako ulipata mimba ya Mungu wetu kwa tendo la Roho Mtakatifu, ukakaa bila kuteketezwa japo moto mkali: Ni wewe kichaka cha moto bila kuteketezwa kilichotanguliwa kufunuliwa waziwazi kwa Musa mpana-sheria.

**IRMOS:** Mwana alizaliwa bila geuzo toka Baba tangu milele, na alitwaa mwili bila mbegu toka Bikira wakati wa mwisho. Tumupazie Yeye Kristu Mungu sauti: Ewe uliyetukuza pembe yetu. Mutakatifu wiko, Bwana.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Pa mabega yake alibeba kondoo aliyepotea na Msalabani anazima zambi yake; tumuimbie Bwana: Wewe mwenyi kuinua uso wetu, ndiwe Mtakatifu, ee Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Roho Mtakatifu aliyemfufua Yesu Kristu muchungaji mkubwa kuzimuni akawaongoza pia Mitume ili wawe wachungaji wa mataifa yote: Tumuabudu katika roho na katika ukweli.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Mwana wa Mungu aliyepata mwili kwa Bikira bila mbegu, kwa uwezo wake alimulinda Mama Mtakatifu bikira hata kisha kuzaa; tumuimbie: Ndiwe Mtakatifu, ee Bwana Mungu wetu.

## KANUNI YA MZAZI-MUNGU.

Mtakatifu Kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Wingu laini kweli, ee Bikira, ndivyo tunavyokutaja kadiri ya manabii, kwani katika wewe Bwana alikuja ku Misri kuvunja miungu ya uwongo na kuwamwangia nuru yake wale waliyomtumikia.

Utukufu kwa Baba...

Mulango wa kufunga tena kisima chenyi kutiwa muhuri, ndivyo kweli walivyokutaja makundi ya manabii, ee Bikira mustahili wa nyimbo zetu, sababu ya kuonyesha waziwazi alama za ubikira wako uliyolinda hata kisha kuzaa.

Sasa na siku zote...

Alipokutambua mustahili wa kuona akili yenyi kupita wazo lolote, Cabrieli, ee Bikira Mtakatifu kamili, akakutangazia habari ya furaha, akakufunulia waziwazi kupata mimba ya neno na kuzaa kwako kwa ajabu.

**KONTAKION**

Ulipofufuka kaburini katika utukufu wa umungu, ulifufua dunia pamoja nawe; wanadamu wanakuimbia kama Mungu, mauti inafifia, Adamu anafurahi, ee Bwana na Eva mwenye kufunguliwa sasa ku vifungo vyake anatangaza kwa shangwe: Ee Kristu, ni wewe mwenye kuleta Ufufuo kwa wote.

**NYUMBA (IKOS)**

Tumuimbie Mungu Mwenyezi aliyefufuka siku ya tatu: Anavunja milango ya Hadeze na anafufua wale waliyolala kaburini; anakubali kuonekana kwa Myroforo: ni wao wa kwanza waliyopokea wokovu; kwa Mitume anawafunulia furaha kama chemchem moja tu ya uzima; wanawake wanaenda na imani kwa Wafuasi kuwatangazia ushindi wa Kristu; Gehena inalalamika, mauti inalia, dunia inashangilia kwa furaha ya milele: Ee Kristu, ni wewe mwenye kuleta Ufufuo kwa wote.

## MASIFU

*Sauti ya kwanza*

**Wimbo ya ufufuo**

Tunasifu, ee Kristu, mateso yako kwa wokovu wetu, na tunatukuza Ufufuo wako.

Bwana, wewe uliyevumilia Msalaba, na uliharibu mauti, na ulifufuka katika wafu, tuliza uzima wetu, kwa kuwa Wewe ni mwenyezi peke yako.

Ee Kristu, wewe uliyeteka Hadeze, na ulifufua mutu, kwa ufufuo wako, utustahilishe kwa moyo safi, tukusifu na kukutukuza.

Tukitukuza ukubali Kwako, unaofaa kwa Mungu, tunakusifu, ee Kristu; ulizaliwa kwa Bikira, na ulikuwa msiyetengana na baba; uliteswa sawasawa na mutu, na ulivumilia Msalaba, kama ulivyotaka; ulifufuka toka Kaburi, sawa ulitoka kwa chumba cha arusi, juu ya wokovu wa dunia, Ee Bwana, utukufu kwako.

**Ingine Wimbo Anatolika**

Wakati ulipopigiliwa pa muti wa Msalaba, wakati ule nguvu ya adui ilikufa; viumbe vilitetemeka kwa woga, na Hadeze ilinyanganywa sababu ya uwezo wako; ulifufua wafu kaburini, na ulifungua Paradizo kwa munyanganyi; Kristu Mungu wetu, utukufu kwako.

Wanawake waheshimiwa kwa Bidii na maombolezo wakashika kaburi yako; wakipata kaburi wazi na wakifundishwa kwa Malaika, muujiza mupya na wa ajabu, walipasha kwa wanafunzi, ya kama Bwana amefufuka, mwenye kuleta rehema kubwa duniani.

Tunaabudu pigo takatifu ya mateso yako, ee Kristu Mungu na kazi kubwa ya ukuhani katika Sayuni, iliyoonekana kwa Mungu katika wakati wa mwisho wa milele; kwani wewe, Jua la haki uliangaza wale waliolala kwa giza, ukiwaongoza kwa Nuru ya milele; Bwana, utukufu kwako.

Musikilize, enyi uzao wa Wayuda, wenye kupenda musukosuko; weko wapi waliojongea kwa Pilato? Watuonyeshe askari waliochunga kaburi; Mihuri ya kaburi iko wapi? Huyu aliyezikwa alihamishwa wapi? Huyu musiyeuzishwa aliuzishwa wapi? Namna gani hazina iliibwe? Juu ya nini munasingizia Ufufuo wa mwenye kusulubiwa, enyi Wayuda wavunja-sheria? Huyu mwenye uhuru katika wafu alifufuka, na analeta rehema kubwa duniani.

Utukufu kwa Baba...

*Elezo: Tafuta Eothinon (Mwimbo wa asubui) ku mwisho ya hii Kitabu.*

*Kisha Eothinon tunaimba hii:*

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Mbarikiwa Ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira; kwa kuwa naye aliye amepata mwili nawe, kuzimu imetekwa, Adamu amerejezwa, laana imekufa, Eva amekombolewa, Mauti imewekwa kifoni, tena sisi tumeofikia uzima; kwa hiyo tukiimba na kupaza sauti umehimidiwa U Kristu Mungu wetu, liyependezwa hivi. Utukufu kwako.

### DOKSOLOGIA MKUBWA

Leo wokovu ulifanyika duniani, tumwimbie mwenye kufufuka toka kaburi na mukubwa wa uzima wetu. Kwa sababu kwa lufu alibomoa mauti na alitupatia ushindi na rehema kubwa.

## SIKU YA MUNGU MANGARIBI KATIKA SAUTI YA KWANZA

*Panefimi martires.*

Ewe Bwana, katika wema wako na katika Neno lako na Roho yako ukaumba ulimwengu. Kisha ukanifanya mimi kuwa mwenyi hai ili nilitukuze, ee Mungu Mwenyezi, jina lako Takatifu; lakini kwa vitendo vibaya nikalizarau: nakuomba, unirehemu.

Ee roho yangu maskini, ukumbuke asili yako kimungu na inchi ya mbinguni, na kwa matendo yako mema ujikaze kuifikia daima, ukatae vitu vyenyi kufifia, kwani bahati yako ni kule mbingu, lakini mwili wako wa dunia utakufa: ndani yako uovu usitawale mema.

Twende, ee roho yangu maskini, katika machozi umufikilie Mungu wa wema wote, ukiungama matendo yako yote mbele ya saa ya hukumu; unifazilie ewe Muumba, na naomba huruma mbele ya Bwana kufunga mulango mbele yangu.

**Wimbo ya Malaika:**

Enyi Malaika Wabila-mwili wenyi kusimama karibu ya kiti cha ezi cha Mungu na kuangaziwa bila kwacha na nuru yake katika mwanga wa nuru ya milele ili miwe nanyi pia nuru, muombeni Kristu ili alete amani na neema ya wokovu ku roho zetu.

Malaika wa milele muliyepokea kweli kwa Mungu muzima uzima usiyoweza kufa, watajiri wa utukufu usiyoweza kupita, ninyi ni watezamaji wakubwa wa hekima yasipo mwisho na mumejazwa na nuru, munaonekana kweli kama taa za kwangaa.

Malaika na Malaika wakuu, wakuu, wenye viti vya ezi, Watawala, Wenye uwezo, Waserafi wa mabawa sita, na Wakeruvi wa macho mengi, ninyi vyombo vya hekima ya Mungu, Majeshi na Fazila, muombeni Kristu ili alete amani na neema ya wokovu ku roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION.**

Gari kimungu ya usafi wenyi kupita wazo lolote, ewe Maria, unichukue mbali na ulimwengu wa zambi zangu, unipeleke ku inchi ya toba, ukinizungusha na ulinzi wako wa nguvu: Una uwezo kama Mzazi-Mungu mwenyezi.

**PROKIMENON YA HII SIKU:**

Siku ya Mungu: Tazama ninyi munaobariki Bwana, ninyi watumishi wote wa Bwana *(mara tatu).*

*Elezo: Kisha:* «Ee Bwana utujalie...». *Maombi ya mpadri.*

**APOSTIKHA**

Bahari ya makosa yangu ni kubwa, ee Mungu Mwokozi; nazama katika shimo la zambi: Kama kwa Petro unipe mukono; uniokoe, ee Mungu wangu, na unihurumie.

Ee Mwokozi, tazama nahukumiwa kwa mawazo yangu na matendo yangu ya ukafiri; unipe nia za toba ili nikuombe, ee Mungu wangu: Uniokoe katika wema wake na unihurumie.

Ee Mungu wa mapendo, kwa maombezi ya Watakatifu wote na ya Mzazi-Mungu, utupe amani na utuhurumie.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION.**

Furaha ya Malaika mbinguni, mulinzi wa wanadamu duniani, ee Bikira Mtakatifu, utuokoe sisi wenye kukukimbilia, kwani kisha Mungu matumaini yetu ni kwako, ewe Mzazi-Mungu.

## MU KAZI MOJA ASUBUI KATIKA SAUTI YA KWANZA

**KATHISMA YA KWANZA.**

Mama yangu alinichukua mimba katika zambi, na kama mpotevu sisubutu kutazama juu mbinguni, lakini mapendo yako inaniotumainia, na napaza sauti kwako*:* Ewe Mungu, unisamehe na uniokoe.

Kama mwenye haki anaokoa, wapi nitajionyesha mimi mwenye zambi? Sikuchukua wala uzito wala joto ya mchana, lakini unihesabie pamoja na wale wa saa ya kumi na moja, ee Mungu wangu, na uniokoe.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION.**

Bikira Safi, Mbarikiwa mbinguni na kutukuza duniani, salamu, Bibi usiyeolewa.

**KATHISMA YA MBILI**

Ewe Bwana, ujiharikishe kunifungulia mikono yako ya ubaba, kwani nilitumia vibaya uzima wangu; tazama hazina ya huruma yako isiyokuisha, ee Mwokozi, usizarau umaskini wa moyo wangu; kwako, ee Bwana, napaza sauti nikijaa na sikitiko*:* Ee Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako.

Korti ni ya hatari, hukumu yako ni ya haki, na matendo yangu ni mbaya; lakini wewe, Mungu wa mapendo, kuja uniokoe na kuniokoe ku azabu; ee Rabi, unilinde ku hali ya wenyi kulaaniwa, na unistahilishe nisimame kuume kwako, ewe Mwamuzi wa haki.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ongoza roho yangu maskini, ewe Bikira Safi, na nisamehe, tazama kuzimuni gani imeangukia na uzito wa zambi zangu, ku saa ya ajabu ya kufa, ee Bikira Takatifu, uniopoe kwa mashetani wenyi kushitaki na ku azabu yote.

## KATHISMA YA TATU

*Ton tafon su Sotir.*

Nilijitenga nawe mbali mno, ewe Bwana, kama Mwana Mpotevu nilitumia vibaya uzima wangu wote; kama mtumwa nilitumikia kila siku tamaa za upumbafu; lakini, wewe Baba, na kuomba, kwa maombezi ya Malaika unipokee kama Mwana mpotevu na uniokoe.

Ee Bwana, utukufu wa mashindano na taji la Washindaji, ndiwe uzuri wa Mashahidi Watukufu*:* Kwa imara yao katika majaribu wakawakimbiza makafiri na wakapokea ushindi mbinguni kwa uwezo wa Mungu; ee Bwana, kwa maombezi yao uniokoe kwa Adui msiyeonekana na uniokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ewe Bikira uliye juu zaidi kuwapita Malaika wabila-mwili na peke yako unapita vyeo vya mbinguni; ulipokea kwa Malaika sifa yenye kukuelekea, pamoja nao umuombe Mwana wako ili aniopoe ku uzulumu wa tamaa.

Elezo: *Sasa tunasoma Zaburi 50 (51).*

## EKSAPOSTILARION

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

## APOSTIKHA YA MASIFU

Ulimwengu ingine umekuongojea, ee roho yangu na Mwamuzi atatangaza siri zako na zambi zako; usidumu katika uovu, lakini ujiharikishe kupaza sauti*:* Ewe Mwamuzi wangu na Mungu wangu, unisamehe na uniokoe.

*Shairi:* Utushibishe upesi kwa huruma yako, nasi tutashangilia na kufurahi siku zetu zote. Utufurahishe kadiri ya siku ulizotutesa, kadiri ya miaka tulipoona mabaya. Matendo yako yaonekana kwa watumishi wako, na utukufu wako kwa wana wao.

Ewe Mwokozi, usimzarau mtumishi wako mfungwa wa uzaifu na zambi, lakini amsha moyo wangu ku toba, unifanye kuwa mtumishi wa shamba lako la mzabibu, ee Bwana, ukinipa mshahara wa saa ya kumi na moja na neema ya wokovu.

*Shairi:* Utamu wa Bwana Mungu wetu uwe juu yetu, na kazi ya mikono yetu uistawishie, ndiyo, kazi ya mikono yetu uiimarishe.

Njooni, enyi mataifa yote, tuimbe mashairi na nyimbo za kiroho kwa kuwatukuza Mashahidi watukufu wa Kristu, Watangazaji wa imani tena taa za ulimwengu, Chemchem isiyokauka ambako kunatiririka maponyesho; kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu, leta amani ku dunia na neema ya wokovu ku roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**
*Ton Uranion tagmaton.*

Uliye Mtakatifu kuwapita Malaika Watakatifu, uliye na utukufu kushinda kiumbe chote; ewe Mzazi-Mungu Malkia wa ulimwengu, wewe uliyemuzaa Mwokozi, katika wema wako, utuokoe ku zambi zetu nyingi na ku hatari katika sala zako takatifu.

## MU KAZI MOJA MANGARIBI KATIKA SAUTI YA KWANZA

**Wimbo ya kutubu.** *Ton uranion tagmaton. Sauti ya kwanza.*
Mawaimbi ya makosa yangu yamenizamisha katika shimo la zambi; napaza sauti kwako, ee Rabi: Uniopoe ku vishawishi nyingi vyenyi kunishinda na ku moto wa milele, ewe Mungu wa wema.

Nilipotopea katika shimo ya mawazo, ku maongezo ya sikitiko, mimi mwenyi mateso, ee Neno la Mungu, natumainia kwako: uniopoe ku mashambulio ya maadui wenyi kuonekana na wasiyoonekana.

Ulisamehe kazi ya mikono yako, ewe Mungu Muumba, kwa mapenzi yako ikajifanya maskini kwa ajili yetu, ewe Neno la Mungu; wewe unayeondoa zambi ya dunia, nyanyua pia mzigo wangu, punguza nira yangu.

**Wimbo ya Mtangulizi Yoane.** *Panefimi martires.*
Ewe Nabii wa ajabu, Mbatizaji na Mtangulizi wa Kristu, tirikiza katika machozi yangu maji mengi isiyokauka ku moyo wangu wenyi kukaushwa na makosa yangu; naomba msaada wako ili nikiokoka kwa ajili yako ku mateso yenyi kunishinda, nimsifu huyu aliyekutukuza.

Ee Nabii mwenyi heri, nainua kwako matumaini ya uzima wangu; wewe uliyembatiza Kristu Yesu, huyu anayeondoa zambi ya dunia, na kuomba, umsihi atakase moyo wangu na aniokoe.

Ewe Muhubiri ya neema ya Kristu uliyewatangazia mataifa yote toba, fanya ili roho yangu maskini idumu katika toba, ee Mtangulizi kimungu, na itimize daima mapenzi ya Bwana ili nikutukuze katika imani na mapendo.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ewe Bikira Safi, peke yako umekuwa makao ya Nuru anayoonyesha Baba wa milele; naelekea basi kwako nikipaza sauti: Angazia na nuru ya fazila roho yangu yenyi giza ya tamaa, na ku siku ya hukumu uiweke katika uwanja zako za nuru.

### PROKIMENON

*Sauti ya ine.*

Bwana atasikia wakati ninapomuita.*(mara tatu).*
*Shairi*: Unijibu wakati ninapoita, ee Mungu wa haki yangu.

### APOSTIKHA

Bahari ya makosa yangu ni kubwa, ee Mungu Mwokozi; nazama katika shimo la zambi*:* Kama kwa Petro mkono; uniokoe, ee Mungu wangu, na unihurumie.

*Shairi:* Nitanyanyula macho yangu kwako, ee mwenye kuikala mbinguni, tazama macho ya watumishi yanaangalia kwa mkono wa Bwana kama macho ya kijakazi kwa mkono wa bibi yake, hivyo macho yetu yanavyoangalia kwa Bwana Mungu wetu hata akatuhurumia.

Ee Mwokozi, tazama nahukumiwa kwa mawazo yangu na matendo yangu ya ukafiri; unipe nia za toba ili nikuombe, ee Mungu wangu*:* Uniokoe katika wema wake na unihurumie.

*Shairi:* Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwani tunayala na kuzarauliwa. Nafsi yetu inayala na kuzarauliwa kwa wenye kuikala na salama tena na kuzarau kwa wenye kiburi.

Enyi Mashahidi Watakatifu, katika uwanja imani yenu ikavunja nguvu ya mashetani pakuwaopoa wanadamu ku udanganyifu, na wakati wa kuondoka kwenu mukapaza sauti: Ee Bwana, sadaka ya uzima wetu ikupendeze, kwani kwa mapendo yetu kwa ajili yako tumezarau mali ya uzima huu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Wewe mwenye kupokea sala za wenye zambi, usizarau mlio ya wenyi kuhuzunika, umuombe Huyu aliyetaka kuzaliwa tumboni mwako safi, ee Bikira Safi, atupe wokovu.

## MU KAZI MBILI ASUBUI KATIKA SAUTI YA KWANZA

### KATHISMA YA KWANZA

Mama yangu alinichukua mimba katika zambi, na kama mpotevu sisubutu kutazama juu mbinguni, lakini mapendo yako inaniotumainia, na napaza sauti kwako*:* Ewe Mungu, unisamehe na uniokoe.

Kama mwenye haki anaokoa, wapi nitajionyesha mimi mwenye zambi? Sikuchukua wala uzito wala joto ya mchana, lakini unihesabie pamoja na wale wa saa ya kumi na moja, ee Mungu wangu, na uniokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Njooni, enyi waamini wote, tumutukuze Mtakatifu Mzazi-Mungu, na tusujudu mbele yake: Ni boma letu imara; anaweza mutusema kwa Mwana aliyezaa; kwa maombezi yake anaweza kutuokoa ku mauti na ku azabu zenyi kushambulia roho zetu.

### KATHISMA YA MBILI

Ewe Bwana, ujiharikishe kunifungulia mikono yako ya ubaba, kwani nilitumia vibaya uzima wangu; tazama hazina ya huruma yako isiyokuisha, ee Mwokozi, usizarau umaskini wa moyo wangu; kwako, ee Bwana, napaza sauti nikijaa na sikitiko*:* Ee Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako.

Korti ni ya hatari, hukumu yako ni ya haki, na matendo yangu ni mbaya; lakini wewe, Mungu wa mapendo, kuja uniokoe na kuniokoe ku azabu; ee Rabi, unilinde ku hali ya wenyi kulaaniwa, na unistahilishe nisimame kuume kwako, ewe Mwamuzi wa haki.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee roho yangu kataa uzaifu na usingizi, wakisha taa ya toba; ukifurahiwa, ondoka ku fujo ya uzima huu sababu ya kwenda mbele ya Mshumba musiyekufa; umwambie: Usinikatae, ewe Neno, unipokee kwa maombezi ya huyu aliyekuzaa.

### KATHISMA YA TATU

*Ton tafon su Sotir.*

Zamani, katika maji ya Yordani, ukambatiza huyu mwenye kutakasa ulimwengu, na mimi mwenyi kufunikwa na mawimbi ya zambi, unioshe ku aibu yote; utuombee daima kwa Bwana mpenda-wanadamu.

Kama ma askari wema, wenyi shauri moja katika imani, bila woga na bila laumu mbele ya makanio ya wazulumu, wahodari, mumenjongea Kristu mkishika Msalaba wake boga. Ku mwisho wa safari na wa mashindano mukapata ushindi wa Juu-mbinguni. Utukufu kwa huyu ambaye nguvu yake ikawa tegemeo yenu, utukufu kwa huyu aliyemivika taji, utukufu kwa huyu anayetenda ndani yenu kwa kutuponyesha.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

*Ton tafon su Sotir.*

Aliporuka kwa furaha tumboni mwa mamae, kwa neema kimungu Mtakatifu Yoane akatambua,ee Bikira, Mungu uliyechukua na akamuabudu mwenye kujaa na imani; Neno uliyepatia mwili, umuombe pamoja na Mtangulizi aokoe watumishi wako.

### EKSAPOSTILARION

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

### APOSTIKHA

Ulimwengu ingine umekuongojea, ee roho yangu na Mwamuzi atatangaza siri zako na zambi zako; usidumu katika uovu, lakini ujiharikishe kupaza sauti*:* Ewe Mwamuzi wangu na Mungu wangu, unisamehe na uniokoe.

Ewe Mwokozi, usimzarau mtumishi wako mfungwa wa uzaifu na zambi, lakini amsha moyo wangu ku toba, unifanye kuwa mtumishi wa shamba lako la mzabibu, ee Bwana, ukinipa mshahara wa saa ya kumi na moja na neema ya wokovu.

Tazama ma askari wa mfalme mkuu*:* Walishindana na amri za wazulumu wa walizarau mateso, kwa usharifu, wakakanyanga na kuvunja kosa lote; walipopokea taji walilostahili wanatupokelea amani kwa Mwokozi na neema ya wokovu kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira mustahili wa nyimbo zetu, Musa aliona fumbo yako na macho yake: ni kichaka kilichowaka moto bila kuteketezwa, kwani moto wa umungu haukuteketeza tumbo lako safi. tena tunakuomba, wewe Mama wa Mungu wetu, ulete amani duniani.

## MU KAZI MBILI MANGARIBI KATIKA SAUTI YA KWANZA

*Panefimi martires.*

Ee Kristu, ulipanua mikono yako safi Msalabani kwa kukomboa kazi ya mikono yako, Adamu aliyeshindwa ku ufalme wa mauti; ewe mpenda-wanadamu ukamufufua kwa uwezo wako mkuu.

Ee Kristu Mungu wetu, uliposulubiwa Msalabani kwa ubinadamu wako, ukaifanya umungu hali ya wanadamu na ukamuua nyoka mbaya; ukatuopoa ku laana tuliyostahiliwa kwa uzito wa muti, ukawa wewe mwenyewe laana kwa ajili ya kuleta baraka duniani na neema ya wokovu.

Ee Rabi ambaye utukufu unapita heshima yote, ilikupendeza kuhesabiwa kuwa bure, ukateswa na lufu ya haya Msalabani katika wema wako kimungu; na katika hii ubinadamu ukapata umilele na uzima kama Paradizoni kwa ajili ya kufa kwako mwilini, ee Bwana mwenyezi.

**Wimbo ya Mzazi-Mungu.**

Aliposimama chini ya Msalaba wa Mwana wake na Mungu wake, Mushuhuda wa uvumilivu wa milele, Bikira Mzazi-Mungu akalalamika akilia: Ole wangu, ee Mwana mupole kabisa, Neno na Hekima ya Mungu, sababu gani hii mateso yasiyo haki? Lakini unataka kuokoa wanadamu.

Aliposimama chini ya Msalaba, Bibi asiyeolewa akapata uchungu na kujehuriwa na akalala: Ee Mwanangu mupendwa, usimkatalie Mwana wake huyu aliyezaa Neno la Mungu; usiniache peke yangu, wewe Mwana wa pekee wa asili moja na Baba.

Wakati nilipokuzaa, sikusikia uchungu, lakini uchungu gani nasikia sasa, ee Neno mwenye kusulubiwa bila haki! Ole wangu, alivyosema Bikira akilia na uchungu, siwezi kuteswa kwa kukuona umeinuliwa Msalabani, ee Bwana mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Kristu, Bikira alipoona kuuawa kwako kwasipo haki, akalalamika na machozi: Ee Mwanangu mpole kabisa, mara ngapi unateswa bila haki! Namna gani umetundikwa juu ya muti, wewe uliyetundika dunia pa maji! Nakuomba, usiniache peke, ee Mfalme wa dunia na mwenye mapendo wa milele, mimi Mama na mutumishi wako.

**PROKIMENON**

*Sauti ya kwanza.*

Hakika wema na rehema zitanifuata siku zote za maisha yangu *(mara tatu).*

*Shairi:* Bwana ni muchungaji wangu; sitapungukiwa na kitu.

**APOSTIKHA**

Msalaba ukasimikwa juu ya Kalvario, ukitutirikizia umilele wa hii chemcherm isiyokauka hata mara moja: Ndiyo ubavu wa mwokozi.

Msalaba wa samani wa Mwokozi kwa sisi ni boma la kweli: Tulipotumainia, wote tumeokoka.

Mashahidi Watakatifu, neema gani kwa ujaa wenu! Ulitoa damu yenu na pokeeni urisi wa mbinguni; kwa jaribu la wakati ndogo furaha yenu yanakaa ya milele; badilisho kweli la ajabu: Kwani mumeacha uharibifu sababu ya kupokea mema ya milele: Sasa unafurahi pamoja na Malaika na munaimba bila kuacha Utatu wa asili moja.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Alipomuona Kristu ametundikwa Msalabani, Bikira akasema: Upanga umechoma moyo wangu kama alivyotangulia kuelea mzee Simeoni; lakini fufuka, ee Mwana musiyekufa, na kuomba, utukuzwe pamoja na Mama yako tena mtumishi wako.

## MU KAZI TATU ASUBUI KATIKA SAUTI YA KWANZA

### KATHISMA YA KWANZA

Ee Bwana, okoa taifa yako na bariki urizi wako. Ukiwapa wafalme kushinda juu ya wakafiri, na kuilinda jamii yako kwa Msalaba wako.

Ewe Kristu, ulipopanda Msalabani, uliharibu uzulumu na nguvu ya adui; apana ao Malaika ao mwanadamu aliyetuokoa, lakini ni Mungu yeye mwenyewe*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Bikira, tunasabitishwa na ulinzi wako, na kwa maombi yako tunaokolewa ku hatari yote na kulindwa kila wakati na Msalaba wa Mwana wako, sisi waaminifu, tunakutukuza.

### KATHISMA YA MBILI

*Tu lithu sfragisthentos.*

Ewe Mpenda-wanadamu, tunasujudu mbele ya muti ya Msalaba wako; ulisulubiwa pa hii, wewe Uzima wa ulimwengu; kwa Mnyanganyi aliyekuamini, ewe Mwokozi, ukamfungulia Paradizo; na akapata heri ya milele alipokulalamikia*:* Bwana, unikumbuke mimi; kama yeye, utupokee sisi tunaokulalamikia*:* sisi wote tumetenda zambi, usituzarau katika wema wako.

Zamani, Silaha ya Msalaba ikafunuliwa kwa mfalme Konstantino katika vita sababu ya kuwa ukumbusho wa ushindi wa imani isiyoweza kushindwa; katika hii Mtakatifu Paulo anajitukuza, inatetemesha nguvu za Hadeze na imekuwa wokovu wa wakristu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Habari ya ajabu na fumbo ya kushangaa! Alivyolalamika Bikira Takatifu na Safi, alipoona ametundikwa pa muti Bwana mwenye kuchukua ulimwengu mikononi mwake na kuhukumiwa na Waamzi na sheria na kusulubishwa Msalabani.

### KATHISMA YA TATU

*Ton tafon su Sotir.*

Ulipanua mikono yako Msalabani, ewe Mungu wa mapendo sababu ya kuleta watu waliyojitenga kwako kwa kutukuza wema wako mkuu; tazama urisi wako, ee Bwana, na angusha adui kwa Msalaba wako wa Samani.

Kwa mateso waliyoteswa Watakatifu kwa ajili yako, tunakuomba ukubali, ewe Mungu wetu, kuponya mateso yetu yote, ee Bwana Mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Mwana-Kondoo jike Safi alipoona Mwana-Kondoo na Mchungaji ametundikwa bila uzima juu ya muti, akalia na kulalamika akisema: Ee Mwanangu, namna gani nitateswa juu ya upendeleo wako usiyokadirika na mateso yako ya kutaka, ewe Bwana wa wema wote?

### EKSAPOSTILARION

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

## APOSTIKHA

Wewe uliyesulubiwa Msalabani kwa kutupatia uzima, tunakuimbia daima kama Rabi na Mwokozi wetu.

Kwa Msalaba wako, ee Kristu, Malaika na wanadamu wakafanya Eklezya moja, kundi moja la kondoo; mbingu na dunia zinafurahiwa: Ee Bwana, utukufu kwako.

Mashahidi watakatifu wenye kustahili sifa yote, apana wala jaribu, wala huzuni, wala njaa, wala uzulumu, wala hatari, wala hasira ya wanyama kali, wala upanga, wala moto ambazo kwa vitisho vyao viliweza kuwatenga mbali na Mungu; lakini ni kwa mapendo kwa ajili yake mulisahau ulimwengu mukiwa wageni ku mwili wenu na mukishindana kwa kuzarau mauti; na tena mukapokea tuzo la kweli la kazi yenu, mukawa warisi wa ufalme wa mbingu: Ombeni kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

*Ton uranion tagmaton.*

Ee Neno la Mungu, aliposimama karibu ya Msalaba, Mama yako Safi akapaza sauti akilia: Ee Mwanangu, namna gani umekufa Msalabani? Ole wangu, Nuru ya macho yangu, uzuri wako umeenda wapi? Wewe mtoto muzuri kabisa wa watu.

## MU KAZI TATU MANGARIBI KATIKA SAUTI YA KWANZA

**Wimbo ya Mitume Watakatifu.** *Panefimi Martires*

Enyi Mitume Watukufu wa Kristu, Wafuasi waliyoitwa na Mungu wetu, Walimu wa ulimwengu muliyopata Bwana, mpatanishi kati ya wanadamu na Mungu, muliungana naye, duniani mulitangaza waziwazi umungu wake na ubinadamu wake kamili.

Enyi Mitume wa Kristu wenyi hekima kabisa, kwa maombezi yenu munipokelee neema ya maarifa ya kiroho, ninyi muliyo kweli kwa hekima walimu na wagawanyi, mulipotangaza nuru ya Mfariji na kuteketeza ku moto uchafu wa moyo wangu, munifanye niwe mstahili wa kuwaimbia nikisema wenyi heri.

Enyi Mitume muliyemuona Neno la Mungu, angazeni roho yangu yenye kuwa na giza ya tamaa, ninyi ambao mafundisho yaliangaza mipaka ya ulimwengu na yalifukuza giza ya miungu ya uongo, mutuombee sasa ili amani na neema ya wokovu yapewe ku roho zetu.

**Wimbo ya Mtakatifu Nikola.** *Ton uranion tagmaton*

Ku kanisa unaruka juu ya maua pamoja na Malaika kama ndege mwenyi kuruka juu kabisa, ewe mwenyi heri Nikola, unalalamika daima kwa Mungu kwa ajili yetu katikati ya majaribu na ya hatari, na kwa maombezi yako unatuokoa.

Ulipokaribia uzuri wa vitu tusipoona, ewe Pateri Mtakatifu kamili ulishika utukufu wa ajabu wa Watakatifu; na unatufunulia waziwazi mafundisho ya mbinguni ya kuonekana kwako kwa milele.

Ewe Pater mletaji-Mungu, kwa nuru ya fazila ulizotimiza, uliangaza uzuri wa mapambo yako takatifu; dumisha kwa ajili yetu jambo ajabu la kuonekana kwako mbinguni; ukituopoa ku hatari yote.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

*Ton uranion tagmaton.*

Ewe Bikira msiyeolewa uliyewapata mimba ya Mungu wetu mu kamilifu, wa nyakati, umekaa tena kweli Bikira kisha kuzaa, ewe kiti na mulango wa ufalme, meza ya siri na kinara chenyi kuangaa na nuru.

**PROKIMENON.**

*Sauti ya tano.*

Uniokoe, ee Mungu, kwa jina lako na unihukumu kwa uwezo wako *(mara tatu).*

*Shairi*: Ee Mungu, sikia ombi langu.

**APOSTIKHA.**

Tota Mitume kinubi cha umoja anachotetemesha Roho Mtakatifu kilifukuza mafumbo yenyi kuongozwa na mashetani na kinatangaza Bwana peke yake, ikiopoa watu ku uwongo wa miungu ya uwongo na ikiwafundisha kwa kusujudu mbele ya Utatu wa asili moja.

*Ton Uranion tagmaton.*

Tushangilie kwa wimbo moja Mitume Petro na Paulo, Luka, Matayo, Marko na Yoane, Andrea, Tomasi, Bartholomeo, Yakobo, Filipo na Simoni: Kwa jamaa lote la Wafuasi tunatolea sifa na nyimbo zetu.

Hakuna mtu hata mmoja hana zambi ile wewe, peke yako Msiyekufa; tena, ewe Mungu wa wema, weka watumishi wako katika nuru ya milele ili waimbe pamoja na Malaika mbinguni, na kwa rehema yako usiangalie zambi zao, lakini uwahurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira mstahili wa nyimbo zetu, Musa aliona fumbo yako na macho yake: Ni kichaka kilichowaka moto bila kuteketezwa, kwani moto wa umungu haukuteketeza tumbo lako safi. Tena tunakuona, wewe Mama wa Mungu wetu, ulete amani duniani.

## MU KAZI INE ASUBUI KATIKA SAUTI YA KWANZA

### KATHISMA YA KWANZA

Wenyi Mitume wenyi hekima muliyovua ulimwengu wote na kupokea kwa Mungu mapendo yake mtuombee sisi tunaoimba sasa*:* Ee Bwana, kwa maombezi ya Mitume wako,okoa watu wako wa Kristu ukilinda roho zetu ku hatari yote.

*Shairi:* Sauti yao imeenea duniani mwote na maneno yao hata miisho ya ulimwengu.

*Tu Lithu sfragisthentos*

Waliposhinda na tete la Msalaba na wavu wa Neno werevu wa Wasemaji, wavuvi wa watu wakaangaza mataifa ili wakutukuze kama Mungu kweli; ee Bwana, chemchem ya nguvu yao, tunakuimbia wimbo wetu wa sifa ya milele*:* Utukufu kwa Baba na kwa Mwana, utukufu kwa Roho wa asili moja, utukufu kwa huyu ambaye Mitume walileta nuru duniani.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ulipopata mimba bila kuteketezwa na moto kimungu, na bila mbegu ulipochirikizisha Bwana Chemchem ya uzima, ee Bikira mjaliwa neema na Mzazi-Mungu, utuokoe sisi tunaotukuza.

**KATHISMA YA MBILI**

*Ton tafon su Sotir.*

Enyi waamini, kwa nyimbo zetu tuwashangilie Mitume wenyi hekima, baragumu ya Kristu; gari yao ilituondoa Kuzimuni ya ukafiri, wakiongoza wanadamu ku bandari ya wokovu na neema ya Roho Mtakatifu.

Duniani imeonekana katika mwili na kwa wakati Nuru toka Nuru ya milewle; ikaangaza ulimwengu sababu yenu, na sisi wote, tulipoangazwa na mafundisho yenu kimungu, enyi Mitume wenyi heri tunatukuza makumbusho yenu takatifu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Sisi wote tunayo wewe msimamizi wetu karibu ya Mungu, ee Bikira tunakimbilia ku hekalu lako takatifu, kuomba msaada na ulinzi wako; ewe Mama Bikira daima, utuopoe ku uovu wa shetani, uwaondoe ku azabu wale wenyi kukutaja mwenye heri.

**KATHISMA YA TATU.**

**Wimbo ya Mt. askofu Nikolas.** *Ton tafon su Sotir.*

Askofu aliyeishi ku Myre mwilini, Mtakatifu Nikolas, ulitolewa kwa manemane ya Roho Mtakatifu; na kwa mpako wa miujiza yako, unawajaza na arufu nzuri ya manukato ya utakatifu wako wale wenye kutaka kutukuza kwa ubani wa nyimbo zao makumbusho yako takatifu.

Wote, tuwasihi Mashahidi wa Kristu wenye kutuombea wokovu wetu, na wote tuendeni kukutana nao katika imani kwa kusamehewa na kuponyeshwa kwa walinzi hawa wa imani wenye kuwafukuza mashetani.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira Safi kamili, Wafuasi na Mitume Watakatifu kwa mafundisho yao yenyi kuongozwa wakawatangazia wote uzazi wako wa ajabu, wakitufundisha kusujudu mbele yako, ewe Mzazi-Mungu; tunakuomba uombe pamoja nao kwa ajili ya wokovu wa watumishi wako waamini.

**EKSAPOSTILARION**

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

**APOSTIKHA**

Toka Mitume Kinubi cha umoja anachotetemesha Roho Mtakatifu kilifukuza mafumbo yenyi kuongozwa na shetani na kinatangaza Bwana peke yake, ikiopoa watu ku uwongo wa miungu ya uwongo na ikiwafundisha kwa kusujudu mbele ya Utatu wa asili moja.

*Ton Uranion tagmaton.*

Tushangilie kwa wimbo moja Mitume Petro na Paulo, Luka, Matayo, Marko na Yoane, Andrea, Tomasi, Bartholomeo, Yakobo, Filipo na Simoni: Kwa jamaa lote la Wafuasi tunatolea sifa na nyimbo zetu.

Enyi Mashahidi Watakatifu, furahini katika Bwana, kwani mumeshindana Wazulumu; wala upanga, wala vema sana; mumeshindana na wafalme na mumewashinda wazulumu; wala upanga, wala moto haukuwaogopesha ninyi, wala wanyama kali waliyorarua mwili wenu, lakini pamoja na Malaika mukamwimbia Kristu na mukapokea taji la mbinguni*:* Ombeni ili tupewe neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

*Ton Uranion tagmaton.*

Tumtukuzeni Bikira kama walivyotufundisha Manabii: Yeye ni chombo cha zahabu ambamo manna inalindwa, kichaka kilichowaka moto bila kuteketezwa, meza, kichi cha ufalme, kinara cha Nuru, mulima usiyochongwa, safina ya agano. tena mulango wa mbingu.

## MU KAZI INE MANGARIBI KATIKA SAUTI YA KWANZA

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.** *Ton Uranion tagmaton.*

Zamani, ku muti uliyokataziwa, baba wa kwanza akaonja mauti; sasa, katika muti wa Msalaba mwamini wote anaepuka ku hukumu mbaya; mwenye pumuzi wote atukuze na amuimbie Bwana aliyesulubiwa kwa kutaka kwake kwa ajili yetu, na kwa lufu yake akaangaza mipaka ya ulimwengu.

Moyo wangu ni mugumu, mimi wote ni mateko ya mawazo mbaya, tazama nahukumiwa na napaza sauti: Ee Neno la Mungu, katika rehema yako sahihisha siri zangu mbaya na vishindo vibaya vya moyo wangu , ee Bwana.

Tunajitukuza katika Msalaba wako, ee Kristu mwenye rehema, katika hii tunapotengua uerevu wa adui, tunaendelea kukuimbia, kwani ulitimiza wokovu duniani kwa ajili yetu wakati, katika rehema na wema wako, ulipanda kwa kutaka kwako Msalabani.

**Wimbo ya Mzazi-Mungu.**

Zamani, Bikira Takatifu kamili alipomwona huyu aliyezaa bila mdegu, hakuweza kuvumilia uchungu lakini kwa machozi akalalamika: Wewe kwa alama moja, unakaza ulimwengu, namna gani umehukumiwa Msalabani, halafu unapanda kuokoa wanadamu?

Bikira Mtakatifu kamili akasema: Ee Neno wa milele kama Baba mbinguni, ninapomwona mwanangu Msalabani, siwezi kusikia ukosefu wa shukrani wa wanadamu; lakini kwa sababu umekuja kuokoa nyumbe, unateswa kwa uvumilivu hii yote.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .**STAVROTHEOTOKION.**

Alipomuona Mwana-Kondoo ametundikwa Msalabani, Bikira Mtakatifu kamili akalalamika akilia: Ee Mwanangu mupole, ni jambo gani hili la ajabu na mupya? namna gani huyu mwenye kushika ulimwengu mkononi mwake anajiachilia kupigiliwa msimari mwilini Msalabani?

**PROKIMENON.**

*Sauti ya sita.*

Kusaidiwa kwangu kunatoka kwa Bwana aliyefanya mbingu na dunia *(mara tatu).*

*Shairi:* Ninanyanyua macho yangu kwa milima.

**APOSTIKHA**

Msalaba ulisimikwa ku Kalvario, ukitutirikizia umilele wa hii Chemchem isiyokauka: Ubavu wa Mwokozi..

Msalaba bora wa Mwokozi ni boma kabisa ya kweli kwa sisi; tulipoutumainia, wote tumeokoa.

Ewe Mungu wa mapendo, kwa maombi ya Watakatifu wote na ya Mzazi-Mungu, utupe amani na utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .**STAVROTHEOTOKION.**
*Panefimi Martires.*

Uchungu aliyeonja zamani Adamu ukautuliza wakati ulipoonja siki na nyongo, ee Mwanadamu mupole ulipotundikwa Msalabani! Ndivyo alivyosema Mzazi-Mungu katika machozi yake. Ewe Mwamzi mwenyi haki, tuliza huzuni kubwa yananiletea mateso yako na fufuko, ee Bwana mwenyezi.

## MU KAZI TANO ASUBUI KATIKA SAUTI YA KWANZA

### KATHISMA YA KWANZA

Ee Bwana, okoa taifa yako na bariki urizi wako. Ukiwapa wafalme kushinda juu ya wakafiri, na kuilinda jamii yako kwa Msalaba wako.

Ewe Kristu, ulipopanda Msalabani, uliharibu uzulumu na nguvu ya adui; apana ao Malaika ao mwanadamu aliyetuokoa, lakini ni Mungu yeye mwenyewe*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . .**STAVROTHEOTOKION.**
*Ton tafon su Sotir*.

Ewe Mwokozi ambaye Msalaba unawakimbiza maadui, sambaza uhalifu kama majivu; tukuza mbele Eklezya yako takatifu, tuliza, ee Bwana, zoruba yenyi kutokea kwa ukali juu yetu; kwa maombezi ya Mzazi-Mungu, uwape waamini wako amani.

### KATHISMA YA MBILI

*Tu lithu sfragisthentos*

Ewe Mpenda-wanadamu, tunasujudu mbele ya muti ya Msalaba wako; ulisulubiwa pa hii, wewe Uzima wa ulimwengu; kwa munyanganyi aliyekuamini, ewe Mwokozi, ukamfungulia Paradizo; na akapata heri ya milele alipokulalamikia*:* Bwana, unikumbuke mimi; kama yeye, utupokee sisi tunaokulalamikia*:* sisi wote tumetenda zambi, usituzarau katika wema wako.

Zamani, Silaha ya Msalaba ikafunuliwa kwa mfalme Konstantino katika vita sababu ya kuwa ukumbusho wa ushindi wa imani isiyoweza kushindwa; katika hii Mtakatifu Paulo anajituuza, inatetemesha nguvu za Hadeze na imekuwa wokovu wa wakristu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Wakati ninapokuona umekufa na bila vazi Msalabani; ee Mwanangu, wema kubwa na Bwana Mwenyezi, upanga umechoma moyo wangu, najeruhiwa vibaya, ndivyo alivyosema Bikira Mtakatifu akilia, yeye tunayeimbia kama Mama wa Bwana na tunayetukuza na imani.

### KATHISMA YA TATU

*Ton tafon su Sotir*.

Ewe Mungu wa mapendo, umepigiliwa Msalabani kwa kutaka kwako ukigeuza hali yetu ya uovu kuwa mungu; na ukamuua nyoka muuaji wa wanadamu; ee Bwana, sabitisha ulimwengu katika imani ya kweli, na kwa Msalaba wako wa samani achisha uhalifu.

Ee Bwana, utukufu wa mashindano na taji la Washindaji, ndiwe uzuri wa Mashahidi Watukufu*:* Kwa imara yao katika majaribu wakawakimbiza makafiri na wakapokea ushindi

mbinguni kwa uwezo wa Mungu; ee Bwana, kwa maombezi yao uniokoe kwa Adui msiyeonekana na uniokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Mwana-Kondoo jike Safi alipoona Mwana-Kondoo na Mchungaji ametundikwa bila uzima juu ya muti, akalia na kulalamika akisema: Ee Mwanangu, namna gani nitateswa juu ya upendeleo wako usiyokadirika na mateso yako ya kutaka, ewe Bwana wa wema wote?

**EKSAPOSTILARION**

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

**APOSTIKHA**

Wewe uliyepigiliwa Msalabani kw akutupatia zawadi ya uzima, tunakuimbia daima kama Rabi na mwokozi wetu.

Katika Msalaba wako, ee Kristu, Malaika na wanadamu wanafanya Eklezya moja, kundi moja; mbingu na dunia zinafurahiwa: Ee Bwana, utukufu kwako.

Njooni, enyi mataifa yote, tuimbe mashairi na nyimbo za kiroho kwa kuwatukuza Mashahidi watukufu wa Kristu, Watangazaji wa imani tena taa za ulimwengu, Chemchem isiyokauka ambako kunatiririka maponyesho; kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu, leta amani ku dunia na neema ya wokovu ku roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

*Panefimi martires.*

Ewe Mungu wa mapendo, umeinuliwa Msalabani na kwa mapenzi yako umetolewa sadaka kama mwana-Kondoo asiye na kilema, mwana mupole kabisa! Ndivyo alivyolalamika katika machozi yake Mwana-Kondoo jike Safi alipomwona Bwana Msalabani; nani mina moyo wenyi kujeruhiwa lakini naimba rehema yako kubwa.

## MU KAZI TANO MANGARIBI KATIKA SAUTI YA KWANZA

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.** *Panefimi martires.*

Zamani nilipokula tunda lililokataziwa, nikafa; nilipovutwa na shauri ya nyoka, ole wangu, nikajitenga ku utkufu wa Mungu; lakini kama zambi ilinishusha ku mauti, ewe mpenda-wanadamu, peke yako mwenye huruma, fanya ili nikae mara ingine katika Paradizo.

Ee roho yangu, ukiacha shuruli yote ya hii uzima, waza ku Saa yako ya mwisho, ku mwisho wako, uwe tayari kwa kutayarisha lufu yako, kusudi kwa rafla mauti yasikupate bila kujua; lakini uwe mwangalivu katika sala na maombolezo mbele ya Bwana.

Regeza majivuno ya tamaa zenyi kunishika mu nguvu zao, tuliza vishindo vyangu vya mchafuo kwa uwezo wake mu umungu, ee Bwana wa milele, ukinipa katika mapendo yako maondoleo ya zambi zangu, ewe mpenda-wanadamu mwenye kuwahurumia wenye zambi, bahari ya rehema na hazina ya wema.

**Wimbo ya Mzazi-Mungu.**

Ee Mungu wa mapendo, kwa maombezi ya Watakatifu wote na ya Mzazi-Mungu, utupe amani na utuhurumie.

Katika uwanja, enyi Mashahidi watakatifu, imani yenu ikavunja nguvu ya mashetani mulipowaopoa wanadamu ku udanganyifu; na wakati wa kukatwa kwenu kichwa mukapaza sauti: Ee Bwana, sadaka ya uzima wetu ikupendeze, kwani kwa mapendo yetu kwa ajili yako tulizarau mema ya uzima huu.

Mashahidi watakatifu, neema gani ku ushujaa wenu! Mumetoa damu yenu na munapokea uriti wa mbinguni; badilisho kweli la ajabu: Kwani mumeacha uovu sababu ya kupokea mema ya milele; sasa munafurahiwa pamoja na Malaika na munaimbia bila kuacha Utatu wa asili moja.

Utukufu kwa Baba. Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Utukufu wa ulimwengu, uliyopandwa kwa watu, na ulizaa Bwana, mlango wa mbinguni, tumusifu Bikira Maria, wimbo wa wasiyo mwili, na pambo ya waaminifu; kwa sababu yeye alikuwa mbingu, na Hekalu la umungu; yeye alipomoa ukuta ya adui, alibadilisha kwa amani, na alifungua ufalme. Basi pakuwa na hii, nanga ya imani, tuiko na mlinzi, Bwana hivi aliyezaliwa Kwake. Kwa hivi kuwa na moyo, kuwa na moyo taifa la Mungu; kwa sababu yeye anagombanisha adui sawa mwenyezi.

**PROKIMENON**

*Sauti ya saba.*

Mungu ni ngoma yangu wa rehema yangu atanitangulia *(mara tatu).*

*Shairi:* Uniponyeshe na adui zangu, ee Mungu wangu.

**APOSTIKHA**

Enyi Mashahidi kustahili sifa yote, apana dunia iliyowaficha, ni mbingu iliyowapokea; milango ya Paradizo imefunguliwa kwa ajili yenu, na huko munakuwa na mti wa uzima; muombeni Kristu alete amani na neema ya wokovu ku roho zetu.

*Shairi:* Mungu ni wa ajabu katika Watakatifu wake.

Mashahidi Watakatifu, neema gani kwa ujaa wenu! Ulitoa damu yenu na pokeeni urisi wa mbinguni; kwa jaribu la wakati ndogo furaha yenu yanakaa ya milele; badilisho kweli la ajabu: Kwani mumeacha uharibifu sababu ya kupokea mema ya milele: Sasa unafurahi pamoja na Malaika na munaimba bila kuacha Utatu wa asili moja.

*Shairi:* Watakatifu walio duniani, wao ni wale wazuri sana ninaopendezwa nao.

Hakuna mtu hata mmoja hana zambi ile wewe, peke yako Msiyekufa; tena, ewe Mungu wa wema, weka watumishi wako katika nuru ya milele ili waimbe pamoja na Malaika mbinguni, na kwa rehema yako usiangalie zambi zao, lakini uwahurumie.

*Shairi*: heri wale uliyochagua, wale uliyochukuwa pamoja nawe, ee Bwana.

**Mwimbo ya wafu.**

Furaha gani ya uzima huu inakaa bila huzuni? Utukufu gani duniani haujui mateso? Yote inafika kama kivuli na kama ndoto ya uwongo; kwa rafla, mauti inaondoa yote, lakini kwa nuru ya uso wako, ee Bwana, na kwa mapenzi ya uzuri wako, ee Kristu Mpenda-wanadamu, uwape wateule wako mapumziko.

Utukufu kwa Baba. Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ewe Bikira Mtakatifu, salamu, ndiwe kama ya Mungu wetu, hazina takatifu ya ulimwengu **,** taa isiyozimika kamwe, makao ya wa milele, hekalu ya Mwana isiyo ya Bwana isiyoweza kuharibiwa; salamu, kwani ulizaa Mwana-Kondoo wa Mungu anayeondoa zambi za dunia.

# MU POSHO ASUBUI KATIKA SAUTI YA KWANZA

## KATHISMA YA KWANZA

*Tu Lithu sfragisthentos*

Kama ma askari wema, wenyi shauri moja katika imani, bila woga na bila laumu mbele ya makanio ya wazulumu, wahodari, mumenjongea Kristu mkishika Msalaba wake boga. Ku mwisho wa safari na wa mashindano mukapata ushindi wa Juu-mbinguni. Utukufu kwa huyu ambaye nguvu yake ikawa tegemeo yenu, utukufu kwa huyu aliyemivika taji, utukufu kwa huyu anayetenda ndani yenu kwa kutuponyesha.

Kwa mateso waliyoteswa Watakatifu kwa ajili yako, tunakuomba ukubali, ewe Mungu wetu, kuponya mateso yetu yote, ee Bwana Mpenda-wanadamu.

*Sauti ya kwanza. Ton tafon su Sotir.*

Wote, tuwasihi Mashahidi wa Kristu wenye kutuombea wokovu wetu, na wote tuendeni kukutana nao katika imani kwa kusamehewa na kuponyeshwa kwa walinzi hawa wa imani wenye kuwafukuza mashetani.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. **THEOTOKION.**

Wakati Gabrieli alisema kwako Bikira, salamu, kwa sauti; Rabi wa wote alichukua mwili, ndani yako safina takatifu, sawa mwenye haki Daudi alivyosema. Ulionekana kuwa munene sana kuliko mbingu, kwa sababu ulichukuwa Muumbaji wako. Utukufu kwa yule alikaa ndani yako; utukufu kwa yule alitoka kwako; utukufu kwa yule alitupatia uhuru, juu ya uzazi wako.

## KATHISMA YA MBILI

Ee Bwana, utukufu wa mashindano na taji la Washindaji, ndiwe uzuri wa Mashahidi Watukufu*:* Kwa imara yao katika majaribu wakawakimbiza makafiri na wakapokea ushindi mbinguni kwa uwezo wa Mungu; ee Bwana, kwa maombezi yao uniokoe kwa Adui msiyeonekana na uniokoe.

Ee Kristu, ulipoondoa, ufalme wa mauti, ukawatirikizia wanadamu uzima wa milele; wale wote wenye kukutumainia, sasa hawakufe lakini wanaishi ndani yako. Ee Bwana, pumzisha roho za watumishi wako na uwaweke kati ya Watakatifu wako; kwa maombezi ya Mzazi-Mungu, uwape neema ya wokovu.

*Ton tafon su Sotir.*

Ee Mwokozi, pumzisha marehemu katika kundi la wenye Haki, pahali pa nuru; walikutumainia wewe, ee mpenda-wanadamu; pokea ombi la kila mmoja kwa ajili ya wazazi wake na watoto wake, na kwa wema wako mkuu hakikisha wale tunakumbuka leo.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. **THEOTOKION.**

Ajabu wa maajabu, ee Mjaliwa neema, kiumbe kinafurahiwa pakukuona; ulipata mimba bila mbegu na ulizaa Nuyu Malaika wenyewe hawaweza kumutazama; ee Bikira Mzazi-Mungu, umuombe kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

## EKSAPOSTILARION

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

## APOSTIKHA

Njooni, enyi mataifa yote, tuimbe mashairi na nyimbo za kiroho kwa kuwatukuza Mashahidi watukufu wa Kristu, Watangazaji wa imani tena taa za ulimwengu, Chemchem isiyokauka ambako kunatiririka maponyesho; kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu, leta amani ku dunia na neema ya wokovu ku roho zetu.

Tazama ma askari wa mfalme mkuu*:* Walishindana na amri za wazulumu wa walizarau mateso, kwa usharifu, wakakanyanga na kuvunja kosa lote; walipopokea taji walilostahili wanatupokelea amani kwa Mwokozi na neema ya wokovu kwa ajili ya roho zetu.

Mashahidi watakatifu wenye kustahili sifa yote, apana wala jaribu, wala huzuni, wala njaa, wala uzulumu, wala hatari, wala hasira ya wanyama kali, wala upanga, wala moto ambazo kwa vitisho vyao viliweza kuwatenga mbali na Mungu; lakini ni kwa mapendo kwa ajili yake mulisahau ulimwengu mukiwa wageni ku mwili wenu na mukishindana kwa kuzarau mauti; na tena mukapokea tuzo la kweli la kazi yenu, mukawa warisi wa ufalme wa mbingu*:* Ombeni kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Enyi Mashahidi Watakatifu, furahini katika Bwana, kwani mumeshindana Wazulumu; wala upanga, wala vema sana; mumeshindana na wafalme na mumewashinda wazulumu; wala upanga, wala moto haukuwaogopesha ninyi, wala wanyama kali waliyorarua mwili wenu, lakini pamoja na Malaika mukamwimbia Kristu na mukapokea taji la mbinguni*:* Ombeni ili tupewe neema ya wokovu.

**Mwimbo ya wafu.**

Katika tendo lako, ee Mwokozi wangu, umeonyesha ya kama ndiwe ufufuo wa wote, Neno ambaye kwa neno lako ukamfufua Lazaro katika wafu; hapo makomeo ya kapasuka na milango ya Hadeze yakapepea, kwa watu mauti yakaonekana kama usingizi, ee Bwana uliyekuja kuokoa ulimwengu na apana kuhukumu, ee Mpenda-wanadamu, uwape wateule wako mapumziko.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Salamu, Maria, Mzazi-Mungu kwani ulizaa Mfalme, Mwokozi na Nuru ya milele.

Elezo: *Kama kuna Alliluya, tunaimba ku Masifu nyimbo za Mashahidi zenyi kutangulia hapa juu, na kama Apostikha tunaimba yafuatayo:*

*Tunaimba hii wimbo ya wafu.*

*Sauti ya kwanza. Panefimi Martires.*

Tunakuomba, ee Mungu Mwokozi*:* Kwa huruma yako uwape marehemu mapumziko na uwaweke katika hema za wenyi haki pamoja na Watakatifu wako katika uwanja wa mbinguni, na kwa huruma yako usiangalie zambi zao, lakini uwape mapumziko.

*Shairi:* Heri wale uliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe, ee Bwana.

Hakuna mutu hata mmoja asiye na zambi ila Wewe, peke yako Msiyekufa; tena, Mungu wa wema, weka watumishi wako katika nuru ya milele ili waimbe pamoja na Malaika mbinguni, na kwa huruma yako usiangalie zambi zao, lakini uwape maondoleo.

*Shairi:* Roho zao zitapumzika katika furaha


Ee Mwokozi, ahadi zako ni isiyokadirika, ni vitu jicho haikuona, sikio halikusikia, na moyo wa mwanadamu haukuzania*:* Kwa huruma yako uwafundisheyo marehemu, ukiwapa uzima wa milele.

*Shairi:* Makumbusho yao ni ya milele.

Ee Bwana, marehemu wako ambao Msalaba wako ulikuwa nguvu na furaha yao wapate katika hii kama msaada ya zambi zao, na kwa damu heshimiwa uliyomwanga kwa ajili ya uzima wetu uwape, katika wema wako, utukufu wako na nuru yako ya milele.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ee Mama Bikira, umuombe Kristu Mwana wako awaondolee Watumishi wake zambi ambao ibada inakutangaza kama Mzazi-Mungu kadiri ya mafundisho na ya neno la ukweli, na uwafanye wastahili utukufu wa Watakatifu katika nuru ya ufalme wa mbingu.



# KIPANDE CHA SAUTI YA PILI

## MU POSHO MANGARIBI

**Wimbo ya Ufufuo.**

Kujeni tumwabudu huyu aliyezaliwa na Baba mbele ya milele, Mungu neno aliyechukuwa mwili, kwa Bikira Maria; kwa sababu alivumiliya Msalaba, alijitoa ku maziko, kama alivyotaka, na alifufuka katika wafu, aliniokoa mimi mtu mpotevu.

Kristu Mwokozi wetu, alizimisha maandiko mabaya ya ndani zetu, kwa kuipigilia Msalabani, na aliharibu nguvu ya mauti. Tuabudu Ufufuo wake wa siku tatu.

Tuimbeni Ufufuo wa Kristu pamoja na Malaika wakuu; kwa maana huyu ni Mkombozi, na Mwokozi wa roho zetu; na maogopesho ya utukufu, na nguvu ya uwezo, eko nakuja tena, kuhukumu dunia aliyeumba.

Malaika alihubiri ya kuwa wewe ni Rabi, mwenye aliyesulubiwa na aliyezikwa, na aliwaambia wanawake; kujeni tazameni, pahali alipolala Bwana, kwani amefufuka, kama alivyosema, kwa kuwa yeye ni mwenyezi; ndiyo maana tunabudu, wewe peke msiye kufa. Kristu Mpaji wa uzima, utuhurumie.

Kwa Msalaba wako ulivunja, apizo la muti; kwa maziko yako uliharibu, nguvu ya mauti; na kwa Ufufuo wako, uliangaza ukoo wa wanadamu; kwa hii, tunalalamika, ee Kristu mwema, na Mungu wetu Utukufu kwako.

Mbele yako Bwana, milango ya mauti ilifunguka na woga; wachungaji wa kuzimu pakukuona walipata woga; kwa maana ulivunja milango ya shaba, na kuzuia makomeo ya chuma, na ulituondoa ku giza, na kivuli cha mauti, na kupasua mafungo yaliyotufunga.

Pakuimba wimbo wa wokovu, tunaimba ku kinywa kujeni wote mu nyumba ya Bwana, tusujudu na tuseme; ee wewe uliyesulubiwa pa muti, na uliyefufuka katika wafu, na uliye mu kifua cha baba, hurumia zambi zetu.

Elezo: *Kama iko tarehe ya Mtakatifu moja mkubwa, tunaimba Doksastikon (Utukufu kwa Baba...) yake, kama hakuna, tunaimba Utukufu...sasa na siku zote... na Theotokion ya Mzazi-Mungu.*

Utukufu kwa Baba. .. Sasa na siku zote. .. **THEOTOKION**.

*Sauti ya mbili*

Kivuli cha sheria kinafifia, kwani ilikuja neema; sawa kichaka kiliwaka moto bila kuteketezwa, hivyo ulizaa Bikira, na ulibaki Bikira; pahali pa nguzo ya moto, jua la uhaki lilipanda pa fasi ya Musa, Kristu, wokovu wa mioyo zetu.

**APOSTIKHA**

Ufufuo wako, ee Kristu Mwokozi, uliangaza ulimwengu nzima, na uliita tena kiumbe chako; Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

Kwa muti (wa Msalaba), ee Mwokozi ulivunja, mafingo ya muti (wa paradizo); na kwa maziko yako uliuwa nguvu ya mauti, na kwa ufufuo wako uliangaza uzao wetu; kwa hii tunapaza sauti kwako; Kristu, mpaji wa uzima, Mungu wetu utukufu kwako.

Wakati ulionekana mwenye kupigiliwa Msalabani, ee Kristu, uligeuza uzuri wa viumbe; waaskari mukuonyesha, ukosefu wa huruma, walichoma ubavu wako kwa mukuki; lakini Waebrania waliomba kufunga kaburi, bila kujua uwezo wako, lakini wewe uliyekubali maziko kwa rehema yako, na ulifufuka kisha siku tatu, Bwana utukufu kwako.

Ee Kristu Mpaji wa uzima, kwa mapendo yako uliteswa juu ya wenyi mauti, ulishuka ku zimu na uwezo wako wote, na wale wanaongojea kuja kwako kule, sawa unaokoa ku mikono ya mwenyi nguvu, tena uliwapa kukaa haiko kuzimu lakini ku Paradizo; na sisi tunayotukuza ufufuo wako siku ya tatu, utupe maondoleo ya zmabi zetu na neema ya wokovu.

Elezo: *Kama iko tarehe ya Mtakatifu moja mkubwa, tunaimba Doksastikon (Utukufu kwa Baba...) yake, kama hakuna, tunaimba Utukufu...sasa na siku zote... na Theotokion ya Mzazi-Mungu.*

Utukufu kwa Baba. .. Sasa na siku zote. .. **THEOTOKION**.

*Sauti ya mbili*

Muujiza mupya kupita miujiza yote ya zamani! Kwani ni nani alijuwa mama kuzaa, pasipo Bwana, na kuchukuwa mikononi mwake, yule anayekumbatia kiumbe chote? Uzazi huu

ni mapenzi ya Mungu; kwa sababu ulimuchukua mu mikono yako, sawa mtoto, ewe Bikira msiye na doa, na ya kama mbele yake uko na hakika ya mama-mzazi; usihii bila kuacha, kwa ajili ya wale wanaokuheshimu, ahurumie na aokoe roho zetu.

**APOLITIKION**

Wakati ulishuka ku mauti, uzima usiyo kufa, hapo uliregeza kuzimu, kwa unara wa umungu wako; na wakati ulifufua wafu waliyolala kuzimuni, ezi zote za mbinguni zilipaza sauti; Mpaji wa uzima Kristu, ee Mungu wetu, utukufu kwako.

**THEOTOKION**

Siri zako zote, zinapita wazo lolote na zote ni utukufu sana, ee Mzazi-Mungu, wewe uliyewekwa alama ya safi, uliyelindwa kwa ubikira, ulijulikana kuwa Mama msema kweli, ulizaa Mungu kweli; umwombe aokoe roho zetu.

## SIKU YA MUNGU ASUBUI KATIKA SAUTI YA PILI

**KATHISMA YA KWANZA**

Wakati msharifu Yosefu aliposhusha mwili wako takatifu Msalabani, akaufunika na sanda mweupe na akaupakaa mafuta ya samani na akauweka mu kaburi mpya; lakini ukafufuka siku wa tatu, ee Bwana, ukaleta ku dunia neema kubwa.

Utukufu kwa Baba...

Karibu ya Kaburi Malaika wa Bwana akawatokea Miroforo na akawaambia: Kwa wafu kunastahili manemane na manukato; mwili wa Kristu umeondolewa ku uharibifu; tafazeli muimbe: Bwana amefufuka, akileta ku dunia neema kubwa.

Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Umetukuzwa kuwapita wote, tunakuimbia, ee Mzazi-Mungu; mauti imeuawa, na Hadeze imevunjwa kwa Msalaba wa Mwana wako; ametufufua ku lufu, ametupatia uzima wa milele; paradizo imepewa mara iongine kwa sisi sababu ya kufurahiwamo kama zamani; tena kwa shukrani tunatukuza mapendo na uwezo wa Kristu Mungu wetu.

**KATHISMA YA PILI**

Wewe usiyekataza jiwe lisifungwe kaburini, katika Ufufuo wako, ukatupatia jiwe la imani, ee Bwana, Utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba...

Kundi la Wafuasi wako linaungana na lile la Myroforo katika furaha; wote pamoja nao tunashangilia hii siku Kuu kwa kutukuza Ufufuo wako Takatifu; kwa haki zao, ee Bwana Mpenda-wanadamu, tunakuomba, uwape watu wako neema kubwa.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Mbarikiwa Ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira; kwa kuwa naye aliye amepata mwili nawe, kuzimu imetekwa, Adamu amerejezwa, Laana imekufa, Eva amekombolewa, Mauti imewekwa kifoni, tena sisi tumeofikia uzima; kwa hiyo tukiimba na kupaza sauti umehimidiwa U Kristu Mungu wetu, liyependezwa hivi. Utukufu kwako.

Elezo: *Kisha Mahimidi (Evlogitaria) tunasoma Ipakoi.*

**IPAKOI**

Ee Kristu Mungu Wanawake wakaenda kaburini kisha mateso Yako kwa kuupakaa mwili wako manukato. Wakaona Malaika ndani ya kaburi na wakashikwa na woga, kwani wakasema: Bwana amefufuka kwa ajili ya kuleta duniani neema kubwa.

## ANAVATHMI

*Sauti ya mbili.*

### ANTIFONON YA KWANZA

Nanyanyua macho ya moyo wangu mbinguni kwako, ewe Mwokozi, uniokoe na nuru yako ya kuangaa.

Ee Kristu wangu, utuhurumie, kwani tulitenda zambi mara nyingi, ku kila saa; mbele ya mwisho utupe neema ya kurudi kwako.

Utukufu kwa Baba. .. Sasa na siku zote. ..

Roho Mtakatifu anatawala, anatakasa na anavuta kiumbe, kwani ni Mungu, w1a asili moja na Baba na mwana.

### ANTIFONON YA MBILI

Bila msaada wa Bwana aliyeko kati yetu, hata mmoja hataweza kujilinda kwa Adui mwenye kutaka lufu yetu.

Ee Mungu wangu, usiwatoe watumishi wako ku meno yao, kwani kama simba maadui zangu wananishambulia.

Utukufu kwa Baba. .. Sasa na siku zote. ..

Utawala na heshima kwa Roho Mtakatifu, maana analeta nguvu kwa kiumbe yote kama Mungu, sasa katika Baba kwa Mwana.

### ANTIFONON YA TATU

Mwenye kwamini Bwana anafanana na mulima Takatifu wa Sayuni: Haratikisika kamwe na majaribu ya adui.

Wao wenye kusihi na Mungu, wasinyoshe mikono yao ku zambi, kwani Kristu hache kuanguka urisi wake chini ya nguvu ya makafiri.

Utukufu kwa Baba. .. Sasa na siku zote. ..

Hekima yote inatoka kwa Roho Mtakatifu, katika yeye neema imepewa kwa Mitume, katika yeye Mashahidi wanapata taji katika mashindano na Manabii wanapokea njozi zao.

### PROKIMENON

*Sauti ya mbili*

Amka, ee Bwana, unisemee ku hukumu: na mkutano ya watu itanizunguka.*(mara tatu).*

*Shairi*: Bwana Mungu wangu, matumaini kwako, uniokoe.

### KANUNI YA UFUFUO YA KRISTU

*Sauti ya mbili.*

### WIMBO YA KWANZA

**IRMOS:** Zamani, jeshi la maaskari wa faraoni likaangushwa shimoni kwa uwezo usiyoweza kushindwa, na sasa Neno aliyejifanya mtu aliondoa uzito wa zambi zetu, Bwana tunayetukuza, kwani amevaa utukufu.

**Wimbo ya Ufufuo ya Kristu.**

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Tulipokosa kufwata amri yako, tukapelekwa mbele ya Mfalme wa hii dunia, lakini Msalaba wako ukamuhukumu; alipokupiga kama mwenye kufa, yeye mwenyewe akapepea, mwenyi kusadiki kwa uzaifu, kwa nguvu ya mkono wako.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Mukombozi wa watu wenyi kufa, Mfalme wa uzima wa milele, uliingia duniani; kwa ufufuo wako ulivunja vifungo vya mauti, na wote pamoja tunakutukuza: Kwani umevaa utukufu.

**THEOTOKION**

Ee Bikira Mtakatifu kamili, ulionekana juu kabisa kuliko kiumbe chote chenyi kusichoonekana wala tunachoona, kwani ulizaa Muumba wakati alivyopenda kutwaa mwili tumboni mwako: Umwombe kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

**IRMOS:** Alipotembea chini ya bahari katika njia mpya, bila woga, bila kulowana, Israeli mpendwa wako akalalamika: Tumuimbie Bwana, kwani amevaa utukufu.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Ee Kristu kwa mateso yako mwilini ukawa nguvu ya wazaifu, kusimama kwa wenyi kuanguka na uzima usiyoharibirika wa wenye kufa, kwani umevaa utukufu.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Anahurumia sura yake iliyoanguka, na anainua sasa ikone yake iliyoharibika yeye Muumba na mwenyi kuleta mambo mapya; aliponawa akawafufua wote, kwani amevaa utukufu.

**KANUNI YA MZAZI-MUNGU:**

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Mungazi kiroho wa zamani, njia ya bahari iliyokauka kwa muujiza yalitangulia kuonyesha kuzaa kwako, ee Bikira Mtakatifu, na tunamtukuza, kwani amevaa utukufu.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Kwa nafsi, uwezo wa aliye-juu, Hekima kamili ya Mungu yenyi nafsi mbalimbali, ee Bikira Mtakatifu kamili, alipochukua mwili kwako, akakaa kati ya wenyi kufa, kwani amevaa utukufu.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Jua la haki aliingia kwa mlango wa tumbo lako usiyoweza kupitwa; alipita katika mlango wenyi kufunga sababu ya kuangaza dunia yote, kwani amevaa utukufu.

**WIMBO YA TATU**

*Eksinthisen i erimos.*

**IRMOS:** Kama mmea ulivyochanua jangwa, vivyo hivyo itachanuka Eklezya kavu ya mataifa ku majilio yako ee Bwana: Moyo wangu umesabitishwa katika yeye.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Katika mateso yako kiumbe kimeangushwa, alipoona kama mtumwa mwenye kutukanwa na makafiri, Mungu akaumba ulimwengu na mkono wake.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe. **THEOTOKION.**

Malaika wakashangaa, watu wakashituka kwa kuzaa kwako, na sisi waaminifu,tunakutukuza kama Mzazi-Mungu.

**IRMOS:** Tazama, upinde wa wenyi nguvu unavunjwa kwa nguvu yako, ee Kristu na wazaifu sasa uwezo wako ni mushipi wao.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Kristu mwenye kutawala viumbe vyote alishushwa chini ya Malaika wakati wa mateso yake aliyoteswa mwilini.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Uliponawa na kuhesabiwa pamoja na makafiri, ukaonekana mwenyi kuangaa kwa wanawake Watakatifu, mwenyi utukufu katika Ufufuo wako.

### KANUNI YA MZAZI-MUNGU:

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Ee Bikira huyu mwenye kupita nyakati zote, kwa sababu Yeye ni Muumba, alijifanya mwana kwa kutaka kwake tumboni mwako.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Tuimbie tumbo pana kuliko mbingu: Katika hii, Adamu akawa kwa shangwei mwana inchi wa inchi ya mbinguni.

### KONTAKION

Ulipofufuka kaburini, ee Mwokozi Mwenyezi, Hadeze ilipoona hii muujiza ikaogopa; watu wakasimama, na walipokuona, biumbe vinafurahiwa kwa ajili yako, Adamu anaungana ku furaha; na dunia, ee Mwokozi wangu, inakuimbia daima.

### NYUMBA (IKOS)

Nuru ya mwenye kukaa katika giza, ndiwe Ufufuo wa ulimwengu; ulileta uzima kwa watu, waaminifu wanafufuka pamoja nawe; ee Mwokozi, unaondoa ufalme wa mauti, ee Neno, unavunja milango ya Hadeze; hii muujiza inasangaza wafu na viumbe vyote vinafurahiwa kwa Ufufuo wako; sisi wote, ee Mpenda-wanadamu, tunatukuza na kushangilia upendeleo wako; na dunia, ee Mwokozi wangu, inakuimbia daima.

## MASIFU

Kila mwenye pumuzi na kila Kiumbe, kila kusifu, ee Bwana, kwa sababu kwa Musalaba uliharibu mauti, kusudi ya kuonyesha kwa mataifa, ufufuo wako katika wafu, kwa maana ni wewe peke Mpenda-wanadamu.

Wayuda wa wewe namna gani wakati askari walipochunga Mfalme walimupotesha? Sababu gani jiwe halikuchunge mwamba wa uzima? Ao watupatiye huyu aliyezikwa, ao wamwabudu huyu aliyefufuka, wakisema pamoja na sisi: Utukufu kwa wingi wa rehema Yako, ee Mwokozi wetu, utukufu kwako.

Furahini, mataifa na mushangilie; Malaika alikaa juu ya jiwe la Kaburi; huyu akatuletea sisi habari njema, akatwambia: Kristu Mwokozi wa watu, alifufuka katika wafu, na akajaza ulimwengu kwa marasi. Furahini, mataifa na mushangilie.

Malaika alileta salamu kwa Mujaliwa na neema, mbele ya kuchukuwa miimba yako, ee Bwana; tena Malaika alisukuma jiwe la Kaburi yako tukufu, katika ufufuko wako. Malaika wa

kwanza pahali pa sikitiko, akapasha habari ya alama ya furaha; Malaika mwengine pahali pa mauti, alitutangazia ya kama Rabi na Muletaji-uzima kwa sisi; kwa hii tunakupazia sauti: Ewe Bwana, Mufazili wa wote, utukufu kwako.

**Wimbo Anatolika**

Wanawake walimimia manukato na machozi, juu ya kaburi yako, na vinywa vyao vilijazwa na furaha, wakati waliposema: Bwana amefufuka.

Mataifa na watu, wasifu Kristu, Mungu wetu, aliyevumilia Msalaba sawa alivyotaka kwa ajili yetu, na aliyebaki siku tatu ndani ya Hadeze waabudu, ufufuko wake katika wafu, kwa ajili yake ulimwengu nzima umeangaziwa.

Ulisulubiwa, ulizikwa, ee Kristu, kama ulivyotaka; ulinyanganya mauti, kwa sababu wewe ni Mungu na Rabi, ukitoa kwa dunia uzima wa milele, na rehema kubwa.

Hakika ninyi wavunja-sheria, mulipofunga jiwe, mulitustahilisha kuona ajabu kubwa; walinzi walijua muzuri sana; leo Kristu alitoka Kaburini, na mulisema: «Mutasema, Wanafunzi wake walikuja kumuiba wakati tulipolala». Nani anaiba maiti, na tena mutupu? Huyu alifufuka kwa uwezo wake, kwa kuwa Yeye ni Mungu, akiacha sanda ya maziko ndani ya Kaburi. Kujeni Wayuda mwone, sababu gani hakubomoa muhuri, huyu aliyeshinda mauti, na aliyeleta kwa uzao wa watu, uzima usiyo na mwisho, na rehema kubwa.

Utukufu kwa Baba...**EOTHINON**

Sasa na siku zote...

Mbarikiwa Ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira; kwa kuwa naye aliye amepata mwili nawe, kuzimu imetekwa, Adamu amerejezwa, Laana imekufa, Eva amekombolewa, Mauti imewekwa kifoni, tena sisi tumeofikia uzima; kwa hiyo tukiimba na kupaza sauti umehimidiwa U Kristu Mungu wetu, liyependezwa hivi. Utukufu kwako.

**DOKSOLOGIA KUBWA**

## SIKU YA MUNGU MANGARIBI KATIKA SAUTI YA PILI

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.** *Ote ek tu ksilu.*

Unipe mawazo ya toba, leta pia nia ya majuto ku roho yangu maskini; uniamushe mu usingizi wangu, geuze moyo wangu mgumu na fukuza giza ya uzaifu wangu ondoa giza ya kutoyumainia, ee Neno, ili nikipata nguvu, niambatane tena sasa nawe na nienda kadiri ya mapenzi yako.

Ee Kristu peke yako ni mwenye rehema, Neno, peke yako ni juu ya mema yote, mvumilivu na mwenye rehema, nasujudu mbele yako tena nakuomba na juhudi, nakusihi na napaza sauti: Uniokoe, nimetenda zambi, uniokoe katika mapendo yako ili kwa ushukuru nikulalamikie: Ee Bwana unisamehe zambi zangu mimi mpotevu, na tangu sasa nitatembea na nuru ya wema wako.

Zambi zote nilizotenda juu yako, ee Mungu wangu, kwa mawazo, kwa maneno, kwa matendo zote naziungama sasa kwako, kwani nilipoteza wakati wote wa hii siku na katika uovu nimefika mpaka mwanzo wa usiku; tena nasujudu mbele yako, nikipaza sauti: Ee Bwana na Mwokozi nimekosa mbele yako, unirehemu na uniokoe.

**Wimbo ya wa Malaika.**

Njooni, kwa mashairi tuwashangilie na nyimbo za kiroho waongozi wa majeshi ya juu; kati ya Malaika wote Wabila-mwili, Malaika Wakuu Wawili wanaongoza makundi na wote waili walipata jina moja: Mfalme wa neema ni Gabrieli, mkubwa wa Sheria na wa nyakati zilizomtangulia Musa ni Mikaeli, mkubwa wa Malaika Wakuu.

Nyota ya Malaika mbinguni, Mwongozi mkuu wa makundi ya Wabila-mwili mwalimu na mtangazaji wa mafumbo ya siri ya Mungu, ee Mikaeli mwenyi heri, mwenyi kutezama umilele, tunakuomba, opoa ku mateso yote na ku hatari yote wale wenyi kukukimbilia; kwani ndiwe mlinzi wetu kwa Bwana mwenyi kukesha juu yetu.

Ewe Mwongozi wa Malaika, salamu, mwalimu wa siri isiyokadirika, mheshimiwa wa Mungu, saidi mkuu wa makundi ya Wabila-mwili, Malaika mkuu Gabrieli, mwenyi kujaa na utukufu na sifa, kwani ulionekana kuwa mtumishi wa mafumbo ya ajabu ya nia ya siri kabisa wakati ulipokuja kututangazia upendeleo wa milele wa Bwana Mungu kwa wanadamu.

Utukufu kwa Baba. .. Sasa na siku zote. ..**THEOTOKION**.

Nikiona saa ya azabu, natetemeka kwa kukumbuka zambi zangu nyingi, nitasema nini? Namna gani nitakimbia haya itaniletea upotevu wa maisha yangu? Nalalamika nikilia: Ee Bikira Takatifu uliyezaa hii johari safi kamili, ndiye Kristu, takasa roho yangu na uniokoe.

**APOSTIKHA**

Kama mwana mupotevu, nimekosa mbele yako, ee Mwokozi*:* Ee Baba pokea toba yangu na unihurumie, ewe Mungu wangu.

Ee Kristu Mwokozi wangu, nafananisha sauti ya mtoza-kodi*:* Unirehemu na unihurumie, ewe Mungu wangu.

Walipokataa furaha za hapa chini Mashahidi Watakatifu, kwani wakapokea hazina za mbinguni, Wakawa wenzao wa Malaika: Kwa maombezi yao, ee Bwana, utuhurumie na utuokoe.

Utukufu kwa Baba. .. Sasa na siku zote. ..**THEOTOKION**.

Mulango wa Bwana usiyoweza kupitwa, wenyi kufungwa kwa siri, ewe Mzazi-Mungu na Bikira mtukufu, pokea sala zetu kwa kuzitolea kwa Mwana wako na Mungu wako ili aokoe roho zetu kwa ajili yako.

## MU KAZI MOJA ASUBUI KATIKA SAUTI YA PILI

### KATHISMA YA KWANZA

Zambi zangu zimetokea nyingi juu yangu kama mawimbi ya bahari na kama mashua baharini na kubwa na mawimbi ya uovu; ee Bwana, uniongoze ku bandari ya amani na uniokoe ukinirudisha tena kwako.

Mimi ni muti kavu, ee Bwana, sitoe tunda la toba, naogopa shoka na moto usiyozimika; ndiyo maana nakuomba, mbele ya mwisho, uniokoe, ee Bwana, ukinirudisha tena kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Chemchem ya rehema, ewe Mzazi-Mungu, utustahilishe na huruma yako; tazama watu wenye zambi, onyesha uwezo wako wa siku zote; tunakutumainia wewe na tunakulalamikia*:* Salamu! Kama alivyofanya zamani Malaika mkuu Gabrieli.

### KATHISMA YA PILI

Kama Daudi mimi pia nakulalamikia*:* Unihurumie, nimetenda zambi; katika machozi ya toba, ee Bwana, safisha zambi zangu na unihurumie.

Unihurumie, ee Mungu, unihurumie, ndivyo alivyolia Daudi juu ya zambi yake, nami nahesabia makosa yangu kuwa mengi sana, lakini sina hata moja ya machozi aliyotoa*:* Unihurumie, ee Mungu, katika wema wako kubwa.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ewe Mzazi-Mungu, usimzarau mtumishi wako mwenye kuhitaji msaada wako, kwani roho yangu inakutumainia wewe*:* Unihurumie.

### KATHISMA YA TATU

Makundi matakatifu kamili ya Malaika mbinguni, ombeni Rabi Mtakatifu wa wema ili wakati wa hukumu ya ajabu atusamehe ku uchungu wa azabu na atuepushe ku uovu wa mashetani, ku giza ya tamaa na ku kitisho yote yenye kutuelemeza wakati tunapokimbilia ku ulinzi wako.

Ewe Bwana mwenye kuvika mbingu na mawingu, umekuwa duniani humo vazi la Mashahidi: Walivumilia mateso ya makafiri na wakaharibu uwongo wa miungu ya uwongo; kwa maombezi yao, utuopoe kwa adui msiyeonekana na utuokoe, ee Mungu Mwokozi.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Nani basi amekwisha sikia ya kwamba mama mmoja ameshunga ubikira na ya kama bikira amezaa? Lakini wewe, ee Mzazi-Mungu, ulitoka salama ku mambo ya watu; ndiyo maana sisi waamini tunakutukuza.

### EKSAPOSTILARION

*(Angalia mu ukurasa 11)*

### APOSTIKHA

Ninapoona matendo yangu ya mazimu, nakimbilia ku rehema yako kwa mfano wa Mtoza-kodi, kama mwana mpotevu na kahaba, na nasujudu mbele yako*:* Mbele ya kunihukumu, ee Mungu wangu, unisamehe na unihurumie kwa wema wako.

Ee Bwana, usitazame zambi zangu, wewe uliyezaliwa kwa Bikira, lakini takasa moyo wangu uifanye kuwa hekalu la Roho Mtakatifu; usinitupe mbali ya uso wako, wewe mwenye wokovu mingi.

Mulipoteswa kwa ajili ya Kristu mpaka kufa, enyi Washuhuda Washindaji wa Bwana, mukatoa mbinguni roho yenu mikononi mwa Mungu, na masalio yenu yanapelekwa duniani kote; makohani na Wafalme wanasujudu mbele hii, na mataifa yote yanapaza sauti kwa furaha*:* Ni ya samani ku macho ya Bwana; lufu ya marafiki zake.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Kama mzeituni wenyi kuchipuka na wenyi kutoa tunda mu wakati wake, Bikira alituzaa kama tunda la uzima sababu ya kuleta neema ya wokovu ku dunia.

## MU KAZI MOJA MANGARIBI KATIKA SAUTI YA PILI

*Sauti ya pili. Ote ek tu ksilu.*

Ee Kristu, peke yako usiye zambi, peke yako Mwema, peke yako chemchem ya wema, tazama mateso yangu, huzuni yangu, zima alama yotye ya vidonda vyangu, na kwa rehema yako okoa mutumishi wako, kusudi nikitenga mbali mawingu ya kutokuamini, ee Mwokozi nikutukuze wema wako mkuu.

Roho maskini, tazama matendo yako, ona na matope gani yanachafuka, ona utupu wako, utengo wako; kwani unahatarishwa kutengana na Mungu na Malaika wake Watakatifu na kutolewa ku mateso ya milele. Kesha basi na ujiharikishe kulalamika: Ee Mwokozi, nimekosa, unihurumie na uniokoe.

Mwili wangu nimeukufuru, nimechafua roho yangu na moyo wangu na kwa mawazo mabaya nimeumiza mahasa yangu yote, nimeharibu masikio yangu na macho yangu, nikisumbua ulimu wangu na maneno ya bure, na tazama mimi wote machukizwa; nasujudu tena mbele yako, ee Kristu Rabi wangu, nikisema: Nimekosa juu yako, unihurumie na uniokoe.

**Wimbo ya Mtangulizi Yoane.**

Nakuomba, ujiharikishe kuniondoa ku vishawishi, ewe Nabii mtukufu wa Bwana, kwa sababu ni bure wametokea madui zangu juu yangu na mashetani wa giza wanatumika kwa kukamata mu wavu roho ya mtumishi wako kama ndege maskini; usiniache mpaka mwisho, lakini wataweza kusikia ya kama ndiwe kimbilio langu, ewe Mtangulizi mwenyi heri.

Toka tunda kavu takatifu kamili, ewe ua nzuri la jangwa, mbayuwayu wa wakati nzuri, ndege inayoimba wimbo nzuri, njiwa wa rangi ya zahabu, fanya ili roho yangu, kwa mateso yake na kwa ukavu wake, itoe tunda la matendo mema na suke lenye kutoa matunda mara mia moja na zaidi ili niweze kukutolea sifa yangu katika Mungu, ewe Mtangulizi mwenyi heri.

Nakuomba, ee Mtangulizi, uniokoe ku moto wa milele, ku giza yasiyonuru, ku hatari yote, ku sikitiko yote, ku mateso na ouvu wote, na japo zambi zangu ambako mimi mwenyewe nilijihukumu, unifanye kuwa mrisi wa sehemu ya wateule sababu ya sala zako, ewe mwenye heri, huko kunakufurahiwa kundi ya Watakatifu, kusikilike furaha isiyokadirika.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Shida na mateso yananishambulia, na namna zote za upotevu zinaweka roho yangu maskini katika hatari, ee Bikira usiyeolewa tena Mama wa Kristu Mungu wetu, uwe sukuni wa mashua yangu pa bahari ya hii uzima; tuliza bahari yenye ukali mkuu na peleke ku bandari ya toba na ya amani huyu mwenyi kukimbilia ku ulinzi wako wa umungu.

**APOSTIKHA**

Kama mwana mupotevu, nimekosa mbele yako, ee Mwokozi*:* Ee Baba pokea toba yangu na unihurumie, ewe Mungu wangu.

Ee Kristu Mwokozi wangu, nafananisha sauti ya mtoza-kodi*:* Unirehemu na unihurumie, ewe Mungu wangu.

Mashahidi Watakatifu wanatuombea na kwa nyimbo zao wanamutukuza Kristu*:* Tangu hapo upotevu wote umemalizika, na ubinadamu umeokolewa kwa imani.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, naweka matumaini yangu yote kwako, unilinde kwa ulinzi wako.

## MU KAZI PILI ASUBUI KATIKA SAUTI YA PILI

## KATHISMA YA KWANZA

Ee roho yangu, kumbuka siku ya ajabu ya hukumu na tetemeka ukiwaza azabu itakayofwata matendo yako milele, tubu na machozi ukilalamika: Ee Mungu wangu, nimekosa juu yako, unihurumie.

Nilipotazama zamiri yangu yenye kuelemewa, ee Bwana, naogopa Korti yako ajabu, kwani huko wokovu hauko katika matendo, lakini kwa sababu kwa mapendo una hazina, unihurumie, ee Kristu Mwokozi na uniokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Mzazi-Mungu, tunakutukuza tukiimba*:* Salamu, Wingu la Nuru yasipo mwisho, Bwana wa utukufu uliyechukua tumboni mwako.

## KATHISMA YA PILI

*Sauti ya mbili*

Kama Daudi mimi pia nakulalamikia*:* Unihurumie, nimetenda zambi; katika machozi ya toba, ee Bwana, safisha zambi zangu na unihurumie.

*Shairi:* Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako.

Unihurumie, ee Mungu, unihurumie, ndivyo alivyolia Daudi juu ya zambi yake, nami nahesabia makosa yangu kuwa mengi sana, lakini sina hata moja ya machozi aliyotoa*:* Unihurumie, ee Mungu, katika wema wako kubwa.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ewe Mzazi-Mungu, usimzarau mtumishi wako mwenye kuhitaji msaada wako, kwani roho yangu inakutumainia wewe*:* Unihurumie.

## KATHISMA YA TATU

Ulishusha katika mawimbi ya Yordani chemchem ya rehema isiyokauka, ee Mtakatifu Yoane; tena nakuomba na nguvu, mimi niliye daima mwenyi kuzama katikati ya bahari ya hii uzima chini ya mawimbi mengi ya tamaa; kwa maombezi yako yenyi kumpendeza Mungu, mkono wako uniongoze ku bandari ya uzima.

Uliwaangaza Mashahidi wako kupita zahabu, na ukawatukuza Watakatifu wako katika wema wako; kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu. Mpenda-wanadamu, leta amani ku uzima wetu, pokea ombi letu kama ubani, wewe mwenye kupumzika kati ya Watakatifu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Hatujaona ao kusikia ya kama Mama amezaa Muumba wake? Ya kama bila ndoa amepata mimba na kunyonyesha huyu mwenye kuleta chakula kwa watu wote? Ni ajabu! Tumbo lako, ee Mzazi-Mungu, limekuwa kiti cha Wakeruvi: Ewe Mjalizwa neema, utuombee.

## EKSAPOSTILARION

*(Angalia mu ukurasa 14)*

## APOSTIKHA

Kwa zambi zangu nimepita mkosefu wote, kwa nani nitafunza toba? Nikilia kama Mtoza-Kodi, nawaza ya kama ni kusumbua mbingu; na nikilia kama kahaba, nachafua dunia na vilio vyangu; uniondolee basi zambi zangu, ee Mungu wangu, na unihurumie.

Ee Bwana, usitazame zambi zangu, wewe uliyezaliwa kwa Bikira, lakini takasa moyo wangu uifanye kuwa hekalu la Roho Mtakatifu; usinitupe mbali ya uso wako, wewe mwenye wokovu mingi.

Mashahidi Watakatifu walipochukua Msalaba wa Kristu kama ukumbusho wa ushindi, waliharibu nguvu ya Shetani, na walipotukuzwa mbinguni, wakawa walinzi wetu wenye kutuombea daima.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Salamu, Bikira Mzazi-Mungu, Hekalu la Mwokozi lisiloweza kuharibiwa, patakatifu ambao Nabii alisema*:* Takatifu ni Hekalu lako, la ajabu kwa wenyi haki.

## MU KAZI MBILI MANGARIBI KATIKA SAUTI YA PILI

**Wimbo ya Usulubisho.** *Ote ek tu ksilu se nekron*

Ee Mwokozi, nilipokuona umepigiliwa Msalabani, Jua likapata giza kwa woga wake, pazia la Hekalu likapasuka katika vipande viwili, udongo ukatetemeka na mawe yakapasuka hazikuweza kuvumilia kuona Muumba wao kuteswa bila haki juu ya mti, hata kama ilikuwa kwa kutaka kwake, na kutukanwa na makafiri.

Alipoangushwa, alipoharibiwa, tazama ameshindwa kabisa huyu nyoka mbaya, wakati wewe mwenyewe kwa mapendo yako kwa wanadamu, ee Bwana, ulitukuzwa Msalabani; Adamu ameopolewa ku laana, ameokoka yeye aliyehukumiwa zamani, na sisi wenyewe tunakuomba: Utuhurumie na utuokoe, na utustahilishe katika Ufalme wako mbinguni.

Umehukumiwa, wewe peke yako Mfalme utakayekuja kuhukumu ulimwengu siku ya Kuja kwako, mara ya pili; unavaa taji la miba, ee Mwokozi, wewe unayekuja kwa mapendo yako kwa wanadamu kuondoa miiba zambi ilitoa; lakini kwa uwezo wako unatia moyoni mwa mwamini wote mwenye kusujudu mbele ya Msalaba wako takatifu maarifa ya huruma yako ya milele.

**Wimbo ya Mzazi-Mungu**

Hazina na furaha ya wahitaji, na kimbilio la wenye njaa, ee Bikira ndiwe matumaini ya mayatima: Tunakutukuza tukilalamika na sikitiko: Ewe Mtakatifu kuwapita Watakatifu wote, ujiharikishe kuwaopoa watumishi wako ku jaribu lolote, ku azabu ya ajabu na ku hukumu ya milele.

Kweli, makosa yangu mengi yamenipita kichwa, ee Bikira Safi, na kwa wingi wa zambi zangu machukua uzito kubwa sana, mimi mwenyi mateso na msiyoweza kusahihishwa; lakini wewe, kwa maombezi yako ya juhudi, ujiharikishe kuniokoa kwani katika wewe wenye zambi wanapata njia yao.

Makimbilia ku ulinzi wako takaitfu kama ku bandari ya wokovu, ee Bikira Mzazi-Mungu Mtakatifu kamili na nakuomba unihurumie: Usimkatae mutumishi wako, lakini umuokoe juu hii mateso ya sasa, wewe mwenyi tabia ya kuhurumia; ee Mama wa Mungu aliye-Juu, utuombee daima na okoa watumishi waamini wako ku mateso yote.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ulipoona ametundikwa Msalabani zabibu ya kuivya uliyozaa bila kulima, ee Bikira, ukalalamika ukilia: Ee Mwanangu, mwanga kinywaji kitamu kitakachomaliza ulevi wa tamaa wakati nitakapokuomba kama Mama, ewe Mungu wa mapendo na Mtakatifu mwema.

**APOSTIKHA**

Uniokoe, ee Kristu Mwokozi, kwa uwezo ya Msalaba wako, wewe uliyemuokoa Petro pa mawimbi, na unihurumie, ee Mungu wangu.

Ee Kristru Mungu wetu, kwa muti wa Msalaba wako, ukafanya muti wa uzima kwa ajili yetu sisi wenye kukuamini wewe; katika hii uliharibu adui aliyekuwa na ufalme wa mauti, ukatupatia tena uzima sisi tuliyouawa na zambi; tena tunakulalamikia: Ewe Mfazili wa ulimwengu, Bwana utukufu kwako.

Kwa kundi, Mashahidi Watakatifu wakashindana na wazulumu, wakasema: Tunashindania Mfalme wa majeshi ya juu; mututeswe kwa mateso ya mwili na ya moto, hatutakana uwezo wa Utatu Mtakatifu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

*Ote ek tu ksilu.*

Ee Bikira Mtakatifu, walipomuweka Mwana wako na Mungu wako Msalabani uchungu gani umepeta ukilia, ukiomboleza na ukilalamika: Ole Mwanangu mpenzi, umeteswa bila haki pakutaka kuokoa ukoo wa Adamu! Ndivyo maana, ee Bikira, tunakusihi na imani: Utupe sisi mema ya Mwana wako.

## MU KAZI TATU ASUBUI KATIKA SAUTI YA PILI

### KATHISMA YA KWANZA

Umetimiza wokovu duniani, ee Kristu Mungu wetu; ulipanua mikono yako takatifu Msalabani kwa kuwakusanya mataifa yote yenye kukuimbia: Ee Bwana, utukufu kwako.

Tunakutolea, ee Bwana, talasimu ya Msalaba wenye kuleta uzima uliyotupoatia kwa wema wako japo uovu wetu; kwa maombezi ya Mzazi-Mungu, linda inchi yetu na wakristu wote, ewe peke yako mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Alipotazama, ee Kristu, lufu yako Msalabani, Bikira Mama yako akalia na uchungu akasema: Ee Mwanangu, ni fumbo gani hii ya kuogopesha? Wewe mwenye kuleta uzima wa milele kwa wote, namna gani unaweza kuteswa na haya kwa kutaka Msalanani na lufu?

### KATHISMA YA PILI

Tunasujudu mbele ya Ikona yako Takatifu, ewe Mungu wa wema, tukiomba maondoleo ya makosa yetu, ee Kristu Mungu wetu, kwani ulipenda kuteswa ulipopanda Msalabani kwa kuokoa kiumbe chako ku utumwa wa adui; na kwa shukrani tunakulalamikia*:* Umejaza ulimwengu na furaha, ewe Mwokozi wetu, ulipokuja kuleta wokovu duniani.

Kwa Msalaba wako uliangaza ulimwengu, uliwaalika waovu ku toba, ewe Mchungaji mwema, usinitenge ku zizi lako, lakini kuja unitafute, ee Rabi, mimi kondoo wako mpotevu; unihesabie katika kundi la wateule wako kwa mapendo yako kwa wanadamu na kwa wame wako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Bikira aliyekuzaa akasimama chini ya Msalaba na hakuweza kuvumilia akikuona umeteswa bila haki, akalia na akapaza sauti akasema: Ee Mwanangu, hali isiyo na mateso, namna gani umeteswa? Naimba na matukuza wema wako kubwa.

## KATHISMA YA TATU

Ninapofananisha ungamo la Munyanganyi, na kulalamikia, ee Bwana wa wema: Unikumbuke katika ufalme wako, unihesabie kama yeye katika wateule, wewe uliyeteswa kwa kutaka kwako kwa ajili yetu.

Heri ni udongo wenye kunyunyiziwa na damu yenu, enyi Washindani wa Bwana, na takatifu ni makao yenye kufunika miili yenu, kwani katika uwanja mulimushinda adui wakati mulimutangaza Kristu na uhodari*:* Kwa maombezi yenu mutupokelee ku wema wake neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ni jambo la ajabu! Ndivyo alivyolalamika Bikira Mtakatifu kamili alipomuona Mwana wake amepigiliwa Msalabani: Huyu mwenye kushika ulimwengu mkononi mwake anateswa mateso ya lufu, wanamuamua na wanamuhukumu huyu mwenye kuwasamehe wote zambi.

## APOSTIKHA

Asulubiwe! Ndivyo walivyolalamika wale uliyojaza na mema yako; na wakaomba wamfungue muovu pahali pa Mfazili wao; na wewe, ee Kristu, ulinyamaza na ulivumilia makelele ya hawa wauaji wa wenyi haki, kwani ulipenda kuteswa na kutuokoa katika mapendo yako.

Kwa kutaka kwako ulipenda kuwa na umaskini wa ubinadamu wetu, ee Kristu Mungu wetu, ulikuja duniani na ukajifanya mtu kwa Bikira na ukateswa hata kufa Msalabani kwa kutukomboa ku utumwa wa adui. Ee Bwana, utukufu kwako.

Ee Kristu, Mashahidi wengi wanakuomba: Katika wema wako kwa wanadamu utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Wakati watu wasiyo na haki walipokutundika Msalabani, ee Mwokozi mwenyi kutuletea uzima, Mama yako Mtakatifu kamili akasimama karibu nawe na akalalamika akilia: Mwanangu mupendwa, nuru ya macho yangu, namna gani unateswa ukipigiliwa Msalabani katikati ya waovu, wewe uliyetundika dunia pa maji?

# MU KAZI TATU MANGARIBI KATIKA SAUTI YA PILI

**Wimbo ya Mitume.** *Ote ek tu ksilu*

Mumeonekana kuwa wanadi wa Neno aliyeonekana duniani, enyi Mitume wa Mungu: Mulifunua wokovu kwa wote, mukawakusanya watu kwa kuwaongoza ku imani na mukavunja ngome za udanganyifu; ni kwa haki enyi Heri, mumepokea heshima na taji la washindaji.

Toka kweli juu mbinguni Malaika wengi wanawashangilia na furaha Malaika Watakatifu, walipowaona wakitangaza kweli imara umwilisho wa Bwana na wakilalamika mbele ya wote: Tazama, Mungu wetu huyu wa mbele ya nyakati, alichukua mwili kama sisi, yeye anayetawala pamoja na Baba na kutukuza pamoja na Roho Mtakatifu.

Enyi Wavuvi wa ulimwengu, mujihakirishe kuopoa roho yangu yenye kukamatwa na ndoano kwa werevu wa adui, na uniokoe ku hatari ninayo katika kutotumainia kwangu, ukinipa

nguvu ya kutoa matunda ya toba, enyi Mitume Watakatifu, ili nikiepuka gehena ya moto, niweze kustahili Ufalme wa mbingu.

**Wimbo ya Mtakatifu Nikolao.**

Ninapozungukwa na vishawishi nyingi, ninapozungushwa katika mawimbi ya hii uzima, ninapozama mu bahari ya hatari, ninapohuzunishwa na huzuni ya namna yote, nakutumainia wewe, ee Pateri Mtakatifu Nikola kwa maombi na kwa maombezi yako kwa Bwana uniopoe ku mateso yote ewe mwenye heri.

Tazama basi nafunikwa kwa mawingu ya kutokuamini na kwa giza ya fazaiko; mara moja moja kisa mbalimabli za huzuni zinanihangaisha, na woga wa hatari unanitesa: Nakuomba, uniokoe, wewe uliyepata heri kwa Mungu, nakuchagua kuwa msimamizi: Ee Baba, unijibu wakati ninapoomba msaada wako.

Ulipopokea neema kwa Mungu, ewe Mtakatifu Nikola, unawaponyesha wote wale wenye kukimbilia ku ulinzi wako; kwani unafukuza pepo wachafu wa mashetani na usimamizi wako unaponyesha magonjwa yote; na sisi pia tunakuomba, umuombe Bwana ili awaokoe ku uovu wote wale wenye kuimbia jina lako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Mama Mtakatifu, kwa ajili yetu ndiwe nguvu na boma ya uzima wetu, kimbilio la kweli la waimbaji wako wale wenye kuwatazama watumishi wako wasizarau msaada wako, kwani ndiwe msimamizi wetu kwa Mungu; ee Bibi wetu, usisahau kuwaokoa watumishi wako.

**APOSTIKHA**

Ee Mwokozi, ulitukuza ulimwengu kote jina la Mitume wakuu: Walifunza mbinguni siri isiyokaddirika, wakawa chemchem ya kuponyesha kwa ajili ya watu, paka kivuli yao iliponyesha wagonjwa; wa kwanza akafanya miujiza, yeye aliyekuwa mvuvi; wa pili, aliyechaguliwa kati ya Wayuda, akasiri na neema kanuni za Mungu; kwa maombezi yao, ewe Mungu wa mapendo, unipe neema ya wokovu.

Tunaposhambuliwa ngambo yote bila haki, tunakimbilia kwako, ewe Mungu wa ukweli, tunakutolea mlio wa Wafuasi wako tukisema: Utuokoe, ee Bwana, tunakufa na tunakuomba, onyesha kwa maadui zetu ya kama unalinda watu wako na unawaokoa hatarini, kwa maombi ya Mitume wako usamehe makosa yetu mengi katika wema wako kubwa: Ee Rabi na Bwana, utukufu kwako.

Kwa imani mulipata utukufu kubwa*:* Apana paka mulishinda adui mulipoteswa, lakini tena mulifukuza mashateni, na munaponyesha magonjwa yote, enyi waganga wa roho na wa miili; enyi Mashahidi Watakatifu, ombeni kwa Mungu ili ahurumie roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira, kwa wema wako unalinda na mukono wa uwezo waamini wote wenyi kukukimbilia mbele ya Mungu mlinzi wetu sisi wakosefu ni wewe, sisi wenyi kuhuzunika katikati ya hatari; tena ewe Mzazi-Mungu aliye-Juu, tunasujudu mbele yako: Opoa watumishi waamini wako ku mateso yote.

## MU KAZI INE ASUBUI KATIKA SAUTI YA PILI

## KATHISMA YA KWANZA

Uliwapa Wavuvi hekima mingi kuliko Wasemaji na ukawatuma duniani kote kama Watangazaji; kwa sababu ya mapendo yako isiyokadirika, ee Kristu Mungu wetu, kwa tegemeo lao uipatie Eklezya yako nguvu, tuma baraka yako kwa waamini wako, ewe peke yako Mpenda-wanadamu na Bwana mwenyi hurumu.

Walipovua mataifa katika nyavu zao, Wavuvi wakafundisha ku mipaka ya ulimwengu kusujudu mbele yako, ee Kristu Mungu wetu, kama mbele ya Baba na ya Roho Mtakatifu*:* Kwa maombezi yao sabitisha Imani yetu, uwatumie watu rehema yako, wewe peke mwenye kupumzika kati ya Watakatifu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Kwa ajili yako, ee Maria Mzazi-Mungu na Bikira daima, tuliweza kushariki ku hali ya Mungu; lakini kwa ajili yetu umemzaa Mungu aliyechukua mwili wetu; na tena, kama alivyo mwenye haki, sisi wote tunakutukuza na ibada.

## KATHISMA YA PILI

Mungu aliyejifanya maskini kwa kutaka kwake akawatuma ninyi diniani kumtajirisha na kuonyesha katika umaskini wa watangazaji ku mipaka ulimwengu hazina ya mbinguni; enyi Mitume muliyotayarisha imani yetu, tunashangilia na ibada makumbusho yenu takatifu.

Wafuasi na washuhuda wa hekima ya Mungu, Mitume Watakatifu wakatokomeza hekima ya mazimu ya wenyi hekima na ya wasemaji kwa mafundisho tu waliyotangaza; wakawapa mataifa hekima ya kumuimbia peke yake Bwana na Muumba kadiri ya imani ya kweli.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ewe Mzazi-Mungu, ndiwe msaada wa wenye kuteswa, mlinzi wa wamaskini, matumaini ya wale wenye kutotumaini, mganga wa magonjwa yasiyoweza kupona, ee Bikira mstahili kamili wa nyimbo zetu, utuombee kwa Bwana.

## KATHISMA YA TATU

Ee Mtakatifu Nikola, uliangaza ulimwengu wote na miangaza ya miujiza yako, unaondoa giza ya mateso, unafukuza ushambulio wa hatari, wewe muombezi wetu mtukufu uliye karibu ya Mungu.

Enyi Mitume, Manabii na Mashahidi, Watakatifu wakuu na Wenyi haki wote, ninyi muliyoshindana vema na kukesha kwa kulinda imani, kwa waminifu wenu kwa Mwokozi mtupokelee sisi kwa wema wake neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Wewe peke yako ulipata bila mbegu mimba ya Mungu wetu na ukakaa bikira kisha kukutana naye: Ewe Safi kamili, nasujudu mbele yako nikilalamika na woga na kwa imani: Uniokoe ku mateso yangu na ku magonjwa, ku hatari yote na ku uhitaji.

## EKSAPOSTILARION

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

## APOSTIKHA

Ee Mwokozi, ulitukuza ulimwengu kote jina la Mitume wakuu: Walifunza mbinguni siri isiyokadirika, wakawa chemchem ya kuponyesha kwa ajili ya watu, paka kivuli yao iliponyesha magonjwa; wa kwanza akafanya miujiza, yeye aliyekuwa mvuvi; wa pili,, aliyechaguliwa kati ya

Wayuda, akafasiri na neema kanuni za Mungu; kwa maombezi yao, ewe Mungu wa mapendo, utupe neema ya wokovu.

Tunaposhambuliwa ngambo yote bila haki, tunakimbilia kwako, ewe Mungu wa ukweli, tunakutolea mlio wa Wafuasi wako tukisema: Utuokoe, ee Bwana, tunakufa, na tunakuomba, onyesha kwa maadui zetu ya kama unalinda watu wako na unawaokoa hatarini, kwa maombi ya Mitume wako usamehe makosa yetu mengi katika wema wako kubwa: Ee Rabi na Bwana, utukufu kwako.

Enyi Mashahidi Washindaji masalio yenu yanaheshimiwa katika mji wote, mu inchi yote, kwani mulishindana na ukarimu na mulipokea taji mbinguni, ninyi ni utukufu wa makohani na wa Wafalme tena mapambo ya ma Eklezya takatifu ya Mungu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Furaha ya wenye kuteswa, mulinzi ambaye kuliteswa bila haki, chakula cha wenye njaa, tulizo la wageni, bakora ya vipofu na tegemeo la wazaifu, msaada na mulinzi wa wenye kuteswa, msaada wa mayatima ndiwe Mama wa Mungu aliye Juu; na wote tunasujudu mbele yako: Utuopoa ku hatari yote.

## MU KAZI INE MANGARIBI KATIKA SAUTI YA PILI

**Wimbo ya Usulubisho**. *Ote ek tu ksilu*

Ee Mwokozi, nilipokuona umepigiliwa Msalabani, Jua likapata giza kwa woga wake, pazia la Hekalu likapasuka katika vipande viwili, udongo ukatetemeka na mawe yakapasuka hazikuweza kuvumilia kuona Muumba wao kuteswa bila haki juu ya mti, hata kama ilikuwa kwa kutaka kwake, na kutukanwa na makafiri.

Alipoangushwa, alipoharibiwa, tazama ameshindwa kabisa huyu nyoka mbaya, wakati wewe mwenyewe kwa mapendo yako kwa wanadamu, ee Bwana, ulitukuzwa Msalabani; Adamu ameopolewa ku laana, ameokoka yeye aliyehukumiwa zamani, na sisi wenyewe tunakuomba: Utuhurumie na utuokoe, na utustahilishe katika Ufalme wako mbinguni.

Ee Mwokozi, wakati watu wasiyo na sheria walipokupigilia Msalabani, wewe, Uzima wa ulimwengu kiumbe chote kilitetemeka kwa woga, kwa uwezo wako wa umungu Ufalme wa Hadeze na wa mauti ukavunjwa; Adamu baba wa kwanza, kwa hii wakati anakulalamikia na furaha: Utukufu ku upendeleo wako, ee Bwana mpenda-wanadamu.

**Wimbo ya Mzazi-Mungu.**

Kwa maombezi ya watumishi wako ututazame, ewe Mtakatifu kamili, utupe chemchem ya machozi sababu ya kusafisha haya ya zambi zetu na kuzima ndimi za moto wa milele; kwani unasikiliza maombi ya wale wenye kukuomba na moyo wao wote, ewe mama wa Bwana.

Ninaposumbuliwa na zoruba ya mawazo, na mutikisiko wa hii uzima, ninapopotezwa na pepo wapotevu wa mfalme wa hii dunia, muovu, ee Bikira Mtakatifu kamili, nalalamika kwako: Ujiharikishe kuniopoa ku hatari yenye kunizunguka ili na moyo wa shukrani, ee Bikira Mjaliwa neema ya Mungu, nitangaze maajabu yako kwa kila mwamini.

Ona uzaifu ambamo napatikana, ona mateso ya roho yangu yenye kuvunjika, ewe Mtakatifu, na upotevu wa moyo wangu; ondoa fitina ya maadui wasiyoonekana wenye kunishambulia na kushindana nami; kwani ulipomzaa Mungu wetu, unaweza hivi kupata wokovu wa waamini wenye kupatikana katika hatari.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Wema gani, ee Mwanangu, rehema gani ya milele! Uvumilivu gani! Ndivyo alivyolalamika Bikira akilia; ee Neno wa milele na msiyekufa, namna paka kusujudu mbele ya mateso yako uliyoteswa kwa kutaka kwako.

**APOSTIKHA**

Uniokoe, ee Kristu Mwokozi, kwa uwezo wa Msalaba wako, wewe uliyemuokoa Petro pa mawimbi, na unihurumie, ee Mungu wangu.

Ee Kristu Mungu wetu, kwa muti wa Msalaba wako, ukafanya muti wa uzima kwa ajili yetu sisi mwenye kukuamini wewe, katika hii uliharibu adui, aliyekuwa na ufalme wa mauti, ukatupatia tena uzima sisi tuliyouawa na zambi; tena tunakulalamikia: Ewe Mfazili wa ulimwengu, Bwana, utukufu kwako.

Walipokataa furaha za hapa chini, Mashahidi. Watakatifu wakapokea hazina za mbinguni, wakawa Wenzao wa Malaika*:* Kwa maombezi yao, ee Bwana, utuhurumie na utuokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

*Ote ek tu ksilu*

Ulipoona ametundikwa Msalabani zabibu ya kuvia uliyezaa bila kulima, ee Bikira, ukalalamika ukilia: Ee Mwanangu, mwanga kinywaji kitamu kitakachomaliza ulevi wa tamaa wakatri nitakapokuomba kama Mama, ewe Mungu wa mapendo na mtakatifu Mwema.

## MU KAZI TANO ASUBUI KATIKA SAUTI YA PILI

### KATHISMA YA KWANZA

*Sauti ya mbili.*

Umetimiza wokovu duniani, ee Kristu Mungu wetu; ulipanua mikono yako takatifu Msalabani kwa kuwakusanya mataifa yote yenye kukuimbia: Ee Bwana, utukufu kwako.

Tunakutolea, ee Bwana, talasimu ya Msalaba wenye kuleta uzima uliyotupoatia kwa wema wako japo uovu wetu; kwa maombezi ya Mzazi-Mungu, linda inchi yetu na wakristu wote, ewe peke yako mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Alipomuona Kristu Mwana wake katika lufu, Mwana-Kondoo jike Bikira akilia akapaza sauti: Uovu gani wametenda waovu! Lakini wewe, Jua; ficha sasa nuru yako: Huyu a;iyeumba ulimwengu ameuawa kwa kutaka kwake na tunaweza kumuona kati ya wenyi kuhukumiwa huyu aliye peke yake Bwana wa Malaika.

### KATHISMA YA PILI

Tunasujudu mbele ya Ikona yako Takatifu, ewe Mungu wa wema, tukiomba maondoleo ya makosa yetu, ee Kristu Mungu wetu, kwani ulipenda kuteswa ulipopanda Msalabani kwa kuokoa kiumbe chako ku utumwa wa adui; na kwa shukrani tunakulalamikia*:* Umejaza ulimwengu na furaha, ewe Mwokozi wetu, ulipokuja kuleta wokovu duniani.

Kwa Msalaba wako uliangaza ulimwengu, uliwaalika waovu ku toba, ewe Mchungaji mwema, usinitenge ku zizi lako, lakini kuja unitafute, ee Rabi, mimi kondoo wako mpotevu; unihesabie katika kundi la wateule wako kwa mapendo yako kwa wanadamu na kwa wame wako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Umetukuzwa kuwapita wote, tunakuimbia, ee Mzazi-Mungu; mauti imeuawa, na Hadeze imevunjwa kwa Msalaba wa Mwana wako; ametufufua ku lufu, ametupatia uzima wa milele; paradizo imepewa mara iongine kwa sisi sababu ya kufurahiwamo kama zamani; tena kwa shukrani tunatukuza mapendo na uwezo wa Kristu Mungu wetu.

## KATHISMA YA TATU

Ninapofananisha ungamo la Munyanganyi, na kulalamikia, ee Bwana wa wema: Unikumbuke katika ufalme wako, unihesabie kama yeye katika wateule, wewe uliyeteswa kwa kutaka kwako kwa ajili yetu.

Ewe Bwana mwenye kuvika mbingu na mawingu, umekuwa duniani humo vazi la Mashahidi: Walivumilia mateso ya makafiri na wakaharibu uwongo wa miungu ya uwongo; kwa maombezi yao, utuopoe kwa adui msiyeonekana na utuokoe, ee Mungu Mwokozi.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Bikira aliyekuzaa akasimama chini ya Msalaba na hakuweza kuvumilia akikuona umeteswa bila haki, akalia na akapaza sauti akasema: Ee Mwanangu, hali isiyo na mateso, namna gani umeteswa? Naimba na matukuza wema wako kubwa.

## EKSAPOSTILARION

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu).*

## APOSTIKHA

Asulubiwe! Ndivyo walivyolalamika wale uliyojaza na mema yako; na wakaomba wamfungue muovu pahali pa Mfazili wao; na wewe, ee Kristu, ulinyamaza na ulivumilia makelele ya hawa wauaji wa wenyi haki, kwani ulipenda kuteswa na kutuokoa katika mapendo yako.

Kwa kutaka kwako ulipenda kuwa na umaskini wa ubinadamu wetu, ee Kristu Mungu wetu, ulikuja duniani na ukajifanya mtu kwa Bikira na ukateswa hata kufa Msalabani kwa kutukomboa ku utumwa wa adui. Ee Bwana, utukufu kwako.

Mulipoteswa kwa ajili ya Kristu mpaka kufa, enyi Washuhuda Washindaji wa Bwana, mukatoa mbinguni roho yenu mikononi mwa Mungu, na masalio yenu yanapelekwa duniani kote; makohani na Wafalme wanasujudu mbele hii, na mataifa yote yanapaza sauti kwa furaha: Ni ya samani ku macho ya Bwana; lufu ya marafiki zake.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

*Ote ek tu ksilu.*

Wakati Mwana-Kondoo jike alipomuona Msalbani Mwana-Kondoo amechomwa misumari, akalia, akaogopa, na akatoa machozi akasema: Hii ni lufu gani, ee Mwanangu, wewe uliyetaka kupasua deni ya Adamu na kukomboa wanadamu ku lufu! Ewe Bwana mpenda-wanadamu, natukuza tendo lako la wokovu.

# MU KAZI TANO MANGARIBI KATIKA SAUTI YA PILI

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.** *Ote ek tu ksilu.*

Ee Bwana, wakati utakapokuja na utukufu wako pamoja na Malaika wako, kuhukumu ulimwengu wote na watu wote watakaposimama bila mavazi mbele yako kwa kuwahesabia matendo yao, hapo, ee Neno, uniweke ku upande wa kondoo zako, ukinipa kule juu mbinguni maondoleo ya zambi yote niliyotenda katika hii uzima.

Kata vifungo vya mateso yangu, toboa jipu ya roho yangu, ewe peke yako mpenda-wanadamu, unipe machozi ya sikitiko, ee Kristu, na nakuomba tuma nuru ku moyo wangu wenyi giza sababu ya kuniopoa ku hatari yoyote, kuzoruba ya mateso na ya majaribu ananiteswa mfalme wa hii dunia, huyu adui wa ajabu.

Ee roho yangu, fikiri wakati wa ajabu wa hukumu huko kiumbe chote kitatetemeka wakati aliye-Juu atakapokea pa kiti cha ufalme wake, akituhukumu kadiri ya matendo yetu; ujiharikishe basi kupatana na Mwamzi wa ulimwengu, ukipaza sauti: Ee Bwana, nimekosa kwako, uniokoe.

**Wimbo ya Mzazi-Mungu.**

Walipokataa furaha za hapa chini, Mashahidi watakatifu wakapokea hazina za mbinguni, wakawa wenzao wa Malaika: Kwa maombezi yao, ee Bwana, utuhurumie na utuokoe.

Mashahidi Watakatifu wanatuombea na kwa nyimbo zao wanamutukuza Kristu: Tangu hapo upotevu wote umemalizika na ubinadamu umeokolewa kwa imani.

Kwani kundi, Mashahidi Watakatifu wakashindana na wazulumu, wakasema: tunashindania Mfalme wa majeshi ya Juu; mututeswe kwa mateso ya mwili na ya moto, hatutakana uwezo wa Utatu Mtakatifu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Kivuli cha Sheria kinafifia, kwani ilikuja neema; sawa kichaka kiliwaka moto bila kuteketezwa, hivyo ulizaa Bikira, na ulibaki Bikira; pahali pa nguzo ya moto, Jua la uhaki lilipanda pa fasi ya Musa, Kristu, wokovu wa mioyo zetu.

**APOSTIKHA**

Mashahidi Watakatifu wanatuombea na kwa nyimbo zao wanamutukuza Kristu*:* Tangu hapo upotevu wote umemalizika, na ubinadamu umeokolewa kwa imani.

Washahidi Watakatifu waliposhika Msalaba wa Kristu kama ushindi, wakavunja nguvu ya shetani, na walipotukuzwa mbinguni, wakawa walinzi wetu wenye kutuombea daima.

Kwa imani mulipata utukufu kubwa*:* Apana paka mulishinda adui mulipoteswa, lakini tena mulifukuza mashateni, na munaponyesha magonjwa yote, enyi waganga wa roho na wa miili; enyi Mashahidi Watakatifu, ombeni kwa Mungu ili ahurumie roho zetu.

**Wimbo ya wafu.**

Kama ndoto wala ua, mwanadamu wote anafifia na anazimia, lakini wakati itakapolia baragumu, itatikisisha wote watakaomka kwa kukutana nawe, ewe Kristu Mungu wetu, halafu, ee Rabi, weka wafu wetu katika hema ya wenye haki, na roho za watumihsi wako katika milele.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, matumaini yangu yote naiweka kwako, unilinde kwa ulinzi wako.

# MU POSHO ASUBUI KATIKA SAUTI YA PILI

## KATHISMA YA KWANZA

Uliangaza Mashahidi kupita zahabu, na Watakatifu wako uliwatukuza katika wema wako; kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu, mpenda-wanadamu, leta amani ku uzima yetu, pokea ombi letu kama ubani, wewe mwenye kupumzika kati, ya Watakatifu.

Heri ni udongo wenye kunyunyiziwa na damu yenu, enyi Washindani wa Bwana, na takatifu ni makao yenye kufunika miili yenu, kwani katika uwanja mulimushinda adui wakati mulimutangaza Kristu na uhodari*:* Kwa maombezi yenu mutupokelee ku wema wake neema ya wokovu wa roho zetu.

Mitume, Manabii na Mashahidi, Watakatifu wakuu na wenyi haki wote, ninyi muliyoshindana vema na kulinda imani, kwa deni munayo kwa Mwokozi mutupokelee ku wema wake neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Mafumbo yako yanapita ufahamu wote, na yote ni tukufu, ee Mzazi-Mungu: Ulikaa bila kosa Bikira na Mtakatifu, na ulikuwa kweli Mama Mzazi wakati ulizaa Mungu wa kweli. Umuombe ili aokoe roho zetu.

## KATHISMA YA PILI

Ewe Bwana mwenye kuvika mbingu na mawingu, umekuwa duniani humo vazi la Mashahidi*:* Walivumilia mateso ya makafiri na wakaharibu uwongo wa miungu ya uwongo; kwa maombezi yao, utuopoe kwa adui msiyeonekana na utuokoe, ee Mungu Mwokozi.

Ee chemchem ya uzima uliye na uwezo pa wote, wazima na wafu, kama Mungu, sikiliza ombi la watumishi wako na utuonyeshe huruma yako; leta maondoleo ya zambi ku roho zenye kukutumainia wewe, ee Mungu wa huruma na wema kubwa.

Ee Bwana, uwakumbuke watumishi wako kwa wema, uwasamehe zambi zote walizotenda mu hii uzima: Hakuna hata mmoja asiye na zambi ila wewe peke mwenye kuweza kuwapa wafu mapumziko.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Mama wa Nuru isiyokadirika, tunakuimbia kwa kukutukuza kama Malaika mbinguni.

## EKSAPOSTILARION

*(Angalia ku mwisho ya hii kitabu)*

## APOSTIKHA YA MASIFU

Mashahidi Watakatifu walipochukua Msalaba wa Kristu kama ukumbusho wa ushindi, waliharibu nguvu ya shetani, na walipotukuzwa mbinguni, wakawa walinzi wetu wenye kutuombea daima.

Ee Kristu, Mashahidi wengi wanakuomba*:* Kwa wema wako kwa ajili ya wanadamu, utuhurumie.

Enyi Mashahidi Washindaji masalio yenu yanaheshimiwa katika mji wote, mu inchi yote, kwani mulishindana na ukarimu na mulipokea taji mbinguni, ninyi ni utukufu wa makohani na wa Wafalme tena mapambo ya ma Eklezya takatifu ya Mungu.

**Nyimbo ya wafu.**

Ole, sikitiko gani inapata roho yenyi kuzimia wakati inatengana na mwili wake! Ole, machozi gani, hakuna mtu wa kuhurumia! Ikitazama ku upande wa Malaika, inaomba bure, ikigeuka ku upande wa wanadamu, haipate Msalaba. Na tena, ee Ndugu zangu wapenzi, tukiangalia ufupi wa uzima, tumuombe Kristu mapumziko ya Wafu na neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ole wangu! Nilitumia vibaya uzima wangu wote! Na tazama nakosa tendo lote njema; ninapoona lufu inajongea, naoghopa hukumu ya Mwana wako na Mungu wako: Ee Bikira Mtakatifu kamili, uniopoe, fanya ili nigeuke mbele ya hii siku, ee Bibi wetu na uniokoe.

Elezo: *Kama kuna Alliluya, tunaimba ku masifu nyimbo za mashahidi zenyi kutangulia hapa juu, na kama Apostikha tunaimba Mifanoi (Prosomia) yafwatayo:*

Sauti ya mbili. *Ote ek tu ksilu*

Ee Bwana, katika lufu yako yenyi kuleta uzima, uliharibu nguvu ya mauti na ya kuzimuni; uliwatirikizia wote uzima wa milele, uliwafufua wafu*:* ndio maana tunakuomba*:* Leta mapumziko kwa marehemu waaminifu, ee Bwana mpenda-wanadamu, na uwastahilishe ku utukufu wako wa milele.

*Shairi:* Heri wale uliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe, ee Bwana.

Kwa kuwawezesha wanadamu kuingia katika Ufalme wako takatifu, ukakubali kufa Msalabani; tena tunakuomba, kwa rehema yako, gawanya Ufalme wako na wale waliyokukuta kwa imani, na uwastahilishe ku heri na ku utukufu wa milele.

*Shairi:* Makumbusho yao ni ya milele.

Tangu milele wafu wanaongojea na woga hukumu yako ya haki mbele ya korti yako ya ajabu*:* leo, ee Bwana na Mwokozi, uwasamehe watumishi wako waliyokukuta kwa imani na uwape heri ya milele.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Njiooni wote tuimbe daima kwa nyimbo zetu tukumtukuza Mama wa Nuru: Ni yeye aliyezaa wokovu wetu, tumwambie basi: Salamu, kwani peke yako ulipata mimba ya Mungu wa m,bele ya nyakati; Salamu wewe uliyezaa Muumba aliyetengeneza sura ya Eva Msalabani; Salamu, mama Mtakatifu kamili na Bikira Msiyeolewa.

# KIPANDE CHA SAUTI YA TATU

## MU POSHO MANGARIBI

**Wimbo ya Ufufuo.** *Sauti ya tatu*

Nguvu ya mauti ilivunjwa kwa Msalaba wako Kristu Mwokozi, na udanganyifu wa Shetani uliharibiwa, basi uzao wa watu, wenye kuokolewa kwa imani, unakutolea nyimbo kila siku.

Ulimwengu uliangazwa, kwa Ufufuo wako Bwana, na Paradizo tena ilifunguliwa; na kiumbe chote mukukusifu, kinakutolea nyimbo kila siku.

Ninatukuza nguvu ya Baba, na ya Mwana, na ninaimba uwezo wa Roho Mtakatifu, umungu usiyogawanywa na usiyoumbwa, Utatu wa asili moja (omousion), unaotawala milele na milele.

**Wimbo Anatolika.**

Tunaabudu, ee Kristu, Msalaba wako muheshimiwa, tunaimba na tunatukuza, Ufufuo wako; kwa sababu ya alama ya mapigo yako, sisi wote tumepona.

Tunamwimba Mwokozi, aliyepata mwili kwa Bikira; Alisulubiwa juu ya sisi, na siku ya tatu alifufuka, kwa ajili ya kutupatia rehema yake kubwa.

Wakati alishuka kwa wale walikua kuzimu, Kristu alitangaza habari njema; akisema, muwe sabiti, sasa minashinda; mimi ni Ufufuo; nitamipandisha ninyi, pa kuvunja milango ya mauti.

Tunasimama bila kustahili, mu makao yako takatifu, tunakutolea wimbo wetu wa mangaribi, na ndani yetu tunapaza sauti; ee Kristu Mungu, uliyeangaza ulimwengu, kwa ufufuo wako siku ya tatu, opoa watu wako, ku mukono wa adui wako, ewe Mpenda-wanadamu.

Maelezo: *Utukufu kwa Baba...(Doksastikon) tunaimba toka Mineo, kama iko Mtakatifu ya hii siku. Sasa na siku zote...(Theotokion) iko hapa chini. Kama hakuna Mtakatifu mkubwa na doksastikon yake, tunaimba Utukufu.. Sasa na siku...na Theotokion ya Ufufuo. Iko hii:*

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Namna gani hatutashangaa, Muheshimiwa kamili, uzao wa Mungu na mtu? Kwa sababu bila kujua mwanaume, ee Bikira usiye na doa, ulizaa Mwana kwa namuna ya mwili pasipo baba, mwenye aliyezaliwa na Baba mbele ya milele pasipo mama, bila kupokea geuzo, ao mchanganyo, ao mgawanyo, lakini mwenye kushika tabia zake nzima za kila moja asili ya yote mbili. Kwa hii, Mama Bikira bibi malkia, umusihi kwa sababu ya wokovu, wa roho ya wale wanakusadiki kwa namuna ya kiorthodoksi, ya kama uko Mzazi-Mungu.

### APOSTIKHA

*Sauti ya tatu*

Kwa mateso yako, ee Kristu, ulileta giza ku jua, kwa nuru ya Ufufuo wako, ulifurahisha ulimwengu, pokea wimbo wetu wa mangaribi, ewe Mpenda-wanadamu.

**Wimbo ya Mtakatifu Yoane Damaskino.**

Bwana ufufuo wako wenyi kuleta uzima, uliangazia pa ulimwengu wote, na uliita tena kiumbe chako ku uharibifu. Na sisi tuliyokombolewa ku mafingo ya Adamu, tunapaza sauti; utukufu kwako, ee Bwana mwenyezi.

Mungu mwenyezi kuwako msiye haribika, kwa wakati uliteswa ku mwili uligeuka; kiumbe hakikupenda kukuona umetundikwa, kilitetemeka kwa woga, kiliimba na kililia unyenyekevu wako, lakini ulishuka kuzimu, ulifufuka siku ya tatu, ulileta ku dunia uzima na rehema yako kubwa.

Sababu ya kukomboa ukoo wetu ku mauti, ee Kristu, ulivumilia lufu; ulifufuka katika wafu siku ya tatu, pamoja nawe ulifufua, wale walikujua sawa Mungu, na uliangaza dunia, Bwana, utukufu kwako.

Maelezo: *Utukufu kwa Baba...(Doksastikon) tunaimba toka Mineo, kama iko Mtakatifu ya hii siku. Sasa na siku zote...(Theotokion) iko hapa chini. Kama hakuna Mtakatifu mkubwa na doksastikon yake, tunaimba Utukufu.. Sasa na siku...na Theotokion ya Ufufuo. Iko hii:*

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Kwa mapenzi ya baba, ulipata katika tendo la Roho Mtakatifu pasipo mbegu, mimba ya Mwana wa Mungu, aliyezaliwa kwa baba pasipo mama, mbele ya milele kuwako, juu ya sisi, alitoka kwako pasipo Baba, ulimzaa ku mwili, ulimuonyesha sawa mtoto. Kwa hii, umwombe pasipo kupumzika, akomboe roho zetu ku hatari.

**APOLITIKION**

Mbingu zifurahiwe, na inchi ishangilie, kwa sababu Bwana ametenda nguvu, kwa mukono wake; na kwa lufu alishinda mauti; na akawa muzaliwa wa kwanza katika wafu; akatuondosha katika tumbo la kuzimu, na akaleta ku dunia huruma kubwa.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote..**THEOTOKION.**

Bikira Mzazi-Mungu tunakuimbia, wewe mupatanishi wa wokovu juu ya ukoo wetu; katika mwili alipata Kwako, Mwana wako na Mungu wetu, alitaka kuteswa Msalabani, juu ya kutukomboa ku lufu, sawa Mpenda-wanadamu.

## SIKU YA MUNGU ASUBUI KATIKA SAUTI YA TATU

### KATHISMA YA KWANZA

*Sauti ya tatu*

Kristu amesimama katika wafu, malimbuko ya wale waliyolala; mzaliwa wa kwanza wa kiumbe, fundi wa ulimwengu wote, ndani yake alifanya upya hali ya ubinadamu iliyoharibika. Ewe mauti, hautawala tena: Ufalme wako umevunjwa na Bwana wa ulimwengu.

Utukufu kwa Baba

Ee Bwana, kwa mwili wako ulionja mauti, ukaondoako uchungu kwa ufufuo wako; kwa hii ulisabitisha ubinadamu, ukaondoa ushindo uliyoazibiwa na laana ya zamani. Ewe Mlinzi wa uzima wetu, Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote. **THEOTOKION**

Ee Mzazi-Mungu mbele ya neema isiyoweza kufafanishwa ya ubikira wako, mbele ya uzuri na ya nuru kimungu ya utakatifu wako, alipoogopa, Gabrieli akapaza sauti akasema: Sifa gani yenye kustahili utakaitfu wako nitaweza kukutolea? Kwa jina gani kubwa nitakutaja? Sijui na imekatazwa. Na tena, nikishika amri niliyopewa, nakuimbia: Salamu, ewe Mjaliwa neema.

### KATHISMA YA MBILI.

*Sauti ya tatu. Tin oreotita.*

Ee Bwana, mbele ya hali imara ya umungu wako, mbele ya mateso ya kutaka uliyoteswa, ilipoogopa, Hadeze ikalia juu ya bahati yake, ikalalamika: Naogopa sana mwili wako usiyoharibika; naona msiyeonekana akinigombanisha na akili; na wale ninaofunga nawasikia wakilalamika: Utukufu ku ufufuo wako takatifu, ee Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba...

Sisi waamini tunatangaza fumbo isiyokadirika wakati tunapotazama kusulubiwa kwako ambako mtu hata mmoja hawezi kusikia na ufufuo wako ambao mtu hata mmoja hawezi kueleza: Kwa hii siku mauti na Hadeze zimenyanganywa, ubinadamu umevaa umilete; na kwa ushukuru tunaweza kuimba: Utukufu ku ufufuo wako Takatifu, ee Kristu Mungu wetu.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Huyu ambaye wazo hata moja haliwezi kusikia na mkono hata moja hauwezi kuzunguka, Neno wa asili moja na Baba na Roho Mtakatifu, ee Mama Mtakatifu, aliyezaliwa kwa fumbo tumboni mwako; moja na yasiyo fujo ni uwezo wa Utatu Mtakatifu ambao Mwana wako alitufundisha kuutukuza duniani kote; na kwa ushukuru tunaweza kuimba: Salamu, ee Bikira Mjaliwa neema.

Elezo: *Sasa tunaimba Mahimidi ya Ufufuo ya Kristu (Evlogitaria).*

### UTII (IPAKOI)

Wa ajabu ku sura yake, Malaika mwenye kuangaa, kwa maneno yake akamwanga umande, akawaambia wabebaji-manukato: Kwa nini munamutafuta katika wafu huyu aliye hai? Alipotosha vyote kaburini, amefufuka! Na kwa mabadiliko yenye kufanyika kaburini mutambue huyu hawezi kugeuka na mumuambieni: Matendo yako ni ya ajabu, Bwana! Kwani uliokoa ubinadamu ku lufu.

*Kisha tunaimba Anavathmi ya sauti ya tatu.*

## ANAVATHMI

### ANTIFONON YA KWANZA

Ee Neno, ulirudisha wageni wa Sayuni toka Babyloni, uniopoe mimi pia ku tamaa zangu kwa kuniongoza ku uzima.

Wao wenye kupanda katika machozi kwa ajili ya Mungu katika upepo wa jua kati wanavuna kwa nyimbo miganda ya furaha juu ya uzima wa milele.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote.

Kwa Roho Mtakatifu kunangaa zawadi zote nzuri kama kwa Baba na kwa Mwana: katika Mungu ulimwengu wote unapata uzima na furaha.

### ANTIFONON YA PILI

Kama Bwana hajenge nyumba ya fazila, tunateswa bure, lakini kama akichunga roho yetu hata mumoja hataweza kuharibu muji wetu.

Ee Kristu, Watakatifu watakuwa siku zote kwako kama tunda la tumbo, na Wana kwa Baba, kwa pumuzi ya Roho Mtakatifu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote.

Roho Mtakatifu ambaye munakaa hekima yote na utukufu wote analeta kwa kiumbe yote uwezo wa kuishi, tumwabudu pamoja na Baba na Neno, kwani ni Mungu.

### ANTIFONON YA TATU

Huyu mwenye kuogopa Bwana na kutembea katika njia zake atakuwa mwenyi heri, atapata uzima wa milele kama chakula.

Ee muchungaji mkuu, tazama na furaha pampeni ya meza wana wako wenye kuchukua matawi ya matendo yao mema.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote.

Katika Roho Mtakatifu munakaa hazina ya utukufu wote na kwake kunatoka neema na uzima wa kiumbe yote: Anapokea pamoja na Baba na Neno heshima ya nyimbo zetu.

## PROKIMENON

Ambieni mataifa ya kama Bwana ni Mfalme; alikaza ulimwengu hautatikisika.*(mara tatu)*

*Shairi*: Mumuimbie Bwana wimbo mpya, mumuimbie Bwana duniani kote.

## KANUNI YA UFUFUO WA BWANA YESU KRISTU.

## WIMBO WA KWANZA

**IRMOS:** Zamani alikusanya maji pa mkusanyo mmoja na mkono wake wa umungu na akatenganisha maji ya bahari kwa ajili ya wana wa Israeli, yeye Mungu wetu Mtukufu kabisa: Tunamtolea yeye peke nyimbo zetu, kwani amevaa utukufu.

Utukufu kwa ufufuo wako, Takatifu, ee Bwana.

Mungu ambaye zamani alihukumu dunia kuchukua miiba kwa ajili ya muovu kama tunda la jasho yake, akapokea ku mkono wa uovu taji la miiba mwilini mwake sababu ya kuondoa laana ya kale, kwani amevaa utukufu.

Utukufu kwa ufufuo wako, Takatifu, ee Bwana.

Mshindaji, alishinda mauti, huyu mauti ilifunika; alipochukua, yeye Mungu wetu, mwili wakuweza kuteswa, hakuogopa mzulumu na akatufufua sisi wote, kwani amevaa utukufu.

Utukufu kwa ufufuo wako, Takatifu, ee Bwana.

Watu wote wanakutukuza kweli kama huyu bila mbegu alizaa Mungu wetu; kwani alishuka tumboni mwako takaitfu na akachukua hali ya wanadamu akazaliwa kwako Mungu-mutu sababu ya kutuokoa.

Utukufu kwa ufufuo wako, Takatifu, ee Bwana.

Kwa damu yake Kristu alikomboa wanadamu ku utumwa wa mzulumu; alipowafanya kuwa mungu, akawaonyesha mambo mapya, kwani amevaa utukufu.

Utukufu kwa ufufuo wako, Takatifu, ee Bwana.

Kristu, hazina ya uzima, alionja mauti kama mwenyi kufa, lakini ni kwa kutaka kwake; kama alivyo msiyekufa, akawafufua wafu, kwani amevaa utukufu.

## KANUNI YA MZAZI-MUNGU

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu utuokoe.

Ee Bikira, mwanadamu wowote anakuja gote mbele ya tunda la tumbo lako mbinguni, duniani na kuzimuni, kwani amevaa utukufu.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu utuokoe.

Mabadilisho ya ajabu tumboni mwako! Mungu mwenyi kutujaza na mema yake anatupatia Roho Mtakatifu na anapokea mwili wetu, kwani amevaa utukufu.

## WIMBO YA TATU.

**IRMOS:** Wewe uliyeumba vitu vyote katika neno lako, katika Roho yako Mtakatifu ukavipeleka ku ukamilifu wao: Ee Rabi mwenyezi, unisabitishe kwa mapendo yako.

Utukufu kwa ufufuo wako, Takatifu, ee Bwana.

Kwa Msalaba wako mwovu akanyamazishwa, akaangukia shimoni aliyo-chimba yeye mwenyewe, lakini unainua uso wa wanyenyekevu, ee Kristu, katika ufufuo wako takatifu.

Utukufu kwa ufufuo wako, Takatifu, ee Bwana.

Ee Kristu, mafundisho yako yalifunika mataifa kama wimbi la maji maangavu linavyowafunika, ee mpenda-wanadamu, mfufuliwa kaburini, ulifufua nuru ya kweli ya Utatu Mtakatifu.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu utuokoe.

Anayesema juu yako anakutukuza, ee mji wa hai wa Mfalme wa mbinguni: Ee Malkia, ni kwa sababu yako Mungu alizungumuza na wanadamu.

Utukufu kwa ufufuo wako, Takatifu, ee Bwana.

Ee Msalaba wa Kristu, usafi wako ulitukomboa ku sadaka ya miungu ya uwongo tangu Mungu wetru Mkuu, Yesu alipanua mikono yake juu ya muti wako.

Utukufu kwa ufufuo wako, Takatifu, ee Bwana.

Ee kaburi mulimoshuka uzima wetu, sisi waaminifu tunasujudu mbele yako: Ndani yako aliwekwa na alisimama Kristu aliye Mungu wetu kweli.

### KANUNI YA MZAZI-MUNGU

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu utuokoe.

Ee Kristu, tawi lililoota juu ya mzizi wa Yesu, Bikira alikuzaa kama ua, kadiri ya onyo la Nabii. Ndiwe Mtakatifu, ee Bwana Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...

Ili tuungane sisi wenyi kufa, ku umungu wako, ukapata mwili wetu kwa Bikira. Ndiwe Mtakatifu, ee Bwana Mungu wetu.

### KONTAKION

Umefufuka leo kaburini, ee Mungu wa huruma, aukituondoa ku milango ya mauti; leo Adamu anashituka kwa furaha, na Eva anacheza kwa furaha, mapatriarke na Manabii wanaiimbia, bila kuchoka nguvu na uwezo wa umungu wako.

### NYUMBA (IKOS)

Leo mbingu na dunia zinacheza kwa furaha na zinamuimbia kwa moyo mmoja Kristu Mungu wetu aliyefufua katika makaburi yao wafungwa wa mauti! Kiumbe chote kimefurahiwa, kinamtolea Muumba wa ulimwengu na Mkombozi wetu nyimbo zenyi kumstahili! Kwani leo, kama chemchem ya uzima, anawaondoa wanadamu ku Hadeze, akiwainua pamoja naye mbinguni; anavunja majivuno ya adui na kukata milango ya Hadeze kwa nguvu na uwezo wa umungu wake.

### EKSAPOSTILARION YA UFUFUO

*(Angalia ku mwisho ya hii kitabu)*

## MASIFU

Kujeni, mataifa yote, mujue nguvu ya fumbo ya ajabu; kwani Kristu Mwokozi wetu, Neno aliyekuwa katika mwanzo, alisulibiwa kwa ajili yetu, na alizikwa kwa kutaka kwake, na alifufuka katika wafu kusudi aokoe ulimwengu. Tumwabudu yeye.

Walinzi, ee Bwana, wakaeleza maajabu yako yote; lakini baraza ya ubatili, wakijaza mukono wao wa kuume kwa zawadi, waliwaza ya kama watafuchika Ufufuo wako, uliyotukuzwa na watu. Utuhurumie.

Dunia yote ilijazwa na furaha, wakati ilipopata maarifa ya ufufuo; kwani Maria Magdalena alikuja kwa Kaburi, na akakuta Malaika amekaa juu ya jiwa, kwa mavazi ya kuangaa, na akasema: sababu gani munatafuta yeye aliye hai katika wafu; Hayuko hapa, lakini alifufuka, kama alivyosema, akiwatangulia kwenda Galilaya.

Katika mwangaza yako, ee Rabi Mpenda-wanadamu, tutaona mwangaza; kwa sababu ulifufuka katika wafu, ukitoa wokovu kwa uzao wa watu, kusudi viumbe vyote vikusifu, uliye peke Msiye-zambi. Utuhurumie.

**Wimbo Anatolika.**

Wanawake wabebaji-manukato, walitoa, ee Bwana, machozi, sawa wimbo wa asubui; kwani wakichukua mikononi mwao manukato ya arufu mzuri, walishika Kaburi yako, wakishugulika kupakaa mwili wako usiyo na doa kwa manukato. Lakini Malaika aliyekaa juu ya jiwe, aliwaletea habari njema; Sababu gani munatafuta Yeye aliyehai wafu. Akishinda mauti; alifufuka, kwa kuwa yeye ni Mungu, akileta rehema kubwa kwa wote.

Malaika aliyeangaa kama umeme, juu ya Kaburi yako iliyoleta uzima, alisema kwa wanawake wabebaji-manukato: Mkombozi aliacha ma kaburi tupu, alinyanganya Hadeze, na alifufuka siku ya tatu kwa kuwa yeye ni Mungu peke na mwenyezi.

Maria Magdalena akikuja kwa kaburi siku ya kwanza ya juma, alikutafuta; lakini sawa hakukupate, akalia, akipaza sauti kwa maombolezo: Ole! Mwokozi wangu, Mfalme wa wote, namna gani uliibwa? Lakini Malaika wawili waletaji-uzima, ndani ya kaburi wakapaza sauti: Kwa nini unalia, ee mwanamuke? Akawaambia: Ninalia, kwani wamemwondoa Bwana wangu toka kaburi, na sijui pahali walipomuweka. Basi alipogeuka nyuma, na wakati alipokuona, akaita mara moja: Bwana wangu, na Mungu wangu, utukufu kwako.

Waebrania walifunga sana uzima ndani ya kaburi; lakini munyanganyi alifungua Paradizo kwa sauti, akapaza na akasema: Huyu aliyesulubiwa pamoja nami kwa ajili yangu, alitundikwa pamoja na Baba; kwa sababu huyu ni Kristu Mungu wetu, mwenye kuwa na rehema kubwa.

Utukufu kwa Baba...

*Elezo: Tafuta Eothinon (Mwimbo wa asubui) ku mwisho ya hii Kitabu.*

*Kisha Eothinon tunaimba hii:*

Sasa na siku zote, hata milele na milele. Amina.

Mbarikiwa Ukupita, ewe Mzazi-Mungu Bikira; kwa kuwa naye aliye amepata mwili nawe, kuzimu imetekwa, Adamu amerejezwa, laana imekufa, Eva amekombolewa, Mauti imewekwa kifoni, tena sisi tumeofikia uzima; kwa hiyo tukiimba na kupaza sauti umehimidiwa U Kristu Mungu wetu, liyependezwa hivi. Utukufu kwako.

**DOKSOLOGIA UKUBWA**

Leo wokovu ulifanyika duniani, tumwimbie mwenye kufufuka toka kaburi na mukubwa wa uzima wetu. Kwa sababu kwa lufu alibomoa mauti na alitupatia ushindi na rehema kubwa.

## SIKU YA MUNGU MANGARIBI KATIKA SAUTI YA TATU

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.**

Nimekosa, ee Bwana Mungu wangu, nimekosa. Ee Neno, unihurumie, usinikatae na machukio yako kwa ajili yangu; lakini kwa rehema na huruma yako moja tu, unipokee mimi ninayerudi kwako katika toba, na unipe nguvu ya kutimiza, ee Mungu wa mapendo, mafundisho yako ya wokovu.

Ujiharishe, ee Bwana, kuniopoa ku mkono wa adui; kwani nimefungwa kwa kosa na nimejitenga mbali na mafundisho yako, ewe Mwokozi, unipe bahati ya kutubu na uniongoze ku nuru ya juto la zambi ili nilie kwa kukumbuka maovu yangu.

Uniopoe, ee Bwana Mungu wangu, ku ugumu wa moyo wangu; unipe machozi mengi sababu ya kusafisha haya ya zambi zangu; uniangaze mu giza yangu, unipe nuru ya maarifa yako, ee Mwokozi, ili nitembee katika usafi wa amri zako kimungu.

**Wimbo ya wa Malaika.**

**E**e Bwana, uliweka makundi ya Malaika wabila-mwili sababu ya kuonyesha kwa wote hazina ya wema wako; uliwaumba kwa kuwasharikisha ku utukufu wako na ku nuru yako, na ili wakutukuze daima kwa sauti yao.

Kubwa ni uwezo, wa Malaika wako, ee Kristu: Wanazunguka duniani kwa namna ya Wabila -mwili, wakilinda Maeklezya ya Mungu na nguvu waliyopewa nawe, ee Bwana, wanaiomba ulimwengu kwako.

Nguvu, wenye uwezo, Watawala, Malaika na Malaika Wakuu, Wakuu, Viti vya ezi, Wakeruvi na Waserafi, munapovaa nuru isiyokadirika na munaposhariki ku hekima kamili ya Mungu, muiombee ulimwengu kwake.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION.**

Tulipopokea mema makubwa kwa ajili yako, ee Bikira Safi, tunamtukuza pamoja na Malaika Mwana wako aliyekubali kuzaliwa tumboni mwako kwa wingi wa wema wake, na aliyetengeneza mara ingine ubinadamu.

### APOSTIKHA

Tunakutolea shairi yetu ya mangaribi na ubani na nyimbo za kiroho: Ee Kristu Mwokozi, hurumia roho zetu.

Ee Bwana, uwezo wa Msalaba wako ni kubwa, uliposimikwa kule Kalvario, unatawala dunia yote, uligeuza wavuvi kuwa Mitume na Wapagani kuwa wingu la Washuhuda wanaomba kwa ajili ya wokovu roho zetu.

Ee Bwana, uwezo wa Msalaba wako ni kubwa, uliposimikwa kule Kalvario, unatawala dunia yote, uligeuza wavuvi kuwa Mitume na wapagani kuwa wingi la washuhuda wanaomba kwa ajili ya wokovu roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Malkia wa utakatifu, utukufu wa majeshi ya mbinguni, wimbo wa Mitume, utimizo wa maandiko ya Manabii, ee Bibi wetu, pokea maombi yetu na nyimbo zetu.

## MU KAZI MOJA ASUBUI KATIKA SAUTI YA TATU

### KATHISMA YA KWANZA

*Sauti ya tatu*

Ee roho yangu, wewe ni mgeni duniani, tubu, kwani uvumbi hauimbake kaburini, na juu ya zambi hakuna ukombozi; tangu sasa lalamikia Kristu Mungu wetu*:* Nimekosa, ee Bwana mwenyi kuvumbua yenyi kuwa moyoni, usinihukumu, lakini unihurumie.

Ee roho yangu, mpaka wakati gani utakaa katika zambi? Mpaka wakati gani utazarau toba? Ona hali ya hukumu na lalamikia Bwana*:* Nimekosa, lakini uniokoe, ee Mungu wangu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Salamu, Maria Mama Mzazi-Mungu na Bikira, mulima takatifu, Paradizo ya Edeni, uliyemzaa Kristu Mungu wetu, yeye peke asiye na baba hapa chini, na katika yeye uzima wa kweli umestawi duniani humu.

### KATHISMA YA PILI

Mbele ya haki ya Korti yako ya ajabu hakuna lazima ya wenyi kushitaki wala ya washuhuda. Vitabu vitafunguliwa na siri zitaonekana; lakini mbele ya wewe kutafuta matendo ya uzima wangu duniani, ee Mungu, unihurumie na uniokoe, ee Bwana.

Ee Bwana, tazama Korti ya ajabu yenyi kuniongojea; nikinyamaza ni matendo yangu yatalalamika; lakini kuja wepesi kutafuta kondoo yako aliyepotea, ee Kristu Mungu wangu, na kwa toba uniongoze ku wokovu wako.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Kwa ajili ya Neno umekuwa hema kimungu, ee Bikira Mzazi-Mungu Mtakatifu kamili mwenyi kuwapita Malaika ku utakatifu; nafunikwa na matope kuwapita wote, nachafuka na tamaa za mwili; unisafishe na mawimbi kimungu, wewe mwqenyi kutupatia kwa maombezi yako neema ya wokovu.

### KATHISMA YA TATU

*Tin oreotita*

Ee Mungu mwenyezi, kwa neno lako uliumba viumbe vya mbinguni na vya hapa chini; wanapotetemeka na woga mbele yako makundi ya Malaika wanakusifu, ee Bwana, wakiangaza na nuru yako mipika ya ulimwengu; na katika wao sisi pia tunakulalamikia: Utuokoe katika mapendo ya moyo wako.

Ushujaa wenu na imara yenu zilishinda uerevu wa adui; ee Mashahidi Washindaji, wenyi kustahili heshima yote, mumestahili heri ya milele; ninyi washuhuda wa Mungu kweli; ombeni kwa Bwana ili aokoe kondoo zake wenyi kumpenda Kristu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Majeshi ya mbinguni yalifurahiwa na mapendo, wanadamu waliogopa wakati salamu ya Malaika ilitolewa kwako, ewe Mzazi-Mungu; duniani kama mbinguni ni Siku Kuu ileile inatoa nuru yake kwa sababu baba wa kwanza amekombolewa ku lufu; pamoja na Malaika, sisi pia tunakulalamikia: Salamu, ewe Mama Mzazi-Mungu Mtakatifu kamili tena Bikira Safi.

**EKSAPOSTILARION YA SIKU**

*(Angalia ku mwisho ya hii kitabu).*

**APOSTIKHA**

Ee Bwana, kusanya akili yangu yenye kutawanyika, takasa miiba ya moyo wangu, kama kwa Petro unipe toba, na kama kwa mtoza-kodi unipe pumuzi, kama kahaba unipe machozi ili nikupazie sauti*:* Uniokoe, ee Mungu wangu, mpenda-wanadamu, peke yako mwenyi huruma.

Mara nyingi, wakati niliimba kwa ajili yako, nilipatikana mu hali ya zambi, na wakati kinywa yangu ilikutukuza, roho yangu ilijivuna; kwa ttoba uniadibishe mimi wote, ee Kristu Mungu wetu, unihurumie na uniokoe.

Njooni mataifa yote, tutukuze makumbusho ya Mashahidi wa Bwana, kwani walipokea kwa Kristu mbele ya Malaika na ya Wanadamu taji la washindi na wanamuomba kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Ee Bikira Mtakatifu mwenye kuwapita Malaika wote mbinguni, inua ombi wanadamu duniani wanamutole Rabi wa ulimwengu ili aokoe waamini wenye kukutambua kweli kama Mzazi-Mungu.

## MU KAZI MOJA MANGARIBI KATIKA SAUTI YA TATU

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.**

Ee Bwana, tamaa za roho yangu na mwili wangu zinanishambulia sababu ya kuniangamiza mara mbili; zinanisukumia ku shimo ya kutotumainia, lakini kama zamani tuliza mawimbi ya bahari, ee Bwana, na unipe tulizo.

Ninapohukumiwa kwa wingi wa zambi zangu, sina nguvu ya kutazama juu ya mbinguni, lakini kama Mtoza-Kodi nalalamika: Ona mateso yangu na unihurumie, ee Mwokozi.

Ee Bwana, kubwa na ya ajabu ni kuja kwako wakati utakapokaa kwa kutoa hukumu ya haki. Usinihukumu, nimetangulia kuhukumiwa, unifazilie, halafu uniopoe ku mateso yote.

**Wimbo ya Mtangulizi Yoane.**

Umeinuka ulimwenguni kama allfajiri ukiangaza mioyo ya wale wenyi kukuimbia, ee Mtakatifu Yoane; angaza roho zetu na akili zetu ili tuweze kukutukuza, ewe Nabii Mtukufu na Mbatizaji wa Mwokozi.

Tunakuomba, uiombee daima ulimwengu wote, ewe Mtangulizi mwenye heri ili tupate neema kimungu ya juu mbinguni na tufunyange kichwa ya muovu kwa ajili ya hazina ya maombezi yako sabiti.

Wakati atakapokuja Bwana kunitenga ku hii hekalu ya mwili, nitaweza kuwa nawe kama msaada, kama boma na mulinzi, ewe Yoane, Nabii na Mtangulizi, ukiniongoza ku nuru isiyopunguka.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Unapoombea daima Kondoo za zizi lako, kwa maombezi yako utuopoe ku mateso yote yenyi kututisha na okoa, ewe Mzazi-Mungu, watumishi wako ku hasira ya Bwana.

### APOSTIKHA

Tunakutolea shairi yetu ya mangaribi na ubani na nyimbo za kiroho*:* Ee Kristu Mwokozi, hurumia roho zetu.

Uniokoe, ee Bwana Mungu wangu*:* Ndiwe wokovu wa Wanadamu; mawimbi ya mateso yananitikisa na nazama kwa uzito wa zambi zangu; unisaidie na mkono wako na uniongoze ku nuru ya toba, ewe Bwana mpenda-wanadamu, peke yako mwenyi huruma.

Nguvu ya mashahidi ni kubwa sana*:* Wanapolala kaburini, wanafukuza pepo za uovu; walishinda nguvu ya adui waliposhindania imani katika Utatu Mtakatifu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Ewe Mzazi-Mungu, mulinzi wa wote wale wenyi kukuomba, unatupatia nguvu na uhodari, tunakutumainia wewe: Umuombee Mwana wako kwa ajili ya watumishi wako wasiyo na mafaa.

## MU KAZI PILI ASUBUI KATIKA SAUTI YA TATU

### KATHISMA YA KWANZA

Ee roho yangu, wewe ni mgeni duniani, tubu, kwani uvumbi hauimbake kaburini, na juu ya zambi hakuna ukombozi; tangu sasa lalamikia Kristu Mungu wetu*:* Nimekosa, ee Bwana mwenyi kuvumbua yenyi kuwa moyoni, usinihukumu, lakini unihurumie.

Ee roho yangu, mpaka wakati gani utakaa katika zambi? Mpaka wakati gani utazarau toba? Ona hali ya hukumu na lalamikia Bwana*:* Nimekosa, lakini uniokoe, ee Mungu wangu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Ee Mzazi-Mungu, nguvu yetu na boma yetu, mpatanishi wa nguvu wa ulimwengu, ewe Bikira mbarikiwa katika wote, kwa maombezi yako okoa watumishi wako ku hatari yote.

### KATHISMA YA PILI

Ee Bwana, unajua shimo ya zambi zangu: Kama kwa Petro unipe mukono na uniokoe.

Wakati mwamzi wa ulimwengu atakapotoa hukumu ya haki, ee roho yangu, utasema nini? Umulalamikie basi mbele ya mwisho: Nimekosa, ee Mungu wangu, lakini unihurumie.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Mwenyi heri Mama Mzazi-Mungu usiyeolewa, ponyesha roho yangu yenye kuregea, kwani nangushwa kwa uzito wa zambi zangu na nakuita, ewe Mzazi-Mungu, katika vilio vya moyo wangu. Unipokee, ee Bikira Takatifu, japo makosa yangu mengi, ili nikijaa na matumaini nikulalamikie: Salamu, makao takatifu ya Bwana Mungu wetu.

**KATHISMA YA TATU**

Tunakimbilia ku kivuli ya mabawa yako, sisi waamini, na kwa roho yetu tunapaza sauti: ee Nabii mwenyi heri na Mtanguliza, tuliza mawimbi ya hatari, ya vishawishi, ya magonjwa; songa fitika ya adui na utuombee neema ya wokovu.

Ee Bwana mwenyezi, uliangaza makumbusho ya Mashahidi wako, uliwapa nguvu ya kufafanisha mateso yako; walishinda bora nguvu ya shetani na wakapokea kipaji cha kuponyesha magonjwa*:* Kwa maombezi yao, ee Bwana mpenda-wanadamu, utupe amani na neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Mtu wote anakimbilia kule anakopata wokovu. katika wewe peke tunapata makimbilio, ewe Mzazi-Mungu, mulinzi wa roho zetu.

**EKSAPOSTILARION**

*(Angalia ku mwisho ya hii kitabu)*

**APOSTIKHA**

Ee Bwana, kusanya akili yangu yenye kutawanyika, takasa miiba ya moyo wangu, kama kwa Petro unipe toba, na kama kwa mtoza-kodi unipe pumuzi, kama kahaba unipe machozi ili nikupazie sauti*:* Uniokoe, ee Mungu wangu, mpenda-wanadamu, peke yako mwenyi huruma.

Mara nyingi, wakati niliimba kwa ajili yako, nilipatikana mu hali ya zambi, na wakati kinywa yangu ilikutukuza, roho yangu ilijivuna; kwa toba uniadibishe mimi wote, ee Kristu Mungu wetu, unihurumie na uniokoe.

Maaskari wa Kristu walivunja woga wote mbele ya wafalme na wazulumu; na uhodari kubwa walimuungama Bwana wa ulimwengu, Mungu na Mfalme wetu, na sasa wanaombea roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Bila mbegu ulipata mimba kwa tendo la Roho Mtakatifu na tunakutukuza tukiimba: Salamu, ewe Bikira Mtakatifu kamili.

## MU KAZI PILI MANGARIBI KATIKA SAUTI YA TATU

**Wimbo ya Usulubisho.**

Kwa kusulubiwa kwako, ee Neno, kiumbe kiligeuzwa, kwa woga Jua halikutoa miangaza yake pazia ya hekalu ikapasuka katika vipande mbili, na kila mtu mwaminifu akaokolewa; tena tunatukuza hazina ya mapendo yako.

Alipochukua mwili wetu kwa kupenda kwake, Bwana Mungu akapigiliwa Msalabani; akainua hali yetu yenye kuanguka wakati alipotukuza mwili wake kadiri ya kutala kwake na mapendo yake ya huruma.

Ee Bwana, maji na damu ya ubavu wako yalibadirisha dunia, na maji unasafisha zambi zetu, na damu yako unasahihisha maondoleo, ewe Yesu Kristu, kwa mapendo yako ya huruma.

**Wimbo ya Mzazi-Mungu.**

Nilipolala katika ukosefu wa shuruli, nilipitisha wakati wa maisha yangu mu uvivu; naogopa sana saa ya kuondoka, lakini kwa maombezi yako uniamushe ku toba, ewe Bikira Safi kamili na uniokoe.

Ponyesha mateso ya moyo wangu, selehisha kosa ya roho yangu, uniruhusu nikuimbie na moyo safi ili nipate huruma, ee Bikira Mtakatifu, siku tutakapohukumiwa.

Ee roho maskini, tia mzigo nyuma, tua ubaya wenyi uzito kubwa; jongea na kulia ukilalamika: Ewe Bikira Takatifu, unistahilishe nichukue nira nzuri ya Mwana wako na Mungu wako.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote... **STAVROTHEOTOKION**.

Upanga ulichoma moyo wako, ewe Mtakatifu kamili wakati ulipomuona Mwana wako Msalabani na ukalalamika: usiniache bila mtoto, ee Mwanangu na Mungu wangu, wewe uliyeniacha bikira hata kisha kuzaa.

**APOSTIKHA**

Ee Kristu, nasujudu mbele ya Msalaba wako wa samani, ulinzi wa dunia na wokovu wa wakosefu, msaada kubwa, ushindi wa ufalme, kisa ya utukufu na ya usharifu.

Mti uliyokatazua ukazaa lufu duniani, mti wa Msalaba ukachanusha uzima wa milele, na tena tunakuabudu, ewe Bwana mfufuliwa; nuru ya uso ituangazie, ewe Mwokozi!

Manabii, Mitume wa Kristu na Mashahidi walitufundisha kuimbia Utatu wa asili moja; wakaleta nuru ku mataifa yenye kupotea*:* Malaika na wanadamu wamekuwa marafiki.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote... **STAVROTHEOTOKION**.

Wakati Kondoo jike aliyekuzaa alikuona umepigiliwa Msalabani, ee Yesu, akilia na kuomboleza, Mama yako Mtakatifu akalalamika: Usimuache bila mtoto huyu unayechunga kuwa Bikira hata kisha kuzaa.

## MU KAZI TATU ASUBUI KATIKA SAUTI YA TATU.

**KATHISMA YA KWANZA**

Msalaba ulisimikwa duniani, ukainuka mpaka mbinguni, apana kwa urefu wa muti wake, lakini kwa sababu katika hii ulitimiza vitu vyote. Ee Bwana, utukufu kwako.

Umetukuzwa pa msonobari, pa mti wa kasuku wa Libano, ewe Mwana-Kondoo wa Mungu, sababu ya kuokoa wale wenyi kuabudu na imani kusulubiwa kwako kwa kutaka*:* Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Tuna Msalaba wa Mwana wako kama fimbo ya nguvu, ee Mzazi-Mungu; katika hii tunashusha majivuno ya adui, sisi wenye kukutukuza daima na moyo wote.

## KATHISMA YA PILI

Ee Kristu, ulipokea bila hasira makofi, sababu ya kuokoa wanadamu; opoa uzima wetu kaburini; ee Bwana, utupe wokovu wako.

*Tin oreotita.*

Walipotazama uwezo wako wa milele na kusulubiwa kwako kwa kutaka, Malaika wakashangaa pa kuona namna gani msiyeonekana ameteswa mwilini, kwani alipenda kuwakomboa wanadamu ku mauti. Na tena tunakuimbia kama chemchem ya uzima, ee Kristru, na tunakutukuza katika ufalme wako mkuu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Kristu, alipoona mwili wako umetundika Msalabani, Mama yako Mtakatifu msiyeolewa akalia machozi akalalamika: Hii ndiyo tuzo la watu wasiyo na shukrani waliyopata mema mengi! Ewe Mwanangu, naimba tena nasifu ypendeleo wako kimungu.

## KATHISMA YA TATU

Ee Bwana, ulivumilia matusi, wewe rabi wa viumbe vyote, sababu ya kunirudishia heshima iliyopotea zamani, na ubavu wako ulichomwa mkuki sababu ya kuopoa shimoni kazi ya mikono yako: Ee mpenda-wanadamu, naimba hazina ya mapendo yako na ya wema wako.

Mulipovikwa silaha za Kristu, mulipovaa silaha za imani, mukapambana na majeshi ya adui na mukawaangusha sabiti; mulisaidiwa na matumaini ya uzima, mukapambana na mateso na makamio ya wazulumu na mukapokea taji, enyi Washuhuda wahodari wa Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Alipokuona umepigiliwa Msalabani, ewe Bwana, mama yako msiyeolewa, Bikira Safi kamili akalalamika: Ole, ewe Mwana mupole kabisa, namna gani watu wasiyo sheria waliweza kukuhukumu Msalabani? Ewe Rabi na Muumba wa vitu vyote, naimba wema wako kubwa.

## EKSAPOSTILARION

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

## APOSTIKHA

Kwa wivu nilifukuzwa Patadizoni, na kwa uzito wa zambi nikaanguka; lakini haukunizarau, ee Bwana, na kwa ajili yangu ukafanana nami; ukajachilia kusulubiwa na ukawa wokovu wangu. Uniongoze ku utukufu wako, ewe Mungu mwenye kuniokoa, utukufu kwako.

Alipoinua mikono mu alama ya Msalaba Musa akamshinda Amaleki mulimani; lakini wewe Mwokozi ulipopanua mikono juu ya Msalaba mheshimiwa ukanikamata mikononi mwako; ukaniokoa ku utumwa wa adui na ukanipa alama ya uzima. Ee Msalaba Mheshimiwa wa Kristu, nasujudu mbele yako.

Kama mwanga, munaangaza ulimwengu hata kufa kwenu, enyi mashahidi Watakatifu; muliposhindana vema, muna uwezo wa kumuomba Kristu ili alete neema ya wokovu ku roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Alipokuona umetundikwa juu ya mti, ewe Kristu wa wema, Nikira Mtakatifu kamili kwa uchungu ya umama akakulalamikia: Ee Mwanangu mpendwa, namna gani watu wasiyo haki wanakuhukumi usulubiwe Msalabani?

## MU KAZI TATU MANGARIBI KATIKA SAUTI YA TATU

**Wimbo ya Mitume.**

Kwa maombezi ya Mitume wako Watakatifu, ewe mpenda-wanadamu peke yako mwenyi huruma, uwape watu wako amani na uwaopoe ku hatari yote waaminifu wenyi kukuimbia na wenyi kusujudu mbele yako.

Enyi washuhuda wa Mungu muliyeona kwa macho, muniopoe ku mishale ya muovu; mwangeni umande wa baridi wa Roho Mtakatifu pa roho yangu yenyi kuungua na mchomo wa zambi, enyi Mitume watakatifu wenyi kumijaza na mema yenu.

Enyi Mitume wa Bwana, sauti yenu takatifu ilisikilika kweili duniani kote sababu ya kutolea kwa Mungu kama ubani wale waliyomuungama.

**Wimbo ya Mtakatifu Nikola.**

Kwa sisi, ewe Nikola mara tatu mwenyi heri, umeonekana kuwa msaada kubwa kabisa, kwani unawaopoa watumishi wako ku hatari yote na ku uhitaji wote, ku majaribu, ku magonjwa, kwa maadui wasiyoonekana.

Ku wakati wa ajabu huko nitaweza kuhuzuria mbele ya Korti yako ya ajabu, msaada wako uniopoe ku azabu na ku giza za inje, ee Mtakatifu Nikola, sababu ya uaminifu uliyo nayo kwa Mungu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Malkia wa viumbe vyote, ona roho yangu yenyi kutawaliwa na tamaa. Ee Bibi Mtakatifu, uisamehe kwa sababu ya dawa ya wepesi ya maombezi yako na uifanye kuwa mtumwa wa mwana wako na Mungu wetu.

**APOSTIKHA**

**Wimbo wa Mitume.**

Sauti yenu ilisikika duniani kote, enyi Mitume Watakatifu, mulivunja miungu ya uwongo na kukatangaza maarifa ya Mungu wa kweli, mukashindana hivi vema, enyi wenyi heri tunaoimbia na kutukuza makumbusho.

Ee Mitume Watakatifu, mulichunga bila kosa mafundisho ya Kristu; muliipokea bila kulipa na mukaipokesha na mapendo, mukiponyesha mateso ya roho zetu na ya miili yetu, na kwa deni munayo kwa Mungu mutuombee ili roho zetu ziokolewe.

Ee Bwana, mashahidi wako walipotegemezwa kwa imani na kusabitishwa kwa matumaini, walipoungana katika roho na mapendo ya Msalaba, wakavunja uzulumu wa adui; walipopokea taji la milele, wanaomba pamoja na Malaika wabila-mwili kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Uzuri wa Malaika watakatifu, utukufu wa Mitume ambao Manabii walitia muhuri wao, mulinzi wa waamini na njia ya wokovu, ee Bikira tunataka kusujudu mbele yako.

## MU KAZI INE ASUBUI KATIKA SAUTI YA TATU

### KATHISMA YA KWANZA

*Tin oreotita.*

Ee Bwana mwenyezi, uliangaza makumbusho ya Mitume wako, uliwapa nguvu ya kufafanisha mateso yako; walishinda bora nguvu ya shetani na wakapokea kipaji cha kuponyesha magonjwa*:* Kwa maombezi yao, ee Bwana mpenda-wanadamu, utupe amani na neema ya wokovu wa roho zetu.

Mitume walinyunyiza dunia yote na mawimbi ya neno-Mungu, walistawisha suke la imani yetu na dunia ikajaa mpaka mwisho wa mipaka yake, kwani ndago imetangua; waliangaza wanadamu wote kwa kuwatolea kwa Kristu Mungu wetu, wakiwabatiza kwa jina la Utatu usiyogawanywa.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

*Tin oreotita.*

Nilipofikiri juu ya hazina ya milele ya huruma yako na juu ya nguvu isiyoweza kushindwa ya uwezo wako, nikakimbilia ku ulinzi wako, na katika sikitiko yenyi kunisonga, katika mashaka ya mawazo yangu ya sikitiko, nakulalamikia toka chini ya moyo wangu. Kuja unisaidie, ee Bikira Mzazi-Mungu, na okoa mtumishi wako msiyestahili.

### KATHISMA YA KWANZA

*Thias pisteos.*

Njooni wote tuwaimbie Mitume watakatifu kama waongozi wetu katika imani. Wakipofukuza uwongo wa miungu ya uwongo, wakatuongoza ku nuru na ku uzima, na wakatufundisha kutukuza Utatu Mtakatifu; tunapoheshimu makumbusho yao takatifu, tunamtukuza na ibada Mwokozi.

Mitume wakuu waliyomuona Mungu, wenye kuangazwana imani ya kweli wakazima kosa lote; wakatajirisha dunia na hazina zao na wanapamba Maeklezya na sifa kuu, wakimuomba Kristu awape waaminifu amani na alete neema ya wokovu ku roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ninapoangamizwa katika shimo ya mateso, naomba bahari ya mapendo yako. Kuja unisaidie, ee Bikira Mtakatifu kamili, nyosha mkono kwa mwaminifu wako, ee Mzazi-Mungu, uniokoe kama Mwana wako alivyomuokoa zamani Petro pa mawimbi; unihurumie mimi mwenyi kuzama katika zoruba ya uhalifu wangu.

### KATHISMA YA TATU

Tunapotukuza mahubiri yako  ya kweli na nuru ya kwangu unayoeneza duniani, ee Mtakatifu Nikola, tunakuimbia na kwa imani tunakulalamikia. Kama ulivyookoa ku lufu wasiyo na zambi, utuokoe nasi pia ku hatari, ku sikitiko na ku mateso yote yenyi kutushambulia.

Kwa imani munaangaa kama nyota za mwanga, enyi Mashahidi watakatifu ambao tunatukuza mashindano; bila woga mbele ya uzulumu wa wazulumu, mukamaliza kafuru ya miungu ya uwongo paka na silaha ya ukweli na ushindi wa Msalaba usiyoweza kushindwa.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ndiwe kiti cha zahabu cha Mfalme wetu, ee Bikira Safi kamili Paradizo yenyi kujaa na maua; kwa neema yako unatumimiya manukato mazuri, kwa sababu ni Mungu yeye mwenyewe

ulichukua tumboni mwako; tunatangaza ukweli wa umama wako takaitfu na tunakutukuza daima.

**EKSAPOSTILARION YA SIKU**

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu).*

**APOSTIKHA**

Sauti yenu ilisikilika duniani kote, enyi Mitume Watakatifu, mulivunja miungu ya uwongo na mukatangaza maarifa ya Mungu wa kweli, mukashindana hivi vema, enyi wenyi heri tunaoimbia na kutukuza makumbusho.

Ee Mitume Watakatifu, mulichunga bila kosa mafundisho ya Kristu; muliipokea bure na mukaipokesha na mapendo, mukiponyesha mateso ya roho zetu na ya miili yetu, na kwa deni munayo kwa Mungu mutuombee ili roho zetu ziokolewe.

Majeshi ya mbinguni ya Malaika Watakatifu walishangaa ushujaa wa mashahidi. katika mwili wao walizarau mateso sababu ya kufananisha mateso ya Kristu Mwokozi, na sasa wanaoimbia roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Malkia wa utakatifu, utukufu wa majeshi ya mbinguni, wimbo wa Mitume, utimizo wa maandiko ya Manabii, ee Bibi wetu, pokea maombi yetu na nyimbo zetu.

## MU KAZI INE MANGARIBI KATIKA SAUTI YA TATU

**Wimbo ya Usulubisho.** *Megali tu Stavru su Kirie...*

Kwa damu yako ya samani na kwa maji ya ubavu wako, ee Bwana mvumilivu, kiumbe kilitakaswa, sifa za miungu wa uwongo zimekaushwa Adamu ameokolewa ku kuanguka na ku mauti, ee Neno, katika kusulubiwa kwako takatifu Msalabani.

Ee mpeda-wanadamu mwenye kupita heshima yote, ulikunywa siki ulitukanwa kwa ajili yetu na uliteswa Msalabani kwa kutaka kwako sababu ya kuokoa wanadamu kuzimuni, ewe Mwema, kwa lufu yako mwenyewe.

Ulipenda kutundikwa Msalabani, ukatolewa mu sadaka kwa Baba yako kwa ajili yetu; hivi ukamaliza sadaka za miungu ya uwongo na ukaharibu ufalme wa mwovu, ee Mfalme wa milele, mtajiri wa wema.

**Wimbo ya Mzazi-Mungu.**

Wingu la nuru ya milele, ee Bikira Maria mjaliwa neema na mtukufu, uniangaze na nuru ya kuongoka kwaki tazama napatikana katika giza ya zambi; kwa maombezi yako uniopoe ku moto ya gehena, ku giza yasiyo na nuru; na fanya ili nishariki ku siku yasipo mangaribi ya Mwana wako, mimi mwenye kukimbilia sasa, ee Bikira Takatifu, ku ulinzi wako takatifu.

Wewe uliyezaa Mumbaji wa wokovu, ee mwenyi heri Bikira Maria umuombe daima ahurumie roho yangu maskini adui aliangushia kuzimuni ya upotevu; usizarau sasa ombi langu na katika wema wako usiyokadirika na usimtenge mtumishi wako ku hazina ya mapendo yako.

Huyu aliyemkamata Adamu mu mtego katika shamba la Edeni ili asimutii Bwana alinikamata na mimi mwenyewe ku ndoano, akanipotezea njia ya kweli; aliponiona nimeanguka

katika shimo la zambi, amejitukuza kwa kuanguka kwangu; umupige na upanga wa maombezi yako, uniopoe ku nyavu zake, ee Bikira, kwa ajili ya mapendo yako.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote... **STAVROTHEOTOKION**.

Ulipomwona Mwana wako ametundikwa Msalabani, ee Bikira Mtakatifu, ukalalamika ukalia: Ole, mwanangu mpenzi, wapi umeenda uzuri uliyopamba hali ya wanadamu?

**APOSTIKHA**

Ee Kristu, nasujudu mbele ya Msalaba wako mheshimiwa, mulinzi wa dunia na wokovu wa wakosefu, msaada kubwa, ushindi wa ufalme, kisa ya utukufu na ya usabiti wa ulimwengu.

Muti uliyokataziwa ukazaa mauti duniani, muti wa Msalaba ukatoa uzima wa milele; tunakuabudu tena, ee Bwana msulibiwa; nuru ya uso wako ituangazie, ee Mwokozi.

Ee Bwana, uweo wa Msalaba wako ni kubwa sana. Uliposimikwa kule Kalvario, unatawala dunia yote; uligeuza wavuvi kuwa Mitume, na wapagani kuwa kundi la washuhuda, wenyi kuombea roho zetu wokovu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote... **STAVROTHEOTOKION**.

Kuna neema duniani kwa ajili ya Msalaba wako, kiumbe kinapata nuru yake na mataifa yanapata wokovu, ndivyo alivyosema Mtakatifu kamili kwa Neno Bwana wake, kwa mimi nina moyo wenyi kuumizwa wakati naona mateso unayoitikia kwa kutaka kwako.

## MU KAZI TANO ASUBUI KATIKA SAUTI YA TATU

### KATHISMA YA KWANZA

Msalaba ulisimikwa duniani, ukainuka mpaka mbinguni, apana kwa urefu wa muti wake, lakini kwa sababu katika hii ulitimiza vitu vyote. Ee Bwana, utukufu kwako.

Umetukuzwa pa msonobari, pa mti wa kasuku wa Libano, ewe Mwana-Kondoo wa Mungu, sababu ya kuokoa wale wenyi kuabudu na imani kusulubiwa kwako kwa kutaka*:* Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

*Tin oreotita*

Kiumbe chote kimefurahiwa pa kukuona, ewe Bwana mvumilivu na furaha ya wote, umepandishwa Msalabani, ndivyo alivyosema Bikira Safi na Mtakatifu kamili, kwani alipata ukombozi kwa ajili yako, ee Mwana mpenzi; kwa muti uliponyesha mwanadamu aliyehukumiwa sababu ya muti; kwa mimi, nina moyo wa sikitiko, siwezi kuteswa pa kukuona umeingia katika mauti.

### KATHISMA YA PILI

*Tin oreotita*

Walipotazama uwezo wako wa milele na kusulubiwa kwako kwa kutaka, Malaika wakashangaa pa kuona namna gani msiyeonekana ameteswa mwilini, kwani alipenda kuwakomboa wanadamu ku mauti. Na tena tunakuimbia kama chemchem ya uzima, ee Kristru, na tunakutukuza katika ufalme wako mkuu.

Ulipochagua kufa Msalabani, ukaupanda moyoni mwa viumbe; kwa kutuokoa ukakubali mwili wako upigiliwe Msalabani, alafu jua likaficha miangaza yake; ni hii aliyoona munyanganyi

akakutambua kama Mungu na kwa imani yake akaingia paradizoni wakati alipokulalamikia: ee Bwana, unikumbuke katika ufalme wako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Kondoo jike Bikira akipoona mwana-Kondoo wake anakusudia kuteswa Msalabani, akasema: Ole wangu, ee Mwanangu, siri gani ya ajabu imenitokea? namna gani unaitikia kufa, wewe uliye wa milele? Naimba, ee Neno, na natukuza mapendo yako ya uvumilivu na mapendo yako ya milele.

**KATHISMA YA TATU**

Ee Kristu, ulipokea bila hasira makofi, sababu ya kuokoa wanadamu; opoa uzima wetu kaburini; ee Bwana, utupe wokovu wako.

Ushujaa wenu na imara yenu zilishinda uerevu wa adui; ee Mashahidi Washindaji, wenyi kustahili heshima yote, mumestahili heri ya milele; ninyi washuhuda wa Mungu kweli; ombeni kwa Bwana ili aokoe kondoo zake wenyi kumpenda Kristu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

*Tin oreotita*

Majeshi ya mbinguni walishikwa na woga nma wale wa hapa chini walishikwa na hofu wakati, ee Bwana, usiye na zambi, ulipenda kuinuliwa Msalabani; Jua likapata giza, mwezi haukutoa miangaza yake, Mama yako kwa machozi akalalamika: Ni ndoto gani hii, ee Mwanangu? Namna gani peke yako unateswa kwa ajili ya wanadamu wote?

**EKSAPOSTILARION**

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu).*

**APOSTIKHA**

Alipoinua mikono mu alama ya Msalaba Musa akamshinda Amaleki mulimani; lakini wewe Mwokozi ulipopanua mikono juu ya Msalaba mheshimiwa ukanikamata mikononi mwako; ukaniokoa ku utumwa wa adui na ukanipa alama ya uzima. Ee Msalaba Mheshimiwa wa Kristu, nasujudu mbele yako.

Kwa wivu nilifukuzwa Patadizoni, na kwa uzito wa zambi nikaanguka; lakini haukunizarau, ee Bwana, na kwa ajili yangu ukafanana nami; ukajachilia kusulubiwa na ukawa wokovu wangu. Uniongoze ku utukufu wako, ewe Mungu mwenye kuniokoa, utukufu kwako.

Njooni mataifa yote, tutukuze makumbusho ya Mashahidi wa Bwana, kwani walipokea kwa Kristu mbele ya Malaika na ya Wanadamu taji la washindi na wanamuomba kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Alipomwanga mawimbi ya machozi, Bikira Mtakatifu akalalamika na kulia akasema: Ee Yesu, nuru njema, namna gani unainama, ee Mwanangu? Wewe uliyeumba ulimwengu kwa neno lako, namna gani umejiachilia sasa kutazamiwa Msalabani, bila pumuzi wala sauti?

## MU KAZI TANO MANGARIBI KATIKA SAUTI YA TATU

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.**

Unifanye mimi kuwa hekalu la Roho wako Mtakatifu, ee Kristu, ukinitakasa ku aibu ya zambi, mimi niliye sasa pango la mashetani; na uwafukuze mbali nami kama ulivyofukuza zamani wachuruzi waliyokufuru Hekalu lako takatifu.

Ee Bwana mwenye kutaka kwa mapendo yako kuokoa watu wote, wenyi haki na waovu, ili hata mmoja wao asikufe, unihesabie mimi pia ku kundi la wateule hata kama nimeishi katika uzembe na nimezarau mafundisho yako, ewe Mungu Mwokozi.

Na uwezo wako usiyoweza kushindwa, ee Bwana, ulikufa kisha usingizi wa hali yako ya mwanadamu kaburini, ukawaamusha pia wafu kaburini tangu Adamu; ndiyo maana tunakuomba uwapumzishe marehemu waaminifu katika uwanja wako wa milele.

**Nyimbo ya Mzazi-Mungu.**

Nilipolala katika ukosefu wa shuruli, nilipitisha wakati wa maisha yangu mu uvivu; naogopa sana saa ya kuondoka, lakini kwa maombezi yako uniamushe ku toba, ewe Bikira Safi kamili na uniokoe.

Ponyesha mateso ya moyo wangu, selehisha kosa ya roho yangu, uniruhusu nikuimbie na moyo safi ili nipate huruma, ee Bikira Mtakatifu, siku tutakapohukumiwa.

Ee roho maskini, tia mzigo nyuma, tua ubaya wenyi uzito kubwa; jongea na kulia ukilalamika: Ewe Bikira Takatifu, unistahilishe nichukue nira nzuri ya Mwana wako na Mungu wako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Namna gani hatutashangaa, Muheshimiwa kamili, uzao wa Mungu na mtu? Kwa sababu bila kujua mwanaume, ee Bikira usiye na doa, ulizaa Mwana kwa namuna ya mwili pasipo baba, bila kupokea geuzo, ao mchanganyo, ao mgawanyo, lakini mwenye kushika tabia zake nzima za kila moja asili ya yote mbili. Kwa hii, Mama Bikira Bibi Malkia, umusihi kwa sababu ya wokovu, wa roho ya wale wanakusadiki kwa namuna ya kiorthodoksi, ya kama uko Mzazi-Mungu.

## APOSTIKHA

Ee Bwana, mashahidi wako walipotegemezwa kwa imani na kusabitishwa kwa matumaini, walipoungana katika roho na mapendo ya Msalaba, wakavunja uzulumu wa adui; walipopokea taji la milele, wanaomba pamoja na Malaika wabila-mwili kwa ajili ya roho zetu.

Manabii, Mitume wa Kristu na Mashahidi walitufundisha kuimbia Utatu wa asili moja; wakaleta nuru ku mataifa yenye kupotea*:* Malaika na wanadamu wamekuwa marafiki.

Ee Bwana, uwezo wa Msalaba wako ni kubwa sana*:* Uliposimikwa kule kalvario, unatawala dunia yote; uligeuza wavuvi kuwa Mitume, na wapagani kuwa kundi la Washuhuda wenyi kuombea roho zetu wokovu.

Tendo lote la ubinadamu ni bure kama haliendelee kisha kufa; hakuna kitu inabakia pa mali, utukufu hautufwate kule juu mbinguni; kwani lufu inapokuja, inapoteza hii yote. Tena, tumuombe Kristu msiyekufa awape marehemu mapumziko katika makao ya furaha ya milele.

Utukufu kwa Baba. Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Katika wote, peke yako ni Mama msiyeolewa, ee Mzazi-Mungu Mtakatifu, umuombe Mfalme Mtakatifu, Mwana wako, atuokoe katika mapendo yake kwa ajili ya wanadamu.

## MU POSHO ASUBUI KATIKA SAUTI YA TATU

### KATHISMA YA MASHAHIDI

*Sauti ya tatu. Tin oreotita.*

Ee Bwana mwenyezi, uliangaza makumbusho ya Mashahidi wako, uliwapa nguvu ya kufafanisha mateso yako; walishinda bora nguvu ya shetani na wakapokea kipaji cha kuponyesha magonjwa*:* Kwa maombezi yao, ee Bwana mpenda-wanadamu, utupe amani na neema ya wokovu wa roho zetu.

Mulipovikwa silaha za Kristu, mulipovaa silaha za imani, mulipambana na majeshi ya adui na mukawaangusha sabiti; muliposaidiwa na matumaini ya uzima, hamukuogope uzulumu na makamio ya wazulumu na mukapata taji, enyi Washuhuda wahodari wa Kristu Mungu wetu.

Kwa imani munaangaa kama nyota za mwanga, enyi Mashahidi Watakatifu ambao tunatukuza mashindano; bila woga mbele ya uzulumu wa wazulumu, mukamaliza kufuru ya miungu ya uwongo paka na silala ya ukweli na ushindi wa Msalaba usiyoweza kushindwa.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Bikira Mzazi-Mungu tunakuimba, wewe mupatanishi ya wokovu juu ya ukoo wetu; katika mwili alipata kwako, Mwana wako na Mungu wetu, alitaka kuteswa Msalabani, juu ya kutukomboa ku lufu, sawa mpenda-wanadamu.

### KATHISMA YA PILI

Ushujaa wenu na imara yenu zilishinda uerevu wa adui; ee Mashahidi Washindaji, wenyi kustahili heshima yote, mumestahili heri ya milele; ninyi washuhuda wa Mungu kweli; ombeni kwa Bwana ili aokoe kondoo zake wenyi kumpenda Kristu.

**Nyimbo ya wafu.** *Tin oreotita*

Ee Bwana, kwa amri yako, wakati tutakapoitwa mbele ya korti yako ya ajabu, usiwahukumu wale waliyokusadiki*:* Sisi wote tumetenda zambi, lakini bila kukurudiria wewe Mungu Mwokozi; na wale uliyochukua pamoja nawe, tunakuomba uwaweke, ee Kristu, kwa wema wako, katika hema ya wenyi Haki na ya Watakatifu.

Utukufu kwa Baba. . .

Chini ya muti wa uchungu tulifai kufa, kwa muti wa uzima wa milele unatufufua, ee Mwokozi, kwa Msalaba wako mheshimiwa uliua mauti, na kwa ajili ya sisi wote ukachemsha uzima wa milele. Kwa wale waaminifu wako waliyokukimbilia, ee Bwana, uwape kuishi katika Ufalme wako.

Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION**

Wale waliyoshinda bahari ya fujo ya hii uzima na waliyompendeza Mungu kuwaita, marehemu watumishi wako waaminifu, ee Bikira Mtakatifu kamili, uwapokee; uwapeleke kwa Mwamuzi Mungu wetu, ukiwaombea kama Mama ambaye Muumba anamupa yote anavyotaka, ili wakombolewe.

### EKSAPOSTILARION

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

## APOSTIKHA

Maaskari wa Kristu walivunja woga wote mbele ya wafalme na wazulumu na uhodari kubwa walimuungama Bwana wa ulimwengu, Mungu na Mfalme wetu, na sasa wanaombea roho zetu.

Majeshi ya mbinguni ya Malaika Watakatifu walishangaa ushujaa wa Mashahidi*:* Katika sura mwili wao walizarau lakini mateso sababu ya kuwa Wafuasi wa mateso ya Kristu Mwokozi, na wanaombea sasa roho zetu.

Kama nyota, munaangaza ulimwengu hata kufa kwenu, ee mashahidi Watakatifu; muliposhindana vema zaidi, muna uwezo wa kumuomba Kristu ili alete neema ya wokovu ku roho zetu.

**Nyimbo ya wafu.**

Sababu gani kuhangaika bure? Safari tunayotembea ni mfupi! Uzima wetu unafifia kama moshi, unasaidia kwa muda kidogo kama majivu na uvumbi na unapotea mbio-mbio. Na tena, tunakuomba mapumziko katika makao yenyi kuangaa furaha yako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Ee Malkia wa utakatifu, utukufu wa majeshi ya mbinguni, wimbo wa Mitume, utimizo wa maandiko ya Manabii, ee Bibi wetu, pokea maombi yetu na nyimbo zetu.

Elezo: *Kama kuna Alliluya, tunaimba ku masifu nyimbo za mashahidi zenyi kutangulia hapa juu, na kama Apostikha tunaimba Mifano (Prosomia) yafwatayo:*

Natukuza Msalaba wako mweshimiwa ambao unaleta heri na uzima kwa waaminifu wenye kukuimbia na mapendo, ee peke yako Bwana mwenyi huruma. Tena tunakuomba, ee Kristu Mungu wetu: Uwape marehemu wetu mapumziko katika makao yenyi kuangaa furaha yako.

*Shairi:* Heri wale uliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe.

Peke yako Bwana wa mapendo na wa huruma, bahari wa wema isiyoweza kufumbuliwa, unajaa mwanadamu, ulimuumba; tunakuomba, ee Kristu Mungu wetu, uwape marehemu wetu mapumziko katika makao yenyi kuangaa furaha yako.

Na makumbusho yao ni ya milele.

Kaburini mwili ulilala usingizi, lakini kwa uwezo wako usiyoweza kushindwa ukafufuka kama Mungu; wale waliyojuwa kaburini wakakutukuza wakikuimbia daima nyimbo zao milele. Na tena tunakuomba, ee Kristu Mungu wetu*:* Uwape merehemu wetu mapumziko katika makao yenyi kuangaa furaha yako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, tunatambua katika wewe taa kiroho iliyoleta nuru ya umungu sababu ya kumukutanisha na hali ya mwanadamu. Umuombe Mwana wako na Mungu wetu ili awape marehemu wetu mapumziko katika makao yenyi kuangaa furaha yako.



# KIPANDE CHA SAUTI INE

## MU POSHO MANGARIBI

**Wimbo ya Ufufuo.**

Tukiabudu bila kuacha Msalaba wako unaoleta uzima, ee Kristu Mungu, tunatukuza ufufuo wako wa siku tatu; kwa sababu ya hii ulifanya mupya asili ya watu iliyoharibika, ee Mwenyezi, na ukatuonyesha njia ya kupanda mbinguni, kwa kuwa wewe ni peke yako Mwema na Mpenda-wanadamu.

Ulifungua lauma ya mutifiwa uasi, ee Mwokozi, wakati ulipoopigiliwa kwa kutaka kwako pa muti wa Msalaba; na wakati uliposhuka, ee Mwenyezi, ku Hadeze, ulikata minyororo ya mauti, kwa kuwa wewe ni Mungu; kwa hii tunaabudu ufufuo wako katika wafu, tukipaza sauti ya shangwe: Ee Mwenyezi, utukufu kwako.

Ulivunja milango ya Hedeza, ee Bwana, na kwa lufu yako, uliharibu ufalme wa mauti; na uliopoa ukoo wa watu toka uharibifu, mukuleta ku dunia uzima na usiyoweza kuharibika na rehema kubwa.

Kujeni mataifa tuimbe, ufufuo wa Mwokozi wa siku tatu; sababu ya hii tulikumbolewa toka minyororo isiyofunguliwa ya Hadeze, na wote tulipata uzima na usiyoweza kuharibika, tukipaza sauti: Ewe uliyesulibiwa, uliyezikwa na uliyefufuka, utuokoe kwa ufufuo wako, wewe peke mupenda-wanadamu.

Malaika na watu, ee Mwokozi, wanaimba ufufuo wako wa siku tatu; sababu ya hii miisho za dunia ziliangazwa, na wote tulikombolewa toka utumwa wa adui, tukipaza sauti: Ewe mwenyezi Mwokozi muletaji-uzima, utuokoe kwa ufufuo wako, wewe peke Mpenda-wanadamu.

Ulivunja milango ya shaba, na kukata mapingo ya chuma, ee Kristu Mungu, na ulifufua uzao wa watu wenye kuanguka; kwa hii tunapaza kwa sauti moja: Ewe Bwana, uliyefufuka katika wafu, utukufu kwako.

Ee Bwana, kuzaliwa kwako kwa Baba ni kwa mbele ya wakati na ya milele; kupata kwako mwili kwa Bikira ni kwasiyofasiriwa na kufafanuliwa kwa watu; na kushuka kwako Hadezeni ni kwa woga kwa shetani na Malaika wake; kwani ukishinda mauti, ulifufuka katika siku tatu, ukiwapa watu uzima usiyoharibika na rehema kubwa.

Utukufu kwa Baba....Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Nabii Daudi alitekuwa Babu-Mungu kwa ajili yako, alikutabiri katika zaburi kwa yule aliyekufanyia maajabu: Malkia anasimama ku mukono wako wa kuume. Kwa sababu Mungu alikuonyesha wewe mama muletaji uzima, yeye aliyetwa mwili toka wewe kwa mapenzi yake bila baba, kusudi aumbe mara ingine mufano yake, iliyoharibika kwa tamaa, na kupata kondoo aliyepotea mulimani, kumubeba ku mabega yake, na kumutoa kwa Baba, kwa kuiunganisha pamoja na Ezi za mbinguni kwa kutaka kwake, na kuokoa dunia, ee Mzazi-Mungu; yeye ni Kristu, mwenye juwa na rehema kubwa zaidi.

### APOSTIKHA

Ee Bwana, ulipopanda juu ya Msalaba, ulizimisha mafingo yetu yakutoka kwa mababu zetu; na uliposhuka ndani ya hadeze, uliopoa wafungwa tangu zamani, ukaleta uzima

usiyoharibika ku uzao wa watu; kwa hii tukiimba tunasifu ufufuo wako, uletao uzima na wokovu.

Wakati ulitundikwa pa muti, ewe peke mwenyezi, ulitikisisha viumbe vyote; na wakati ulipowekwa kaburini, ulifufua wale waliokaa katika makaburi, ukaleta uzima na usiyoweza kuharibika ku uzao wa watu; kwa hii tukiimba tunasifu, ufufuo wako wa siku tatu.

Taifa la wavunja-sheria, ee Kristu, lilikutoa kwa Pilato, na kukuhukumu usulubiwe, na lilionekana lasiyo na shukrani kwa mwema; lakini kwa kutaka kwako ulivumilia maziko, na ulifufuka katika siku tatu kwa uwezo wako, kwa kuwa wewe ni Mungu, mwenye mutuletea uzima wa milele na rehema kubwa.

Wanawake wakishika kaburi yako, kwa machozi walikutafuta; lakini wakati hawakukupata, walilia, waliombolezwa na walisema: Ole wetu! Mwokozi wetu, Mfalme wa wote; namna gani uliibwa? Fasi gani iko mwili wako wenyi kuleta uzima? Lakini Malaika akawajibu: Musilie, alisema, lakini mwendeni kuhubiri, ya kama Bwana alifufuka, mwenye kutupatia shangwe; kwa kuwa peke ni mwenye huruma.

Utukufu kwa Baba....Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Inama na usikie kusihi kwa watumishi wako, ee Safi kamili; simamisha mageuzo ya misiba yetu; utufungue toka kila taabu, kwani tuiko na wewe peke yako kama nanga imara na haki, na tuliisha kupata ukingo wako. Tusipate haya, ee Bibi-Malkia, wakati tunapokuita; ujiharikishe kwa maombi yetu tunayokulilia kwa imani: Salamu, Bibi-Malkia, musaidizi wa wote, furaha na ukingo, na wokovu wa nafsi yetu.

### APOLITIKION

*Sauti ya ine.*

Wakati wanawake-wanafunzi wa Bwana, walipofundisha na Malaika kuhubiri habari ya furaha ya ufufuo, na walipotupa hukumu kwa mababu zetu, wakasema kwa Mitume kwa kujisifu: Mauti imenyanganywa, Kristu Mungu alisimama, kwa kuleta duniani rehema kubwa.

### THEOTOKION

Siri ya kificho tangu milele iliyokuwa isijulikane na Malaika, imeonekana duniani katika wewe, ee Mzazi-Mungu; maana Mungu alitwaa mwili kwa ushirika, bila muchanganyo, na alikubali Msalaba kwa kutaka kwake kwa ajili yetu; juu ya hii akifufua Muumbwa wa kwanza, akaokoa toka lufu nafsi yetu.

## SIKU YA MUNGU ASUBUI KATIKA SAUTI YA INE

### KATHISMA YA KWANZA

Walipoona mlango wa kaburi, na wasipoweza kuvumilia mwangaza wa Malaika wa nuru, Wanawake Watakatifu Wabebaji-manukato wakaogopa na wakasema: Wamemuimba huyu aliyemfungulia Mnyanganyi Paradizo? Ameamka, huyu mbele ya Mateso yake alitangaza Ufufuo wake? Kweli amefufuka, Kristu Mungu wetu, akiwapa wale wa ku Hadeze uzima wa milele na kuwafufua.

Utukufu kwa Baba...

Ee Mungu Mwokozi, ulipenda kuteswa Msalabani kwa kutaka kwako, wanadamu wakakuweka kaburini mupya wewe ambaye neno linakusanya mipaka ya ulimwengu; na katika Ufufuo wako wenyi kuleta uzima mauti ikafungwa monyororo na ikanyanganywa, wafungwa wa Hadeze wakalalamika: Kristu amefufuka, anakaa milele kama chemchem ya uzima.

Sasa na siku zote.**THEOTOKION**. *Kateplagi Iosif*.

Yosefu aliogopa alipoona siri yenye kupita ubinadamu, akakumbuka manyonya yenyi kufunikwa na umande, ee Mzazi-Mungu, wakati ulipopata mimba bila mbegu, akakumbuka kichaka kilichowaka moto bila kuteketezwa, akakumbuka tawi la Haaroni lililochamuka; mume wako na mlinzi wako akakushuhudia mbele ya makohani akalalamika: Bikira amezaa na amekaa bikira hata kisha kuzaa.

**KATHISMA YA MBILI**

*Takhi prokatalave.*

Ee Mwokozi msiyekufa, umefufuka, ukisanyika dunia yote pamoja nawe; kwa uwezo wako, ee Kristu Mungu wetu, ulivunja ufalme wa mauti, ee Mungu wa mapendo, uliwaonyesha watu wote Ufufuo. Wewe mwenye kutupenda, tunakutukuza.

Utukufu kwa Baba... *Kateplagi Iosif.*

Aliposhuka toba uwanja wa mbinguni, Gabrieli akajongea ku jiwe huko kulipatikana mwamba wa uzima wetu; mwenyi kuvaa mavazi meupe, akawaambia wanawake wenyi kulia: Msilie, maana muna daima huyu munapenda, muwe na moyo, kwani amefufuka kweli, huyu munayetafuta mukilia; nendeni mukawaambie Mitume: Bwana amefufuka.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Ee Bikira Mtakatifu, kundi la Malaika wakashangaa mbele ya siri ya ajabu ya kuzaa kwako kimungu. Namna gani huyu, kwa alama moja, anakusanya ulimwengu anachukuliwa mikononi mwako kama mtoto? Namna gani Mungu wa mbele ya nyakati anakuwa na mwanzo? namna gani ananyonyeshwa huyu mwenye kulisha mwanadamu wote na wema wake usiyokadirika? Na tena, Malaika wanapokushangilia wanakutukuza kweli kama Mzazi-Mungu.

**MAHIMIDI YA UFUFUO YA KRISTU**

**IPAKOI**

Ee Kristu, Wabebaji manukato, watangazaji wa kwanza wa ufufuo wako, wa ajabu, wakaenda mbio kwa Mitume wakasema: Kristu amefufuka kama Mungu, analeta duniani neema kubwa.

## ANAVATHMI SAUTI YA INNE.

**ANTIFONON YA KWANZA**

Tangu ujana wangu, tamaa zenye kunishambulia zilinizunguka, lakini wewe, ee Mwokozi wangu, unilinde na uniokoe.

Adui wote wa sayuni wanyamazishwa na Bwana; wewe kama nyasi yenye kuungua inapokauka.

Utukufu kwa Baba....Sasa na siku zote...

Roho yote inaishi kwa neema ya Roho Mtakatifu na inaishi na usafi wote kwa kwanga ku Utatu moja katika siri takatifu.

**ANTIFONON YA PILI**

Ee Bwana, napaza nguvu sauti kwako rohoni mwangu, sikio lako, ee Mungu wangu, lisikilize sauti yangu.

Kila mwanadamu anayemutumainia Bwana hatahuzunika kamwe.

Utukufu kwa Baba....Sasa na siku zote...

Mawimbi ya neema yenye kunywesha kiumbe yote sababu ya kuchanua uzima yanachirizika kwa Roho Mtakatifu.

### ANTIFONON YA TATU

Nitainua moyo wangu kwako, ee neno, hata moja ya furaha ya uzima huu isinikokotee ku mateso ya hapa chini.

Kama mtoto anavyomupenda mama yake, hivi tena tunapashwa kumupenda Bwana.

Utukufu kwa Baba....Sasa na siku zote...

Roho Mtakatifu anatueneza na utajiri hekima, mawazo na maarifa ya Mungu. katika Neno alifunua nia ya milele ya Baba.

### PROKIMENON

Simama, ee Bwana, kuja unisaidie, na utukomboe kwa ajili ya utukufu wa jina lako.*(mara tatu).*

*Shairi*: Ee Mungu, tulisikia na masikio yetu, mababu zetu walituambia tendo ulilofanya ku wakati wao, zamani za kale.

## KANUNI YA UFUFUO YA KRISTU

### WIMBO WA KWANZA

*Thalasis to erithreon pelagos*

**IRMOS:** Alipovuka pa kavu Bahari Nyekundu, Israeli wa zamani akafukuza jangwani nguvu ya Amaleki kwa msaada wa mikono ya Musa aliyopanua mu alama ya Msalaba.

Utukufu kwa Ufufuo wako, takatifu, ee Bwana.

Ulisimamisha kuanguka kwetu wakati ulipoinuliwa juu ya muti wa Msalaba mheshimiwa, ukatuokoa ku mti wa hatari, ee Mungu wa wema na Bwana mwenyezi.

Utukufu kwa Ufufuo wako, takatifu, ee Bwana.

Kaburini na mwili wako, kuzimuni na roho yako, kama Mungu, ku Paradizo pamoja na Mnyanganyi, umekaa pa kiti cha ufalme pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, ewe Kristu uliye popote na kuujaza ulimwengu.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe. **THEOTOKION.**

Kwa mapenzi ya Baba ulipata mimba ya Mwana wa Mungu bila mbegu kwa msaada wa Roho Mtakatifu; ukazaa mwilini huyu asiye na mama mbinguni na bila baba alizaliwa kwako sababu ya kutuokoa.

*Anikso to stoma mu.*

Utukufu kwa Ufufuo wako, takatifu, ee Bwana.

Kwa mateso yako, uliponyesha wanadamu, kwa damu yako Takatifu ukawafanya kuwa wapya; kwa nguvu yako uliharibu mwenyi uwezo ambaye zamani, ee Bwana, alivunja kazi ya mikono yako.

Utukufu kwa Ufufuo wako, takatifu, ee Bwana.

Ee Bwana wa ulimwengu na Mungu uliyejifanya, kwa lufu yako umekuwa ufufuo wa wafu; nguvu ya mauti ilipotea wakati ilipambana na uzima wa milele.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe. **THEOTOKION.**

Ee Mungu wetu, Bikira aliyekuchukua na mkuu kupita Ezi za mbinguni, kwani tumbo lake limekuwa Hekalu yako ya uzima, mulima wako takaitfu.

**KANUNI YA MZAZI-MUNGU**

**IRMOS:** Roho yangu imezama kama wapanda frasi wa Farao, nakuomba kwa bahari ya hali isiyoteseka, wewe uliyezaliwa kwa Bikira, ili kwa ngoma na mateso ya mwili wangu niimbe wimbo wa ushindi.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Watu walishituka, mataifa yakahangaika, ufalme wa nguvu ikaangushwa, wakaogopa mbele ya Mwana wako kwani, ee Bikira, alikuja Mfalme mshindaji wa mzulumu, na aliokoa dunia yote kuzimuni.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Huyuy anayekaa Juu mbinguni amekuja kwa wenyi kufa. Kristu alitaksa makao yake na akaifanya imara. Kwani peke yake kisha kuzaa Mzazi wa Muumba amekaaa johari ya ubikira.

**WIMBO WA TATU**

*Efrenete epi si.*

**IRMOS:** Eklezya yako, ee Kristu, inafurahiwa ndani yako na inakulalamikia, ee Bwana, ndiwe nguvu yangu, kimbilio yangu na tegemeo yangu.

Utukufu kwa Ufufuo wako, takatifu, ee Bwana.

Mti wa uzima, Mzazabibu katika roho na ukweli ametundikwa Msalabani, chemchem ya chakula cha kila mwanadamu.

Utukufu kwa Ufufuo wako, takatifu, ee Bwana.

Ee Bwana mkuu na wa hatari uliyeharibu majivuno ya Hadeze, Mungu msiyeharibika, unaamka tena na mwili wako.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe. **THEOTOKION.**

Peke yako, ee Mzazi wa Mungu wangu, umekuwa msimamizi wa hazina ya ajabu kwa ajili ya wanadamu: Tunakuimbia tena, salamu.

Utukufu kwa Ufufuo wako, takatifu, ee Bwana.

Ee Mwokozi, nyoka alinikazia meno yenye kumwanga sumu, lakini ukayavunja kwa misumari yaliyotoboa mikono yako, ee Mungu mwenyezi. Kwani hakuna hata mmoja kati ya Watakatifu aliye Mtakatifu kama Wewe.

Utukufu kwa Ufufuo wako, takatifu, ee Bwana.

Ee mpenda-wanadamu, ulipenda kuonekana kaburini kama mufu mwenye kufufuka na ukazifungulia roho zilizokuwamo tangu Adamu milango ya Hadeze. Kwani hakuna mmoja kati ya Watakatifu aliye Mtakatifu kama Wewe.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe. **THEOTOKION.**

kama udongo usiyolimwa, ulitoa suke la uzima lewnyi kuleta umilele kwa kila mtu mwenyi kuungana nayo katika roho. Ewe Mtakatifu mwenye kupumzika na utukufu kati ya Watakatifu.

**KANUNI YA MZAZI-MUNGU**

**IRMOS:** Toka Juu mbinguni ulishuka duniani kwa kutaka kwako, wewe mwenye kutawala uwqezo wote, na toka chini ya Hadeze uliinua hali nyenyekevu ya wanadamu. Kwani hakuna Mtakatifu mwingine, ila wewe, mpenda-wanadamu.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Hali ya wanadamu ilitakaswa kwa ajili yako ilipopambana na moto kimungu. Kama chini ya majivu ya mkate, ee Bikira Mtakatifu kamili, ulivumilia bila kukuharibu moto wa Mungu uliyokulinda sana.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote... **THEOTOKION.**

Ni nani huyu, karibu kweli na Mungu, anapita ku ukuu daraja za Malaika? Peke yake ni mama Mzazi-mwenyi kuangaa katika nuru ya ubikira, kwa sababu alizaa Mwenyezi duniani.

### KONTAKION

Mwokozi na Mkombozi wangu alifufua wafu wote, na nguvu yake ya umungu aliwaondoa ku minyororo ya kaburi; akavunja milango ya Hadeze, na kama Rabi mkuu akafufuka siku ya tatu.

### NYUMBA (IKOS)

Mfufuliwa katika wafu, Kristu chemchem ya uzima, alitoa kaburini siku ya tatu, hii siku alivunja milango ya mauti, kwa uwezo wake mwenyewe aliua Hadeze, akakata uchungu wa mauti na akawafungua Adamu na Eva. Tumwimbie, sisi wote wanadamu, kwa ushukuru tumutolee sifa daima, kwani peke yake ni Mungu Mwenyezi na Rabi aliyefufuka siku ya tatu.

### EKSAPOSTILARION

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

## MASIFU

**Wimbo ya Ufufuo.**

Ewe uliyevumilia, Msalaba na lufu, na ulifufuka katika wafu, Bwana Mwenyezi, tunasifu Ufufuo wako.

Pa Msalaba wako, ee Kristu, ulituopoa toka fingo ya Kale, na kwa lufu yako uliharibifu Shetani, mwenye jeuri kwa hali yetu, na kwa ufufuo wako ulijaza vyote kwa furaha; kwa hii tunapaza sauti kwako: Ewe Bwana, uliyefufuka katika wafu, utukufu kwako.

Pa Msalaba wako, ee Kristu Mwokozi, utuongoze kwa ukweli wako, na utuokoa toka mitego ya adui; Ewe uliyefufuka katika wafu, utufufue sisi tuliyoanguka katika zambi, myolosha mukono wako, ee Bwana Mpenda-wanadamu, kwa upatanisho ya watakatifu wako.

Pasipo kujitenga toka kifua cha Baba yako, ee Mwana wa pekee Neno la Mungu, ulikuja duniani kwa kupenda-wanadamu, ukijifanya mtu bila ugeuzo, na ulivumilia katika mwili Msalaba na lufu, ee Msiyeteswa katika umungu; ukifufuka katika wafu, ulipatia uzima usiyokufa kwa uzao wa watu, sawa yako Mwenyezi.

**Wimbo Anatolika.**

Ulikubali lufu kwa mwili, ukifanya biashara kusudi ya kutupatia uzima usiyokufa, ee Mwokozi; na ulikaa ndani ya kaburi, kusudi utuopoe katika Hadeze, ukitufufua pamoja nawe, ukiteswa sawasawa na mtu, lakini ukifufuka sawasawa na Mungu; kwa hii tunakupaza sauti: Utukufu kwako, ee Bwana mletaji-uzima, peke yako mpenda-wanadamu.

Mawe ilipasuka, ee Mwokozi, wakati Msalaba wako ulipozamishwa ndani ya pahali pa mufupa wa kichwa; wakati ulipowekwa ndani ya kaburi sawa mwenye kufa, zamu ya milango wa hadeze walitetemeka; na kwa sababu uliharibu nguvu ya mauti, uliwapa wafu wote uzima usiyoharibika, kwa ufufuo wakop, ee Mwokozi; Bwana mletaji-uzima, utukufu kwako.

Wanawake walitamani kuona Ufufuo wako, ee Kristu Mungu, Maria Magdalene alijiharikisha kufika, alipata jiwe limefingirishwa mbali na kaburi, na Malaika mwenye kukaa na kusema: Kwa nini munatafuta yeye aliyehai katika wafu? Alifufuka, kwa kuwa yeye ni Mungu, kwa kuokoa ulimwengu.

Eko wapi Yesu, muliyefikili kuchunga? Museme, Wayuda? Eko wapi huyu muliyeweka ndani ya kaburi, muliyofunga jiwe kwa muhuri? Mulete maiti, mwenye muliyekataa uzima; Mulete muzikwa, ao musadiki kwa Mfufuliwa; ikiwa basi mukinyamaza Ufufuo wa Bwana, mawe yatapata sauti, na kabisa jiwe limefingirishwa mbali na kaburi. rehema yako ni kubwa! Siri wema yako ni kubwa! Mwokozi wetu, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba...**EOTHINON**
*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu).*

## SIKU YA MUNGU MANGARIBI KATIKA SAUTI YA INE

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.** *Os geneon en martisin.*

Tuende, ee roho yangu maskini, usujudu mbele ya Mungu na lia na machozi ya kibukutu ukisema: Nimekosa mbele ya mwisho tafuta huruma kwa Muumba na umulalamikie na moyo wote: Ee Mungu wangu, usikatae malalamiko yangu, usizarau sikitiko ya moyo wangu, ee Bwana, katika rehema yako kubwa.

Usiku ma mchana, adui mbaya mwenyi kunigombanisha hache kunikamata ku mtego yake na ananisukumia ku upotevu wangu katika shimo ya uovu, lakini wewe, peke yako mwema, uniopoe ku uzulumu wake na ku uhitaji wote; ee Yesu Mwokozi wangu mwema, uniokoe ku namna yote ya azabu.

Naweka ndani yangu mawazo ya mateso yenyi kunitenga mbali nawe; mafundisho yako, ee Bwana, nilivunja pahali pa kutenda mema, lakini itika, ee Bwana, kukaa ndani yangu kwa wingi wa huruma yako na unifundishe kufanya mapenzi yako, katika wema wako na mapendo yako kwa wanadamu.

**Wimbo ya Malaika.**

Ulitayarisha makundi ya Malaika na majeshi ya mbinguni sababu ya kuwa makao nzuri ya nuru yako, vyombo vitakatifu kamili: Washuhuda wa utukufu wako wakizunguka kiti chako cha umungu, wakitimiza amri zako na nguvu, wenyi uwezo na kujaa na juhudi sababu ya kutimiza mapenzi yako, ee Bwana Mpenda-wanadamu.

Ulipotaka kuonyesha habari ya mapendo yako, wewe wa milele, ku mwanzo ukaumba na mkono wa uwezo kwa mapenzi yako ya umungu makundi ya Malaika, majeshi yao ya nguvu. Kwani ilifai kwe;li mema mengi yenee na neema yako ijae tele.

Waserafi wa mabawa sita, Wakeruvi wa macho mengi na wenye vitu kubwa vya Ezi wanasimama karibu nawe, wakiangaa na nuru yako ya kuangaa pamoja na Malaika, Malaika

Wakuu, Wafalme, Wakuu, Watawala, Wenye Uwezo, wakishangilia utukufu wako kimungu, ee Mwenyezi, wanatuombea kwako.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote... **THEOTOKION**.

Ee Bikira Mtakatifu kamili mwenye kunisabitisha daima kwa Bwana katika maombi yako na ulinzi wako imara, tuliza vishawishi, nyamazisha mawimbi ya tamaa zangu, fariji moyo wangu wenyi ku huzunika, nakusihi, jaza roho yangu na neema yako ili nikutukuze kweli.

**APOSTIKHA**

Ee Bwana, nilitaka kuzima katika vidonda vyangu daftari ya zambi zangu ili kuamini kuangu kukupendeze katika muda wa maisha yangu, lakini kwa hila yake adui akasirika juu ya roho yangu*:* Ee Bwana, mbele ya mwisho uniokoe.

Mwenyi kuzama gani akifika ku bandari yako hataokolewa? Mgonjwa gani hatapata maponyesho kwako? Ee Muumba wa wote na mganga wa wagonjwa, Bwana, mbele ya mwisho uniokoe.

Ee Kristu Mungu wetu, unapotukuzwa katika makumbusho ya Watakatifu wako, kwa maombezi yao ututumie neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote... **THEOTOKION**.

Salamu, wingi la kuangaa, salamu, kinara cha nuru, salamu, kikombe ambamo Manna ililindwa, salamu, tawi la kuchanuka la Aaroni, Kichaka chenye kuwaka moto bila kuteketezwa, Taa, Kiti cha ufalme na Mulima takatifu, salamu, mulango wa siri, salamu, matumaini ya waaminifu.

## MU KAZI MOJA ASUBUI KATIKA SAUTI YA INE

### KATHISMA YA KWANZA

Ee Bwana, rudisha kwako roho yangu maskini, kwani nimetumia vibaya maisha yangu yote katika zambi, unipokee kama mwanamuke mwenye zambi na uniokoe.

Ninapovuka bahari ya hii uzima, natazama shimo ya zambi zangu, na nisipojuwa wapi nitaenda, nakulalamikia kama Petro*:* Uniokoe; ee Kristu Mungu wangu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote... **THEOTOKION**.

Siri ya ajabu na muujiza haujaonekana! namna gani Bikira alikuchukua wewe Muumba wa ulimwengu, na akakaa Bikira kisha kuzaa? Wewe aliyezaa sabitisha imani yetu, tuliza mataifa na leta amani ku dunia katika mapendo yako kwa wanadamu.

### KATHISMA YA PILI

*Takhi prokatalave.*

Sisi wote pamoja tukimbilieni mbio ku chumba cha Bwana Arusi sababu ya kusikiliza sauti nzuri ya Kristu Mungu wetu*:* Njooni, enyi marafiki wa utukufu wa mbinguni; na kama zamani mabinti wenye akili, tuangaze taa yetu katika imani.

*Kateplagi Iosif.*

Tazama, ee roho yangu, namna gani tutahuzuria ku hukumu*:* Kwa hii wakati wa woga viti vitasimikwa; hapo Mwamzi wa haki atahukumu matendo ya kila mmoja; tazama, moto wa hatari umetayarishwa sababu ya kufunika vitu vyote kama bahari kali. Ee roho yangu, tubu mbele ya mwisho.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Ni wewe kweli Mzazi-Mungu na kama mama unauwezo wa kumuomba Mwana wako na Mungu wetu alinda waaminifu wenye kukukimbilia; katika wewe kuna nguvu yetu na makimbilio yetu, ndiwe boma letu, bandari yetu ya wokovu na peke yako mlinzi wa wanadamu.

**KATHISMA YA TATU**

*Takhi prokatalave.*

Ee Utatu Mtakatifu, Malaika wabila-mwili wanakuimbia daima kwa vinywa vyao kiroho na wanaposimama na woga mbele yako, ee Mungu katika watu tatu, wanalalamika: Ndiwe Mtakatifu. Kwa maombezi yao hurumia basi kazi mikono yako ilifanya, wewe peke yako mpenda-wanadamu.

Leo Majeshi ya mbinguni wanapoikumbuka Mashahidi washindaji, wanakuja kuangaza moyo wa waaminifu na wanaangazisha neema ulimwenguni; kwa maombezi yao, ee Mungu Mwenyezi, utupe neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Kwa huyu aliyelishwa Hekaluni, katika Patakatifu ya Watakatifu, mwenye kupambwa na hekima, na imani na ubikira Safi, malika Mkuu Gabrieli akamuletea habari ya mbinguni: Salamu, Bikira mbarikiwa na mjaliwa na utukufu, Bwana ni pamoja nawe.

**EKSAPOSTILARION**

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu).*

**APOSTIKHA**

Mimi ni mpotevu kati ya kondoo zako wa siri na nakimbilia kwako, ewe Mchungaji mwema*:* Ee Mungu, unihurumie.

Ee Mwokozi, unisafishe na machozi yangu, mimi mwenyi kuchafuka na zambi nyingi; tena nasujudu mbele yako*:* Nimekosa, ee Mungu; unihurumie.

Namna gani hatutashangaa, ee Mashahidi Watakatifu, mashindano kubwa muliyoshindana? Katika mwili wenu mulishinda adui Wabila-mwili wakati mulipomuungama Kristu na mulipovaa silaha ya alama ya Msalaba; ndio maana mulipokea uwezo wa kufukuza mashetani na kushindana adui: Ombeni daima kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Okoa watumishi wako ku hatari yoyote, ee Mzazi-Mungu na Bikjira mbarikiwa, ili tukutukuze kama matumaini ya roho zetu.

## MU KAZI MOJA MANGARIBI KATIKA SAUTI YA INE

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.** *O eks ipsistu klithis.*

Ukifwasa mwanamuke mkanaani, umufwate Kristu, ee roho yangu, na umulalamikie mara nyingi. Unihurumie, ee Bwana, sina na mtoto mwenye pepo mchafu, lakini mwili wa uasi; nakuomba, fukuza homa na tuliza umotomoto wa tamaa, kwa woga wako uipatishe haya, kwa maombezi ya Bikira Mtakatifu kamili aliyepata mimba yako na kukuzaa, ee Kristu, Mfazili mwenye kujaa na huruma, na kwa maombezi ya watakatifu wote.

Ee Kristu, zamani, ulimutuma Nabii Yona kwa Wavuvi wa Ninawe kuwatangazia toba; na kwa kwongoka kwao wakageuza hasira yako kuwa mapendo, wakatoka salama ku hasira ya uharibifu; kwa mimi pia mtumishi wako msiyestahili, ee mpenda-wanadamu, tuma nguvu ya msaada wako ili niongoke sababu ya kutoka ku maovu yangu mengi; na uniongoze mu njia ya

toba kwa machozi ya uchungu na kwa malalamiko na uniopoe ku makosa yangu mengi katika huruma yako.

Wewe uliyekuja duniani kuokoa waovu, ukiwaalika wanadamu ku toba, ee Bwana wa mapendo, unihurumie kwa wema wako, hata kama nimekukosea zaidi kuliko wote, unionyeshe njia ya kuongoka na uniokoe katika mapendo yako; unipe mawazo ya sikitiko, unipe wema, usawa, ukweli na unyenyekevu, ee Mungu Mwokozi, katika huruma yako na mapendo yako.

**Wimbo ya Mtangulizi Yoane.** *Edokas simiosin.*

Ee Mtakatifu Yoane Mbatizaji Mtangulizi mwenyi heri, kwa maombezi yako angaza roho yangu yenyi kutiwa giza kwa uovu wa nyoka na ongoza hatua zangu ili nifwate njia sawa yenyi kupeleka ku furaha, uzima, ili mimi mtumishi wako nisiye na mafaa nikipata kwako hii ninajitaji, niweze kukutukuza daima na nguvu.

Chipuki la tasa, ee Mtangulizi mwenyi heri, fanya ili roho yangu, kavu kwa matendo mema, kwa maombezi yako na kwa toba iweze kutoa tunda mbele ya Mungu ili mimi mtumishi wako nisiwe na mafaa, nikiokoka, nikutukuze sababu ya miujiza yako na ya maombezi yako ya furaha.

Ee Mwamuzi mwenyi haki zaidi, mpenda-wanadamu, mwenyi kuvumbua yenyi kuwa moyoni mwa mwanadamu, Bwana usiyekumbuka zambi zetu, ku wakati wa hukumu usinifunike na haya japo uovu wangu, ee Neno la Mungu, lakini kwa maombezi takatifu ya Mtangulizi, uiinamie tangu sasa na uniokoe mimi mwenyi mateso, nakuomba na nakusihi, ee Yesu, hazina ya huruma na Mwokozi wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

Mimi ni Esau mupya, ee Bikira Mtakatifu kamili, peke yangu naonekana mwenyi mateso na mwenyi tamaa kupita wote, peke yangu naondolewa nguvu ya umungu; nami basi atalilia mateso yangu? Nani ataonea huruma upotevu wangu? Ndio maana nakulalamikia mbele ya mwisho: Nimekosa, ee Bibi wetu, lakini uniokoe kama zamani Mwana wako alivyookoa kahaba.

**APOSTIKHA**

Ee Bwana, nilitaka kuzima katika vidonda vyangu daftari ya zambi zangu ili kuamini kuangu kukupendeze katika muda wa maisha yangu, lakini kwa hila yake adui akasirika juu ya roho yangu*:* Ee Bwana, mbele ya mwisho uniokoe.

Mwenyi kuzama gani akifika ku bandari yako hataokolewa? Mgonjwa gani hatapata maponyesho kwako? Ee Muumba wa wote na mganga wa wagonjwa, Bwana, mbele ya mwisho uniokoe.

Ee Bwana Mpenda-wanadamu uliyepokea uvumilivu wa Mashahidi wako Watakatifu, pokea pia heshima ya nyimbo zetu, ukitupatia kwa maombezi yao neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**

*Edokas simiosin.*

Makao takatifu kamili ya Mfalme mkuu, ee Bikira mwenyi kustahili nyimbo zetu, nakuomba, takasa akili yangu yenyi kuchafuka na zambi nyingi na uifanye iwe makao ya furaha ya Utatu Mtakatifu ili mimi mtumishi wako nisiye na mafaa, nikiokolewa, nitukuze uwezo wako wa rehema yako kubwa.

# MU KAZI PILI ASUBUI KATIKA SAUTI YA INE.

## KATHISMA YA KWANZA

Ee Bwana, rudisha kwako roho yangu maskini, kwani nimetumia vibaya maisha yangu yote katika zambi, unipokee kama mwanamuke mwenye zambi na uniokoe.

Ninapovuka bahari ya hii uzima, natazama shimo ya zambi zangu, na nisipojuwa wapi nitaenda, nakulalamikia kama Petro*:* Uniokoe; ee Kristu Mungu wangu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Neno la Baba, Kristu Mungu wetu, tunajuwa ya kama alitwaa mwili tumboni mwako, ee Mzazi-Mungu na Bikira safi, mbarikiwa katika wote, na bila kuacha tunakuimba kwa kukutukuza.

## KATHISMA YA PILI

Ninapovuka bahari ya hii uzima, natazama shimo ya zambi zangu, na nisipojuwa wapi nitaenda, nakulalamikia kama Petro*:* Uniokoe; ee Kristu Mungu wangu.

*Kateplegi Iosif.*

Roho na moyo zinapochafuliwa kwa giza ya tamaa na furaha ya hii uzima, siwezi kuwaza sikitiko, lakini wewe, ee Mwokozi, unihurumie kwa meteso yangu na unipe nikumbuke sikitiko ili mimi pia nikulalamikie mbele ya mwisho. Ee Bwana wa mapendo, japo uovu wa mtumishi wako wa kutotumaini kwnagu, ee Kristu Mwokozi uniokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, tunakutukuza tukiimba: Salamu, Wingu ya Nuru yasipo mwisho, Bwana wa utukufu uliyechukua tumboni mwako.

## KATHISMA YA TATU

*Takhi prokatalave.*

Njiwa wa jangwa, Mbatizaji wa Bwana, alipohubiri kuongoka na kuonyesha Mungu aliyejifanya mtu, Kristu, akawa mwombezi wa mukosefu wote, kwani anasaidia daima wale wote wenye kuzama mu hii uzima. Kwa maombezi yake, ee Kristu, okoa dunia iliyo yake.

Walipovaa silaha ya Msalaba wako, ee Kristu Mungu wetu, Mashahidi wako wakashinda uerevu wa adui; wakaangaa kama nyota, wakaongoza wanadamu; kwa wale wenyi kuwaomba na imani wanawaponyesha kwa maombezi yao, okoa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Wewe peke yako ulipata mimba ya Muumba wa ulimwengu na peke yako ulipamba wanadamu na uzazi wako, ee Bikira Safi kamili, uniokoe ku nyavu za adui, uniweke pa mwamba wa mafundisho ya Kristu, ukimusihi daima huyu aliyepata mwili tumboni mwako.

## EKSAPOSTILARION

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu).*

## APOSTIKHA

Mimi ni mpotevu kati ya kondoo zako wa siri na nakimbilia kwako, ewe Mchungaji mwema*:* Ee Mungu, unihurumie.

Mawimbi ya makosa yangu yananizunguka, ee Mwokozi, na nisipoweza kushindana juu ya wingi wao kali, nasujudu mbele yako, ewe peke sukani; kama kwa Petro, uninyoshee mkono kwa ajili ya mapendo yako kwa wanadamu na uniokoe.

Ee Mashahidi Watakatifu, tunashangaa mashindano yenu, kwani, mulipovaa mwili usiyokufa, mulifukuza adui msiyeonekana; mumeteswa mateso kali zaidi bila woga mbele ya wazulumu; sasa mumepata kwa Kristu utukufu wenyi kustahili, yeye mwenyi kuleta neema ya wokovu ku roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Ee Malkia Mzazi-Mungu, wewe utukufu wa wakristu, funika haya ya makufuru ya makafiri na fanya nyakundu uso wa wale hawataka kusujudu mbele ya Ikona yako Takatifu, ewe Mtakatifu kamili.

## MU KAZI PILI MANGARIBI KATIKA SAUTI YA INE

**Wimbo ya Usulubisho.** *Edokas simiosin.*

Ee mpenda-wanadamu uliyetangulia kuniumba kwa udongo, ukanitengeneza kwa uso wako, kwa bahati ukanipa heri Paradizoni; na wakati nilipodanganywa kwa muti wa maarifa, nikaharibika, ukaniamusha ku mauti, ukajifanya mwenyi kufa kama sisi na ukajiachilia kusulubiwa, ee Bwana msiyekufa, kwa huruma yako kubwa na kwa kutaka kwako kwa milele.

Kwa mapendo yake yasipo mipaka Muumba na Bwana wangu bila kuacha kifua cha Baba, akajishusha yeye mwenyewe na akashuka duniani, akachukua hali ya mtumwa kwa wema wake tumboni mwa Bikira kwa kutaka kwake; Msalabani msiyekufa akateswa mwilini, na alipoharibu nguvu ya mauti akaokoa wanadamu.

Ee Bwana, uliposulubiwa kwa kutaka kwako, ukasulubisha zambi pamoja nawe, ee Kristu, ukazima laana ya zamni kwa mikono yako yenye kutobolewa na misumari na ukapasua hukumu ya baba wa kwanza na mkuki uliyochomwa ubavu wako, naimbia mateso yako, ee Bwana, natukuza ufufuo wako. katika hii ulileta uzima kwa wote wale waliyouawa kwa mateso.

**Wimbo ya Mzazi-Mungu.**

Safisha haya ya moyo wangu maskini, ee Mzazi-Mungu mstahili kamili wa nyimbo zetu, safisha vidonda na mateso zambi iliiletea, sabitisha pia akili yangu yenyi kugeukageuka ili katika mateso yangu nitukuze, mimi mtumihsi msiyestahili, ulinzi wako wa nguvu na kubwa.

Ee Bikira Mzazi-Mtakatifu kamili, leta nguvu na uhodari ku roho yangu zaifu na yenyi kuregea ili kwa woga mapendo itimize amri za Kristu; hapo nitatoka salama ku moto kali na kwa sababu yako nitapokea urisi wa mbinguni na uzima wasipo mwisho katika furaha ya milele.

Giza za ajabu za mauti zinashambulia roho yangu, ee Mchumba kimungu, mateso ya shetani yananiogopesha: kwa wema wako uniopoe ku ufalme wao na uniogoze, ee Bikira Mtaaktifu kamili, ku bandari ya wokovu na ku nuru yasipo mangaribi pamoja na Watakatifu wote.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Bikira Mtakatifu kamili alipomuona Kristu ameondolea uzima japo ameuwa muovu, akamulalamikia kwa uchungu huyu aliyetoka tumboni mwake na akimshangaa kwa uvumilivu

wake: Usimsahau mjakazi wako, ee Mwana mpenzi, mpenda-wanadamu, usikawe kusikiliza hamu yangu.

**APOSTIKHA**

Ee Kristu, ulitupatia Msalaba takatifu kama silaha isiyoweza kushindwa. Katika hii tunakutukuza, kama washindaji, mashambulio ya adui.

Ee Kristru, tunapokuwa daima na msaada wa Msalaba wako, tunaweza kuepuka ku wavu wa adui.

Kwa deni munayo kwa Mwokozi, ee Mashahidi watakatifu, mutuombee daima sisi wakosefu, mukiomba maondoleo ya zambi zetu na neema ya wokovu ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **STAVROTHEOTOKION.**

*Os geneon en Martisin.*

Alipomuona Mwana-Kondoo na mchungaji Msalabani, Mama jike la Kondoo aliyekuzaa akamwambia na uchungu wake wa umama. Ee Mwanangu mpenzi, hii ni tuzo la watu wasiyo na shukrani waliyopata mambo yako ya maajabu. Lakini nataka kutukuza mapendo yako kimungu na isiyokadirika.

## MU KAZI TATU ASUBUI KATIKA SAUTI YA INE

### KATHISMA YA KWANZA

Umetukomboa ku laana ya Sheria kwa Damu yako heshimiwa; ulipigiliwa Msalabani na kuchomwa Mkuki, ukawa kwa wanadamu chemchem ya umilele; ee Mwokozi wetu, utukufu kwako.

Ewe Kristu Mungu, uliyeinuliwa kusudi Msalabani, uipe jamii ile jipya iliyo na jina lako, rehema yako. Uwafurahishe wafalme wetu waaminifu na nguvu yako, ukiwatunza na kushinda juu ya washindanao, wakifurahiwa kwa agano lako jipya, silaha, ya amani, alama isioshindika.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **STAVROTHEOTOKION.**

*Kateplagi Iosif.*

Karibu ya Msalaba Kondoo jike Mtakatifu, mama wa mwana-Kondoo mkombozi, akahuzunika na akasema katika woga wa ndoto yake: Ni mambo gani hii ya ajabu na mupya? Mwana mupole, namna gani unasulubiwa kwa kutaka kwako Msalabani na kufa lufu ya machukizo? Ee Muumba, natukuza mapendo yako isiyokadirika.

### KATHISMA YA PILI

Ujiharikishe kutangulia, ee Kristu Mungu wetu, mbele ya sisi kuwa watumwa wa maadui wenyi kukufuru na kutuegemeza; wale wenyi kutugombanisha ywapunguze kwa Msalaba wako, wajuwe nguvu ya imani ya kweli, kwa maombezi ya Mzazi-Mungu, peke yako mpenda-wanadamu.

Ulipigiliwa Msalabani sababu ya kutuita kati ya wapagani, ee Mpenda-wanadamu, ulipanua mikono kwa kutaka kwako na ukaitika ili ubavu wako uchomwe mkuki. Ee Mungu wa mapendo, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Wakati Mama msiyeolewa alipokuona Msalabani, akalia machozi na akasema akilalamika: Ni mambo gani hii ya ajabu, ee Mwanangu? Namna gani watu wasiyo na shukrani wamekupigilia Msalabani, wewe uliye uzima wa milele, nuru ya macho yangu?

**KATHISMA YA TATU**

*O Ipsothis en to stavro.*

Kisha kuanguka mbaya ku Paradizo adui alikoletesha kwa shauri ya uchungu, ukanisimamisha kule kalvario, ee Kristu, ukitengeneza Msalabani laana ya zamani; na ulipomuua yule nyoka ambaye werevu umeniua, ukanifanyika zawadi ya uzima wako. Ee Bwana, utukufu ku usulubisho wako.

Mashahidi wako walipamba Eklezya kwa damu yao ulimwenguni kote*:* Inapovaa sufi na kitani, kwa kinywa yao, inakuimbia, ee Kristu Mungu wetu*:* Onyesha huruma yako kwa hawe watu walio wako, leta amani kwa watawala wetu wote na neema ya wokovu ku roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Alipokuona umetundikwa Msalabani, Kondoo Jike Bikira, akasema akilia: Ni mapendo gani hii isiyokadirika, ee Neno mwenyezi, namna gani kundi la wenyi kuhukumu wanasubutu kuhukumu sasa Mungu mwenye kupashwa kuhukumu ulimwengu? naimbia, ee Bwana, huruma yako isiyokadirika.

**EKSAPOSTILARION**

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

**APOSTIKHA**

Msalaba wako umekuwa boma kwa sisi, ee Yesu Mwokozi wetu. Sisi waaminifu hatuna lakini matumaini ingine ila wewe Bwana uliyepigiliwa mwilini mwako pa hii na ukatupatia neema ya wokovu.

Kwa wale wenyi kukuogopa, ee Bwana, uliwapa alama ya Msalaba wako mheshimiwa. Katika hii ulishinda ufalme na nguvu za gehena na ukatuleta ku furaha ya zamani; na tena tunatukuza mapendo yako kwa ajili yetu na tendo lako la wokovu, ee Bwana mwenyezi na mwokozi wa roho zetu.

Ee Mashahidi Watakatifu, tunashangaa mashindano yenu, kwani, mulipovaa mwili usiyokufa, mulifukuza adui msiyeonekana; mumeteswa mateso kali zaidi bila woga mbele ya wazulumu; sasa mumepata kwa Kristu utukufu wenyi kustahili, yeye mwenyi kuleta neema ya wokovu ku roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **STAVROTHEOTOKION.**

*Os geneon en Martisin.*

wakati mama yako alipoona Msalaba ambapo ulitandazwa, misumari na mkuki uliyochoma ubavu, na machozi akalalamika: Ole wangu, ee mwanangu mpenzi! Namna gani watu wasiyo haki wamemuua huyu mwenyi kuleta uzima kwa wale wa ku Hadeze? Fufuka sasa kwa ajili ya furaha ya wale wenyi kukupenda.

## MU KAZI TATU MANGARIBI KATIKA SAUTI YA INE

**Wimbo ya Mitume.** *Os geneon en Martisin.*

Muliposhindana kwa moyo imara, mukamshinda adui, mukalindwa na silala ya Roho Mtakatifu na mukaharibu nguvu ya mashetani, kama mateka mukawanyanganya roho za wanadamu. Tunawaimbia hata milele, enyi Mitume watukufu wa Bwana.

Ee Bwana walipotandaza wavu wa imani mu alama ya Msalaba, Mitume wako watakatifu kumi na wawili wakavua mataifa yote sababu ya kuwaleta kwako na wakakausha mawimbi ya uchungu ya tamaa zetu; ndio maana, nakuomba, kwa maombezi yao yenyi kukupendeza kusikiliza, unitoshe ku shimo la zambi.

Tutukuzeni leo kwa nyimbo takaitfu Mitume Watakatifu kumi na wawili waliyochaguliwa na Mungu, tukimuimbia Petro na Paulo, Andrea na Yoane, Yakobo, Matayo, Simoni na Tomasi, Luka na marko, Filippo na Bartholomeo pamoja na Mitume weingine makumi saba.

**Wimbo ya Mtakatifu Nikolas**

Neema kimungu ya Roho Mtakatifu ikakupakaa myron takatifu, wewe arkiaskofu wa Myre katika Lukia ambaye fazila zikanukia dunia yote, na mwenye kufukuza uvundo wa tamaa zetu sababu ya manukato ya maombi yako, ee Nikola; na ndio maana tunaimbia na kutukuza na ibada makumbusho yako takatifu.

Taa yasipo mwisho, nyota ya ulimwengu kote yenyi kuangaa katika uwanda wa Eklezya, ee Nikola, unangaza dunia yote, unafukuza giza za hatari nyeusi, ukipoteza baridi ya kutokuamini sababu ya kutuletea utulivu na amani, kwa haki zako tunakuita mwenyi heri.

Katika ndoto za sasa na zilizopita uliokoa, ee Mtakatifu Nikola wale waliohatarishwa kuuawa bila haki, kwa rehema yako ukilinda kwa heshima kuu waaminifu wenyi kuomba msaada wako, ee rafiki ya Malaika na padri mtakatifu, mshindani wa Manabii na wa wenyi haki wa nyakati zote.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

*Os geneon en Martisin.*

Wewe ambaye tumbo lilimupokea Mungu ambaye fasi hata moja haiwezi kumpokea, na ambaye kwa kuwapenda watu akajifanya mtu kama sisi aliyepata kwako hali yetu ya ubinadamu mateso yangu, lakini kwa wepesi unihurumie na uniokoe, ukiniopoa ku tendo la upotevu la adui.

**APOSTIKHA**

Uliangaza kundi la Mitume, ee Kristu, kwa Roho yako Mtakatifu; kwa maombezi yao, ee Bwana, safisha pia uovu wa zambi zetu na utuhurumie.

Wafuasi wako wasipo kufunza Roho Mtakatifu aliwafanya kuwa walimu, na kwa uzuri wa maneno yao yenyi kusikilika katika lugha yote akapoteza kosa, ee Kristu Mungu wetu mwenyezi.

Zabihu mzima, sadaka za kiroho, ee Mashahidi Watakatifu, zabihu zenyi kumpendeza Bwana Mungu wetu, Kondoo wenyi kumjua Bwana wao Mtakatifu na mwenyi kuwajua ambao zizi halifunguliwa kwa mbwa-mwitu, ombeni kwa Mchungaji Mwema ili pamoja nanyi atupeleke pia ku fasi ya mapmziko.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Utuopoe ku hatari yote, ee Mama wa Kristu Mungu wetu, uliyezaa Muumba wa ulimwengu, ili tukuimbie daima: Salamu, Mulinzi wa roho zetu.

# MU KAZI INE ASUBUI KATIKA SAUTI YA INE

## KATHISMA YA KWANZA

Mitume wafalme na Walimu wa ulimwengu, ombeni kwa Rabi wa ulimwengu ili alete amani ku dunia na neema ya wokovu ku roho zetu.

*Takhi prokatalave.*

Ee Kristu, Mitume wako waliangaa kama mwana ulimwenguni, wanaangaza roho zetu na nuru ya mafundisho yako takatifu; katika wao uliondoa uwongo wa miungu ya uwongo, wanaangaza dunia na mafundisho ya imani. Kwa maombezi yao okoa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira, ujiharikishe kupokea maombi tunayokutolea; ee Bibi mtakatifu kamili, uyapeleke kwa Mwana wako na Mungu wetu. Tuliza huzuni ya wale wenyi kukimbilia kwako; tengua werevu wa mwovu na haribu ukali, wa adui mwenyi kushindana na watumishi wako.

## KATHISMA YA PILI

*Takhi prokatalave.*

Enyi Mitume watukufu, sauti yenu ilienea duniani kote, ikapofusha hekima ya hapa chini, na ikawaondoa wanadamu ku shimo ya kosa, inamuonyesha kila mwanadamu njia ya wokovu. Ni haki kweli tuwaite wenyi heri.

Ee Mwokozi, uliwachagua waafuasi wako duniani kama watangazaji wa imani, wakiwapeleka wanadamu ku maarifa ya Mungu; wanaangaza ulimwengu na miangaza ya neno lako, wakipanda kweli mbegu ya ibada, kwa maombezi yao okoa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Ee Malkia, sikiliza mtumishi wako ambaye roho yenyi huzuni inalalamika kwako; uniondolee zambi zangu hizi nyingi zaidi; kwani mchana na usiku ni wewe uliye ulinzi wangu imara; uniopoe ku gehena ya moto, ee Mzazi-Mungu na uniweke kuumbe kwa Mwana wako na Muumba wetu.

## KATHISMA YA TATU

*Takhi prokatalave.*

Ujiharikishe kutangulia, ee mwenyi heri padri Nikola, okoa watumishi wako ku hatari yenyi kututeswa na kutuegemezwa; kwa ajili ya deni unayo kwa Muumba Mungu wetu ujiharikishe kusaidia wale wenyi kukuomba na imani, ukiwapa msaada na ulinzi wako.

Mashahidi wako, ee Bwana, kwa ajili ya mashindano walioshindana walipokea kwako, Mungu wetu, taji ya milele, waliposukumwa na nguvu yako waliangusha wazalimu na kuondoa nguvu ya mashetani; kwa maombezi yao okoa roho zetu, ee Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Kwa maana katika viumbe vyote wewe umekaa juu, tunaweza kukuimbia kama inavyofaa. Ndio maana, ee Mzazi-Mungu, tunakuomba utufanyie hii zawadi ya kutuhurumia.

## EKSAPOSTILARION

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu).*

**APOSTIKHA**

Uliangaza kundi la Mitume, ee Kristu, kwa Roho yako Mtakatifu; kwa maombezi yao, ee Bwana, safisha pia uovu wa zambi zetu na utuhurumie.

Wafuasi wako wasipo kufunza Roho Mtakatifu aliwafanya kuwa walimu, na kwa uzuri wa maneno yao yenyi kusikilika katika lugha yote akapoteza kosa, ee Kristu Mungu wetu mwenyezi.

Ni heshimiwa, ee Bwana, lufu ya marafiki zako. Kwa upanga, moto ao kwa baridi wakatoa uzima wao katika matumaini ya kupata tuzo ya matendo yao, na kuvumilia kwao kukawaletea kwako, ee Mwokozi, neema wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Peke yako, ee Bikira Safi na Mtakatifu uliyezaa Mungu wetu, umuombe kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

## MU KAZI INE MANGARIBI KATIKA SAUTI YA INE

**Wimbo ya Usulubisho** *Edokas simiosin.*

Wakati viumbe vilikuona umesulubiwa, vikageuka na vikaogopa; inchi ikatikisika, ikahangaika, kwa woga pazia ya Hekalu ikapasuka, ee Neno mvumilivu, wakati waliyokutukana; mawe yakapasuka kwa woga na jua halikutoa miangaza yake, likakutambua wewe Muumba wake.

Deni ya Adamu wa kwanza aliyokopa tangu milele ikapasuliwa wakati walipochoma ubavu wako kwa mkuki; na tangu kufukuzwa kwao wanadamu, walipotakaswa kwa mawimbi ya damu yako, wakaanza kukulalamikia: Utukufu ku uwezo wako, ee Bwana, utukufu kwa kusulubiwa kwako kimungu, ee Yesu mwenyezi na Muumba wa roho zetu.

Namna gani kundi la watu wasiyo na sheria wanasubutu kukuhukumu wewe mwamzi wa milele ambaye zamani jangwani ukaleta sheria kwa Musa aliyemuona Mungu; tena namna gani hawakuogopa wakati waliona uzima wa milele amekufa Msalabani? Namna gani hawakushika moyoni mwao ya kama peke yako ndiwe Bwana na Rabi wa viumbe byote?

**Wimbo ya Mzazi-Mungu.**

Napepa kwa mapigo ya mashetani, wananisukumia ku shimo ya upotevu. Ee Malkia, unihurumie, unisabitishe pa mwamba wa fazila na zuia fitina ya waovu ili niweze kutimiza amri za Mwana wako na Mungu wetu na kupata hivi maondoleo ya zambi siku ya hukumu.

Naangukia mikononi mwa wanyanganyi wauaji na nilinyanganywa kwa nguvu vazi la milele la utukufu wa juu mbinguni; wamenijeruhi bila huruma na wameniacha mwenyi kuzimia pahali penye kulaaniwa. Ee Bikira Safi kamili, nakuomba, ujiharikishe, uninyoshee mkono wako na unisimamishe.

Ninapolala kitandani mwa uzembe na ninapopitisha maisha yangu katika uvivu, naogopa wakati wa kuondoka. Nyoka mbaya asipasue roho yangu kwa ukali wake mbaya! Na tena, ee Mzazi-Mungu na Bikira Mtakatifu, mbele ya mwisho ujiharikishe kuamusha toba rohoni mwangu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Jua na mwezi walipokuona umetundikwa Msalabani, ee mpenda-wanadamu, yote mbili ikaficha miangaza yao, ee Jua la haki, Yesu Kristu, na misingi ya dunia ikaogopa ukubwa wako; Mama yako kwa moyo wenyi kujehuriwa akakulalamikia: Utukufu ku huruma yako, ee hazina ya wema.

**APOSTIKHA**

Ee Kristu, ulitupatia Msalaba takatifu kama silaha isiyoweza kushindwa. Katika hii tunakutukuza, kama washindaji, mashambulio ya adui.

Ee Kristru, tunapokuwa daima na msaada wa Msalaba wako, tunaweza kuepuka ku wavu wa adui.

Ee Kristu Mungu wetu, unapotukuzwa katika makumbusho ya Watakatifu wako, kwa maombezi yao ututumie neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Usinililie, ee Mama, hata kama ukiona ametundikwa Msalabani Mwana na Mungu aliyetundika inchi pa maji na akawa Muumba wa viumbe vyote; kwani nitafufuka na kutukuzwa, na kwa nguvu yangu ya kimungu nitaharibu ufalme wa gehena nitapoteza nguvu ya hadeze na nitaopoa wafungwa wote ku uovu wake sababu ya kuwapeleka kwa Baba yangu, kwa mapendo yangu kwa ajili yao.

## MU KAZI TANO ASUBUI KATIKA SAUTI YA INE

### KATHISMA YA KWANZA

Umetukomboa ku laana ya Sheria kwa Damu yako heshimiwa; ulipigiliwa Msalabani na kuchomwa Mkuki, ukawa kwa wanadamu chemchem ya umilele; ee Mwokozi wetu, utukufu kwako.

Ewe Kristu Mungu, uliyeinuliwa kusudi Msalabani, uipe jamii ile jipya iliyo na jina lako, rehema yako. Uwafurahishe wafalme wetu waaminifu na nguvu yako, ukiwatunza na kushinda juu ya washindanao, wakifurahiwa kwa agano lako jipya, silaha, ya amani, alama isioshindika.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Bikira Mtakatifu alipoona sadaka aliyotolewa Rabi kwa kutaka kwake, kwa machozi na malalamikio akapaza sauti: Ee Mwanangu mpenzi, lufu gani ulichagua? Namna gani umesulubishwa Msalabani katika ya waovu wewe Jua la haki, Mungu wetu? Mwana mvumilivu, nakutukuza.

### KATHISMA YA PILI

Ujiharikishe kutangulia, ee Kristu Mungu wetu, mbele ya sisi kuwa watumwa wa maadui wenyi kukufuru na kutuegemeza; wale wenyi kutugombanisha ywapunguze kwa Msalaba wako, wajuwe nguvu ya imani ya kweli, kwa maombezi ya Mzazi-Mungu, peke yako mpenda-wanadamu.

Ulipigiliwa Msalabani sababu ya kutuita kati ya wapagani, ee Mpenda-wanadamu, ulipanua mikono kwa kutaka kwako na ukaitika ili ubavu wako uchomwe mkuki. Ee Mungu wa mapendo, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Bikira safi na mama ya Kristu Mungu wetu, upanga ulichoma moyo wako wakati uliona Mwana wako na Mungu wako Msalabani*:* Umuombe bila kuacha kwa ajili ya maondoleo ya zambi zetu.

**KATHISMA YA TATU**

Kwa mapendo yako yasipo mipaka, ulikufa Msalabani kwa kutaka kwako kwa ajili yetu na ulihukumiwa bila haki sababu ya kuopoa wanadamu ku hukumu na ku laana ya zamani; ndiyo maana, ee Neno, tunasujudu mbele ya Msalaba wako.

Leo, majeshi ya mbinguni wanapokumbuka Mashahidi washindaji wanakuja kuangaza moyo wa waaminifu na wanaangazisha neema ulimwenguni; kwa maombezi yao, ee Mungu mwenyezi, utupe neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Alipokuona umetukuzwa Msalabani, mama yako Mtakatifu, ee Neno la Mungu, akalia kwa umama na akasema: Hii ni mambo gani ya ajabu, ee mwanangu? Wewe uliye uzima wa ulimwengu namna gani unaweza kushuka ku mauti? Lakini kwa huruma yako unapenda kuwafufua wafu.

**EKSAPOSTILARION**

*(Angalia ku mwisho ya hii kitabu).*

**APOSTIKHA**

Msalaba wako umekuwa boma kwa sisi, ee Yesu Mwokozi wetu. Sisi waaminifu hatuna lakini matumaini ingine ila wewe Bwana uliyepigiliwa mwilini mwako pa hii na ukatupatia neema ya wokovu.

Kwa wale wenyi kukuogopa, ee Bwana, uliwapa alama ya Msalaba wako mheshimiwa. Katika hii ulishinda ufalme na nguvu za gehena na ukatuleta ku furaha ya zamani; na tena tunatukuza mapendo yako kwa ajili yetu na tendo lako la wokovu, ee Bwana mwenyezi na mwokozi wa roho zetu.

Ee Mashahidi Watakatifu, mumukuwa marafiki ya Malaika mulipomtangaza Kristu uwanjani, mulizarau furaha za hii dunia, mukishika kweli nanga ya imani, ninyi ni Chemchem ya kuponyesha ya Wazaifu*:* Ombeni daima kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Bwana, wakati Bikira Mama yako alipokuona umetundikwa Msalabani, akashangaa na akasema: Namna gani umepigiliwa Msalabani, ee Bwana mvumilivu na mwanangu mpenzi? Namna gani makafiri, ee Neno, walipigilia mikono na miguu yako misumari na kumwanga damu ya Mungu wetu.

## MU KAZI TANO MANGARIBI KATIKA SAUTI YA INE

*Ithelon dakrisin.*

Vunja, ee Bwana Mungu wangu, tamaa za moyo wangu zenyi kuzuru; ukivunja makao ya mwili wangu sababu ya kuifanya hekalu la Roho Mtakatifu, adui wa roho yangu atafanya zamu bure. Mbele ya kupotea kwangu kwa mwisho, ee Bwana, uniokoe.

Ee Bwana wa huruma, ulinipa adui kwa mafaa ya adibisho yangu kama kibanzi na zawadi yangu; uovu uliyo ndani yake unanisaidia lakini kama jaribu ambayo japo ni mbaya inaongoza ku mema. Mbele ya kupotea kwangu kwa mwisho, ee Bwana, uniokoe.

Ee Bwana, ulivumilia mateso na lufu kwa ajili yangu sababu ya kuniopoa, ee chemchem ya uzima, ku mateso na ku uharibifu wa mauti sababu ya kunifanya msiyeteswa kama zamani, ee Mwokozi, uniamushe kaburini humo zambi iliniweka na uniokoe mbele ya lufu ya milele kunikamata.

**Wimbo ya Mashahidi.**

Zabihu mzima, sadaka za kiroho, ee Mashahidi watakatifu, zabihu zenyi kumpendeza Bwana Mungu wetu, Kondoo wenyi kumjua Bwana wao Mtakatifu na mwenyi kuwajua ambao zizi halifunguliwe kwa mbwamwitu, ombeni kwa Mchungaji mwema ili pamoja nanyi atupeleke pia ku fasi ya mapumziko.

Ni heshimiwa, ee Bwana, lufu ya marafiki zako. Kwa upanga, moto ao kwa baridi wakatoa uzima wao katika matumaini ya kupata tuzo ya matendo yao, na kuvumilia kwao kukawaletea kwako, ee Mwokozi, neema wokovu.

Kwa deni munayo kwa Mwokozi, ee Mashahidi watakatifu, ombeni daima kwa ajili ya sisi waovu, mukituombea maondoleo ya zambi zetu na neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Nabii Daudi aliyekuwa Babu-Mungu kwa ajili yako, alikutabiri katika zaburi kwa yule aliyekufanya maajabu*:* Malkia anasimama ku mukono wako wa kuume. Kwa sababu Mungu alikuonyesha wewe mama muletaji-uzima, yeye aliyetwaa mwili toka wewe kwa mapenzi yake bila baba, kusudi aumbe mara ingine mufano yake, iliyoharibika kwa tamaa, na kupata kondoo alliyepotea mulimani, kumubeba ku mabega yake, na kumutoa kwa Baba, kwa kuiunganisha pamoja na Ezi za mbinguni kwa kutaka kwake, na kuokoa dunia, ee Mzazi-Mungu; yeye ni Kristu, mwenye kuwa na rehema kubwa zaidi.

**APOSTIKHA**

Ee Kristu Mungu wetu, unapotukuzwa katika makumbusho ya Watakatifu wako, kwa maombezi yao ututumie neema ya wokovu.

Ee Bwana Mpenda-wanadamu uliyepokea uvumilivu wa Mashahidi wako Watakatifu, pokea pia heshima ya nyimbo zetu, ukitupatia kwa maombezi yao neema ya wokovu.

Zabihu mzima, sadaka za kiroho, ee Mashahidi Watakatifu, zabihu zenyi kumpendeza Bwana Mungu wetu, Kondoo wenyi kumjua Bwana wao Mtakatifu na mwenyi kuwajua ambao zizi halifunguliwa kwa mbwa-mwitu, ombeni kwa Mchungaji Mwema ili pamoja nanyi atupeleke pia ku fasi ya mapumuziko.

**Nyimbo ya wafu**

Pamoja na roho za wenyi haki kamilifu, ee Mwokozi, pumzisha roho ya watumishi wako na uichunge hii mu uzima wa heri uliyo karibu nawe, ewe rafiki ya wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . . **THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, matumaini na ulinzi wetu, hatuogope fitina za adui, kwani unalinda roho zeru.

## MU POSHO ASUBUI KATIKA SAUTI YA INE

### KATHISMA YA KWANZA

*Sauti ya ine. Takhi prokatalave.*

Walipovaa silaha ya Msalaba wako, ee Kristu Mungu wetu, Mashahidi wako wakashinda uerevu wa adui; wakaangaa kama nyota, wakaongoza wanadamu; kwa wale wenyi kuwaomba na imani wanawaponyessha kwa maombezi yao, okoa roho zetu.

Mashahidi wako walipamba Eklezya kwa damu yao ulimwenguni kote*:* Inapovaa sufi na kitani, kwa kinywa yao, inakuimbia, ee Kristu Mungu wetu*:* Onyesha huruma yako kwa hawe watu walio wako, leta amani kwa watawala wetu wote na neema ya wokovu ku roho zetu.

Mashahidi wako, ee Bwana, kwa ajili ya mashindano walioshindana walipokea kwako, Mungu wetu, taji ya milele, waliposukumwa na nguvu yako waliangusha wazalimu na kuondoa nguvu ya mashetani; kwa maombezi yao okoa roho zetu, ee Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . .Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, kwa ajili yako, fumbo ya ficho na ambayo hata Malaika hawakujua ilifunuliwa kwa sisi duniani*:* Mungu amejifanya mutu bila kuchanganya hali zake mbili katika hii muungano, na kwa kutaka kwake aliteswa Msalabani kwa ajili yetu sababu ya kumfufua Adamu na kuokoa roho zetu ku mauti.

**KATHISMA YA PILI**

*Takhi prokatalave.*

Leo, kwa kuwakumbuka Mashahidi washindaji, majeshi ya mbinguni wanakuja kuangaza moyo wa waaminifu na wanaangazisha neema ulimwenguni; kwa maombezi yao, ee Mungu mwenyezi, utupe neema ya wokovu.

Ee Kristu Mungu wetu, kwa uwezo na wema wako leta mapumuziko ku roho za waaminifu waliyokuja kwako toka ku vitu visivyodumu, kwa maombezi ya Mzazi-Mungu, samehe makosa yao ya zamani, hurumia kazi ya mikono yako, ee peke yako mpenda-wanadamu.

Walipopita muda mfupi wa hii uzima, waaminifu wakakuja kwako, ee Bwana wa wema. Kwa wale uliyopatia mapumziko uwaweke kuume kwako siku ya hukumu bila kuangalia zambi walizotenda.

Umeonekana kuwa msaada wa waaminifu, kimbilio la wote na maombezi ya furaha; ee Bikira Mtakatifu na mchumba kimungu, onekana sasa kwa yule mwenyi kufa katika imani kuwa mpatanishi na mulango wa wokovu wenyi kuwaongoza ku uwanda kubwa ya Paradizo.

**EKSAPOSTILARION**

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu).*

**APOSTIKHA**

Ee Mashahidi Watakatifu, mumukuwa marafiki ya Malaika mulipomtangaza Kristu uwanjani, mulizarau furaha za hii dunia, mukishika kweli nanga ya imani, ninyi ni chemchem ya kuponyesha ya Wazaifu*:* Ombeni daima kwa ajili ya roho zetu.

Ee Mashahidi Watakatifu, tunashangaa mashindano yenu, kwani, mulipovaa mwili usiyokufa, mulifukuza adui msiyeonekana; mumeteswa mateso kali zaidi bila woga mbele ya wazulumu; sasa mumepata kwa Kristu utukufu wenyi kustahili, yeye mwenyi kuleta neema ya wokovu ku roho zetu.

Ee Bwana, lufu marafiki zako ni heshimiwa*:* Kwa upanga, kwa moto ao kwa baridi, walitoa uzima wao katika matumaini ya kupata tunzo ya matendo yao, na uvumilivu wao uliwafaidia kwako, ee Mwokozi, neema ya wokovu.

**Wimbo ya wafu.**

EeBwana, kwa wema wako pumzisha watumishi wako katika uwanja wako humo wanapumzika watakatifu wote.

Utukufu kwa Baba. . .

Wapi tamaa za dunia? Wapi wadanganyo yenyi kupita? Wapi zahabu na feza na makelele ya Watumishi? Hii wote ni uvumbi na bure; njioni tumuimbie Mfalme msiyekufa*:* Bwana, leta mema yako ya milele na uwape marehemu wetu mapumziko katika heri ya milele.

Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Peke yako Bikira Safi na Mtakatifu uliyezaa Mungu wetu, umuombe kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Elezo: *Kama kuna Alliluya, tunaimba ku masifu nyimbo za mashahidi zenyi kutangulia hapa juu, na kama Apostikha tunaimba Mifano (Prosomia) yafwatayo:*

Fumbo ya woga ni ile ya lufu! Namna gani roho yetu inaondolewa mwilini mwake; inatengana na umoja wenyi kulingana? Namna gani mapatano ya kweli inavunjwa kwa mapenzi kimungu? Tena tunakuomba leta mapumziko kwa marehemu waaminifu katika hema ya watakatifu wako, ee mpenda-wanadamu na chemchem ya uzima.

*Shairi:* Heri wale uliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe, ee Bwana.

Kwa waaminifu lufu ni usingizi tangu ulipumzika kaburini, wewe Rabi wa ulimwengu wote, na kuharibu ufalme wa mauti; tena tunakusihi*:* Leta mapumziko kwa marehemu waaminifu katika hema ya Watakatifu, ee mpenda-wanadamu na chemchem ya uzima.

*Shairi:* Na makumbusho yao ni ya milele.

Katika wewe tumepata haki na utakatifu, na ukombozi wa roho zetu; unatuongoza kwa baba wenyi kusubutishwa na kukombolewa kwani ulichukua malipizi ya zambi zetu; na sasa tunakuomba*:* Leta mapumziko kwa marehemu waaminifu katika nuru na furaha, ee Bwana; mfazili na Mwokozi wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Mufuatana na unabii, ee Bikira, tunakutukuza kama Mzazi-Mungu*:* Ni Mungu ulizaa kwa namna ya ajabu; amejifanya mutu tumboni mwako sababu ya kutukomboa ku zambi iliyotufunga; umuombe tena sasa aangaze marehemu Watumishi wako kwa nuru yake.



# KIPANDE CHA SAUTI YA TANO

## MU POSHO MANGARIBI

**Wimbo ya Ufufuo.** *Sauti ya tano*

Kwa Msalaba wako muheshimiwa, ee Kristu, ulipatiya shetani haya, na kwa ufufuo wako ulifanya uchungu wa zambi kuwa bure, na ulituokoa toka milango ya mauti; tunakutukuza, ee Mwana wa pekee.

Huyu anayeleta ufufuo ku ukoo wa watu, alipelekwa kama kondoo kuchinjwa; wafalme wa hadeze wakatetemeka mbele yake, na milango ya maumivu iliyanyuliwa; kwani Kristu, Mfalme wa utukufu, aliingia, akiwaambia wafungwa: Tokeni, na wale walio katika giza, mujionyeshe.

Ajabu kubwa! Muumba wa wasioonekana, akiteswa kwa mwili kwa ajili ya kupenda wanadamu, akafufuka sawasawa na musiyekufa. Kujeni wazao wa mataifa, tumuabudu huyu; kwani kwa wema wake tukiondoshwa toka udanganyifu, tumefundishwa kuimba Mungu mmoja, katika aina tatu.

**Wimbo Anatolika.**

Tunautoa kwako uabudu wa mangaribi, ewe Nuru isiyomwisho uliyeangaza dunia kama katika kioo kwa mwili katika mwisho ya milele, na ulishuka mupaka Hadeze, na kule ulizambalisha giza, ukaonyesha nuru ya ufufuo kwa mataifa; Bwana muletaji-nuru, utukufu kwako.

Tumusifu Kristu, mkubwa wa wokovu wetu; kwani wakati huyu alipofufuka katika wafu, dunia imeokolewa katika udanganyifu, kundi la Malaika wanafurahi, udanganyifu wa mashetani unatoka; Adamu aliyeanguka amefufuka, na shetani ameharibiwa.

Askari walinzi waliambiwa kwa wavunja-sheria: Mufiche ufufuo wa Kristu, na mukamate feza, na museme: Wakati tulipolala mufu aliimbwa toka kaburi. Nani aliona, nani alisikia siku moja watu wanaimba mufu? Na tena mwenye kupakaliwa na manukato na uchi, mwenye kuacha manguo yake ya maziko ndani ya kaburi? Musidanganyiwe, Wayuda; mufundishwe maneno ya manabii, na mujue ya kama kweli huyu ni Mukombozi wa dunia na mwenyezi.

Bwana, uliyenyanganya Hadeze, na ulishinda mauti, Mwokozi wetu, uliyeangaza dunia, kwa Msalaba wako muheshimiwa, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Katika Bahari Nyekundu, wakati moja mufano wa Bibi-arusi musiyeolewa ulijionyesha. Kule Musa alikuwa mugawanyi wa maji, hapa Gabrieli alikuwa mutumishi wa ajabu. Wakati ule Israeli alipita vilindini bila kulowanishwa, sasa Bikira alizaa Kristu bila mbegu; Bahari kisha kupita kwa Israeli ilibaki isiyowezekana kupita; Musiyeolewa kisha kuchukua Emmanueli, alibaki bila kuharibiwa. Mungu ndiwe uliye na uliyekuwako, na uliyefunuliwa sawasawa na mutu, utuhurumie.

### APOSTIKHA

Tunakutukuza kwa sauti ya nyimbo, ee Kristu Mwokozi, mwenye kutwaa mwili bila kugawanyika toka mbingu; kwani ulikubali Msalaba na lufu, kwa ajili ya ukoo wetu, kwa kuwa wewe ni Bwana mpenda-wanadamu; ukinyanganya milango ya Hadeze, ulifufuka katika siku tatu kwa kuokoa nafsi yetu.

Wakati ubavu wako ulipochomwa, ee Muletaji-uzima, ulichirizika mitoni ya usamehe, ya uzima na ya wokovu wa wote; tena ulikubali lufu kwa mwili, ukituletea uzima usiyokufa; na wakati ulipokaa kaburini, ulituopoa, ukitufufua pamoja nawe katika utukufu sawasawa na Mungu; kwa hii tunapaza sauti: Bwana mpenda-wanadamu, utukufu kwako.

Usulubisho wako na kushuka kwako katika Hadeze ni mambo ya ajabu, ee mpenda-wanadamu, kwani ukimunyanganya, na ukifufua pamoja nawe wafungwa toka zamani katika utukufu sawasawa na Mungu, ulifungua Paradizo, na uliwastahilisha kuipokea; kwa hii utupe usamehe wa zambi zetu, sisi tuliyosifu ufufuo wako wa siku tatu, na utustahilishe tuwe wakaaji wa Paradizo, kwa kuwa wewe peke yako ni mwema.

Wewe mwenye kupokea mateso katika mwili kwa ajili yetu, na ulifufuka siku ya tatu katika wafu, utuponyeshe toka tamaa ya mwili wetu, na utufufue toka makosa ya hatari, ee mpenda-wanadamu, na utuokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Bikira uheshimiwa kamili, uko hekalu na mulango, nyumba na kiti cha Mufalme; kwa wewe Kristu, Bwana na Mukombozi wangu, alifunuliwa kwa wale waliokaa katika giza; eko jua la haki, akitaka kwangaza wale walioumbwa kwa mufano wake kwa mikono yake; kwa hii, mwimbiwa kamili, kwa sababu uko na uhodari ya umama mbele yake, upatanishe bila kuacha, kwa kuokoa nafsi yetu.

### APOLITIKION

Neno lasipo mwanzo pamoja na Baba na Roho, huyu alizaliwa kwa Bikira kwa ajili ya wokovu wetu; basi, waaminifu, tumwimbie na tumwabudu; kwani mapenzi yake katika mwili, alipanda juu ya Msalaba, akavumilia lufu, na alifufua wafu, katika ufufuo wake muheshimiwa.

### THEOTOKION

Salamu, mulango wa Bwana usioweza kupitwa; salamu, ukuta na kivuli cha wale waliokimbilia kwako; salamu, kivuko bila kutikisika, na musiyeolewa, uliyezaa katika mwili Muumba na Mungu wako; usiache kupatanisha kwa ajili ya wale walikuimbia, na walioabudu Mwana wako.

## SIKU YA MUNGU ASUBUI KATIKA SAUTI YA TANO

### KATHISMA YA KWANZA

Kwa mashairi na nyimbo zetu tusifuni Msalaba mweshimiwa wa Bwana, tutukuzeni Kaburi, tutukuzeni Ufufuo wako takatifu, kwani Mungu wetu amewafufua wafu kaburini, akanyanganya ufalme wa mauti na kuharibu nguvu ya shetani, nuru yake ikasimama juu ya wafungwa kuzimuni.

Utukufu kwa Baba...

Ee Bwana, ulihesabiwa kati ya wafu, wewe uliyeua mfalme wa mauti, uliwekwa kaburini, wewe mwenye kwacha makaburi tupu; duniani kaburi yako ikalindwa na maaskari, kuzumuni ukawafufua wafu walioyolala tangu milele. Ee Mungu mwenyezi ambaye ulimwengu hauwezi kuzungusha, ee Bwana, furaha yetu, utukufu kwako.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Salamu, mlima takatifu aliyopanda Bwana, salamu, kichaka kisipoteketezwa, salamu, kilalo cha dunia cha kwenda kwa Mungu, wewe mwenyi kupoleka ku uzima wa milele, salamu, ee Bikira msiyeolewa uliyezaa wokovu wa roho zetu.

**KATHISMA WA MBILI.**

Ee Bwana, kisha ufufuo wako siku ya tatu, wakati Mitume walisujudu mbele yako, Petro akalalamika: Wanawake walikuwa na nguvu ile mimi sikuwa nayo! Munyanganyi akakutambua kama Mungu lakini mimi nimekukana. Utaniita mfuasi kisha hii yote? Ao utanirudisha ku nyavu zangu? Pokea toba yangu, ee Mungu wangu na uniokoe.

Utukufu kwa Baba...

Ee Bwana, makafiri walikusulubisha Msalabani katikati ya wanyanganyi, walichoma ubavu wako kwa mkuki; ee Mungu wa mapendo, uliitika kuzikwa kaburini, wewe uliyevunja milango ya Hadeze, na ukafufuka siku ya tatu; wanawake walikuja wapezi kukuona, wakawatangazia Mitume Ufufuo. Ee Mungu aliye-juu ambaye Malaika wanaimbia, umetukuzwa, ee Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote..**THEOTOKION**.

Bibi auri asiyeolewa na mzazi-Mungu aliyebadilisha mateso ya Eva kuwa furaha, sisi waaminifu tunakuimbia na tunasujudu kwako; kwa maana ulituondoa toka laana ya zamani, ee Bikira Mtakatifu kamili mwenye kustahili nyimbo zetu, umuombe kwa ajili ya wokovu wetu.

Elezo*: Kisha waimbaji wanaimba Mahimidi ya Ufufuo na kisha msomaji anasoma Ipakoi:*

Walipoogopeshwa kwa mwangaza wa Malaika, walipoangazwa kwa nuru ya ufufuo, Mirofori wakaenda mbio kwa Mitume wakasema: Tangazieni mataifa yote habari njema ya Ufufuo wa Bwana wenye kutenda hapa chini maajabu ya nuru na kutupatia neema kubwa.

## ANAVATHMI.

*Sauti ya tano.*

**ANTIFONON WA KWANZA**

Ee Mwokozi, katika taabu yangu nakuimba kama Daudi, okoa roho yangu ku ulimi mbaya.

Kwa wao wenye kukaa jangwani uzima ni heri: Wanaruka pa mabawa ya mapendo ya umungu.

Utukufu kwa Baba...sasa na siku zote...

Ni Roho Mtakatifu mwenyi kusabitisha ulimwengu wenyi kuonekana na usiyeonekana, akishika uwezo kubwa, ni mmoja kweli wa Utatu Mtakatifu.

**ANTIFONON WA PILI.**

Ee roho yangu, tuinuke mlimani, pahali patakapotoka msaada.

Ee Kristu, mkono wa kuume ukae pa mimi kama bawa na unilinde ku njia yote mbaya.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...

Kwa Roho Mtakatifu tuungame umungu tukisema: Ndiwe uzima mapendo, akili, nuru, Mungu wa wema unayetawala milele.

**ANTIFONON WA TATU.**

Wakati waliponiambia: Tuingieni viwanjani mwa Bwana, nilipandisha maombi yangu kwa yeye, mwenye kujazwa na sherehe na furaha.

Katika nyumba ya daudi munafanyika siri ya ajabu, kwani moto unateketeza wazo mbaya.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...

Ni Roho Mtakatifu mwenyi kuleta uzima ku ulimwengu, kwani anajaza kiumbe yote na uzima kama, Baba na Neno.

**PROKIMENON.**

Fufuka, Bwana Mungu wangu, kwani unatawala kwa milele. *(mara tatu).*
Kituo: Nataka kukushukuru, ee Bwana, moyoni mwangu na kutangaza maajabu yako.

**KANUNI YA UFUFUO YA YESU KRISTU**

**MWIMBO YA KWANZA**

**IRMOS:** Farasi na wapanda farasi wakaangushwa katika bahari Nyekundu kwa huyu mwenyi kuharibu mashindano, Kristu mwenyi kunyanyua mikono yake, Mwokozi anayetukuza Israeli wakati anapoimba wimbo wa ushindi.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Ee Kristu, Sinagogi ubebaji-miiba ya Waebrania, alipokataa mapendo yote ya umama kwa ajili yako, akakuvika taji la miiba, wewe mfazili uliyeopoa mkubwa wa uzao wetu ku mimea ya zambi.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Ee chemchem ya uzima, kwa kuniondoa kuzimuni huko nilikoanguka, uliinamia huko bila kuangukiamo; ulipovumilia bila huzuni uharibifu wangu wa kuoza, ukanipakaa manukato nzuri ya umungu wako.

Mtakatifu kamili ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Huzuni na laana zimeondolewa, kwani Mujaliwa-neema, Bikira mbirikiwa ametokeza furaha ya waaminifu, amenchukua Kristu kama ua, yeye aliye baraka ya dunia na mipaka yake.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Huyu aliyejiachilia kupigiliwa mwilini Msalabani na aliyeopoa ku laana ya zamani mwanadamu aliyeangukwa na muti, tumwimbie kama peke yake ni mstahili wa nyimbo zetu, kwani amevaa utrukufu.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Kristu aliyefufuka katika wafu na kaburini sababu ya kusimamisha mwanadamu mwenyi kuanguka na kumukalisha karibu ya Baba mbinguni, tumuimbie kama peke yake ni mstahili wa nyimbo zetu, kwani amevaa utukufu.

Mtakatifu kamili ee Mzazi-Mungu, utuokoe. **THEOTOKION,**

Ee Mzazi-Mungu na Bikira Mtakatifu kamili, Mungu aliyepata mwili tumboni mwako, bila kuacha Baba mbinguni, umuombee daima ili aokoe ku hatari yoyote wale aliyeumba kwa mkono wako.

## KANUNI YA MZAZI-MUNGU.

**IRMOS:** Farasi na wapanda farasi...

Mtakatifu kamili ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Ee Bikira na Mama Mtakatifu kamili, Nuru alipokaa ndani yako Kristu akaeneza duniani nuru ya umungu wake wa kuangaa: Umuombee aangaze wote wale wenyi kukuimbia.

Mtakatifu kamili ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Ulipopambua na nuru ya fazila zako, ee Bikira Mtakatifu kamili na kujazwa na neema, kwa mwanga wa Roho Mtakatifu ukapata ukuu wenyi kuangaa. Huyu mwenyi kuvika ulimwengu na uzuri wake.

Mtakatifu kamili ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Ku Sinai kichaka kilichotangulia zamani kukuonyesha hakikuteketezwa kwa moto: Ulikuwa Bikira wakati ulipozaa na ulikaa Bikira, ee Mama, katika fumbo isiyosikilika.

## MWIMBO YA TATU

**IRMOS:** Ulikaza dunia kadiri ya matengeneo yako na japo uzito wake ukaitungika imara. Sabitisha Eklezya yako, ee Kristu, pa mwamba imara wa amri zako, kwa wema wako na mapendo yako kwa ajili ya wanadamu.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Ee Kristu, walikupa nyongo, wale walionyonya asali ya mwamba wakati uliyowafanyia maajabu jangwani; na kwa kukosa kwao shukrani, pahali pa manaa wana wa Israeli wakakunywisha siki!

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Zamani, wale waliomueka Kristu uzima wetu kaburini wakalindwa na wingi la nuru; lakini alipofufuka kwa kutaka kwake, akawapa waaminifu nuru chini ya kivuli cha siri alipowafunika Roho Mtakatifu.

Mtakatifu kamili ee Mzazi-Mungu, utuokoe. **THEOTOKION,**

Bila kujua Bwana ukawa mama wa huyu Mungu ambaye ndani yake munangaa nuru ya baba isiyoharibika; haukujua uchungu wa Mama wazazi, na kwa sababu ulizaa Neno aliyejifanya mtu, kwa imani ya kweli tunakuita Mzazi-Mungu.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Ee Kristu, uliamka kaburini sababu ya kuwaokoa ku uvumbi wa mauti, wewe chemchem ya uzima, wale wenyi kuimbia kusulubiwa kwako kwa kutaka.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Ee Kristu, Myroforo wakajiharikisha sababu ya kupakaa manukato mwili wako takatifu, lakini hawakukupata, wakarudi na wakatukuza ufufuo wako takatifu.

Mtakatifu kamili ee Mzazi-Mungu, utuokoe. **THEOTOKION,**

Ee Bikira Safi, umuombee daima Huyu aliyezaa tumboni mwako ili awaokoe ku upotevu wote wale wenyi kukuimbia kama Mzazi-Mungu.

**KANUNI YA MZAZI-MUNGU.**

**IRMOS:** Ulikaza dunia....

Mtakatifu kamili ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Mungazi ambapo aliye-Juu anashukia mpaka kwa sisi sababu ya kutengeneza hali ya kuharibika. Ni hivi, ee Bikira, umeonekana kwetu, kwani ni kwa ajili yako Mungu Mwema kamili amepatikana kati yetu.

Mtakatifu kamili ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Ee Bikira Mtakatifu iliyotangulia kukusudiwa, iliyojulikana mbele ya nyakati kwa Munmgu mwenyi kujua vyote, kwa nyakati hizi za mwisho inafunuliwa tumboni mwako, ukipokea utimizo wake.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...

Ee Bikira Mtakatifu kamili, hukumu ya laana ya zamani imefutwa kwa upatanisho wako kimungu; kwani Bwana ameonekana katika wewe, peke yako pambo la wanadfamu, na kwa wema wake kubwa anawamwangia wote baraka.

**KONTAKION**

Ee Mwokozi wangu mwenyezi, ulivunja milango ya Kuzimuni huko ulikoshuka sababu ya kuwafufua wafu, ee Muumba, na uliharibu uchungu wa mauti, Adamu ameopolewa ku laana, na sisi, ee Bwana, tunakulalamikia, kwa mapendo yako kwa wanadamu, utuokoa.

**NYUMBA (IKOS)**

Wanawake waliposikia maneno ya Malaika, wakaacha kulia, walipofurahi kwa woga wakaona ufufuo wako; na tazama Kristu alipojongea, akawaambia: Muwe na moyo, furahini, maana nimeshinda dunia na nimewaokoa wafungwa; jiharikisheni kuwapasha Wafuasi habari ya kama nimewatangulia ku Galilea sababu ya habari watakaotangaza. Na sisi, ee Bwana, tunakulalamikia: Kwa mapendo yako kwa wanadama, utuokoe.

## MASIFU

Bwana, wakati kaburi ilipotiliwa muhuri kwa wavunja-sheria ulitoka katika kaburi, sawa ulizaliwa kwa Mzazi-Mungu; Malaika wako wasiyo-mwili hawakujua namna gani ulitwaa mwili; Askari waliokuchunga, hawakusikia wakati gani alifufuka; kwa sababu hii mambo ya ajabu ilifichwa kwa wenye kutafuta; lakini miujiza hii zimeonekana kwa wenye kuabudu siri kwa imani na wanaoimba: Uturudishie shangwe na rehema kubwa.

Bwana, ukivunja mapingo ya milele, ukikata minyororo, ulifufuka toka kaburi, ukiacha sanda, kusudi ya kuishuhudia kweli maziko yako ya siku tatu; na ulitangulia kwa Galilaya, mwenye kulindwa katika pango. Rehema yako ni kubwa, ee Mwokozi msiyesikilikwa! Utuhurumie.

Bwana, wanawake walienda kwa haraka kaburini, kusudi wakuone, ewe Kristu, uliyeteswa kwa ajili yetu; na wakifika, walikutanisha Malaika mwenye kukaa juu ya jiwe, lenye kufingirishwa kwa sababu ya woga, naliwapazia sauti, akisema: Bwana alifufuka; museme kwa Wanafunzi, ya kama alifufuka katika wafu, mwenye kuokoa nafsi yetu.

Bwana, kama vile ulitoka japokuwa kaburi imefungwa, vivyo hivyo uliingia wakati milango ilipofungwa, na ulionekana mbele ya Wanafunzi wako, kwa kuwaonyesha mateso ya mwili wako, uliyokubali, ee Mwokozi muvumilivu; sawa na mutu, muzaliwa wa ukoo wa Daudi, ulivumiulia mapigo; lakini sawasawa na Mwana wa Mungu, uliopoa dunia. Rehema yako ni kubwa, ee Mwokozi msiyesikilikwa! Utuhurumie.

Bwana, mfalme wa milele, Muumba wa vyote, mwenye kukubali kwa ajili yetu katika mwili usulubisho na maziko, kwa kutuopoa sisi wote toka Hadeze, wewe ni Mungu wetu; hatumujui mwengine ila wewe peke yako.

Bwana, nani atakayehadisia maajabu yako ya nuru kabisa? Ao nani atakayejulisha siri ya ajabu? Kwa maana ukijifanya mtu kwa ajili yetu, kama ulivyotaka, ulionyesha uwezo wako kwa mamlaka; kwa sababu kwa Msalaba wako ulifungua Paradizo mbele ya munyanganyi, na kwa maziko yako ulivunja mapingo ya Hadeze, na kwa ufufuo wako uliwinisha ulimwengu. Ewe mwenye rehema, utukufu kwako.

Wanawake mabebaji-manukato, asubui mapema wakishika kaburi yako, walitafuta kupakaa manukato, ewe Neno na Mungu msiyekufa; na wakati waliposikia maneno ya Malaika, walirudi kwa furaha, kusudi wajulishe wazi kwa Mitume, ya kama ulifufuka, Uzima wa wote na unaleta duniani usamehe na rehema kubwa.

Wachungaji wa kaburi yenye kupokea Mungu, walisema kwa Wayuda: Namna gani shuri yenu ilikuwa mawazo ya bure? Munachoka bure kupima kuchunga huyu msiyeweza kufungwa; mukitaka kuficha Ufufuo wa Msulubiwa, mulikionyesha wazi. Ee, namna gani mutanguzo wenu ulikuwa mawazo ya bure! Sababu gani munafikili kuficha hii isiyofichwa? yafazali mutusikilize, na mupate kuamini kwa kweli ya jambo. Malaika kama umeme akishuka toka mbinguni, alifingirisha jiwe; kwa ajili ya hii tulikuwa kama wafu kwa woga; na kwa sauti kunwa alisema kwa wanawake wabebaji-manukato wenyi mioyo mikuu: hamwone lufu kwa wachungaji, na upasuko wa muhuri, na kuwa tupu Hadeze? kwa nini munatafuta Yeye kama mufu, aliyeharibu uwezo wa hadeze, na aliyevunja uchungu wa mauti? Mwende kwa haraka na mupashe habari njema ya ufufuko kwa Kweli alifufuka Bwana mwenye kuwa na rehema kubwa.

Utukufu kwa Baba...**EOTHINON**
*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu).*

Sasa na siku zote...Mbarikiwa ukupita, ewe Mzazi-Mungu...

**DOKSOLOGIA KUBWA**

## SIKU YA MUNGU MANGARIBI KATIKA SAUTI YA TANO

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.** *Kheris askitikon.*

Ole wangu, ee Mungu wa rehema na Bwana wangu, nilichokoza hasira yako; ee Kristu, mara ngapi, nimeahidi kuongoka na kwa upumbafu wangu nilidanganyika ku kiapo changu. Ya kwanza, nimechafua vazi nyeupe la ubatizo wangu, bila kuangalia agano langu kwako; kisha

nilivunja hii agano yapili nilikufanyia mbele ya Malaika na ya watu wakati nilipovaa vazi la huzuni; lakini wewe Mwokozi, mbele ya mwisho unihurumie na uniokoe.

Ee roho maskini, utasema nini wakati wa hukumu? Nani atakuokoa ku hukumu ya haki, ku moto wa milele na ku namna yote ya mateso? Hakuna hata mmoja, kama haupate fazili ya Bwana wa huruma ukikataa matendo yako mbaya sababu ya kuishi namna yenyi kumpendeza Bwana, ukilia kila siku juu ya zambi nyingi unazotenda kila wakati kwa matendo , kwa maneno, kwa mawazo na umuombee Kristu akupe maondoleo kamili ya zambi zako.

Ee Mwokozi, tabia mbaya ya zambi isinishinde! Shetani asinitawale daima akinipiganisha wala kunitiisha ku utumwa wake. lakini uniondoe ku uzulumu wake wa kuuzi na ku giza wa azabu; ee mpenda-wanadamu, unitawale fanya ili mimi wote niwe wako, ee Neno na niishi kadiri ya mapenzi yako, ili katika wewe nipate mapumziko, rehema, maondoleo na neema ya wokovu.

**Wimbo ya Malaika.**

Ee Malaika Watakatifu Wakuu, tamaa mbaya zinanizulumu, zinapofusha macho ya moyo wangu na zinanizuia kuona njia za wokovu; napotea ninapotembea na natelemuka katika mashimo ya Hadeze, lakini wakati ninapokumbuka miujiza yenu, napona ku ubaya wote. Naweza sasa kupata fazili yenu! Jiharikisheni kuzima moto wa tamaa zangu, mukiniondolea mateso yangu na mukiniongoza ku nuru ya wokovu.

Ee Malaika Watakatifu Wakuu, muovu alikuwa na utukfuu uleule kama ninyi wakati zamani alipokuwa mmoja wenu akiitwa kwa jina la Luciferi; lakini adui mbaya akaangushwa duniani na akatupwa gizani, sasa ananisukuma kuharibu pamoja naye sura ya Muumba ambayo nilitukuzwa nayo; lakini kama nimeanguka, Kristu ameniinua; muonekane basi kuwa walinzi wangu na wasimamizi wangu, mukiombea roho yangu maskini maondoleo ya zambi na neema ya wokovu.

Kwa maana niliumbwa kwa mfano wa Mungu na kupokelewa kati yenu, sikupashwe kuanguka wote nu utumwa wa adui! Lakini chini ya uongozi na mlaanifu sikuwafuasa ninyti, nilivunja amri na nikanguka ku utukufu wa Muumba, na tazameni nakuwa mutumwa, ee Malaika Watakatifu wakuu wa Bwana; munapoona nimezunguka na shimo ya tamaa, munipe mkono kwa kuniongoza mu njia ya mbingu ili kwa maombezi yenu nipate wokovu na utukufu wa uzuri wangu wa zamani.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION.**

Nazama katika giza ya mateso, unitumie nuru, ee Bikira na Mama uliyepata mimba na kumzaa mwilini Nuru ya ukweli; uniondoe kuzimuni ya kutokuamini, sabitisha hatua zangu pa mwamba wa uzima wa kweli, taja ku hukumu mashetani wenyi kuniashambulia bila kupumzika; ujiharikishe kutuliza mateso ya moyo wangu, wewe matumaini ya mipaka ya ulimwengu mwenyi kuleta ku dunia neema ya wokovu.

**APOSTIKHA**

Ee Bwana, siache kutenda zambi, nasahau mapendo uliyonizungusha*:* ponyesha ugumu wa moyo wangu; peke yako Mungu wa wema, unihurumie.

Ee Bwana, sina hata woga juu yako lakini natenda maovu; mtu gani haogopi mwamzi ku korti? Mgonjwa gani akitamani kupona, anasirikisha mganga wake kama mimi? Ee Bwana mvumilivu na mwenyi kujaa mapendo, tazama uzaifu wangu na unihurumie.

Ee Mashahidi wakuu muliyozarau mema ya hii uzima sababu ya kupambana vema na mateso, hamukuzeka katika matumaini yenu ya heri, lakini kwa uriti mukapokea ufalme wa

mbinguni; na kwa sababu muna uwezo wa kumdai Mungu mwema, mumuombe amani ya dunia na neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION.**

Ni fumbo kubwa na ya ajabu! Wa milele anatwaa mwili na Mama yake anakaa Bikira hata kisha kuzaa, kwani yeye ni Mungu, yuhu aliyeitwa mwili tumboni mwake; tumulalamikie pamoja na Malaika na tumuimbie: Ndiwe Mtakatifu, ee Kristu Mungu wetu, wewe uliyejifanya mtu kwa ajili yetu, ee Bwana, utukufu kwako.

## MU KAZI MOJA ASUBUI KATIKA SAUTI YA TANO

### KATHISMA YA KWANZA

Ee roho yangu, wakati atakapokaa mwamzi na Malaika watakapokuwa huko, kwa sauti ya baragumu na mbele ya tanuru ya moto utafanya nini wakati utakapopelekwa ku hukumu? Hapo matendo yako ya giza yataonekana, hapo mawazo yako ya siri yatastakiwa; mbele ya mwisho umwambie Kristu Mungu wetu*:* Wewe mwenye kusoma mioyo unihurumie mimi muovu.

*Shairi:* Ee Bwana, usinihamakie kwa kasirani yako, wala usiniazibu kwa gazabu yako.

Ee roho yangu, vitu vya hapa chini vinadumu muda mfupi tu, vila vya Juu-mbinguni vinakaa milele, naona korti, mwamzi amekaa juu kiti chake naogopa kuhukumiwa; ee roho yangu, tubu mbele ya mwisho. Hukumu hai takuwa na huruma.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

*Ton sinanarkhon Logon.*

Ulinzi usiyoweza kushindwa matumaini imara na ya kweli, bandari na boma la mwenyi kukukimbilia wewe, ee Mama Mtakatifu na Bikira daima, pamoja na Malaika umsihi Mwana wako na Mungu wako alete amani duniani, rehema na neema kubwa.

### KATHISMA YA PILI

Tukesheni ili tuende kukutana na Kristu na vyombo vyetu vyeyi kujaa mafuta na taa zetu zenyi kuwaka kusudi tuweze kuingia katika nyumba yake ya arusi; kwa sababu mbele ya milango yenyi kufungwa nu bure tutamulalamikia Mungu, unihurumie.

Ninapolala kitandani mwa zambi zangu, sina na matumaini ya kuokolewa; usingizi na uzaifu zinaahidia roho yangu azabu, lakini wewe, ee Mungu uliyezaliwa kwa Bikira, uniunue ili nikuimbie: Ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Uliye Mtakatifu kuwashinda Wakeruvi, uliye Juu zaidi kuliko mbingu, ee Bikira mstahili kamili wa nyimbo zetu, wakati tunapokutambua kweli kama Mzazi-Mungu, tunapata wokovu japo makosa yetu na ulinzi katika majaribu; usichoke kutuombea, ewe ngome la wenyi mauti tena makimbilio ya roho zetu.

### KATHISMA YA TATU

Naogopa Korti ya ajabu na hukumu ya kweli ya Mwamuzi, kwani zamiri yangu inanishitaki bila kupumzika; nilipoishi katika uzaifu tazama nashikwa na woga; kwa maombezi yenu takatifu muniokoe ku moto wa milele, enyi Malaika Takatifu wakuu, walinzi wa waaminifu.

Leo imeangaa makumbusho ya mashahidi na mbingu ikaongezaka mwangaza wake: Malaika wanashangilia pamoja nasi kama wanadamu duniani; Mashahidi wanamuomba Mungu ili ahurumie roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Gabrieli alikuletea na ajabu duniani, Salamu ya mbinguni, kwani alipomwona Muumba wa Malaika amejifanya mtu tumboni mwako, akaimba wimbo wa shangwe kwa heshima yako, sababu ya kuwafundisha wenyi mauti ya kwamba peke yako, ee Bikira, umeonekana kwa watu wote kama asili ya furaha yao.

### EKSAPOSTILARION YA SIKU

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

### APOSTIKHA

Ole, wangu! Tazama nafanana na mtini usiyozaa matunda! Naogopa laana na shoka, lakini wewe mtunza-bustani wa mbinguni, ee Kristu Mungu wetu, stawisha roho yangu yenyi kukauka, unipokee kama mwana mpotevu na unihurumie.

Ee Bwana, usitazame wingi wa zambi zangu, wewe Bikira alizaa; zima makosa yangu yote, na unipe mawazo ya kuongoka; peke yako mpenda-wanadamu, unihurumie.

Litukuzwe jeshi la mfalme wa mbinguni! Kwani walipozaliwa duniani mashahidi washindaji hawakutumainia cheo cha Malaika: Walipozarau mwili na kuteswa mateso yao, wakastahili utukufu wa Malaika; kwa maombezi yao, ee Bwana, utuhurumie neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Tuliza huzuni ya roho yangu yenyi kusikilitika, ee Bikira Mtakatifu kamili na mzazi-Mungu mwenyi kupanguza hapa chini machozi ya macho yetu; ni wewe mwenyi kufukuza uchungu wa wenyi mauti na kumaliza laana ya wakosefu; katika wewe, ee Bikira, uko matumaini yetu na msaada wetu.

## MU KAZI MOJA MANGARIBI KATIKA SAUTI YA TANO

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.** *Kheris askitikon*

Ee Mwokozi, vunja ugumu wa moyo wangu mashetani waliweka na unipe machozi mengi ya toba; hapo nitalilia zambi zangu nyingi, nitatakaswa ku wazo lolote zaifu, nitaokolewa ku giza za kusahau na nitafika ku akili ya mema; sikiliza na unihurumie, ee Bwana, ondoa mateso ya uzulumu ku roho yangu maskini ili katika wewe nipate mapumziko na nitimize mapenzi ya umungu wako.

Ee Bwana wa wema wote, nainua kwako mikono yangu na midomo yangu yenyi kuchofuka, moyo wangu umechukizwa na mawazo mabaya; ole wangu! Macho yangu haione nuru, roho yangu imechafuka tamaa, imefunikwa na furaha mbaya bila mimi kichukizwa; ee mpenda-wanadamu, uninyoeshee mikono yako takatifu, uniokoe, ee Mwokozi, unitakase ku zmabi zangu nyingi mno, na kwa rehema yako kubwa unilinde ku hatari yote.

Ee Yesu, kausha mito ya uchafu, tenga mabonde yenyi kujaa matope, kwa wema wako uipatie moyo wangu machozi mengi ya huzuni; kama mwana mpotevu nimejitanga mbali nawe, nimeondolewa matumaini yote ya mema yake. Ee Bwana mwenyi kujaa na rehema, usinizarau

mimi muovu kusudi adui mkali na mdanganyi asinikamate mimi wote mu utawala wake; ee Bwana, ujiharikishe kuniokoa ku uzulumu wake.

**Wimbo ya Mtangulizi Yoane.**

Tazama naungushwa mimi wote, napigwa bila matumaini ya kuponyeshwa. Unitunze, ee Mushuhuda wa Kristu na Mtangulizi, nakimbilia ku ulinzi wako kimungu; ee mwenyi heri, unisamehe hii siku ya ajabu nitakapoonekana mbele ya korti kwa kupata azabu yangu; nakuomba, uniopoe ku mateso yoyote ya juu mbinguni, usidanganye matumaini yangu kwako, lakini umuombe Bwana mwenyi kuleta ku dunia neema ya wokovu.

Kinara cha nuru yote, Mtangulizi wa Jua ndiye Kristu, uniangazie miangaza yako, nanguka katika ya zambi, uniondoe shimoni mwa zambi, ukiniamsha kwa sauti yako nzuri; wewe zamani kwa kuzaliwa kwako ukamurudishia baba yako sauti yake, nakuomba, ingoza sasa sauti yangu ili kwa imani na mapendo nimtukuze mpenda-wanadamu, Mungu Mwokozi mwenye kuleta ku dunia neema ya wokovu.

Ee Mwenyi heri, ulikuwa hekalu la Mungu, Nabii, Mtangulizi na Mtangazaji wa chemchem ya uzima wa milele mwenyi kukaa katika moyo wako; umuombe yeye daima kwa ajili ya wale wenyi kuja kukutukuza katika hekalu lako takatifu; Ili wawe hekalu za Roho Mtakatifu na wajongee kwa mwana, na sisi wenyewe tutukuze kwa nyimbo zetu ulinzi wako na maombezi yako ya furaha, wewe uliyekuwa mkubwa kati ya wana wa watu kadiri ya ushuhuda wa Bwana mwenyewe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira Mtakatifu, kwa maombezi yako mengi, simamisha mito ya tamaa zangu kausha bahari ya zambi, zangu; fanya ili nifike ku bandari ya mapenzi yako ya umungu, zamisha shimoni mwa upotevu maadui ambao kila siku wanazunisha roho yangu na wanaihangaisha na furaha mbaya. Jaza moyo wangu la huzuni yangu ukimuomba Kristu Mungu wetu mwenyi kuleta ku dunia neema ya wokovu.

**APOSTIKHA**

Ee Bwana, siache kutenda zambi, nasahau mapendo uliyonizungusha*:* ponyesha ugumu wa moyo wangu; peke yako Mungu wa wema, unihurumie.

Ee Bwana, sina hata woga juu yako lakini natenda maovu; mtu gani haogopi mwamzi ku korti? Mgonjwa gani akitamani kupona, anasirikisha mganga wake kama mimi? Ee Bwana mvumilivu na mwenyi kujaa mapendo, tazama uzaifu wangu na unihurumie.

Ee Bwana walipolindwa na nguo ya imani, waliposabitisha na alama ha Msalaba, Mashahidi wako Watakatifu walivumilia mateso; walishinda vema uwongo na nguvu ya shetani; kwa maombezi yao, ee Mungu Mwenyezi, tuma amani duniani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Sisi waaminifu tunakutaja mwenyi heri, ee Bikira Mzazi-Mungu, na tunakutukuza kama inavyofaa, muji imara, boma isiyoweza kuharibika, mlinzi muhodari na makimbilio ya roho zetu.

## MU KAZI PILI ASUBUI KATIKA SAUTI YA TANO

### KATHISMA YA KWANZA

*Sauti ya tano.*

Ee roho yangu, wakati atakapokaa mwamzi na Malaika watakapokuwa huko, kwa sauti ya baragumu na mbele ya tanuru ya moto utafanya nini wakati utakapopelekwa ku hukumu? Hapo

matendo yako ya giza yataonekana, hapo mawazo yako ya siri yatastakiwa; mbele ya mwisho umwambie Kristu Mungu wetu: Wewe mwenye kusoma mioyo unihurumie mimi muovu.

Ee roho yangu, vitu vya hapa chini vinadumu muda mfupi tu, vila vya Juu-mbinguni vinakaa milele, naona korti, mwamzi amekaa juu kiti chake naogopa kuhukumiwa; ee roho yangu, tubu mbele ya mwisho. Hukumu hai takuwa na huruma.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira uliyestawisha ua kimungu, Safina ya agano, kinara na chombo cha zahabu, meza takatifu huko kunako pumzika mkate wa uzima, umuombe Mwana wako, Mungu wetu pamoja na Mtangulizi Mtakatifu ili awape neema ya wokovu wale wenyi kukutambua kama Mzazi-Mungu.

## KATHISMA YA PILI

Lilia ukosefu wako, ee roho yangu, ongoka mbele ya mwisho, kataa makelele ya hii uzima, ambatana na Mungu wa wema. Yeye peke yake kwa mapendo yake kwa wanadamu atakuokoa.

Sisi wote wakosefu tusikilize sauti ya Bwana na Mchungaji mkuu. Alionekana mwilini duniani kwa ajili yetu, akawaita wakosefu kama mimi kwa kutubu; muwe na moyo, msiogope, mateso ni zaifu, mshahara ni bora.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Mama na Bikira daima, fumbo kubwa ya kuzaa kwako kimungu, namna isiyokadirika ya kupata kwako mimba inajulikana kweli kwa sisi; utukufu wako unasangaza mawazo yetu na unahangaisha mawazo yetu, ee Mzazi-Mungu, na unaenea pa sisi wote kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

## KATHISMA YA TATU

Elisabeti alifunguliwa ku utasa, Bikira alichunga ubikira wake wakati alipopata mimba tumboni mwake kwa sauti ya Gabrieli; na Yoane Mtangulizi akaruka tumboni mwa mama yake wakati alipomtambua rumboni mwa Bikira Rabi na Mungu wake aliyejifanya mtu kwa ajili ya wokovu wetu.

Majeshi ya mbinguni walishangaa ushujaa wa Mashahidi watakatifu, kwani na mwili wa mauti walishinda vema adui msiyeonekana kwa uwezo wa Msalaba na wanamuomba Bwana wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu Mtakatifu kamili, mulinzi wa wakristu, okoa watu wako wenyi kukuiya na matumaini na kivugutu; Fukuza haya ya mawazo yetu ya kutangatanga ili tukulalamikia: Salamu, Mama Bikira daima.

## EKSAPOSTILARION YA SIKU

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

## APOSTIKHA

Ole, wangu! Tazama nafanana na mtini usiyozaa matunda! Naogopa laana na shoka, lakini wewe mtunza-bustani wa mbinguni, ee Kristu Mungu wetu, stawisha roho yangu yenyi kukauka, unipokee kama mwana mpotevu na unihurumie.

Ee Bwana, usitazame wingi wa zambi zangu, wewe Bikira alizaa; zima makosa yangu yote, na unipe mawazo ya kuongoka; peke yako mpenda-wanadamu, unihurumie.

Mashahidi Watakatifu walishindana duniani, walipotolewa motoni na kuangamizwa majini, sasa wanaweza kuimba*:* Tumepita katika moto na katika maji na umetupatia mapumziko. Ee Bwana, kwa maombezi yao, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Matumaini ya wasiyo matumaini, uzima katika huzuni, mulinzi wa mwenyi kukukimbilia, ee Bibi Mtakatifu, Bikira na Mzazi-Mungu, toka juu mbinguni ututumie msaada wako.

## MU KAZI PILI MANGARIBI KATIKA SAUTI YA TANO

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.** *Kheris askitikon.*

Ee Bwana, tuliza mashambulio ya mashetani wanayonyanganya juu yangu, juu ya roho yangu maskini sababu ya kuinua na kunipeleka ku upotevu kamili; ondoa mitego na fitina wanayofanyika kila mchana na kila usiku, uniopoe ku werevu wao, ee Bwana, tuliza zoruba kali ya hii uzima, nakusihii, ee Kristu, kwa wema wako, uniokoe ku gehena na ku giza ya milele, wakati utakapokuja na utukufu kuihukumu dunia.

Wakati vitabu vitakapofunguliwa siku ya kuja kwako kwa ajabu na wote watakapoonekana mbele yako kwa kuongojea hukumu, wakati moto utakapowaka mbele ya korti na baragumu itakapolia, nitafanya je mimi mwenyi mateso, mimi mwenyi kustakiwa kwa zamiri yangu, mimi mwenyi kuhukumiwa ku moto wa milele? nakuomba basi mbele ya mwisho uniondolee zambi zangu, ee Kristu Mungu wetu mwenye kuleta neema ya wokovu duniani.

Ee Kristu, ulichukua Msalaba wako pa mabega yako, ukatembea katika Mateso yako; kwa sisi tuliyotaka kuishi ndani yako, ukatuonyesha namna gani tunaweza kutukuzwa na kuishi pamoja nawe; wewe mwenyewe utustahilishe sisi pia tushariki ku Mateso yako na ku utukufu wako tukipita vilevile kwa lufu yako, ee Bwana, regeza vishindo vya mwili wangu, toboa viungo vyangu na misumari ya woga wako kimungu; fanya ili mu hii dunia niwe kama nimekufa, niishi paka na amri zako za umungu.

**Wimbo ya Mzazi-Mungu.**

Nalia na nalalamika kwa uchungu nikiwaza hesabu ya ajabu, sina na neno hata moja la kusema juu ya matendo yangu; na tena mbele ya kufika kwa rafla mwisho wa hii uzima, mbele ya mundu, ya lufu na hukumu, mbele ya mimi kulipa haki yangu kule kuiko moto ya milele, katika giza za inje, huko nyungunyungu anatafuna daima wakosefu, ee Bikira Mtakatifu kamili, unipe maondoleo ya zambi zangu na neema kubwa.

Ndiwe kweli kiti cha Wakheruvi, uliye juu kabisa kati ya viumbe vyote, kwani Neno Takatifu alikaa ndani yako sababu ya kutengeneza hali yetu; kwa wema akatoka kwako mwenyi kuchukua mwili wetu, akavumilia mateso Msalabani kwa ajili yetu na kama Mungu akatufanyia zawadi ya ufufuo wake Takatifu; na kwa sababu ulipatanisha na Muumba hali yetu iliyohukumiwa, tunakushukuru na tunakulalamikia: Kwa maombezi yako utupe maondoleo ya zambi zetu na neema kubwa.

Bikira Mtakatifu akalalamika akilia: Hata mara moja wakati hauwezi kukausha machozi ya macho yangu, ee Mwanangu mpendwa. Nuru yenyi kuangaza nyota yote, chemchem ambako taa kubwa za mbinguni zilipata mwangaza wao, ndani yake ulimwengu wote unapata kipaji cha kusihi, yanifaa nini kuona mchana, wakati Jua langu amelala? Nuru bora, namna gani unaacha kuangaa, wewe nuru ya uso wangu, ee Mwanangu? Tangu sasa nitanawisha na machozi yangu mboni za macho yangu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Zamani Mama Kondoo jike alipoomuona Mwana-kondoo wake amejiharikisha kutolewa sadaka, akaenda haraka kumusindikisa akisema: Ee Mwanangu mupole kabisa, unaenda wapi? Kristu muvumilivu, kwa ajili ya nani unatembea bila kukawia, ee Yesu mpendawa, Bwana wa rehema na asiye na zambi? Unijibu kwa mtumishi wako, ee Mwanangu, usinyamaze, ee Mungu wa mapendo, mbele ya mama aliyekuzaa, chemchem ya uzima mwenyi kuleta neema ya wokovu duniani.

### APOSTIKHA

Msalaba wako, ee Kristu Mungu wetu, japo ni mti, imevaa lakini uwezo kimungu; inapoonekana waziwazi duniani; inaleta wokovu rohoni mwetu na tunaposujudu mbele ya hii, tunakutukuza, ee Mwokozi, utuhurumie.

Ee Kristu, muda kidogo kisha kusimika mti wa Msalaba, udanganyifu ukakimbia, neema ikastawika mara ya pili; si mateso ya mwenyi kuhukumiwa, lakini kwa sisi imeonekana kama ukumbusho wa wokovu; Msalaba ni boma letu, nguvu yetu, Msalaba ni chombo cha furaha yetu.

Enyi Mashahidi watakatifu, mutuombee ili tusafishwe zambi zetu*:* Kwani mulipokea neema ya kutuombea.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

*Kheris askitikon.*

Ee Yesu, aliposimama karibu ya Msalaba, huyu aliyekuzaa akalia na kulalamika, akasema: Sivumilie kukuona umepigiliwa juu ya muti, wewe Mtoto niliyezaa. Ningaliweza kukimbia uchungu kama Bikira, mateso gani mateswa moyoni mwangu yenyi kupasuka! Tazama linatimizika neno la Simeoni, kwani upanga umechoma moyo wangu; lakini sasa fufuka, ee mwanangu, okoa wale wenyi kukutukuza kwa nyimbo.

## MU KAZI TATU ASUBUI KATIKA SAUTI YA TANO

### KATHISMA YA KWANZA

Pahali pa mfupa ya kichwa pamekuwa Paradizo*:* Kwa muda kidogo kisha kusimika mti wa Msalaba, palepale ikastawisha mzabibu wa uzima*:* Ee Bwana furaha yetu, utukufu kwako.

Ee Mwokozi, mti wa Msalaba wako umeleta wokovu duniani; uliitika kupigiliwapo sababu ya kuondoa laana ya wenyi kufa*:* Ee Mwokozi furaha yetu, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Ee Kristu, alipokuona umesulubiwa Msalabani kwa kutaka kwako kama mwana-kondoo asiye na kosa, Mama yako akalia na akalalamika kwa huzuni*:* Ole wangu, alivyolalamika, namna

gani imezimika nuru ya macho yangu? Namna gani unakula kama muovu katikati ya wanyanganyi, ee Mwanangu, wewe Mfalme wa ulimwengu.

## KATHISMA YA PILI

Enyi Waaminifu, tumuimbie na kumtukuza Bwana mfufuliwa, huyu aliyetaka kutukomboa, kwani yenye mwenyewe alipigilia Msalabani zambi za wenyi kufa, akiopoa wanadamu ku udanganyifu sababu ya kutuingiza katika ufalme wa mbinguni.

Ee Mwokozi wewe uliyependa kuteswa Msalabani sababu ya kuwaokoa wanadamu ku mauti, sisi waaminifu tunakuimbia na ku kuabudu, kwani unatuangaza na uwezo kwa Msalaba, sisi wote tunatukuza mapendo yako ya huruma, ee chemchem ya uzima tena Bwana mwenyezi.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mjaliwa neema kwa Msalaba wa Mwana wako uwongo wa miungu ya uwongo ukaondolewa, na nguvu ya mashetani ikashindwa; ndio maana sisi waaminifu tunakuimbia daima kama inavyofaa, tunakutukuza na kukusifu kweli kama Mzazi-Mungu.

## KATHISMA YA TATU

Uaguzi wa Manabii umetimizika, tazama, nia yako ya zamani inatimia. Kwa kutaka kwako, ee Mfalme wa wote, ulijishusha mwilini na kwa ajili yetu unaitika kupanda Msalabani sababu ya kufiyapo; ndiyo maana, ee Neno, tunatukuza upendeleo wako wenyi kupita wazo lolote.

Umetupatia miujiza ya mashahidi wako Watakatifu kama boma isiyoweza kushindwa: Kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu haribu fitina ya wapagani, kwa wema wako na kwa mapendo yako kwa wanadamu sabalisha utawala wa imani.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mwanangu mpendwa, wakati, naona macho yako imefungwa, hapo nuru yangu imezimika, kwani sivumilie kuona jua, nilitaka, ee Neno, kuondoa macho; fichama, ee nuru ya jua; huyu neno lake lilikupa kuangaa anafunga macho Msalabani.

## EKSAPOSTILARION YA SIKU

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

## APOSTIKHA

Ee Bwana, zamani mfano wa Msalaba wako ilipoonyeshwa kwa Nabii Musa, ikashinda maadui zako, apa sasa tunayo tunaomba msaada wa Msalaba wako: Sabitisha Eklezya yako na uwape Wakristu, kama zamani kwa Mtakatifu Konstantino, na mapendo yako mengi, ee mpenda-wanadamu, makumbusho ya washindanji.

Ee Kristu, Msalaba wako uletaji-uzima, uliharibu nguvu ya Hadeze na uliokoa wanadamu; ulipoondoa watu kuzimuni huko walikolala, ukamfungulia mnyanganyi Paradizo; na tunaposujudu mbele ya hii, tunakutukuza, ee Mwokozi, utuhurumie.

Ee Bwana, waliposhinda katika mashindano yao, Washindani wa Malaika Wabila-mwili, Mashahidi wako walivumilia mateso; kwa matumaini moja walifurahia mema iliyoahidiwa; kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu, leta amani duniani na neema ya wokovu ku roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Ee Neno, wakati kondoo jike Bikira alipokuona wewe Mwana-Kondoo umepelekwa kuchinjwa, akalalamika: Ni mambo gani hii ya ajabu! Namna gani makafiri wanachinja huyu mwenyi kuleta uzima kwa wanadamu? Ee Mwanangu, rehema yako kwa ajili yetu ni kubwa.

## MU KAZI TATU MANGARIBI KATIKA SAUTI YA TANO

**Wimbo ya Mitume.** *Kheris askitikon*

Enyi Mitume muliyotumwa duniani kote kama mishale ya makali ya mwenyezi, kwa wepesi mukaregeza mishale ya moto na ya ajabu ya mashetani, sababu ya kutenga mbali ibada ya miungu ya uwongo na kuwafundisha watu wote imani, mukiwafanya kuwa kondoo za Kristu Mungu wetu aliye kweli Mchungaji mkubwa, na akawatuma ninyi wenyi heri kati ya mbwa-mwitu kutuliza ukali wao kwa njia ya imani.

Enyi Wafuasi wa neno la Mungu mwenyi kujifanya mtu aliyeishi pamoja na wanadamu kwa mapendo yake mengi na aliyetwaa kweli hali yao sababu ya kuwafanya kuwa miungu, mulifwata na hekima nyayo zake kimungu, mukafafanisha pia umaskini wake, mukaacha vitu vyote; na tena mukakataa hata kanzu ya pili, kwa safari yenu hamukuchukua wa mfuko wa safari wala bakora, sasa, ee Mitume Watukufu, munaonja uriti wa hazina za mbinguni.

Kwa maombezi yenu mbele ya Bwana, ee Mitume wenyi heri, mutuopoe ku masubuko ya vishawishi, ku midomo mbaya ya makafiri wenyi kuleta fitina, ku nia mbaya ya mashetani na ku ubaya wa wanadamu, ku zoruba na tufani, kwa kusaga meno na ku azabu ingine yote; na mumuombe ili kwa utawa na kazai aturudishie tupate fazila, uriti wa ufalme wa mbingu na neema kubwa.

**Wimbo ya Mtakatifu askofu Nikola.**

Salamu, mkubwa mtukufu, makao safi ya fazila, mfano takatifu wa ukuhani wa uKristu, mchungaji mkubwa na taa ya nuru, wewe mwamuzi wa washindaji ambaye wenyi kuomba wanasikilizwa na kuhurumiwa; unainama ku maombi ya wazaifu, ndiwe daima msaada wa wepesi, wokovu, na ulinzi wa waaminifu wenyi kutukuza makumbusho yako takatifu. Umuombee Kristu alete ku roho zetu neema kubwa.

Salamu, akili ya utakatifu, makao safi ya Utatu Mtakatifu, nguzo ya Eklezya, tegemeo ya waaminifu na msaada wa wenyi kuzulumiwa; nyota ambaye kila wakati maombezi ya nuru yanaondoa giza za majaribu na huzuni, ee Nikola mkuu, bandari ya amani huko wanakimbilia kwa ajili ya wokovu wao wale wenyi kuzungukwa na mawimbi ya masubuko ya hii uzima, umuombee Kristu alete neema kubwa ku roho zetu.

Salamu, mjaliwa juhudi ya Mungu, wewe mwenyi kuokoa ku lufu wale wanaopashwa kufa bila haki kwa sababu ya uwezo wako wa ajabu wala ya ndoto huko ulionekana; chemchem yenyi kutiririka ku Myre katika Likia, unapamwangia pia roho manemane nyingi na kufukuza arufu mbaya ya tamaa; upanga wenyi kukata ndago ya udanganyifu, jembe lenyi kupepeta mafundisho ya nyasi ya Arius, ee Nikola mtukufu mkuu, umuombee Kristu alete neema kubwa ku roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Nalalamika katikati ya zambi zangu nyingi, katika upofu wangu, giza ya akili yangu, mwenyi kujaa na huzuni na sikitiko. Angaza macho ya roho yangu, ee Bikira Mtakatifu uliyezaa Nuru yasiyo mangaribi yenyi kuangaza mipaka ya ulimwengu na maarifa yake ya nuru; mwangia akili yangu mwanga wa maombezi yako, ee Mtakatifu kamili ili niweze mimi pia kuwa mwana wa nuru, ukimuomba Kristu neema ya wokovu kwa ajili ya ulimwengu.

**APOSTIKHA**

Ee Wafuasi wa Mwokozi washuhuda muliyoona kwa macho mafumbo ya Kristu, mulitangaza huyu hatuwezi kuona na asiye na mwanzo, mukasema: Ku mwanzo Neno alikuwako, hamukuumbwa mbele ya Malaika wala si watu mulifundishwa hayo, lakini kwa hekima ya Juu-mbinguni, ndio maana tunawasihi muombee roho zetu kwa Bwana kwa ajili ya deni munayo kwake.

Tuwaimbie Mitume wa Bwana kwa nyimbo nzuri. Walipovaa silaha ya Msalaba wakamaliza udanganyifu wa miungu ya uwongo wakati walionekana kuwa washindaji na wenyi kuvaa taji ya ushindi, ee Bwana, kwa maombezi yao, utuhurumie.

Katika nguvu yenu imara hamukumukana Kristu, ee Mashahidi Watakatifu muliyoteswa mateso ya namna yote, lakini mulishinda nguvu ya wazulumu na mukalinda bila kosa imani sababu ya kupita duniani kwenda mbinguni; umuombe amani ya dunia na neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Salamu, Mjaliwa neema, Mama wa Kristu Mungu wetu, kwani Mfalme wa utukufu alionekana kwako na Roho Mtakatifu alikufunika kivuli chake; kwa deni unayo kwake umuombe kwa ajili yetu juu ya wokovu wa roho zetu.

## MU KAZI INE ASUBUI KATIKA SAUTI YA TANO

**KATHISMA YA KWANZA** *Ton sinanarkhon Logon.*

Tuwaimbie kwa mashairi na nyimbo za kiroho Mitume watakatifu waliyomuona Neno na kumtumikia Kristu, kwani, wanamuomba Kristu kwa ajili yetu sisi tunaikutukuza makumbusho yao takatifu.

Tuwaimbie Mitume waliyohubiri kwa mwaminifu wowote kadiri ya imani ya kweli mafundisho ya kweli ya Bwana, wakakataa giza za fitina, wakaeneza nuru ya kiroho duniani, na neema ya mafundisho kimungu, nawanaomba kwa ajili ya wokovu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira msiyeolewa, Bibi Bikira daima, tunakuimbia pamoja na washuhuda wa Mungu, kwani katika wewe Mwenyezi alifanya maajabu; huyu aliyezaliwa kwa Baba mbele ya nyakati alitwaa mfano wetu, akakaa rumboni mwako na ikamupendeza kuzaliwa na mwili wetu sababu ya ukombozi na wokovu wa wanadamu.

**KATHISMA YA PILI**

Kwa nyimbo zetu tuwaimbie Mitume kama washuhuda wa Neno tena wahubiri takatifu waliovua kiroho mataifa katika nyavu zao, kwani walituongoza ku maarifa ya Kristu pa kuokoa wanadamu wote ku udanganyifu sababu ya kuwaingiza katika ufalme wa mbingu.

Wafuasi wa Mwokozi, Mitume wa Mungu muliyopanda neno la wokovu mpaka ku mipaka ya ulimwengu na kueneza nuru kwa yoyote aliyekaa katika giza na kivuli cha mauti, angazeni pia roho yangu kutiwa giza na uweushi wa tamaa kwa ajili ua maombezi yenu, ee Mitume wenyi hekima wa Bwana.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira takatifu, bola la watu wenyi kukutumainia, utuopoe ku kiwishi yote, ku huzuni yote na ku hatari yote; pamoja na Mitume wa Kristu umuombe Mwana wako kwa ajili ya wokovu wa wote wale wenyi kukutolea nyimbo zao.

**KATHISMA YA TATU**

Ee Bwana, Wavuvi wasiyo kufunza wakanyamazisha wenyi hekima na wakafunga kinywa cha wasemaji walipohubiri fumbo isiyokadirika ya kuja kwako mwilini, na wakawa waalimu wenyi hekima wa mataifa, wakiangaza mipaka ya ulimwengu na nuru ya maarifa ya Mungu; kwa maombezi yao utupe sisi neema ya wokovu.

Mashahidi wako, ee Bwana, kisha wewe walikunywa kikombe cha mateso yako, walikataa furaha za hii uzima; wakawa wenzao wa Malaika. Kwa maombezi yao, ee Bwana, samehe roho zetu na leta neema ya wokovu ku roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ujiharikishe kutusaidia na kutulinda, onyesha watumishi wako huruma yako, ee Bikira Mtakatifu, tuliza mawimbi ya mawazo yetu ya upumbafu, ee Mzazi-Mungu, inua roho yangu yenyi kuanguka, ee Bikira, najua lakini ya kama unaweza kufanya hii yote unataka.

**EKSAPOSTILARION YA SIKU**

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

**APOSTIKHA**

Ee Wafuasi wa Mwokozi washuhuda muliyoona kwa macho mafumbo ya Kristu, mulitangaza huyu hatuwezi kuona na asiye na mwanzo, mukasema: Ku mwanzo Neno alikuwako, hamukuumbwa mbele ya Malaika wala si watu mulifundishwa hayo, lakini kwa hekima ya Juu-mbinguni, ndio maana tunawasihi muombee roho zetu kwa Bwana kwa ajili ya deni munayo kwake.

Tuwaimbie Mitume wa Bwana kwa nyimbo nzuri. Walipovaa silaha ya Msalaba wakamaliza udanganyifu wa miungu ya uwongo wakati walionekana kuwa washindaji na wenyi kuvaa taji ya ushindi, ee Bwana, kwa maombezi yao, utuhurumie.

Katika mateso Mashahidi wakalalamika kwa furaha*:* Hii ndio njia ya sisi kupatana na Mungu; kwa malipo ya vidonda vyenyi kujaa katika miili yetu, tutapokea mavazi meupe ya ufufuo; pahali pa matusi tutapokea utukufu wa mbinguni; pahali pa gereza tutapata Paradizo; pahali pa kuhukumiwa kama waovu tutakuwa pamoja na Malaika mbinguni. Ee Bwana, kwa maombezi, okoa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira uliyechaguliwa katika wote, sikiliza mwito wetu, leta ku roho zetu hii yanaomba kwa imani utuopoe ku mateso na uchungu, kwa maombezi ya Mitume. Kama Mzazi-Mungu, unaweza kufanya yote ile unataka.

## MU KAZI INE MANGARIBI KATIKA SAUTI YA TANO

**Wimbo ya Usulubisho**. *Kheris askitikon.*

Ee Bwana wa mapendo na Mwokozi wangu, ulipotaka kuisha mateso na haya ya wenyi kufa, ukavumilia haya ya Msalaba; ukaonja nyongo sababu ya kuondoa uchungu wetu, ee Rabi, ubavu wako takatifu ukachomwa mkuki sababu ya kuponyesha roho zetu zenyi kujeruhiwa; ndio maana tunaimbia kusulubiwa kwako tukufu, na tunaposujudu, tunatukuza mkuki, sifongo na tawi ambazo katika hizi unaleta amani na neema ya wokovu duniani.

Ee Kristu, alipotangulia kuonyesha Mateso yako, mtumishi wako Musa akainua nyoka ya shaba sababu ya kuwaponyesha watu ku vidonda vya sumu ya nyoka; na wakati wa kusulubiwa kwako Msalabani, ee Bwana mvumilivu, dunia ilipookolewa ku maumivu ya nyoka, ikainuliwa mpaka mbinguni; ndio maana tunaimbia kwa furaha uwezo wako na tunatukuza Msalaba wako takatifu, tunaposujudu mbele ya hii, ee Mpenda-wanadamu, katika hii kiumbe chote kinapata mwisho wa maumivu yake na neema ya wokovu.

Ee Mpenda-wanadamu, ulipotaka kunyanganya amri iliyokamatiwa juu ya Adamu na kuisha mateso yote, ee Muumba, ukaitika kutobolewa misumari, ee Kristu usiye na zambi; wakati mkuki inachoma ubavu wako, ee neno, unazuia upanga kali kutufungia mlango sisi watumishi wako; ndio maana tunaimbia na kutukuza uwezo wako na tunatukuza Msalaba wako takatifu, tunaposujudu mbele ya hii, ee Mpenda-wanadamu, katika hii kiumbe chote kinapata mwisho wa maumivu yake na neema ya wokovu.

**Wimbo ya Mzazi-Mungu.**

Ee Bibi wetu, ninapo uchanga wa roho yangu umejaa daima na mateso nzito na zambi zangu nyingi, sisubutu kutazama juu mbinguni; ninapoinama chini, nakulalamikia moyoni mwangu. Unihurumie, wewe ambaye tumbo lako takatifu lilizaa Mungu wa huruma, unionyeshe maajabu yako mengi, ee Bikira, na unapoinua mikono yako safi na takatifu kwa Mwana wako, kwa maombezi yako unipokelee wokovu.

Zoruba, mawimbi na kivumbi zimenishika katika bahari ya hii uzima na zimenisukumia kuzimuni ya kutotumainia; kwa maombezi yako, ee Bikira Mtakatifu kamili, ongoza moyo wangu ku bandari safi ya uzima, ku mageuzo na kuongoka kamili; ona uzaifu wangu, sikiliza mambo yangu, uninyoeshee mkono wako wa msaada sababu ya kuniinua, ee Mstahili kamili wa nyimbo zetu uliyezaa Kristu Mungu wetu ili alete neema ya wokovu duniani.

Ole wangu, nimejitwika zambi kubwa, naogopa kupatikana mbele ya Mwana wako. ee Bikira, namna gani basi sitaogopa hukumu yake? Mbele ya Korti kunatiririka mtoni ya moto na Malaika weko kule wengi sababu ya kuangushiamo wakosefu; tena mbele ya mwisho wa hii uzima, ee Bikira Mtakatifu kamili, nakuomba umuombe Mwamuzi mpenda-wanadamu anihurumie, anipe maondoleo na neema ya kubwa.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Alipochukua juu yake hali yangu yote, Muumba Mungu wetu akaitwaa akataka kutengeneza hali ya zamani iliyoanguka katika Adamu; akaitika kutobolewa na misumari anaponyesha sasa ile mikono iliyopanuliwa zamani ku mti uliyokataziwa; alipoona hayo, Mtakatifu kamili akalalamika: Ee Mwanangu, sababu gani hii uvumilivu ya ajabu? ee Kristu, namna gani nitaweza kuvumilia kuona amesulubiwa Msalabani huyu mwenye kushika ulimwengu wote mkononi mwake?

**APOSTIKHA**

Ee Bwana, zamani mfano wa Msalaba wako ilipoonyeshwa kwa nabii Musa, ikashinda maadui zako, hapa sasa tunayo kweli, tunaomba msaada wa Msalaba wako. Sabitisha Eklezya

yako na uwape Wakristu kama zamani kwa Mtakatifu Konstantino na mapendo yako mengi, ee mpenda wanadamu, makumbusho ya Washindaji.

Msalaba wako, ee Kristu Mungu wetu, japo ni mti, imevaa lakini uwezo kimungu; inapoonekana waziwazi duniani; inaleta wokovu rohoni mwetu na tunaposujudu mbele ya hii, tunakutukuza, ee Mwokozi, utuhurumie.

Ee Mashahidi wakuu muliyozarau mema ya hii uzima sababu ya kupambana vema na mateso, hamukuzeka katika matumaini yenu ya heri, lakini kwa uriti mukapokea ufalme wa mbinguni; na kwa sababu muna uwezo wa kumdai Mungu mwema, mumuombe amani ya dunia na neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

*Kheris askitikon.*

Ee Mwanangu, pakuona ubavu wako umechomwa na mkuki, najeruhiwa na upanga kali wa huzuni na rohoni mwangu hamuwezi kukosa lalamiko hata ndogo. Ndivyo alivyosema Mtakatifu kamili, mshuhuda wa Mateso yako na aliopoona kutolewa kwako Sadaka bila haki, akaongeza akilia. Iko wapi habari njema yenye kunielekea? Eko wapi huyu aliyeniambia: Salamu? Wapi kuzaliwa kwa ajabu? Eko wapi Petro rafiki yetu? Ee Bwana, utukufu ku uvumilivu wako wa ajabu!

## MU KAZI TANO ASUBUI KATIKA SAUTI YA TANO

### KATHISMA YA KWANZA

Ee Mwokozi, mti wa Msalaba wako umeleta wokovu duniani; uliitika kupigiliwapo sababu ya kuondoa laana ya wenyi kufa*:* Ee Mwokozi furaha yetu, utukufu kwako.

*Ton sinanarkhon Logon.*

Kwa mapendo yako, uliteswa Msalabani kwa kutaka kwako, ukaondoa kama Mungu Mwenyezi, laana ya zamani iliyostahiliwa sababu ya tunda iliyokataziwa, ndio maana tunaimba na kutukuza Mateso yako takatifu na kimungu, ee Bwana, na tunaposujudu mbele ya hii, tunatukuza daima wokovu wako wenyi kupita akili yote.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Aliposimama karibu ya Msalaba wa Bwana, Mzazi-Mungu akalalamika akilia: Ole wangu, ee Mwanangu mpendwa. Ole wangu, ee Nuru ya macho yangu, namna gani umepanuliwa Msalabani wewe uliyetandaza mbingu kama nguo na uliyetokeza kuzimuni chemchem ya maji kwa mapenzi yako?

### KATHISMA YA PILI

Ee Mwokozi wewe uliyependa kuteswa Msalabani sababu ya kuwaokoa wanadamu ku mauti, sisi waaminifu tunakuimbia na ku kuabudu, kwani unatuangaza na uwezo kwa Msalaba, sisi wote tunatukuza mapendo yako ya huruma, ee chemchem ya uzima tena Bwana mwenyezi.

Pahali pa mfupa ya kichwa pamekuwa Paradizo*:* Kwa muda kidogo kisha kusimika mti wa Msalaba, palepale ikastawisha mzabibu wa uzima*:* Ee Bwana furaha yetu, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Ee Kristu, alipokuona umesulubiwa Msalabani kwa kutaka kwako kama mwana-kondoo asiye na kosa, Mama yako akalia na akalalamika kwa huzuni*:* Ole wangu, alivyolalamika, namna gani imezimika nuru ya macho yangu? Namna gani unakula kama muovu katikati ya wanyanganyi, ee Mwanangu, wewe Mfalme wa ulimwengu.

**KATHISMA YA TATU** *Ton sinanarkhon Logon.*

Adamu aliona uchungu wa muti uliyokataziwa wakati wivu wa nyoka ukamuongoza ku upotevu wake; lakini, uliposulubiwa Msalabani, akavuna uzima na kwa sababu ya muti wa Msalaba anakaa tena mara ingine ku inchi ya mbinguni; nyoka amepondwa, mauti imeangamizwa na tunakutukuza, ee Bwana Mungu wetu.

Leo imeangaa makumbusho ya mashahidi na mbingu ikaongezaka mwangaza wake*:* Malaika wanashangilia pamoja nasi kama wanadamu duniani; Mashahidi wanamuomba Mungu ili ahurumie roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Akilia kwa uchungu Mzazi-Mungu akasema: Cabrieli alinipasha habari ya wokovu; namna gani basi furaha inageuka kuwa uchnugu? Namna gani mitaonekana bila mtoto, mimi niliyekuzaa bila kujua mume, ee mwanangu, wewe Mwokozi wa roho zetu?

**EKSAPOSTILARION YA SIKU**

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

**APOSTIKHA**

Ee Kristu, muda kidogo kisha kusimika mti wa Msalaba, udanganyifu ukakimbia, neema ikastawika mara ya pili; si mateso ya mwenyi kuhukumiwa, lakini kwa sisi imeonekana kama ukumbusho wa wokovu; Msalaba ni boma letu, nguvu yetu, Msalaba ni chombo cha furaha yetu.

Ee Kristu, Msalaba wako uletaji-uzima, uliharibu nguvu ya Hadeze na uliokoa wanadamu; ulipoondoa watu kuzimuni huko walikolala, ukamfungulia mnyanganyi Paradizo; na tunaposujudu mbele ya hii, tunakutukuza, ee Mwokozi, utuhurumie.

Litukuzwe jeshi la mfalme wa mbinguni! Kwani walipozaliwa duniani mashahidi washindaji hawakutumainia cheo cha Malaika*:* Walipozarau mwili na kuteswa mateso yao, wakastahili utukufu wa Malaika; kwa maombezi yao, ee Bwana, utuhurumie neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION**.

Bikira akilia machozi akamwambia Kristu: Tuliza mateso ya roho yangu yenyi kusumbuka, kwani kama kwa Mateso yako unaokoa wenyi kufa, ee Neno, unaumiza roho yangu. Wewe Nuru yangu bora, Mwanangu, Muumba wangu, nakuimbia, ee Bwana muvumilivu.

## MU KAZI TANO MANGARIBI KATIKA SAUTI YA TANO

**Wimbo Ya Rabi wetu Yesu Kristu.** *Kheris askitikon*

Wakati roho yangu itakapotengana na mwili wake kwa amri ya huyu aliyekusanya zamani uvumbi na roho, hurumia mtumishi wako, ee Kristu; uniopoe kwa wenyi kunishambulia wasiyoonekana wanaoongojea sababu ya kunirarua na kunifanya kuwa mateka ya meno yao; na unistahilishe kukaa mahali pa mapumziko huko hakuna uchungu, na malalamiko, huko kunatiririka furaha, huko kunasikilika makelele ya siku kuu na furaha ya wateule.

Ninapoogopa saa ya mwisho na makelele ya woga ya mashetani, nakulalamikia rohoni mwangu yenyi kuelemewa. Kwa uwezo wako haribu, ee Bwana, mazuio yao na fitina zao na usiruhusu niwe mchezo wa uzulumu wao mbaya; tazama uso wangu wa haya, uwe msikilivu wa huzuni yangu, opoa roho yangu maskini ku uchungu wake, ee Mungu wa mapendo mwenyi kuleta ku dunia neema kubwa.

Ee Mwokozi, kama mwanamuke Mkanani, nakulalamikia mimi pia: Ponyesha roho yangu na uiokoe ku matusi ya mashetani na ya maadui wenyi kuihangaisha zaidi, wakiharibu ndani yangu sura yako, ee Bwana, na wakipeleka nguvu zangu na akili yangu ku mawazo ya bure na ya haya; nakuomba uyafukuze rohoni mwangu sababu ya kupandamo woga wako wa kweli, na unipe nimalize kwa unyenyekevu katika amani masalio ya maisha yangu.

**Wimbo ya Mashahidi.**

Ee Bwana walipolindwa na nguo ya imani, waliposabitisha na alama ha Msalaba, Mashahidi wako Watakatifu walivumilia mateso; walishinda vema uwongo na nguvu ya shetani; kwa maombezi yao, ee Mungu Mwenyezi, tuma amani duniani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Ee Mashahidi watakatifu, mutuombee ili tusafishwe zambi zetu*:* Mulipokea neema ya kutuombea.

Katika nguvu yenu imara hamukumukana Kristu, ee Mashahidi Watakatifu muliyoteswa mateso ya namna yote, lakini mulishinda nguvu ya wazulumu na mukalinda bila kosa imani sababu ya kupita duniani kwenda mbinguni; umuombe amani ya dunia na neema ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Katika Bahari Nyekundu, wakati moja mufano wa Bibi-Arusi musiyeolewa ulijionyesha. Kule Musa alikuwa mugawanyi wa maji, hapa Gabrieli alikuwa mutumishi wa ajabu. Wakati ule Israeli alipita vilindini bila kulowanishwa, sasa Bikira alizaa Kristu bila mbegu; Bahari kisha kupita kwa Israeli ilibaki isiyowezekana kupita; Musiyeolewa kisha kuchukua Emmanueli, alibaki bila kuharibiwa. Mungu ndiwe uliye na uliyekuwako, na uliyefunuliwa sawasawa na mutu, utuhurumie.

**APOSTIKHA**

Ee Mashahidi wakuu muliyozarau mema ya hii uzima sababu ya kupambana vema na mateso, hamukuzeka katika matumaini yenu ya heri, lakini kwa uriti mukapokea ufalme wa mbinguni; na kwa sababu muna uwezo wa kumdai Mungu mwema, mumuombe amani ya dunia na neema ya wokovu wa roho zetu.

*Shairi:* Heri wale uliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe, ee Bwana.

Nikikumbuka Nabii aliyesema*:* Mimi ni uvumbi na matope, mimi pia nilitazama kaburini, niliona mifupa yenye kukauka na nikasema*:* Huyu ndiye mfalme, mtajiri, askari, maskini mwenyi haki muovu? Ee Bwana, kwa mapendo yako kwa wanadamu, pumzisha watumishi wako pamoja na wenyi haki.

*Shairi:* Na makumbusho yao ni ya milele.

Ee Bwana, uliniumba, ukaniwekea mkono, ukaniinua na ukaniambia*:* Utarudi udongo. Uniongoze katika njia yenyi kwenda kwako, unisamehe makosa yangu, na kwa mapendo yako kwa wanadamu, uniokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Bikira mbarikiwa, tunakusihi kama Mzazi-Mungu, utuombee wakovu wa roho zetu.

## MU POSHO YA ASUBUI KATIKA SAUTI YA TANO

## KATHISMA YA KWANZA

Ee Bwana, kisha wewe mashahidi wako walikunywa kikombe cha mateso yako, walikataa furaha ya hii uzima; wakawa marafiki za Malaika. Kwa maombezi yao, ee Bwana, leta maondoleo na neema ya wokovu ku roho zetu.

Majeshi ya mbinguni walishangaa ushujaa wa mashahidi watakatifu, kwani na mwili wa mauti walishinda vema adui msiyeonekana kwa uwezo wa Msalaba na wanamuomba Bwana wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

salamu, mulango wa Bwana usiyoweza kupitwa, salamu, boma na ulinzi wa wale wenyi kukukimbilia, salamu, bandari yenyi kutupatia makimbilio ya kweli, ee Bikira msiyeolewa uliyezaa mwilini Muumba na Mungu wako, uwaombee daima wale wenyi kumuimbia Mwana wako na kusujudu mbele yake.

## KATHISMA YA PILI

Umetupatia miujiza ya mashahidi wako Watakatifu kama boma isiyoweza kushindwa*:* Kwa maombezi yao, ee Kristu Mungu wetu haribu fitina ya wapagani, kwa wema wako na kwa mapendo yako kwa wanadamu sabalisha utawala wa imani.

Ee Mungu Mwokozi, kwa wema wako na kwa mapendo yako kwa wanadamu, pamoja na wenye haki pumzisha watumishi wako na uwaruhusu wakae katika uwanja wako, usihesabie makosa yao ya kujua na yasipokujua, ya kutaka na yasipo kutaka.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira Mzazi-Mungu, Bibi msiyeolewa uliyechukua Mwokozi wa dunia kumzaa katika ukamilifu wa hali mbili, umsihi pamoja na Manabii wataaktifu, mashahidi na Watakatifu wote juu ya amani ya dunia na wokovu wa roho zetu.

## EKSAPOSTILARION YA SIKU

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

Elezo: *Kama kuna Alliluya, tunaimba ku masifu nyimbo za mashahidi zenyi kutangulia hapa juu, na kama Apostikha tunaimba Mifano (Prosomia) yafwatayo:*

## APOSTIKHA
## (WIMBO YA WAFU).

*Sauti ya tano. Kheris askitikon.*

Kwa nuru ya uso wako, ee Kristu, kwa mema wako, pumzisha marehemu katika mahali pa baridi, karibu ya maji ya mapumziko, katika kifua cha Abrahamu; kule kuangaa nuru yako safi na kunatiririka chemchem ya heri, kule makundi ya watakatifu wanafurahiwa na wanatukuza wema wako kimungu, pumzisha pia watumishi wako ukiwapa neema ya wokovu.

*Shairi:* Heri wale uliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe, ee Bwana.

Ee mpenda-wanadamu na Bwana wa ulimwengu, wale wenyi kutoka ku vitu visipodumu na wanakuja kwako uwape waimbie na kutukuza uwezo wako; uwafanye wangae na uzuri wako, wapate mapendezi yako na huruma yako na waonje furaha safi zaidi, kule makundi ya Malaika na watakatifu wengi wanafurahiwa pumzisha pia watumishi wako ukiwapa neema ya wokovu.

*Shairi:* Na makumbusho yao ni ya milele.

Kule wanaimba makundi ya ma Nabii, ya Mitume na ya Mashahidi na wale wote waliyohakikishwa tangu milele kwa Mateso yako ya wokovu na kwa bei ya damu uliyokomboa

nayo mwanadamu mfungwa wa zambi, mahali hapo pumzishapo marehemu waaminifu na kwa mapendo yako kwa ajili yao uwape maondolea ya zambi zao; kwani duniani ulikuwa peke yako asiye na zambi, peke yako Mtakatifu na peke yako mwenyi uhuru kati ya wafu; pumzisha pia watumishi wako ukiwapa neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira Mtakatifu kamili, ulituopoa, sisi tuliyotumikia chini ya sheria ya zambi, wakati ulipata tumboni mwako mimba ya Muumba wa sharia, Mfalme na Mungu wetu ambaye ndani yake tunahakikishwa kwa zawadi ya ukarimu; umuombe sasa andike katika Kitabu cha uzima roho za wale wenyi kukuimbia, ee Mzazi-Mungu, ili wakiokolewa kwa usimamizi wako, tupate kwa Mwana wako ukombozi tunaposujudu mbele ya huyu mwenyi kuleta duniani neema ya wokovu.

# KIPANDE CHA SAUTI YA SITA

## MU POSHO MANGARIBI

**Wimbo ya Ufufuo.**

Ee Kristu, ikiweza kushinda juu ya Hadeza, ulipanda juu ya Msalaba, kusudi ufufue pamoja nawe,wao waliokaa katika giza ya mauti, wewe uliye na uhuru katikati ya wafu. Wewe uliyechirizika uzima toka nuru yako, ee Mwenyezi na Mwokozi, utuhurumie.

Leo Kristu akishinda mauti, alifufuka, kama alivyosema na akaleta shangwe ku ulimwengu, kusudi wote tupaze sautim, na tuseme wimbo hivi: Chemchem ya uzima, Nuru isiyoweza kukaribiwa, Mwenyezi na Mwokozi, utuhurumie.

Ewe Bwana, uliye katika viumbe vyote, tutakimbilia wapi sisi wenye zambi? Juu ya mbinguni? Wewe unakaa. katika Hadeze? Ulishinda mauti. Katika chini ya bahari? Kule ni mukono wako, ee Rabi. Tunakimbilia kwako, tukikusujudu tunakusihi: Ewe Uliyefufuka katika wafu, utuhurumie.

Kwa Msalaba wako, ee Kristu, tunajisifu, tunaimba na tunasifu ufufuo wako; kwa kuwa wewe ni Mungu wetu, hatumujui mwengine ila wewe peke yako.

Tukimuhimidi Bwana daima, tunasifu ufufuo wake; kwa sababu akivumilia Msalaba, aliangamiza lufu kwa lufu yake.

Ututukufu kwa uwezo wako, ee Bwana, kwani uliharibu huyu aliyekuwa na nguvu za lufu, na ulitufanya mupya kwa Msalaba wako, ukitupatia uzima na usiyoweza kuharibika.

Maziko yako, ee Bwana ilivunja na ilikata minyororo ya hadeze. Ufufuo wako katika wafu, uliangaza dunia, ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote... **THEOTOKION**.

*Sauti ya sita*

Nani hatakuita wewe Mwenye heri, Bikira Mtakatifu kamili? Nani hataimba kuzaliwa kwa Mwana wako bila mume? Kwani Mwana wa pekee aliyeangaa mbele ya wakati kwa Baba, yeye vilevile alitokea kwa wewe uliyesafi, akitwaa mwili usiyosemwa; yeye ni Mungu sawasawa na hali yake, na akajifanya mtu kwa kadiri ya hali ya watu kwa ajili yetu; yeye hagawanyike kwa uso mbili, lakini anajulikana kwetu katika hali mbili bila muchanganyo. Umusihi, ee Bikira mutaratibu na heriu daima, kwa murehemu nafsi yetu.

## APOSTIKHA

Ufufuo wako, ee Kristu Mwokozi, unaimbiwa kwa Malaika mbinguni; na utustahilishe sisi wa dunia, tunakutukuza kwa mioyo safi.

Ulivunja milango ya shaba, na ulikata mapingo ya Hadeze, kwa kuwa wewe ni Mungu Mwenyezi, ukifufua uzao wa watu walioanguka; kwa hii na sisi tunaita kwa sauti moja: Ewe Bwana, uliyefufuka katika wafu, utukufu kwako.

Kristu akitaka kutusimamisha tena toka anguko la zamani, anapigiliwa musalabani na anawekwa kaburini; lakini wanawake wabebaji-manukato wakimutafuta kwa machozi na maombolezo, walisema: Ole kwetu! Ee, Mwokozi wa wote! Namna gani ulikubali kukaa kaburini? Japo ulitaka kukaa kule, namna gani uliibwa? namna gani uliondoshwa? Pahali gani mwili wako uletaji-uzima ulifichwa? Lakini, ee Rabi, kama ulivyoahidi, onekana kwetu, na simamisha machozi ya maombolezo yetu. Wakati wanawake walipolia, Malaika aliwaambia kwa sauti kubwa: Musilie, na museme kwa Mitume ya kama Bwana alifufuka, akileta duniani usamehe na rehema kubwa.

Ukisulibiwa kama ulivyotaka, ee Kristu, na kwa maziko yako ukinyanganya mauti, ulifufuka siku ya tatu, kwa wewe ni Mungu kwa utukufu, ukileta duniani usiyomwisho, na rehema kubwa.

Utukufu kwa Baba...sasa nasiku zote...**THEOTOKION**

*Sauti ya inne.*

Muumba na Mukombozi wangu, Bwana Kristu, ewe Safi kamili, akitoka ku tumbo lako, na akinivaa, aliopoa Adamu toka apizo la kale; kwa hii tunakuita bila kuacha, ewe Safi kamili, kwani wewe wiko Mzazi-Mungu na Bikira kweli, na tunasema «Salamu» ya Malaika: salama, Bibi-Malkia, mulinzi na kivuli na wokovu wa nafsi yetu.

## APOLITIKION

*Sauti ya sita.*

Majeshi ya Malaika pa kaburi yako, na walinzi walikuwa kama wafu; Maria alisimama kaburini, akitafuta mwili wako usiye na doa. Ulinyanganya Hadeze bila kujaribiwa kwake. Ulikuta Bikira, ukileta uzima. Ewe Bwana uliyefufuka katika wafu, utukufu kwako.

**THEOTOKION**

Ewe uliyeita Mama yako mubarikiwa, ulikuja kwa mateso kama ulivyuotaka; uliangaa kwa Msalaba, kwani ulitaka kutafuta Adamu; ukasema kwa Malaika: Mufurahi pamoja nami, kwa kuwa ilipatikana feza iliyopotea. Ewe uliyefanya yote na akili, utukufu kwako.

## SIKU YA MUNGU ASUBUI KATIKA SAUTI YA SITA

### KATHISMA YA KWANZA

Hadeze ilisikitikia kufungukwa kwa kaburi na maria Magdalena aliwalalamikia Mitume waliyofichama: Enyi Watumishi wa mzabibu, tokeni, tangazeni habari ya Ufufuo; kwani Bwana amefufuka akileta duniani neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba.

Ee Bwana, Maria Magdalena alisimama karibu ya Kaburi yako na akazania ya kama mwenye shamba, na machozi yake akalalamika: wapi umeweka Uzima wa milele? Wapi ulificha huyu mwenye kukaa pa kiti cha Wakheruvi? Kwani walinzi wake wameogopa; unirudishie Bwana wangu ao lalamika pamoja nami: Wewe ambaye unapotoka kaburini, unafufua wafu, ee Bwana, utukufu kwako.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Gedeoni alitangulia kuonyesha kupata kwako mimba Daudi aliangaza kuzaa kwako, kwani Neno alishuka tumboni mwako kama mvua juu ya manyonya, ee Mzazi-Mungu na ukachipukiza bila mbegu, ee Udongo takatifu Mjaliwa-neema, wokovu wa dunia, Kristu Mungu wetu.

### KATHISMA YA PILI

Uzima wetu ulilala kaburini na jiwe lilifunjwa, maaskari walimuchunga Kristu kama ni juu ya kukesha kwa kumulinda Mfalme; lakini alipopofusha maadui zake, Bwana akafufuka kaburini.

Utukufu kwa Baba.

Yona alitangulia kuonyesha kuwekwa kwako kaburini, Simeoni akafasiria ufufuo wako kimungu, ee Bwana masiyekufa; ulishuka kaburini kama mufu, wewe mwenye kuvunja milango ya Hadese; lakini ukafufuka bila kuharibika, ee Bwana, kwa ajili ya wokovu wa dunia, ee Kristu Mungu wetu, ukawangaza wale waliyolala katika giza ya mauti.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION**.

Ee Mzazi-Mungu na Bikira Mbarikiwa, umuombe Mwana wako, Kristu Mungu wetu alisulubiwa Msalabani kwa kutaka kwake na aliyefufuka katika wafu alete wokovu ku roho zetu.

*Elezo: Kisha waimbaji wanaimba Mahimidi ya Ufufuo ya Kristu. Kisha wanasoma Ipakoi.*

### IPAKOI.

Ee Kristu, kwa lufu yako ya kutaka na yenye kuleta uzima, ulivunja milango ya Hadeze; ee Mungu, unatufungulia Paradizo ya zamani; ulipofufuka katika wafu, unanyanganya uzima wetu kuzimuni.

# ANAVATHMI.

## ANTIFONON YA KWANZA.

Nanyanyua macho mbinguni Kwako, ee Neno la Mungu; katika huruma yako uniokoe ili niishi ndani yako.

Ee Neno, utuhurumie, tunajazwa na machukio mengi, kama vyombo vya uteuzi, utufanye kuwa wapya.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...

Roho Mtakatifu ni mwanzo wa wokovu, na wakati anapopuliza pa mumoja palepale anamuondoa ku shuruli za dunia, anamuoa mabawa ya kupanda mpaka mbinguni.

## ANTIFONON YA MBILI.

Bila Bwana aliyekuwa pamoja nasi, hata mumoja wetu hakuweza kushindana mbele ya Werevu wa Adui, lakini Washindaji watatukuzwa.

Ee Neno, Roho yangu isiwe imateka ya meno yao! Nitakimbia je kwa maadui, mimi nilie mateka ya zambi?

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...

Ni kwa Roho Mtakatifu kutubariki na kututakasa, kutupa maarifa na amani: Anatenda kama Baba na neno.

## ANTIFONON YA TATU.

Wao wenye kumwegemea Bwana wanaogopesha maadui; wanastahili mastajabu kwani wanatazama mbinguni.

Ee Mwokozi, Sehemu ya wenye haki wanapofazaliwa na msaada wako, hawatanyosha kamwe mkono wao juu ya nguvu ya makafiri.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...

Kwa Roho Mtakatifu kuna uwezo wa ulimwengu: Malaika mbinguni na wenye pumuzi hapa chini wanamwabudu yeye.

## PROKIMENON.

*Sauti ya sita.*

Ee Bwana, amsha uwezo wako na kuja utusaidie. *(mara mbili).*
*Shairi*: Mchungaji wa Israeli, tega sikio, wedwe unayechunga Yosefu kama Kondoo.
Ee Bwana, amsha uwezo wako na kuja utusaidie.

## EVANGELION YA ASUBUI (EOTHINON)

## KANUNI YA UFUFYO YA BWANA YESU KRISTU

## WIMBO YA KWANZA

*Sauti ya sita.*

**IRMOS**: Wakati wana wa Israeli walipotembea kuzimuni kama pakavu na walipomuona mzulumu ameangamizwa kwa mawimbi hapo wakalalamika: Tumuimbie Mungu wetu wimbo wa ushindi.

Utukufu kwa ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Wakati ulipanua mikono yako Msalabani, ee Mungu wa wema, ulitimiza mapenzi ya Baba yako; tunakuimbia tena na moyo mmoja wimbo wa ushindi.

Utukufu kwa ufufuo wako takatifu, ee Bwana.
Ee Rabi wa uzima, ilipojaa na woga kama mjakazi, kwa amri yako mauti ikajongea kwako: katika hii ukatupatia Ufufuo na uzima wa milele.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe. **THEOTOKION**.
Ulimupokea Muumba wako kama alivyotaka yeye mwenyewe; akachukua mwili bila mbegu tumboni mwako; ee Bikira Mtakatifu kamili, ndiwe kweli Malkia wa dunia aliyeumbwa.

Utukufu kwa ufufuo wako takatifu, ee Bwana.
Mwamuzi akahuzunia kwa kutaka kwake ku baraza ya Pilato kama mshtakiwa juu ya hukumu isiyo ya haki na mkono wa ukafiri ukapiga uso wa Mungu ambaye mbingu na dunia zinatetemekea.

Utukufu kwa ufufuo wako takatifu, ee Bwana.
Ee Mwokozi, ulipanua mikono yako Takatifu juu ya Msalaba wako wenyi kuleta uzima na takatifu na ukakusanya, ee Bwana, ili wakuje, mataifa yenyi kusujudu tena mbele ya Usulubisho wako tukufu.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe. **STAVROTHEOTOKION**.
Ee Mwokozi, alipolia machozi mengi, Mtakatifu kamili akasimama karibu ya Msalaba wako, na alipoona matone ya damu yako yakitelemuka ku ubavu wako, ee Kristu, akatukuza mateso yako makubwa.

## KANUNI YA MZAZI-MUNGU.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.
Alipokulka tunda la muti uliyokataziwa, Eva akaingiza laana; lakini ukaiondoa, ee Bikira Mtakatifu, wakati ulipozaa Kristu kama malimbuko ya baraka.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.
Wewe uliyezaa Kristu, hii ushanga yenyi nuru kimungu ondoa giza ya mateso yangu, ee Bikira Mtakatifu, na zoruba ya maovu yangu kwa sababu ya nuru ya sifa zako ya ukarimu.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.
Kwa macho ya kiroho Yakobo alitangulia kuona kwa fumbo matumaini ya mataifa. Mungu aliyetwaa mwili kwako na aliyetukomboa kwa usimamizi wako takatifu.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.
Pahali pa wafalme wa kabila ya Yuda, ni Mwana na Mungu wako, ee Bikira Mtakatifu, ambaye, alipokuja kuitawala dunia na mipaka yake, anaitawala sasa na ufalme wake wa kweli.

## WIMBO WA TATU

*Sauti ya sita. Uk estin Agios os Si.*

**IRMOS:** Hakuna hata mumoja aliye Mtakatifu kama wewe, ee Bwana Mungu wangu, kwa wema wako ulitukuza nguvu ya waaminifu, na pa jiwe imara kukiri jina lako.

Utukufu kwa ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Wakati viumbe vilimuona Mungu, amesulubiwa mwilini mwake, vikatetemeka kwa woga, lakini vikalindwa kwa mukono wa huyu aliyesulubiwa kwa ajili yetu.

Utukufu kwa ufufuo wako takatifu, ee Bwana.
Lufu iliharibu nguvu ya mauti; tangu hapo imelala bila nguvu, kwa sababu naikuweza kuvumilia ushambulio kimungu wa uzima, na ufufuo umepewa kwa watu wote.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe. **THEOTOKION**.
Ee Bikira Mtakatifu kamili, majabu ya kuzaa kwako kimungu inapita ulimwengu na sheria zake: Ni Mungu Mwenyewe uliyechukua imara tumboni mwako na umekaa bikira hata kisha kuzaa.

Utukufu kwa ufufuo wako takatifu, ee Bwana.
Kisha siku tatu Kaburini, kwa Ufufuo wako uletaji uzima ukawafufua wafu wa zamani; walipokombolewa ku hukumu, wakaimba na furaha: Umekuja, ee Bwana, ni wewe, ee Mkombozi.

Utukufu kwa ufufuo wako takatifu, ee Bwana.
Ee Mwokozi, utukufu ku ufufuo wako wenyi kutukomboa ku mauti, kaburini na ku Hadeze; ee Mwenyezi, kwa nyimbo zetu tunakuimbia: Ee Bwana mpenda-wanadamu, nakuna hata mmoja aliye Mtakatifu kama wewe.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe. **THEOTOKION**.
Ee Bikira Mtakatifu kamili, ulipoona tunda la tumbo lako amechomwa mkuki, moyo wako ukachoimwa na kwa woga ukasema: Ee Mwanangu, hii ndio shukrani ya watu hawa.

**KANUNI YA MZAZI-MUNGU.**

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.
Ee Mzazi-Mungu, alipotwaa tumboni mwako mwili wangu wa mauti na wenyi kuanguka, kwa wema wake usiyokadirika Bwana akaufanya kuwa wa milele, akaungana nayo daima.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.
Ee Bikira mbarikiwa, makundi ya Malaika walipomwona Mungu kutwa mwili tumboni mwako, wakashikwa na woga, na kama Mzazi-Mungu wanakutukuza kwa nyimbo zao daima.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.
Ee Mzazi-Mungu, nabii Danieli aliruka alipoona Mulima wa kiroho, mwamba usiyochongwa na mkono wa mwanadamu ambao uwezo uliharibu sanamu za mashetani.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote... **THEOTOKION**.
Sisi wenyi mauti hatuna na lugha wala neno lenyi kuweza kukutukuza kama inavyostahili, ee Bikiora, wewe ambaye kwako Kristu chemchem ya uzima alitwaa mwili tumboni mwako.

**KONTAKION**

Na mkono wake wenyi kuleta uzima Bwana chemchem ya uzima, Kristu Mungu wetu, alitosha wafu wote ku giza ya Hadeze, akawapa wanadamu wote ufufuo, ndiye kweli Mwokozi wetu, uzima wetu, Ufufuo wetu na Mungu wa ulimwengu.

**NYUMBA (IKOS)**

Ee Chemchem ya uzima, tunaimbia na ibada Msalaba wako na kaburi yako na tunasujudu mbele ya hii; kwani ulifunga hafeze na minyororo, ee Bwana msiyekufa, na kama Mungu mwenyezi akawafufua wafu pamoja nawe; ukavunja milango ya hadeze na ukaharibu ufalme wa mauti. Sisi wenyi mauti tunakuimbia na mapendo, wewe ambaye ulipofufuka, ukaharibu nguvu ya adui mbaya; wale wote waliyokutumainia wewe ukawafufua, ukaopoa dunia ku mishale ya nyoka, kwa uwezo wako wa pekee, ee Bwana, ulitukumboa kwa adui aliyetupoteza; ndio maana tunaimbia na ibada Ufufuo wako wenyi kutuokoa, ee Mungu wa ulimwengu.

## MASIFU

*Sauti ya sita.*

Msalaba wako, ee Bwana, ni uzima na ufufuo kwa watu wako; na tukitumainia kwake, tunakuimbia wewe, Mungu wetu, uliyefufuka, utuhurumie.

Maziko yako, ee Rabi, ilifungua Paradizo kwa uzao wa watu; na tukikombolewa katika uharibifu, tunakuimbia wewe, Mungu wetu, uliyefufuka. Utuhurumie.

Pamoja na Baba na Roho, tumwimbie Kristu, aliyefufuka katika watu, na tupaze sauti kwa yeye: Ewe ni uzima na ufufuo wetu. Utuhurumie.

Katika siku tatu ulifufuka, ewe Kristu, toka kaburi, kama ilivyoandikwa, ukiamusha pamoja nawe Baba yetu; kwa hii uzao wa watu tunakutukuza na tunaimba ufufuo wako.

**Wimbo Anatolika.**

Bwana, siri ya ufufuo wako ni kubwa na ya ajabu, kwani ulitoka kaburini, kama Bwana Arusi mwenye kutoka chumbani mwake na kwa lufu uliharibu mauti, kusudi uopoe Adamu; kwa hii mbinguni Malaika wanacheza, na duniani watu wanatukuza wema wako uliyofanyika kwetu, ee Mpenda-wanadamu.

Enyi Wayuda wavujua-Sheria, iko mihuri na feza muliyoleta kwa askari? Mali haikibwa, lakini alifufuka sawa mwenyezi; ninyi muzazike, muliyekataa Kristu, Bwana wa utukufu, aliyeteswa na aliyezikwa, na aliyefufuka katika wafu; tumwabudu Yeye.

Japo kaburi lilitiliwa mihuri, japo muliweka wachungaji, na mulitia chapa, namna gani mulinyanganyiwa, enyi Wayuda? Milango ilipokuwa imefungwa, Mfalme alitoka; ao mutuonyeshe mufu ao mumwabudu sawasawa na Mungu na mwimbe pamoja nasi. Utukufu, ee Bwana, kwa Msalaba wako na kwa ufufuo wako.

Wanawake wabebaji-manukato, walishika, ee Bwana, kwa maombolezo kaubri yako yenye kupokea uzima; wakikamata manemane, walitafuta kupakaa mwili wako usiyo na doa; lakini walikuwa Malaika mwenye mavazi ya kuangaa, aliyekaa juu ya jiwe, na akasumbulia nao, akasema: kwa nini munbamulilia yeye aliyechirizika uzima kwa dunia toka ubavu wake? Kwa nini munatafuta kaburini yeye Msiyekufa, kama mwenye kufa? Muzuri mwende kwa haraka, mutangaze kwa Wanafunzi wake, furaha ya ufufuo wake tukufu, kwa ajili ya dunia; kwa hii utuangaze na sisi, ee Mwokozi, utupe usamehe na rehema kubwa.

Utukufu kwa Baba...**EOTHINON**

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu).*

Sasa na siku zote...Mbarikiwa ukupita, ewe Mzazi-Mungu...

**DOKSOLOGIA KUBWA**

## SIKU YA MUNGU MANGARIBI KATIKA SAUTI YA SITA

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.** *Olin apothemeni.*

Ee Neno, usiyetamainia mauti, lakini kuongoka kwa waovu, ee Kristu wa mapendo makuu na Bwana ambaye unahurumia daima Mtumishi wako, marudi kwako, unisamehe makosa niliyokusirikisha nayo zaidi, unihurumie wakati nasujudu kukuomba, kwani kwa ajili yangu unaonyesha shimo ya huruma yako kimungu wakati, japo uovu wangu, unaniokoa katika mapendo yako.

Peke yako Mpeda-wanadamu unataka wokovu wa wote na amabaye mapendo inawaita wakosefu wote waongoke, ee Rabi, usikumbuke hata mara moja haya ya matendo mbaya niliyotenda mbele ya macho yako, bila kuogopa azabu kali ya mkono wako; ndio maana tunasujudu nikilalamika na nikilia, katika roho naanguka ku miguu yako sababu ya kupata maondoleo ya zambi zangu.

Pokea ombi langu, wewe mwenye kupenda kila mtu aokolewe, usinitupe mbali ya uso wako, japo uovu wangu na zambi zangu nyingi ambazo tangu ujana wangu nilipita na wanadamu wote; nasujudu na machozi mbele yako. Unionyeshe huruma yako na rehema yako, ee Bwana wa utukufu, Baba wa mapendo na wa wema, usimkatae maskini mwenyi kukusihi.

**Wimbo ya wa Malaika.**

Kwa ma sauti yao, makundi ya Malaika wanaimba milele nyimbo zao za siku Kuu wakati wanapoona katika nuru uzuni wako wa kuangaa wa wanapojazwa na mwanga wako, ee Mungu wa wema; wanapokuwa wasikivu daima wa vitu vyenyi kutezamiwa na wakati wanapopokea na kivugutu mwanga wa furaha, wanaombea na matumaini roho zetu.

Ee Mwokozi, kwa ulinzi wa Malaika linda kondoo zako wewe uliyeweka majeshi yao, kwa neno na mapenzi yako, ukifukuzia mbali yao vishawishi mashambulio ya Wapagani na nguvu ya fitina; uliwakomboa kweli kwa damu yako na ukazima hukumu ya sheria na ya zambi; fanya ili wakiopolewa ku huzuni yenyi kuwasonga, waweze kukutukuza na imani ya kweli.

Watawala, wenyi uwezo, vitu vya ezi, Wakeruvi na Waserafi pamoja na Malaika na Malaika Wakuu wanazungulusha na heshima utukufu wako kimungu na kiti chako takatifu; fazila na uwezo zinatukuza ufalme wako, zikishangaa maongozi na heshima yako, ee Kristu, na wanaombea na matumaini roho zetu.

Utukuku kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION.**

Nilipotelemuka katika shimo ya mawazo yangu, nilipotii ku udanganyifu wa mdanganyi, na mateso yangu nakimbililia, ee Bibi Mtakatifu, ku huruma yako ya ajabu, ee Bikira Mtakatifu, kwa maombezi yako ya furaha. Usiondoe ku majaribu na vishawishi, uniokoe? Ewe Mtakatifu kamili, ku mashambulio ya shetani, ili nikuimbie na mapendo, nikutukuze na nisujudu mbele yako, nikikutukuza, ee Bibi wetu mwenyi heri daima.

### APOSTIKHA

Sina na machozi ya toba, nakuomba tena, ee Mungu Mwokozi*:* Mbele ya mwisho uniongoze na unipe toba ili niepuke ku azabu.

Ku siku ya ajabu ya majilio yako hatutaweza kusikia, ee Kristu*:* Siwajui ninyi! Kwani matumaini yetu ni kwako hata kama sisi ni wazaifu na hatushike amri zako; ee Mwokozi, tunakuomba, samehe roho zetu.

Ee Kristu, Mashahidi wako waliteswa mateso mengi, mwisho wakapokea utukufu mbinguni ili waombee roho zetu.

Utukuku kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION.**

Tukifafanisha sauti ya Malaika Mkuu, tuimbie na ibada makao ya mbinguni, mulango kweli wa kufunga: salamu, ambaye katika wewe tumepewa Mwokozi wa ulimwengu, Kristu chemchem ya uzima na Mungu wetu; kataa, ee Bibi wetu, ma adui wa imani yetu wenyi kutuolemeza uzalimu wao; wajue nguvu ya mkono wako, ee Bikira Mtakatifu, matumaini ya wakristu.

## MU KAZI MOJA ASUBUI KATIKA SAUTI YA SITA

### KATHISMA YA KWANZA

Nawaza siku ya ajabu ya hukumu na nalilia matendo yangu mabaya; nitasema nini kwa Mfalme msiyekufa? Nitasubutu nemna gani kumtazama Mwamuzi wangu mimi maskini? Ee Baba Mwema kamili, Mwana wa pekee na Roho Mtakatifu, unihurumie, ee Bwana.

Ee Mungu wa mapendo, kwa machozi yangu mengi; mahali hapa ulipochagua kwa kuketi na kutoa hukumu ya haki usifumbuo siri za moyo wangu ili nisipate haya mbele ya Malaika wako, lakini, ee Mungu wangu, unihurumie, ee Bwana.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . **. THEOTOKION.**

Matumaini, ngao na bandari ya wenye kukukimbilia, mulinzi wa uliwmegu, Mzazi-Mungu mwema, umwombe kabisa pamoja na Malaika huyu uliyezaa, Mungu mwenye kutupenda zaidi, aokoe roho zetu ku hatari yoyote, ee Bikira Mtakatifu na peke yako mbarikiwa.

### KATHISMA YA PILI

Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, urazi wote umetukosa; kama maskini waovu tunakutolea hii ombi*:* Utuhurumie, ee Bwana.

Ee Bwana, utuhurumie sisi wenyi kukutumainia wewe; usitusirikie, usikumbuke maovu yetu, lakini kwa wema wako ututazame sasa na utuopoe kwa maadui zetu; kwani ndiwe Mungu wetu, na sisi ni watu wako; sisi wote ni kazi ya mikono yako, ni jina lako tunaita daima.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . **. THEOTOKION.**

Mwanzo wa wokovu wetu ni hatari ya Gabrieli kwa Maria wakati Malaika alikuja, hakukataa salamu; hakusita kama Sara katika hema, lakini akasema: Mimi ni mtumishi wake Bwana, nitendewe vile ulivyosema.

### KATHISMA YA TATU

Ee roho yangu, unapoishi bila kushurulika, unasahau siku ya ajabu ya hukumu, amka na chagua kuongoka, rudia kwa Kristu na umulalamikie: Ee Mungu wa mapendo, usikumbuke zambi zetu nyingi wakati utakapokuja kutuhukumu, ee Bwana.

Kwa Wenyi hali ni nuru ya milele*:* Walipoangazwa na nuru yako, Watakatifu wanangaa daima kama nyota kuangaa, wakififisha taa ya makafiri; kwa maombezi yao, ee Bwana na Mwokozi, angaza roho yangu na uniokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . **. THEOTOKION.**

Mzazi-Mungu mtukufu, aliye mtakatifu kuwapita Malaika watakatifu, tunamuimbia daima kwa kinywa na kwa roho na tunamtambua kama Mzazi-Mungu, kwani alizaa kweli Bwana aliyejifanya mtu na anaombea imara roho zetu.

**APOSTIKHA**

Ee Mwokozi, ponyesha vidonda vya moyo wangu wenyi kujeruhiwa na zambi nyingi, kwani ndiwe mganga wa roho na wa miili; kwa wale wenyi kukuomba unawasamehe zambi, unipe machozi ya toba na maondoleo ya makosa yangu*:* Ee Bwana mwenyezi, unihurumie.

Nilipotwaliwa nguvu, adui akanipiga mshale wa zambi, lakini wewe, ee Mganga wa roho na wa miili, ponyesha vidonda vya roho yangu; ee Mungu wa mapendo, unihurumie.

Ee Bwana, kukumbuka mashahidi wako ni siku Kuu kubwa kwa viumbe vyote; dunia ya wanadamu inafurahi pamoja na Malaika mbinguni; kwa maombezi yao, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. **. . THEOTOKION.**

Kwa neno la Malaika Mkuu uliyopokea, ukawa kiti cha Wakheruvi na ulichukuwa mikononi mwako, ee Mzazi-Mungu, matumaini ya roho zetu.

## MU KAZI MOJA MANGARIBI KATIKA SAUTI YA SITA

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu**

*Olin apothemeni.*

Tangu ujana wangu nilitumikia fuarha na mimi wote nimekuwa mchezo wa mwili na wa tamaa zenyi kuniamuru amri yao; bila kutazama roho yangu, ee Mwokozi, nimezarau amri zako, lakini wewe Muumba wangu, wewe peke yako usiye na zambi, unapojuwa uzaifu wangu, ee Bwana, kwa huruma yako unisamehe zambi nilizotenda tangu ujana wangu bila kujua wala kwa kujuwa, kwa matendo ao kwa mawazo, peke yako mwenye kutuhurumia,

Nani ataniopoa ku hii mwili wenyi kuniletea lufu na nani ataokoa roho yangu ku majaribu na vishawishi? Inanizulumu kwa nguvu kwa kupenda kwake furaha na inajichukiza juu ya roho, ole wangu, katika uzaifu inanizulumu mara ingine; na siwezi kushindana na uzaifu wake, ee Bwana, lakini usiruhusu, ee Muumba, matope yashinde roho, wewe ambaye kwa furaha yako uliweka ndani yangu pumuzi yako ya uzima.

Ee Bwana msiyekufa, wakati kwa amri yako utakapotaka kutenga roho yangu ku vifungo vya mwili, unisamehe ile siku, ukinitumia Malaika mpole kunitafuta na mwenyi kuniletea furaha, mwenyi kuniokoa ku nguvu za giza, akinipa nguvu ya kutimiza salama kupanda mbinguni na ya kujiharikisha kusujudu bila kuhukumiwa mbele ya kiti chako cha ajabu, ee Mungu wa wema.

**Wimbo ya Mtangulizi Yoane.**

Kwa ajili ya uovu wangu nastahili hukumu, lakini nasujudu mbele yako wewe uliyetukuzwa kuliko wote, nakusihi kwa moyo wangu wote. Tazama roho yangu ya huzuni, wewe uliyeangaa mbele ya furaha yetu, ee Mtangazaji wa toba, tazama vidonda vya roho yangu, uniokoe katika maombi yako takatifu, ee Mtangulizi, na kwa maombezi yako kwa Bwana.

Tazama nahukumiwa kwa ajili ya zambi zangu, mimi wote naangukia katika shimo ya kutotumainia, najazwa na uovu, na giza, nachafuka na furaha mbaya, napotea; naangukia tena ku miguu yako. Usinikatae, lakini uniokoe, ee rafiki ya Bwana tena Mtangulizi mwenyi heri.

Opoa roho yangu ku mauti, ku uchungu wa zambi, uipatie uzima kwa utimizo wa mafundisho ya Kristu na kwa nguvu ya maombezi yako; zuia maadui wasiyoonekana wenyi kunigombanisha daima; uniongoze katika njia sawa ya wokovu na ku mapumziko ya mbinguni, kwa maombezi yako kwa Mungu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . **. THEOTOKION.**

Alama ya hasira ni chuki, inaonekana katika ukali katika hii, namna mbalimbali ya hasira yanatiririka bila haya kinywani mwa waovu, wakiwakokotea katika moto ya gehena wale wenyi kuwafwata, ni kama inavyoandikwa; na tena, ee roho yangu, uwe macho, kimbia ukali, hasira, chuki, hasira nyingi na yote namna ya chuki, umulalamikie Mzazi-Mungu; ee Bibi wetu, uniokoe.

**APOSTIKHA**

Sina na machozi ya toba, nakuomba tena, ee Mungu Mwokozi*:* Mbele ya mwisho uniongoze na unipe toba ili niepuke ku azabu.

Ku siku ya ajabu ya majilio yako hatutaweza kusikia, ee Kristu*:* Siwajui ninyi! Kwani matumaini yetu ni kwako hata kama sisi ni wazaifu na hatushike amri zako; ee Mwokozi, tunakuomba, samehe roho zetu.

Ee Kristu, Mashahidi wako waliteswa mateso mengi, mwisho wakapokea utukufu mbinguni ili waombee roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . **. THEOTOKION.**

Geuko ya wenye-taabu, na uponyesho wa wagonjwa, uko Bikira Muzazi-Mungu. Okoe muji na taifa, Amani kwa wapigani, utulivu wa wateswa, peke yako mulinzi wa waaminifu.

## MU KAZI MBILI ASUBUI KATIKA SAUTI YA SITA

**KATHISMA YA KWANZA**

Nawaza siku ya ajabu ya hukumu na nalilia matendo yangu mabaya; nitasema nini kwa Mfalme msiyekufa? Nitasubutu nemna gani kumtazama Mwamuzi wangu mimi maskini? Ee Baba Mwema kamili, Mwana wa pekee na Roho Mtakatifu, unihurumie, ee Bwana.

Ee Mungu wa mapendo, kwa machozi yangu mengi; mahali hapa ulipochagua kwa kuketi na kutoa hukumu ya haki usifumbuo siri za moyo wangu ili nisipate haya mbele ya Malaika wako, lakini, ee Mungu wangu, unihurumie, ee Bwana.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . **. THEOTOKION.**

Mwana tena Neno la Mungu, aliyezaliwa kwa Baba mbele ya nyakati, bila msaada wa mama, kwa nyakati za mwisho akazaliwa mwili tumboni mwako mwa ubikira, ee Mzazi-Mungu. Utuombe atuondolee zambi zetu mbele ya mwisho.

**KATHISMA YA PILI**

Utuhurumie, ee Bwana, utuhurumie, kwa kuwa sisi watu wenye zambi, hatuna teto yoyote kukuileta, ila ombi huu tunakutolea kwako, uliye Rabi, utuhurumie.

Ee Bwana, utuhurumie, kwa kuwa tunategemea kwako. Usituazibu sana, wala kuzikumbuka zambi zetu. Lakini hata sasa utangalie, kama mwenye huruma, ukatuokoe na maadui wetu. Kwa kuwa wewe u Mungu wetu, tena sisi watu wako. Sisi zote viumbe vya mikono yako; jina lako tunaliita.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Matumaini ya ulimwengu, bikira Mzazi-Mungu, naomba ulinzi wako wa pekee wenye kuongoza heshima; hurumia taifa lenye kusongana ku upande wako, umusihi Mungu ili atuonyeshe mapendo yake akiokoa roho zetu ku azabu zote, ee Bikira mbarikiwa katika wote.

**KATHISMA YA TATU**

Kama ulivyowaonyesha watu njia za uzima, ee Mtakatifdu Yoane, ulipowalalamikia. Tengenezeni mioyo yenu kwa Bwana, okoa roho yangu yenye kuelemezwa za zambi, huruma ugumu wa akili yangu, kwa maombezi yako uniokoe ku azabu ya milele, ee Mtangulizi wa mwokozi.

Kama washindani katika uwanja, ndivyo walivyopigana wazulumu juu ya mashahidi; makundi ya Malaika waliwatayarishia taji la Washindaji; hekima yao iliwasangaza wazulumu na wafalme; walimushinda shetani walipomuungama Kristu. Wewe uliyewapa nguvu, ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira Mtakatifu kamili, nakimbilia kwako nikitafuta wokovu, ee Mzazi-Mungu, zambi zangu ni ningi mno; tazama roho yangu zaifu, umuombe Mwana wako na Mungu wetu anisamehe matendo yangu mbaya, peke yako Bikira mbarikiwa katika wote.

**APOSTIKHA**

Ee Mwokozi, ponyesha vidonda vya moyo wangu wenyi kujeruhiwa na zambi nyingi, kwani ndiwe mganga wa roho na wa miili; kwa wale wenyi kukuomba unawasamehe zambi, unipe machozi ya toba na maondoleo ya makosa yangu*:* Ee Bwana mwenyezi, unihurumie.

Nilipotwaliwa nguvu, adui akanipiga mshale wa zambi, lakini wewe, ee Mganga wa roho na wa miili, ponyesha vidonda vya roho yangu; ee Mungu wa mapendo, unihurumie.

Ee Bwana, kama hatunolikuwa na usimamizi wa watakatifu wako na matumaini ya wema wako wa huruma, namna gani tutasubutu kukuimbia, ewe Mwokozi mwenye kutukuzwa milele na Malaika? Wewe mwenyi kuvumbua yenyi kuwa moyoni mwa wanadamu, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Hakuna mutu aliyekimbilia kwako na kutoka mwenyehaya, ee Bikira Mzazi-Mungu. Lakini anaomba neema, na anapata zawadi, kwa ajili ya vilivyo faa alivyoomba.

## MU KAZI PILI MANGARIBI KATIKA SAUTI YA SITA

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.** *I apegnosmeni.*

Ee Bwana mwenyi kutaka kuwaokoa wanadamu wote, tazama ombi langu, ulisikilize, usikatae kulia kwangu; nani alafu akikujongea akiomba hataokolewa palepale? nani aliyekulalamikia na moyo wake bila kusikilizwa palepale? Kwani, unapatikana mwepesi kwa huruma yako kwa wote wale wenyi kutafuta wokovu kwako.

Ee Mungu wa mapendo, kwa mapendo yako kwa ajili yangu, uniondoe shimo ya zambi, uniamushe ku shimo ya furaha, usiruhusu niwe mchezo wa shetani, usinikatalie mafumbo yako ya ajabu, lakini mbele ya mwisho wangu, ee Bwana wa huruma, pokea sikitiko na machozi yangu na uniokoe ku mateso yangu.

Lia, ee roho yangu, mbele ya mwisho, sujudu na toba mbele ya Muumba, umutolee machozi yako kwa moyo wako wote, umwambie Kristu, ukijaa na huzuni. Ee Neno, nimekosa,

unipokee japo zambi zangu nyingi, ee Mwamuzi wa hiki, usinichukie, unitazame, na kwa huruma wako wa milele usinitupe katika moto, ee Bwana mvumilivu.

**Wimbo ya Mzazi-Mungu.**

Arusi ya Bwana Arusi wa mbinguni ni tayari, ndivyo wanayosema watangazaji; ewe roho yenyi kuchafuka, kwa nini unakawia? kweli, mavazi yako iko mchafu sababu ya matendo yako mbaya; ole wako, namna gani utafanya kwa kuingia? Mbele ya mwisho sujudu, ukimulalamikia na moyo wako wote Bikira daima. Ee Bikira Mtakatifu, unitakase, unisafishe kwa hisopo ya maombezi yako na unistahilishe ku arusi ya mwana wako ili nikutukuze daima.

Ee Bikira, Nabii Isaya kwa usafi wa roho yake akaonea mbali ya kama unapashwa kuzaa Muumba wa viumbe vyote, kwani, ee Mtakatifu kamili, tangu zamani ulionekana peke yako usiye na doa; ndio maana nakuomba utakase unajisi wa moyo wangu na unisharikishe ku nuru kimungu ya Mwana wako ili nisimame kuume kwake wakati atakapokaa, kama inavyoandikwa, kuhukumu dunia yote.

Ee Rabi, zamani kahaba alipomwangia manukato yake ku miguu yako, akaokolewa ku zambi zake zote; kwa munyanganyi ilitosha kumkumbuka mtumishi wako na palepale ikamwingiza katika Paradizo; na mimi maskini nitafanya nini? Sina wala manukato wale sikitiko. Unihurumie bure, unisamehe, ee Neno la Mungu, kwa maombezi ya Mama wako Mtakatifu kamili uliyeleta duniani kama makimbilio ya waovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . **. STAVROTHEOTOKION.**

Ee Mwanangu, Waamzi wa Israeli wakaamua kukuhukumu ufe, wakakusambisha kama mshitakiwa mbele ya baraza ya hukumu, ewe Mwokozi mwenyi kuwahukumu wazima na wafu; wakakupeleka ku hukumu ya Pilato, wao makafiri, lakini wakatangulia kukuhukumu mbele ya maamzi; nikiona haya najeruhiwa na nagawanya, ee Bwana, hukumu yako, kwani nataka kufa kuliko uzima wenyi kujaa na malalamiko, ndivyo alivyosema Mzazi-Mungu peke yake mwenyi huruma.

**APOSTIKHA**

Ee Bwana, kwa watu wako Msalaba wako ni uzima na ulinzi; tunapotumainia, tunakuimbia: ee Mungu uliyesulubiwa mwilini, utuhurumie.

Ee Bwana, Msalaba wako uliwafungulia wanadamu milango ya Paradizo; tunapokombolewa kaburini, tunakuimbia: Ee Mungu uliyesulubiwa mwilini, utuhurumie.

Mashahidi watukufu wakaaji wa inchi ya mbinguni, walipoanindana duniani wakateswa mateso mengi; kwa maombezi yao na kwa maombi yao, ee Bwana, utulinde.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . **. STAVROTHEOTOKION.**

Ee Kristu, wakati alipokuona umesulubiwa, Msalabani huyu aliyekuzaa akalalamika: Ee Mwanangu, ni fumbo gani hii ya ajabu naona, namna gani unaweza kufa mwilini kutundikwa Msalabani, ee Mfalme wa uzima?

## MU KAZI TATU ASUBUI KATIKA SAUTI YA SITA

### KATHISMA YA KWANZA

Ee Kristu, tangu ilisimikwa muti wa Msalaba wako, ukaregeza nguvu za mauti; Hadeze ikajiharikisha kumeza huyu atakayerudisha na woga. Ee Mungu Mtakatifu, ulituonyesha wokovu na tunakutolea utukufu*:* Ee Mwana wa Mungu, utuhurumie.

Ee Bwana, wana wa Israeli walikuhukumu ukufe, wewe uzima wa ulimwengu wote; wao waliyovuka Bahari Nyekundu kwa sababu ya bakora ya Musa, wakakupigilia misumari Msalabani; wao waliyofunza sali ya mwamba, wakakupa nyongo kuwa chakula; lakini uliteswa kwa kutaka kwako ili tukombolewe ku utumwa wa adui. Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Kristu, Mama Bikira daima aliyekuzaa alipokuona umeteswa kwa ajili yetu Msalabani, moyo wake ukachomwa kwa huzuni na akalia; Kwa maombezi yake, utuhurumie.

## KATHISMA YA PILI

Leo limetimia neno la Nabii*:* Tazama tunasujudu mahali palipokanyanga miguu yako, ee Bwana, tulipoonja muti wa wokovu, tumefunguliwa ku mateso yetu na ku zambi kwa maombezi ya Mzazi-Mungu.

Ee Bwana, Msalaba wako, imetakaswa*:* Inawaponyesha wale waliyeregea katika zambi; katika hii tunakuomba*:* Utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Alipomuona Mungu aliyezaa mwilini ametundikwa Msalabani kama mufu, kwa machozi Bikira akalalamika: Ee Mwanangu, kuvumilia kwako kumenisangaza! Namna gani makafiri walikupigilia misumari kama muhukumiwa Msalabani, wewe Mwamzi wa haki na Bwana pake yako?

## KATHISMA YA TATU

Kwa mutu wa kwanza muti uliyokataziwa katika shamba la Edeni ukamuletea kufa, wakatipo kule Kalvario muti wa Msalaba unastawisha uzima; Adamu akadanganywa kwa uovu wa adui, lakini wakati Kristu aliposulubiwa juu ya muti, akasemehewa na karudi katika paradizo, kalalamika: Utukuzwe muti wa Msalaba.

Watakatifu walishindana mashindano bora, wakapokea kwako tunzo ya Washindaji; na walipozarau hukumu ya makafiri, wakapata utukufu wa milele; kwa maombezi yao, ee Mungu wetu, utupe sisi neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Mzazi-Mungu na Bikira mbarikiwa, umuombe Mwana wako, Kristu Mungu wetu, aliyejiachilia kupigiliwa Msalabani sababu ya kuokoa ulimwengu ku udanganyifu, ahurumie roho zetu.

## APOSTIKHA

Natumainia Msalaba wako, ninapotukuzwa katika hii, nalalamika: Ee Bwana Mpenda-wanadamu, shusha majivuno ya wale wasiyotambua ya kuwa ndiwe kweli Mungu-mutu.

Tunapolindwa na boma la Msalaba wako, tunashindana na adui bila kuogopa werevu wake na mashambulio yake, kwani mwenyi majivuno ameangamizwa na ameshindwa kwa uwezo wa Kristu aliyesulubiwa juu ya muti.

Makumbusho ya mashahidi inawafurahisha wale wenye kumuogopa Bwana*:* Waliposhindana juu ya Kristu, wakapata utukufu mbinguni, na sasa wana uwezo wa kuomboa roho zetu wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Alipokuona umetundikwa Msalabani, Mzazi-Mungu Mtakatifu kamili kwa machozi akakulalamikia: Ee Mwanangu na Mungu wangu, ee mwanangu mupenzi, namna gani unaweza kuteswa hii Mateso isiyo ya haki?

## MU KAZI TATU MANGARIBI KATIKA SAUTI YA SITA

**Wimbo ya Mitume.** *Olin apothemeni.*

Walipopokea nguvu ya mbinguni ya Roho Mtakatifu, Mitume wa Kristu wakafukuza majeshi ya adui; wakanyamazisha wenyi hekima na wakawashinda wafalme, bila elimu wala maarifa, bila kanzu ya chuma na bila silaha ya vita, paka na Evangeli, walifanya maajabu kwa neno la kweli na wakawasukuma watu ku muti Kristu, sasa wanaombea na nguvu roho zetu.

Kwa mapendo yao kwa ajili yako, Mashahidi watukufu wakajikatalia wao wenyewe, wakakufwata na moyo wao wote; kwa kukufwata na walipobeba Msalaba wao sababu ya kutii ku amri yako, wakaacha dunia, na kwa uriti wakapokea mbingu na wakawaongoza watu kwa kukufahamu, ee Bwana. Walipokuwa wasiri wako milele, ni na nguvu wanaombea sasa roho zetu.

Nilipoishi maisha yangu yote katika uzaifu, nafika ku mwisho bila matunda, nachukua paka mzigo mbaya wa matendo yangu mbaya, ee Mungu wa wema, ewe Mpenda-wanadamu, uyazime kwa nguvu ya mapendo yako na unipe niyasikitike, uniongoze ku wokovu, kwa maombezi matakatifu ya Mitume wako, ee Mungu wangu, pamoja na yale ya huyu aliyekuzaa.

**Wimbo ya Mtakatifu Nikola.**

Ee mwenyi heri Nikola, unihurumie mimi, ninayesujudu mbele yako, angaza macho ya roho yangu ili nitazama kwa usafi wote Bwana mwenyi kutuangaza na unihurumie.

Uniopoe, ee Mtakatifu Nikola, kwa maadui wenyi kunipeleleza ili wanitendee ubaya, wewe uliye na deni kwa Mungu; uniokoe ku haya, Mtakatifu mkuu na uniopoe kwa watu wa damu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bibi Mtakatifu tena Mzazi-Mungu uliyezaa duniani Muumba wa ulimwengu, pamoja na Mitume watakatifu umuombe kila siku kwa wema wake atuokoe ku mateso na atuondolee zambi zetu.

### APOSTIKHA

Ee Kristu, zamani wafuasi wako walipotikiswa katika chombo, wakalalamika: ee Rabi, utuokoe, tunakufa. Sasa sisi wenyewe tunalalamika: Ee Mwokozi Mpenda-wanadamu, tunakuomba, utuopoe ku hatari yoyote.

Ee Bwana, Mitume wako waligusa chini ya bahari kwa nyavu zao, urefu wa Ufalme kwa mafundisho yao; kwa mahubiri yao walitafuta maarifa makuu ya chini kabisa, kwa imani yao makatezamia moyo wako wa milele, wakahubiri duniani Mwana wako asiye wa nyakati; kwa maombezi yao na kwa yale ya watakatifu wote, utuhurumie.

Ee Bwana, Msalaba wako umekuwa kwa Mashahidi utukufu usiyeweza kushindwa; walipoona lufu iliyowapeleleza na walipotangulia kuona uzima gani unawaongojea, wakapata nguvu kwa matumaini waliyokutumainia wewe; kwa maombezi yao, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, ndiwe kweli Mzabibu uliyestawisha tunda la uzima; ee Bibi wetu, tunakuomba: Katikati ya Mitume na ya watakatifu wote, uombe kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

## MU KAZI INE ASUBUI KATIKA SAUTI YA SITA

### KATHISMA YA KWANZA

Kama ulivyoonekana katikati ya Wafuasi wako ukiwapa amani, kuja pia kati yetu, ee Mungu Mwokozi na uniokoe.

Mulivyoonekasna nuru kimungu duniani, kwa mafundisho yenu ya hekima muliangaza ulimwengu na kwa maarifa ya Mungu mulifukuza giza za miungu ya uongo, mukiangaa na mwanga safi wa Utatu Mtakatifu na mukiona watu wengi ku udanganyifu wa giza, enyi Mitume wa Mwokozi.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Utufungulie mulango wa huruma, ewe Mzazi-Mungu mubarikiwa. Tukikutumaini wewe, tutakuwa bila kuanguka. Kwako tutaziepuka taabu; Kwa kuwa wewe wokovu wa muzao wa wakristu.

### KATHISMA YA PILI

Ee Bwana, makumbusho ya Mitume wako inakumbusha Mateso ya Edeni; katika hii viumbe vyote vinafurahiwa, na kwa maombezi yao utupe, ee Bwana, amani na neema ya wokovu.

Ee Bwana, Mitume wako kumi na wa wili wameonekana duniani kama jua lenyi mianga kumi na miwili; katika wao ukateketeza giza ya udanganyifu, katika wao ukangaza roho za watumishi wako; katika wao, ee Bwana wa huruma, tunakuomba utuokoe sisi pia.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bibi Mtakatifu tena Mzazi-Mungu uliyezaa duniani Muumba wa ulimwengu, pamoja na Mitume Watakatifu umuombe kila siku kwa wema wake atuopoe ku mateso na atuondolee zambi zetu.

### KATHISMA YA TATU

Walipojazwa vyombo vyao kwa sababu ya wavu wa imani, Wavuvi wa watu wakaondoa ku shimo ya udanganyifu wote wale waliyotolewa kwa Mungu wetu kama waabudu kwa kumutukuza daima.

Ee Bwana, makumbusho ya Mitume wako inatukumbusha Paradizo na shamba ;a Edeni; katika hii viumbe vyote vinafurahiwam na kwa maombezi yao, ee Bwana, utupe amani na neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Tunaposimama katika hekalu ya utukufu, tunazania kuwa mbinguni, ee Mzazi-Mungu, mulango wa mbinguni, utufungulie mulango wa huruma yako.

### APOSTIKHA

Ee Kristu, zamani Wafuasi wako walipotikiswa katika chombo, wakalalamika: Ee Rabi, utuokoe, tunakufa! Sasa, sisi wenyewe tunalalamika: Ee Mwokozi Mpenda-wanadamu, tunakuomba, utuopoe ku hatari yoyote.

Ee Bwana, Mitume wako waligusa chini ya bahari kwa nyavu zao, urefu wa ufalme kwa mafundisho yao; kwa mahubiri yao walitafuta maarifa makuu ya chini kabisa, kwa imani yao wakatezamia moyo wako wa milele, wakahubiri duniani Mwana wako asiye wa nyakati; kwa maombezi yao na kwa yale ya Watakatifu wote, utuhurumie.

Mungu wetu akawa wa ajabu kwa Watakatifu aliyochagua. Mume na furaha na sherehe ninyi wote wenyi kumutumikia, kwani amewatukuza ninyi katika ufalme wa mbinguni: Tunawaomba ninyi musitusahau.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Umejaliwa na vipaji kimungu, ee Bikira Mtakatifu kamili na Mzazi-Mungu, kwani ni Mmoja wa Utatu Mtakatifu, Kristu chemchem ya uzima, uliyezaa mwilini kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

## MU KAZI INE MANGARIBI KATIKA SAUTI YA SITA

**Wimbo ya Usulubisho.** *Triimeros anestis Kriste.*

Ee Mpenda-wanadamu, Bwana mvumilivu, Mungu wa mapendo na wa huruma, namna gani unatolewa na kufa Msalabani kwa ajili ya wanadamu? Tunatukuza huruma yako kwa sisi.

Ee Bwana mvumilivu, unateswa kwa kupigwa, kusulubiwa, unafezeheshwa, unataka kutukomboa ku mkono wa mudanganyifu na unateswa yote hii, ewe Mungu wa mapendo peke yako mwenyi kutupatia uzima.

Ee muchungaji Mwema, ulipanda Msalabani na ulipanua mikono ukasema: Njioni kwangu mangaziwe, enyi watu wenyi mauti wneyi kutiishwa ku giza ya udanganyifu, Mimi ni Nuru! Ee chemchem ya nuru, utukufu kwako.

**Wimbo ya Mzazi-Mungu.**

Ee Bikira, inua roho yangu yenyi kuelemezwa na mzigo mzito wa zambi zangu. Kama Mama una uwezo wa kumsubitisha upesi Mwokozi ambaye yeye mwenyewe alikuja kuinua roho zaifu; pasua pia daftari ya zambi zangu kwa huruma yako kubwa na kwa usimamizi wako takatifu.

Tazama, nakosa matumaini sababu ya zambi zangu, nilipochafuka kwa makosa yangu, nilipozarau mafundisho takaitfu. Usinitupe mabli ya uso wako; ndiwe kweli matumaini yangu na ulinzi wangu. Ee Mzazi-Mungu, sikiliza mwito wangu, unitakase ku uovu wote kwa huruma yako kubwa na kwa usimamizi wako takatifu.

Unifungulie mlango wa toba, unipe chemchem ya machozi, unipe kiasi na huzuni; wewe peke yako nakutaja kama ulinzi wangu wa kweli; matumaini yangu yote naiweka kwako; usinifukuze nikijaa na haya, lakini kwa huruma yako kubwa unipokee na uniokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Alipokuona umepigiliwa Msalabani, Mtakatifu kamili akalalamika: Ee Mwanangu na Mungu wangu, ni habari gani mupya na isiyoonekana, hii Mateso unayoteswa kwa mapendo yako ya milele.

### APOSTIKHA

Ee Bwana, kwa watu wako Msalaba wako ni uzima na ulinzi; tunapotumainia, tunakuimbia: Ee Mungu uliyesulubiwa mwilini, utuhurumie.

Ee Bwana, Msalaba wako uliwafungulia wanadamu milango ya Paradizo; tunapokombolewa kaburini, tunakuimbia: Ee Mungu uliyesulubiwa mwilini, utuhurumie.

Ee Kristu, Mashahidi wako waliteswa mateso mengi, mwisho wakapokea utukufu mbinguni ili waombee roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Zamani, Bikira aliposimama chini ya Msalaba pamoja na Mfuasi wakati wa kusulubiwa, kwa machozi akalalamika: Ole wangu, namna gani unateswa, ee Bwana mwenyi kuwapa watu wote uzima wa milele.

## MU KAZI TANO ASUBUI KATIKA SAUTI YA SITA

### KATHISMA YA KWANZA

Leo limetimia neno la Nabii*:* Tazama tunasujudu mahali palipokanyanga miguu yako, ee Bwana, tulipoonja muti wa wokovu, tumefunguliwa ku mateso yetu na ku zambi kwa maombezi ya Mzazi-Mungu.

Ee Kristu, tangu ilisimikwa muti wa Msalaba wako, ukaregeza nguvu za mauti; Hadeze ikajiharikisha kumeza huyu atakayerudisha na woga. Ee Mungu Mtakatifu, ulituonyesha wokovu na tunakutolea utukufu*:* Ee Mwana wa Mungu, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Bikira Mzazi-Mungu, peke yako kondoo asiye na kilema, wakati ulimwona huyu uliyezaa tumboni mwako safi, kwa machozi ukalalamika: Ee Mwanangu mupole, naimbia tendo lako la wokovu.

### KATHISMA YA PILI

Ee Bwana, Msalaba wako, imetakaswa*:* Inawaponyesha wale waliyeregea katika zambi; katika hii tunakuomba*:* Utuhurumie.

Ee Bwana, wana wa Israeli walikuhukumu ukufe, wewe uzima wa ulimwengu wote; wao waliyovuka Bahari Nyekundu kwa sababu ya bakora ya Musa, wakakupigilia misumari Msalabani; wao waliyofunza sali ya mwamba, wakakupa nyongo kuwa chakula; lakini uliteswa kwa kutaka kwako ili tukombolewe ku utumwa wa adui. Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Aliposimama karibu ya Msalaba, Bikira na Mama wa Huyu aliyezaa mwilini bila uchungu, kwa uchungu wake na umama akalalamika: Sitavumilia kukuona umeuawa na umetundikwa Msalabani, wewe mwenye kuleta duniani pumuzi kwa kila mwenyi uzima, ee Mwanangu na Mungu wangu.

### KATHISMA YA TATU

Ee Muti mbarikiwa wa Msalaba, unapoponyesha wagonjwa na kufukuza mashetani, nguvu na mulinzi wa waminifu, utukufu wa Wafalme, usabiti kweli wa waorthodoksi, tegemeo ya Eklezya ya Kristu, uwe ulinzi wetu, matumaini yetu na boma letu.

Kwa wenyi haki ni nuru ya milele. Walipoangazwa na nuru yako, Watakatifu wanangaa daima kama nyota za kuangaza, wakififisha taa ya makafiri; kwa maombezi yao, ee Bwana na Mwokozi, angaza roho yangu na uniokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu Mtakatifu kamili, usiniache katika muda wote wa maisha yangu, usinitoa ku ulinzi wa wanadamu, lakini wewe mwenyewe unilinde na unihurumie.

**APOSTIKHA**

Natumainia Msalaba wako, ninapotukuzwa katika hii, nalalamika: Ee Bwana Mpenda-wanadamu, shusha majivuno ya wale wasiyotambua ya kuwa ndiwe kweli Mungu-mutu.

Tunapolindwa na boma la Msalaba wako, tunashindana na adui bila kuogopa werevu wake na mashambulio yake, kwani mwenyi majivuno ameangamizwa na ameshindwa kwa uwezo wa Kristu aliyesulubiwa juu ya muti.

Ee Bwana, kukumbuka mashahidi wako ni siku Kuu kubwa kwa viumbe vyote; dunia ya wanadamu inafurahi pamoja na Malaika mbinguni; kwa maombezi yao, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira Mama Mtakatifu, kwa ubinadamu wangu walinipigilia Msalabani nilikuwa na niliwekwa bila uzima kaburini; kwa umungu wangu, ni katika utukufu nitafufuka siku ya tatu.

## MU KAZI TANO MANGARIBI KATIKA SAUTI YA SITA

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.** *I apegnosmeni*

Uniokoe ku gehena yenyi kuniongojea, uniondoe ku moto ya milele, ee Mwamuzi wa haki, nimekwisha kuhukumiwa; fanya ili nitoke salama, ee Neno la Mungu, ku zoruba yenyi kutaka kuniangamiza; natetemeka, nikiwaza zambi zangu nyingi; nasujudu mbele yako nikilia, ee Mpenda-wanadamu, na sikitiko ya moyo wangu, nikikuomba ee Bwana, uhuruma yako.

Nani hatanililia? Kwa ubaya wangu nimevunja amri ya Bwana; nilikaa katika Hadeze pahali pa Paradizo; utamu wa tunda umegeuka kuwa uchungu wa nyongo; nimejitenga ku utukufu wako na ku ule wa Malaika, lakini kubali kuongoka kwangu, kwa mapendo yako kwa wanadamu, ee Mungu wa mapendo na wa huruma.

Ee chemchem ya uzima, weka marehemu waaminifu wote pa inchi ya wazima, mahali pa mapumziko, katika hema za mbinguni, kule kunangaa uso wako na nuru, kule wenyi haki wanaonja raha kubwa, furaha na amani, bila kutazama zambi walitenda kwa maneno, kwa matendo, za kujua wala bila kujua, ee Bwana wa wema.

**Wimbo ya mashahidi.**

Ee Kristu, Mashahidi wako waliteswa mateso mengi, mwisho wakapokea utukufu mbinguni ili waombee roho zetu.

Mashahidi watukufu wakaaji wa inchi ya mbinguni, walipoanindana duniani wakateswa mateso mengi; kwa maombezi yao na kwa maombi yao, ee Bwana, utulinde.

Ee Bwana, Msalaba wako umekuwa kwa Mashahidi utukufu usiyeweza kushindwa; walipoona lufu iliyowapeleleza na walipotangulia kuona uzima gani unawaongojea, wakapata nguvu kwa matumaini waliyokutumainia wewe; kwa maombezi yao, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. **THEOTOKION**

Nani hatakuita wewe mwenye heri, Bikira Mtakatifu kamili? Nani ataimba kuzaliwa kwa Mwana wako bila mume? Kwani Mwana wa pekee aliyeangaa mbele ya wakati kwa Baba, yeye vilevile alitokea kwa wewe uliyesafi, akitwa mwili usiyosemwa; yeye ni Mungu sawasawa na hali yake, na akajifanya mutu kwa kadiri ya hali ya watu kwa ajili yetu; yeye hagawanyike kwa uso mbili, lakini anajulikana kwetu katika hali mbili bila muchanganyo. Umusihi, ee Bikira mutaratibu na heri daima, kwa kurehemu nafsi yetu.

**APOSTIKHA**

Ee Bwana, Mashahidi wako hawakukukana, hawakujitenga ku mafundisho yako: Kwa maombezi yao utuhurumie.

**Wimbo ya wafu.**

*Shairi:* Heri wale uliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe, ee Bwana.

Kwa neno lako la uumbaji uliniruhusu nizaliwa na niishi, kwa kunifanya mtu mzima uliunganisha ndani yangu yenyi kuonekana na isiyoonekana, kwa udongo ukaumba mwili wangu, ukanipa vilevile roho kwa pumuzi yako kimungu na yenyi kuleta uzima; ndie maana, ee Mungu Mwokozi, uwapumzishe watumishi wako katika hema za wenyi haki pa inchi ya wazima.

*Shairi: Na makumbusho yao ni ya milele.*

Adamu akapata uchungu wakati alipoonja tunda iliyokataziwa zamani katika shamba la edeni, kwani nyoka akamwingiza sumu yake, na katika huyu mauti yenyi kuwaangamiza wanadamu ikaingia duniani; lakini Bwana alikuja, akamuua yule nyoka na akatupatia mapumziko; tumulalamikie: Ee Bwana Mwokozi zamehe wale uliyochukuwa pamoja nawe, na uwapumzishe kati ya wateule wako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. **THEOTOKION**

Ee Kristu, kwa maombezi ya huyu aliyekuzaa, ya Manabii, ya Mitume, ya Mashahidi, ya Wakubwa wa dini, ya Wenyi heki, ya Wenyi heri, na kwa maombezi ya Watakatifu wote, uwape marehemu watumishi wako mapumziko ya milele.

## MU POSHO ASUBUI KATIKA SAUTI YA SITA

### KATHISMA YA KWANZA

Kama washindani katika uwanja, ndivyo walivyopigana wazulumu juu ya mashahidi; makundi ya Malaika waliwatayarishia taji la Washindaji; hekima yao iliwasangaza wazulumu na wafalme; walimushinda shetani walipomuungama Kristu. Wewe uliyewapa nguvu, ee Bwana, utukufu kwako.

Watakatifu walishindana mashindano bora, wakapokea kwako tunzo ya Washindaji; na walipozarau hukumu ya makafiri, wakapata utukufu wa milele; kwa maombezi yao, ee Mungu wetu, utupe sisi neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. **THEOTOKION**

Wewe uliyemuita Mama yako «Mwenyi Heri» na uliyeteswa kwa kutaka kwako, nuru yako iliangaa Msalabani, kwani ulitaka kwenda kumtafuta Adamu; ukawaambia Malaika: Furahini

pamoja nami, kwani imepatikana drakma iliyopotea. Wewe uliyefanya yote kwa hekima, utukufu kwako, ee Bwana Mungu wetu.

**KATHISMA YA PILI**

Ee Bwana, makumbusho ya mashahidi wako inatukumbusha Paradizo na shamba ;a Edeni; katika hii viumbe vyote vinafurahiwam na kwa maombezi yao, ee Bwana, utupe amani na neema ya wokovu.

Kweli, yote ni ya bure! Uzima unapita kama ndoto, kama kivuli, wafu wanaogopoa bure, kama yanavyosema Maandiko; wakati tutakapoondoka Mlimwenguni, tutakaa lakini kaburini, maskini kama watajiri. Na tena, ee Kristu Mungu wetu, kwa mapendo yako kwa wanadamu, uwape marehemu watumishi wako mapumziko.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. **THEOTOKION**

Mulinzi wa nguvu na makimbilio ya wafu, ee Mzazi-Mungu na Bikira Maria, wewe uliyezaa kwa wakati. Mwana asiye wa wakati na Neno la Mungu, kama Mama umuombe daima pamoja na Malaika, Mashahidi na Watawa Watakatifu aokoe marehemu waaminifu.

## APOSTIKHA

*Nyimbo za Rabi*

Ee Bwana, kukumbuka mashahidi wako ni siku Kuu kubwa kwa viumbe vyote; dunia ya wanadamu inafurahi pamoja na Malaika mbinguni; kwa maombezi yao, utuhurumie.

Ee Bwana, kama hatungelikuwa na usimamizi wa watakatifu wako na matumaini ya wema wako wa huruma, namna gani tutasubutu kukuimbia, ewe Mwokozi mwenye kutukuzwa milele na Malaika? Wewe mwenyi kuvumbua yenyi kuwa moyoni mwa wanadamu, utuhurumie.

Makumbusho ya Mashahidi inawafurahisha wale wenye kumuogopa Bwana*:* Waliposhindana juu ya Kristu, wakapata utukufu mbinguni, na sasa wana uwezo wa kuomboa roho zetu wokovu.

Mungu wetu alifanya maajabu katika watakatifu aliyochagua. Furahini na shangilieni ninyi wote wenyi kumutumikia, kwani aliwatukuza ninyi katika ufalme wa mbingu*:* Tunawaomba ninyi msitusahau.

*Wimbo ya wafu.*

Adamu akapata uchungu wakati alipoonja tunda iliyokataziwa zamani katika shamba la Edeni, kwani nyoka akamwingiza sumu yake, na katika huyu mauti yenyi kuwaangamiza wanadamu ikaingia duniani; lakini Bwana alikuja, akamuua yule nyoka na akamupatia mapumziko; tumulalamikie*:* Ee Bwana Mwokozi samehe wale uliyochukuwa pamoja nawe, na uwapumzishe kati ya wateule wako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. **THEOTOKION**

Ni wewe Mungu wetu, uliumba ulimwengu na hekima na ukaijaza na vitu vyote, ee Kristu, uliwatuma manabii kwa kutangaza majilio yako na Mitume kutangaza mapendo yako ya juu mbinguni: Wamoja waliagua kuja kwako, wengine kwa ubatizo waliangaza mataifa; kwa mateso yao Mashahidi wakapata kisa ya hamu yao na kundi yao inaomba kwako pamoja na yule aliyekuzaa. Ee Mungu, pumzisha roho za wale uliyochukua, na utustahilishe ku ufalme wa mbinguni, wewe ambaye, kwa kuzima hukumu yangu, uliteswa Msalabani, Mwokozi wangu na Mungu wangu.

**EKSAPOSTILARION YA SIKU**
*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

Elezo: *Kama kuna Alliluya, tunaimba ku masifu nyimbo za mashahidi zenyi kutangulia hapa juu, na kama Apostikha tunaimba Mifano (Prosomia) yafwatayo:*

**APOSTIKHA**
**(Wimbo ya wafu)**

*Sauti ya sita.. Olin apothemeni.*

Ee Bwana, kwa mapendo isiyokadirika unaye kwa ajili yetu na kwa chemchem isiyokwisha ya wema wako, pokea wafu katika inchi ya wazima, uwaweke katika hema ya milele, ukiwawekea furaha ya mema waliyotamainia, kwani ulimwanga damu yako, ee Kristu, kwa kuikomboa dunia na bei ya uzima wake.

*Shairi:* Heri uliyochagua, wale uliyochukua pamoja ee Bwana.

Kwa sisi kuishi uliitikia kufa, ulitirikisha chemchem ya uzima, kwa waaminifu unawapa heri ya milele*:* Uipane pia kwa wale waliyolala katika matumaini ya ufufuo, kwa wema wako zima zambi zao zote, kwani peke yako usiye na zambi; utuonyeshe mapendo yako ili litukuzwa jina lako, na tukiokolewa nawe, ee Kristu, tukutukuze milele.

*Shairi:* Na makumbusho yao ni ya milele.

Ee Kristu, tunajuwa ubwana wako kimungu juu ya wazima na wafu; uwape watumishi waaminifu wako waliyomupata mfazili wao pekee yako makao ya watule wako, mahali pa baridi, katika utukufu wa Watakatifu wako, kwani ndiwe Mungu uliye na huruma na mwenyi kuokoa kwa wema wako wale uliyeumba kwa mfano wako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira Mtakatifu kamili, ni wewe makao ya Mungu, ulimulinda tumboni mwako na bila ndoa ulizaa mtu mmoja mwenyi hali mbili; umuombe Mwana wa pekee na mzaliwa wa kwanza aliyeacha salama ubikira wako hata kisha kuzaa awape waaminifu waliyolala na ibada mapumziko katika heri na nuru ya milele.

*Shairi:* Na makumbusho yao ni ya milele.

Ee Kristu, tunajuwa ubwana wako kimungu juu ya wazima na wafu; uwape watumishi waaminifu wako waliyomupata mfazili wao pekee yako makao ya watule wako, mahali pa baridi, katika utukufu wa Watakatifu wako, kwani ndiwe Mungu uliye na huruma na mwenyi kuokoa kwa wema wako wale uliyeumba kwa mfano wako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira Mtakatifu kamili, ni wewe makao ya Mungu, ulimulinda tumboni mwako na bila ndoa ulizaa mtu mmoja mwenyi hali mbili; umuombe Mwana wa pekee na mzaliwa wa kwanza aliyeacha salama ubikira wako hata kisha kuzaa awape waaminifu waliyolala na ibada mapumziko katika heri na nuru ya milele.

Kristu akitimiza unabii wa Daudi, katika Sayuni alifunua ukubwa wake kwa wanafunzi. Alijionyesha ya kama inafaa wasifu, na watukuze daima, pamoja na Baba na Roho Mtakatifu. Zamani watu walimusifu yeye, aliyekuwa Neno bila mwili, na sasa wanamusifu yeye aliyetwaa mwili kwa ajili yetu, na aliyekufa sawasawa na mutu, na aliyefufuka kwa mamlaka yake sawa mpenda-wanadamu.

Ulishuka Hadezeni, ewe Kristu, kama ulivyotaka, ulinyanganya mauti, kwani wewe ni Mungu na Rabi; na ulifufuka katika siku tatu, na toka minyororo ya Hadeze na toka uharibifu ulifufua Adamu pamoja nawe, aliyeita na aliyesema: Utukufu kwa Ufufuo wako, wewe peke mpenda-wanadamu.

Uliwekwa kaburini, sawa mwenye kulala, ewe Bwana na ulifufuka katika siku tatu, kama mwenyezi, ukifufua Adamu pamoja nawe toka uharibiofu wa mauti, sawa mwenyezi.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Ulijulishwa kama mama kuliko asili, ee Mzazi-Mungu; ulibaki Bikira isiyosikilikwa kwa neno na mawazo; na ajabu ya uzazi toka kwako, usiyoweza kufasiriwa katika lugha; kwani uchukuo wa mimba yako, ewe uliye Safi, ni wa ajabu, na namna ya mimba ni isiyosikilikwa; kwani popote Mungu anataka, usawa wa hali unashindwa; kwa hii sisi wote tukikujuwa sawa Mama wa Mungu, tunakushihi bila kushoka: Umupatanishe kwa wokovu wa nafsi yetu.

**APOSTIKHA**

Ulifufuka toka kaburi, ee Mwokozi wa dunia, na ulifufua watu pamoja na mwili wako; Bwana, utukufu kwako.

Kujeni tumwabudu yeye aliyefufuka katika wafu, na aliyeangaza wote; kwani yeye alituopoa, toka uzulumu wa Hadeze, kwa ufufuo wake wa siku tatu, akitupatia uzima na rehema kubwa.

Chini ya Hadeze ulikoshuka, ee Kristu, ulinyanganya mauti, na ulipofufuka katika siku tatu, ulitufufua sisi pamoja nawe, tuliyotukuza ufufuo wako wa uwezo, ee Bwana mpenda-wanadamu.

Ulionekana mustaajabu, ee Bwana, ukilala katika kaburi kama mwenye kulala usingizi. Tena ulipofufuka katika siku kama mwenyezi, ulifufua Adamu pamoja nawe, aliyepaza sauti: Utukufu ku ufufuo wako, ewe peke mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Sisi wote wanadamu, tukikimbilia chini ya kivuli yako, ee Bibi-Malkia, tunapaza sauti kwako: Mzazi-Mungu matumaini yetu, utuondoshe toka makosa isiyohesabiwa, na uokoe nafsi yetu.

# KIPANDE CHA SAUTI YA SABA
## MU POSHO MANGARIBI ESPERINOS MKUBWA
## STIKHIRA YA UFUFUO

Kujeni tushangilie kwa Bwana, aliyevunja nguvu ya mauti, na aliyeangaza uzao wa watu, tukipaza sauti pamoja na wasio-mwili: Muumba na Mwokozi wetu, utukufu kwako.

Mwokozi ulivumilia Musalaba na maziko kwa ajili yetu; sawasawa na Mungu kwa lufu yako uliua mauti; kwa hii tunaabudu ufufuo wako wa siku tatu; Bwana, utukufu kwako.

Wakati Mitume walipoona usimamao wa Muumba, walistaajabu wakiita sifa ya malaika. Hii ni utukufu wa kanisa, hii ni utajiri wa ufalme. Bwana, uliyeteswa kwa ajili yetu, utukufu kwako.

**INGINE STIKHIRA- ANATOLIKA**

Japo ulikamatwa, ewe Kristu, kwa wavunja-sheria, lakini wewe ni Mungu wangu na sifazaike; ulipigwa fimbo mugongoni, na sikuikataa; ulipigiliwa musalabani, na sikuificha; Ninajisifu kwa ajili ya ufufuo wako; kwani lufu yako ni uzima wangu. Bwana mwenyezi na mupenda-wanadamu, utukufu kwako.

Kristu akitimiza unabii wa Daudi, katika Sayuni alifunua ukubwa wake kwa wanafunzi. Alijionyesha ya kama inafaa wasifu, na watukuze daima, pamoja na Baba na Roho Mutakatifu. Zamani watu walimusifu yeye, aliyekuwa Neno bila mwili, na sasa wanamusifu yeye aliyetwaa mwili kwa ajili yetu, na aliyekufa sawasawa na mutu, na aliyefufuka kwa mamulaka yake sawa mupenda-wanadamu.

Ulishuka Hadezeni, ewe Kristu, kama ulivyotaka, ulinyanganya mauti, kwani wewe ni Mungu na Rabi; na ulifufuka katika siku tatu, na toka minyororo ya Hadeze na toka uharibifu Adamu pamoja nawe, aliyeita na aliyesema: Utukufu kwa ufufuo wako, wewe peke mupenda-wanadamu.

Uliwekwa kaburini, sawa mwenye kulala, ewe Bwana, na ulifufuka katika siku tatu, kama mwenyezi, ukifufua Adamu pamoja nawe toka uharibifu wa mauti, sawa mwenyezi.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...THEOTOKION

Sauti ya saba

Ulijulishwa kama mama kuliko asili, ee Muzazi-Mungu; ulibaki Bikira usiyosikilikwa kwa neno na mawazo; na ajabu ya uzazi toka kwako, usiyoweza kufasiriwa katika lugha; kwani uchukuo wa mimba yako, ewe Uliye safi, ni wa ajabu, na namna ya mimba ni isiyosikilikwa; kwani popote Mungu anataka, usawa wa hali unashindwa; kwa hii sisi wote tukikujuwa sawa Mama wa Mungu, tunakusihi bila kuchoka: Umupatanishe kwa wokovu wa nafsi yetu.

## APOSTIKHA SAUTI YA SABA

Ulifufuka toka kaburi, ee Mwokozi wa dunia, na ulifufua watu pamoja na mwili wako; Bwana, utukufu kwako.

Kujeni tumwabudu yeye aliyefufuka katika wafu, na aliyeangaza wote; kwani yeye alituopoa, toka uzulumu wa Hadeze, kwa ufufuo wake wa siku tatu, akitupatia uzima na rehema kubwa.

Chini ya Hadeze ulikoshuka, ee Kristu, ulinyanganya mauti, na ulipofufuka katika siku tatu, ulitutufua sisi pamoja nawe, tuliyotukuza ufufuo wako wa uwezo, ee Bwana mupenda-wanadamu.

Ulionekana mustaajabu, ee Bwana, ukilala katika Kaburi kama mwenye kulala usingizi. Tena ulipofufuka katika sisku tatu kama mwenyezi, ulifufua Adamu pamoja nawe, aliyepaza sauti: Utukufu ku ufufuo wako, ewe peke mupenda-wanadamu.

### THEOTOKION YA APOSTIKHA

Sisi wote wanadamu, tukikimbilia chini ya kivuli yako, ee Bibi,Malkia, tunapaza sauti kwako: Mzazi-Mungu matumaini yetu, utuondoshe toka makosa isiyohesabiwa, na uokoe nafsi yetu.

## APOLITIKION  SAUTI YA SABA

Uliharibu mauti kwa musalaba wako;  ulifungua Paradizo kwa munyanganyi;
ulibadilisha maombolezo ya wanawake wabebaji manukato, na uliamuru Mitume wako kuhubiri, kwamba ulifufuka, ee Kristu Mungu, ukileta duniani rehema kubwa.

## THEOTOKION  SAUTI YA SABA

Ewe Mwimbiwa kamili kama hazina ya ufufuo wetu, ututoshe sisi wenye kukuamini, toka shimo na vilindi vya makosa yetu; kwani wewe uliokoa wenye daraka ya zambi; ku uzao wa wokovu. Wewe ni Bikira mbele ya kuzaa, na Bikira katika kuzaa, na tena Bikira kisha kuzaa.

## SIKU YA MUNGU ASUBUI KATIKA SAUTI YA SABA

### KATHISMA YA KWANZA

Uzima wetu alilala kaburini, jiwe lilifungwa, maaskari walimulinda Kristu kama wanavyokeshea Mfalme; Malaika walimutukuza kama Mungu asiyekufa, wakatipo wanawake watakatifu wakalalamika: Bwana amefufuka, akileta neema ya wokovu duniani.

Kwa maziko yako ya siku tatu ulinyanganya ufalme wa mauti, kwa ufufuo wako wenyi kuleta uzima uliinua wanadamu ku uvumbi wa kaburini, ee Kristu Mungu wetu, mpenda-wanadamu, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Kristu Mungu wetu aliyesulubiwa kwa ajili yetu alifufuka na aliharibu nguvu ya mauti; ee Mzazi-Mungu, umuombe daima aokoe roho zetu.

### KATHISMA YA PILI

Ee Kristu Mungu wetu, japo kaburi ilifungwa, kama Uzima ulivyokufikia kule kaburini, na japo milango ilifungwa, ulionekana kwa Wafuasi wako ewe Ufufuo wa milele, ukitupatia mara ingine moyoni mwetu Roho wa ukweli kwa rehema yako kubwa.

Wanawake Watakatifu walikwenda mbio kaburini, wakilia machozi na wakichukua manukato; na wakati maaskari walikulinda kama Mfalme wa ulimengu, wakasema: Nani atatufingirishia jiwe kaburini? Lakini sauti ya Wabila-mwili ikasikilika ikawaambia: Amefufuka, Malaika wa baraza kuu, mshindaji wa mauti! Ee Mungu mwenyezi ambaye na fasi hata moja haiwezi kuzunguka, ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Salamu, Mjaliwa neema, Bikira Mzazi-Mungu, bandari na mulinzi wa wanadamu wote; Mkombozi wa ulimwengu amejifanya kwako mutu: Peke yako Mama na Bikira; unapobarikiwa daima na kujazwa na utukufu, umuombe Kristu Mungu wetu alete amani ku inchi yote wanaokaaa watu.

### IPAKOI

Ulichukua hali yetu, uliteswa mwilini mwako Msalabani; uniokoe, ee Kristu Mungu kwa ufufuo wako, ewe Mpenda-wanadamu.

## ANAVATHMI

*Sauti ya saba*

### ANTIFONON YA KWANZA

Bwana, wewe uliyerudisha wafungwa wa Sayuni toka upotevu wao, unirudishie mimi pia uzima ukiniopoa wa tamaa.

Huyu anayepanda jua kati katika machozi, kufunga na huzuni atavuna furaha kama chakula cha uzima wa milele.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Roho Mtakatifu ni chemchem ya hazina kimungu; analeta hekima, woga, ufahamu, sifa na utukufu, uwezo na heshima ni kwake.

## ANTIFONON YA PILI

Kama Bwana mwenyewe hajenge roho yetu kuwa nyumba, tunateswa bure; bila yeye maneno na matendo hayatakoma.

Watakatifu wanasitawsiha mafundisho ya ubaba na nguvu ya Roho Mtakatifu kama tunda la tumbo kwa namna ya upokeleo wa mtoto.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Kitu yote ya Roho Mtakatifu ina zawadi ya kuishi: Mungu wa mbele ya milele ni Mungu wa ulimwengu, nuru isiyokaribika, uzima wa milele.

## ANTIFONON YA TATU

Wao, wenye kumuogopa Bwana wanapata njia za uzima; sasa na siku zote wanapokea utukufu wa milele.

Unapoona Wana wako pempeni ya meza kama mimea ya mizeituni, ujiharakishe kuwapeleka kwa Kristu, Mchungaji mkubwa, katika sherehe na furaha.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Roho Mtakatifu ni hazina ya neema, lindi ya unara na ya maamzi ya ndani; wa utukufu pamoja na baba na Mwana; anastahili usujudu uleule.

## PROKIMENON

Fufuka, ee Bwana Mungu wangu, na inusha mkono wako, usisahau maskini mpaka ku mwisho. *(mara tatu).*

Kituo: Nataka kukushukuru na moyo wangu wote, na kutangaza maajabu yako yote

# KANUNI YA UFUFUO YA BWANA YESU KRISTU

## WIMBO YA KWANZA

*Sauti ya saba.*

**IRMOS:** Ee Bwana, kwa alama yako inchi kavu ikatokea ku maji, hii iliyokuwa zamani yenyi hali ya maji, na wakati walipoivuka pakavu, wana wa Israeli wakakuimbia wimbo wa ushindi.

Utukufu kwa ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Ee Bwana, walipokuhukumu na hukumu isiyona hali, ni uzulumu wenyewe wa mauti uliyohukumiwa ku mauti: Mfalme wa giza asipoweza chochote juu yako, akakataliwa kweli.

Utukufu kwa ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Ilipokujongea, Hadeze haikuweza kuponda mwili wako na mema yake; mataya yake yakavunjwa kabisa, wakati wewe Bwana Mungu Mwokozi kwa kumaliza mateso ya mauti, ukafufuka siku ya tatu.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.**THEOTOKION.**

Uchungu wa Eva umeisha, zawadi ya babu wa wanadamu: Bila kusikia uchungu ukazaa kwa ubikira, na tunapojua ya kwamba wewe ni Mzazi-Mungu, ee Bikira Mtakatifu kamili, tunakutukuza.

Utukufu kwa ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Mwokozi alitirikiza Msalabani chemchem mbili za uzima kwa ubavu wake uliyochomwa mkuki: Tumwimbieni, kwa maana amevaa utukufu.

Utukufu kwa ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Mjeni kaburini aliyefufuka siku ya tatu, Kristu anamupa kila mwenyi kufa matuamini ya uzima wa milele: Tumwimbieni, kwa maana amevaa utukufu.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.**THEOTOKION.**

Peke yako ulichunga ubikira hata kisha kuzaa; kwani ulizaa mwilini Muumba wa ulimwengu; tunakulalamikia: Salamu.

## KANUNI YA MZAZI-MUNGU.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Ee Bikira uliyezaa Bahari ya mapendo ya milele, nakuomba takasa roho yangu kwa mwanga wako wa nuru, ili niimbe kweli bahari isiyofumbuliwa ya maajabu yako.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Ee Bikira Mtakatifu kamili, alipotuona wote tumejeruhiwa, tumetobolewa kwa mishale ya zambi, Neno akatuona huruma, Mungu mkuu kwa mapendo yake akaungana na mwili aliyopata kwako kwa namna isiyokadirika.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Mtakatifu kamili, mwili wa wanadamu uliyoshindwa kwa mauti ukarudi ku udongo kaburini; lakini wewe uliyepeta mimba ya Mungu aliye hai ukaupatia uzima wa milele.

## WIMBO YA TATU

**IRMOS:** Ee Bwana na Mwokozi, ku mwanzo kwa Neno lako lenyi uwezo ulisabitrisha mbingu na nguvu zake zote katika Roho Mtakatifu, fundi wa ulimwengu; unisabitishe juu ya jiwe imara ya maungamo ya imani yetu tunayokuaminia.

Utukufu kwa ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Ee Bwana wa huruma, wakati ulipanda Msalabani kluteswa kwa kutaka kwako kwa ajili yetu, ukavumilia vidonda vyenyi kutupatia amani na wokovu; katika hii, ee Mungu wa mapendo, waaminifu wote wakapatanishwa na baba yako wa milele.

Utukufu kwa ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Ee Kristu, ulinitakasa ku kidonda cha roho yangu nyoka aliniumizaka tena ulimiangaza wakati nilikaa katika giza kaburini; niliposhuka ku Hadeze, ukanifufua pamoja nawe kwa Msalaba wako.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.**THEOTOKION.**

Ee Mwokozi, kwa maombezi ya Mama yako Bikira, leta amani duniani, ushindi ku maeklezya yetu juu ya dui; ee Bwana, stahilisha ku utukufu wako imara huyu mwenyi kukutukuza.

Utukufu kwa ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Uliteswa mateso Msalabani, ulimfungulia mnyanganyi Paradizo: ee Mungu mwenyi kutujaza na mema, mpenda-wanadamu, sabitisha roho yangu ili mitimize mapenzi yako ya pekee.

Utukufu kwa ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Ulipofufuka siku ya tatu, ukapambazusha alfajiri ya uzima duniani ambapo unaleta uzima; ee mpenda-wanadamu, sabitisha roho yangu ili nitimize mapenzi yako ya pekee.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.**THEOTOKION.**

Ee Bikira Mama wa Mungu wetu, ulipopapa mimba bila mbegu na ulipoondoa uchungu wa Eva, umuombe huyu aliyepata mwili tumboni mwake aokoe kondoo za zizi lako.

## KANUNI YA MZAZI-MUNGU.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Ee Bikira Mama, aliponidanganya na tamaa ya kufanana na Mungu, nyoka akaniangushishisha toka mbinguni mpaka duniani, lakini huyu aliye mwenye rehema aliponionyesha huruma na alipofanana nami.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Ee Bikira Mama, furaha ya wote, atukuzwe tunda la tumbo lako: Kwa ajili ya dunia ulizaa kweli shangwe na furaha yenyi kuondoa daima sikitiko ya zambi, ee Bibi, usiyeolewa.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Ee Bikira Mama, ni uzima na nuru ulizaa, kwa ajili yetu ulizaa amani ya milele yenyi kumaliza mashindano ya zamani ya mwanadamu juu ya Mungu kwa imani katika Baba Mtakatifu na neema mpya aliyotujalia.

## KONTAKION

Tokea sasa nguvu ya mauti haiwezi kuzuia wafu, kwani Kristu alishuka kuvunja na kuharibu nguvu za mauti; Hadeze imefungwa minyororo, manabii wanafurahiwa wote pamoja. Wanasema: Mwokozi, anaonekana kwa wale wenyi kudumu katika imani; kujeni, enyi waaminifu, tushariki ku Ufufuo.

## NYUMBA (IKOS)

Leo gehena, Hadeze na mauti zinatetemeka mbele ya mmoja wa Utatu Mtakatifu; dunia inapepea milango ya gehena inaogopa pakukuona; viumbe vyote vinafurahiwa pamoja na manabii, vinakuimbia wimbo wa heshima yako, ewe Mungu na Mkombozi wetu mwenyi kuharibu nguvu ya mauti. Tulalamike na furaha na shangwe kwa ajili ya Mfalme: Tazama mti wenyi kumurudisha Adamu na Wazao wake wote katika paradizo, kujeni, enyi waaminifu, tushariki ku Ufufuo.

## EKSAPOSTILARION

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu).*

# MASIFU

*Sauti ya saba.*

Kristu alifufuka katika wafu, akifungwa minyororo ya mauti; inchi upashe habari njema ya furaha kubwa; ninyi mbingu musifu utukufu wa Mungu.

Tukiona ufufuo wa Kristu, tumusujudu Yesu Bwana Mtakatifu, aliye pekee yake bila zambi.

Tunaabudu bila kuacha ufufuo wa Kristu; kwani yeye alituopoa sisi kwa maovu yetu. Mtakatifu ni Bwana Yesu, aliyetuonyesha Ufufuo.

Tutamurudishia Bwana nini, kwa ukarimu wake wote aliyetutendea? Kwa ajili yetu Mungu alikuja katika watu; kwa ajili ya hali yetu iliyoharibika zaidi, Neno alijifanya mwili, akakaa kwetu; Mtenda-mema alikuja kwa watu wasiyo na shukrani; Mwopozi kwa wafungwa; Jua la haki kwa wenye kukaa katika giza; juu ya Msalaba yeye ni msiyeteswa; katika Hadeze yeye ni Nuru; katika lufu yeye ni uzima; yeye ni Ufufuko kwa wenye kuanguka; tumupazie sauti: Mungu wetu, utukufu kwako.

**Wimbo Anatolika.**

Ulivunja milango ya Hadeze, ee Bwana, na uliharibu nguvu ya mauti kwa uwezo wako kubwa. Ulifufua pamoja nawe wafu, toka milele waliolaka katika giza, kwa Ufufuko wako mutukufu wa kimungu, kwani wewe uko Mfalme wa wote, na Mungu Mwenyezi.

Kujeni tushangilie kwa Bwana, na tufurahiwe katika ufufuko wake; kwa sababu alifufua wafu pamoja nawe, toka minyororo ya Hadeze isiyofunguliwa, na sawasawa na Mungu alileta duniani uzima wa milele na rehema kubwa.

Malaika aliyeangaa kama umeme, alikaa juu ya jiwe la kaburi iliyopokea uzima, na alipasha habari njema kwa wanawakew wabebaji-manukato, akasema: Bwana alifufuka, kama alivyowaambia ninyi; mukawahubiri wanafunzi wake ya kama anawatangulia kwenda Galilaya, na analeta duniani uzima wa milele na rehema kubwa.

Kwa nini mulikataa jiwe kubwa la pembe, ee Wayuda wavunja-sheria? Huyu ni jiwe aliyewekwa na Mungu katika Sayuni, aliyechirizika maji toka jiwe jangwani, na aliyechemusha kwa ubavu wake uzima usiyokufa; huyu ni jiwe, aliyechongwa mulimani mwa Bikira, pasipo mapenzi ya mutu, ni Mwana wa mutu, mwenye kuja juu ya mawingu ya mbingu, na mwenye karibia huyu Muzee wa siku, kama Danieli alivyosema; na ufalme wake ni wa milele.

Utukufu kwa Baba...**EOTHINON**
*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

Sasa na siku zote...Mbarikiwa ukupita, ewe Mzazi-Mungu...

**DOKSOLOGIA KUBWA**

## SIKU YA MUNGU MANGARIBI KATIKA SAUTI YA SABA

Tazama, ee roho yangu, ona huruma na wokovu wa Mungu wetu. Alikuja duniani akiinamisha mbingu sababu ya kukuinua juu masubuko ya mateso yako na kukuweka juu ya jiwe imara ya imani. Hii ni ajabu yenyi kutuogopesha! Utukufu kwa kujishusha kwako, ee Bwana mpenda-wanadamu.

Ee roho yangu, ona matendo yako mbaya, shangaa hii dunia inakuletea tena, radi isikuteketeze, nyama kali wa pori wasikurarue, Jua la nuru lisiache kwangaza kwa ajili yako; inuka, tubu na umulalamikie Bwana. Nilikosa juu yako, lakini unihurumie.

Ee Bwana mwenyezi tulipotumainia wewe, tunakuomba utuokoe ku namna yote ya hatari na ku mvua kali ya mateso yetu ili tuishi uzima wetu na amani, na tukitakaswa, siku ya hukumu tupate kwako, ee Bwana, wema na maondoleo.

**Wimbo ya wa Malaika.**

Ee Kristu, ulifanya Malaika wako kama ndimi za moto, ukatufumbulia harara yao na tena ukatuonyesha akili ya nafsi yao. Ee Bwana mwenyezi, utukufu kwako.

Wenye viti vya ezi, Wakheruvi na Waserafi, wenyi mamlaka, Watawala na wenye uwezo, Malaika na Malaika Wakuu na Wafalme wanakuimbia: Ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Wanadamu wote pamopja na Malaika wanakulalamikia: Salamu! Ee Mzazi-Mungu, kwani katika kuzaa uliwapatia wokovu.

**APOSTIKHA**

*Sauti ya saba.*

Nakuja kwako kama mwana mpotevu, ee Mungu wa wema, nasujudu mbele yako, unipokee kama mmoja wa watumishi wako*:* Ee Bwana, unihurumie.

Kama msafiri aliyeanguka katika mikono ya wanyanganyi, mimi mwenyewe nilianguka katika zangu, roho yangu imejerihiwa kama yeye*:* Kwa nani nitakimbilia mimi maskini ila kwa Mungu wa huruma mwenyi kuponyesha roho zetu kama mganga wa hekima? Vimwangie roho yangu neema ya wokovu.

Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu, matumaini ya Mitume tena furaha ya Mashahidi waliyotangaza Utatu wa asili moja usiyotengana.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Ulipomupa Mungu wetu mwili, unapita makundi ya Malaika; na mimi mwenyi kupita mtu wowote kwa zambi zangu, ole wangu, najazwa na woga; sisubutu hata moja kukuomba wewe Malkia na Mzazi-Mungu; usiepuke kunitazama, lakini uje wepesi kunisaidia ukinionyesha njia ya wokovu.

## MU KAZI MOJA ASUBUI KATIKA SAUTI YA SABA

### KATHISMA YA KWANZA.

Ee roho yangu, tubu, jongea ukilia na kulalamika, umuambie mganga wa roho na wa miili*:* Ee mpenda-wanadamu, uniopoe ku zambi zangu; unitendee kama kahaba, munyanganyi na Mtoza-kodi, ukisisamehe makosa yangu, ee Bwana, uniokoe.

Sikufananisha toba ya Mtoza-kodi, sikulia kama kahaba; moyo wangu mgumu hauniruhusu salehisho ya hii namna*:* Ee Bwana mpenda-wanadamu, katika wema wako uniokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION**.

Ee Mzazi-Mungu tena Bikira asiye na doa, umuombe Mwana wako pamoja na majeshi ya Juu-mbinguni ili awasamehe zambi waaminifu wneyi kukuimbia.

**KATHISMA YA PILI.**

Ulizima na kusamehe kukana kwa Petro na makosa ya Mtoza-kodi wakati ulipoona kulia na malalamiko*:* Ee Bwana mpenda-wanadamu, utukufu kwako.

Ee roho yangu, ujitayarishe katika hii uzima sababu ya kukosa kuhangaika kule juu mbinguni; hautakuwa na mtu wa kukusaidia: Wala mali, wala utawala, wala mfalme, wala rafiki, lakini paka ushuhuda wa matendo yako na huruma ya Bwana Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Uliye kweli mtukufu kuwashinda Wakeruvi, ee Bikira Mtakatifu, kwani wasipoweza kuvumilia nuru ya umungu wanatimiza kazi yao wakijifunika macho na mabaya yao, lakini wewe mwenyewe uliweza kumtazama Neno aliyejifanya mutu umuombe daima kwa ajili ya roho zetu.

**KATHISMA YA TATU.**

Wewe uliyepokea kulia kwa Petreo na uliyemuhakikisha mtoza-Kodi alipolalamika, pokea pia toba ya roho yangu, na kwa huruma yako uniokoe, ee Mungu Mwokozi.

Ee Mashahidi watakatifu, mutuombee maondoleo ya zambi zetu ili tuokolewe ku mateso ya mauti na ku hatari yoyote.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Uliye na utukufu kuwapita Majeshi ya mbinguni, umekuwa hekalu kimungu, ee Mzazi-Mungu na Bikira daima, kwani ulizaa Kristu, Mwokozi wa roho zetu.

**APOSTIKHA**

Ee Mwokozi, usinikate na shoka kama mtini usiyozaa matunda, ongojea miaka mingi, unisamehe zambi zangu, nyunyizia roho yangu machozi ya toba na nitakutolea matunda yenyi kustahili.

Kama Jua la haki, angaza mioyo ya wale wenyi kukuimbia*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Ee Kristu, tunaposhangilia makumbusho ya Mashahidi wako Watakatifu tunakuimbia tukisema*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, tunakutolea salamu kwako, kwani unawashinda Malaika ulipozaa Mungu wetu.

## MU KAZI MOJA MANGARIBI KATIKA SAUTI YA SABA

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.**

Ee Bwana na Mungu wa mapendo, kwa hekima yako unipe nikuogope moyoni mwangu; unipe nikupende kwa roho yangu yote, unipe niogope matendo ya muovu ili nitimize mapenzi yako ya wokovu, kwani ni wewe Mungu wetu na ulisema: Ombeni mutapewa.

Tazama mimi nakuwa zihaka ya mashetani, haya ya wanadamu, huzuni ya wenyi haki wote, sikitiko ya Malaika watakatifu, mchafuo wa hewa, wa inchi na wa maji, nimechafua roho

yangu, mwili wangu na akili yangu, kwa matendo yangu ya upumbafu nimekuwa adui wa Mungu; Ole wangu, ee Bwana, nimekosa juu yako, nimekosa, unihurumie.

Nakuomba, ee Bwana, uwe mvumilivu kwa mimi msiyezaa matunda; usinikate na shoka kama muti usiyozaa m,atunda, unihurumie ku mvunjo wa mauti, usinitume katika moto; kwa ombi langu fanya ili nitoe matunda, ukinipa kwa wema wako, wakati wa kutubu ili nizime, kwa machozi yangu, zambi zangu nyingi, ee Kristu Mwokozi wangu.

**Wimbo ya Mtangulizi Yoane.**

Ulipopamba Eklezya ya Kristu na maneno yako matakatifu, unaileta kama bibi asuri safi kamili na unaitayarisha, ee Mtangulizi Mtakatifu, kwa kumufwata Bwana na utii wote; kwa uwezo unayo sasa uwe kwake mlinzi na msimamizi ili iopolewe ku mashambulio ya shetani, ee Nabii mwenyi heri.

Ee Mtangulizi, ulipoangaza roho yangu na nuru ya kiroho, fukuza mbali ya hii giza za furaha mbaya na tamaa za mwili; kwa uwezo unayo sasa onekana kuwa mulinzi wangu na msimamizi wangu ili niopolewe.

Wewe uliye mkubwa kuliko manabii wote, uliyeweka mihuri juu ya sheria, wewe ambaye utakatifu kubwa unapita wanadamu, wewe Mtangulizi na Mtangazaji wa kuja kwa kwanza kwa Kristu, Bwana wa toba tena mfano wa utakatifu, uwape watumishi wako wokovu ili tuopolewe ku woga na ku hatari, ee Nabii mwenyi heri.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Salamu, Malkia, hazina takatifu ya ubikira safi kabisa, salamu makao takatifu ya Mungu wetu, salamu wewe mwenyi kuwaletea waaminifu wokovu, salamu, ee Bibi wetu, usiyeolewa.

**APOSTIKHA**

Nakuja kwako kama mwana mpotevu, ee Mungu wa wema, nasujudu mbele yako, unipokee kama mmoja wa watumishi wako*:* Ee Bwana, unihurumie.

Kama msafiri aliyeanguka katika mikono ya wanyanganyi, mimi mwenyewe nilianguka katika zangu, roho yangu imejerihiwa kama yeye*:* Kwa nani nitakimbilia mimi maskini ila kwa Mungu wa huruma mwenyi kuponyesha roho zetu kama mganga wa hekima? Vimwangie roho yangu neema ya wokovu.

Enyi Mashahidi Watakatifu mulioshindana bora na kutukuzwa mbinguni muombeni Bwana aokoe roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Kwa maombezi ya Mzazi-Mungu, leta amani ku uzima wetu wakati tunapokulalamikia: Ee Bwana wa mapendo, utukufu kwako.

## MU KAZI PILI ASUBUI KATIKA SAUTI YA SABA

### KATHISMA YA KWANZA

Ee roho yangu, tubu, jongea ukilia na kulalamika, umuambie mganga wa roho na wa miili*:* Ee mpenda-wanadamu, uniopoe ku zambi zangu; unitendee kama kahaba, munyanganyi na Mtoza-kodi, ukisisamehe makosa yangu, ee Bwana, uniokoe.

Nilipoangamia katika bahari ya hii uzima, nazama katika mawimbi ya zambi zangu, lakini wewe, ee Bwana, nyosha mkono uniokoe kama Petro, ee mpenda wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee mulinzi na makimbilio ya wakristu, ni wewe Bikira Mzazi-Mungu. Umsihi Mwana wako pamoja na Mtangulizi ili tupate rehema kwake.

**KATHISMA YA PILI**

Sikufananisha toba ya Mtoza-kodi, sikulia kama kahaba; moyo wangu mgumu hauniruhusu salehisho ya hii namna*:* Ee Bwana mpenda-wanadamu, katika wema wako uniokoe.

Ulizima na kusamehe kukana kwa Petro na makosa ya Mtoza-kodi wakati ulipoona kulia na malalamiko*:* Ee Bwana mpenda-wanadamu, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bwana, tuko watu wako, kondoo za zizi lako, rudisha kwako watoto wako wenyi kutawanyika, kwa ujito wako kusanya kondoo wenyi kupotea, kwa maombezi ya Mzazi-Mungu hurumia kondoo zako, ee Mchungaji mwema, peke yako mpenda-wanadamu na Bwana usiye na zambi.

**KATHISMA YA TATU**

Ee Bwana, kwa wema wako safisha aibu ya roho yangu na hisopo ya mapendo yako; kwa rehema yako unihurumie, ukinitakasa, ee Mwokozi ku matope ya tamaa; kwa maombezi ya Mtangulizi wako, okoa kazi ya mikono yako, peke yako mwenyi huruma.

Ee Bwana, Mashahidi wako waliposhindana duniani wakamshinda adui tena wakaharibu uwongo wa miungu ya uwango; na tnea wakapokea ku mkono wako taji ya washindaji, ee Bwana na Mungu wa wema mwenyi kutupatia neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Unaonea mateso yangu huruma na unawaona wakaaji wa dunia. Hurumia watu wasiyo na nguvu, ee Mzazi-Mungu tena Bikira mtukufu; ujiharikishe kuombea sababu ya kutuepusha ku mwisho wenyi huzuni; ee Bikira Mtakatifu na safi kamili, umuombe Mungu wa wema aokoe roho zetu.

**APOSTIKHA**

Ee Mwokozi, usinikate na shoka kama mtini usiyozaa matunda, ongojea miaka mingi, unisamehe zambi zangu, nyunyizia roho yangu machozi ya toba na nitakutolea matunda yenyi kustahili.

Kama Jua la haki, angaza mioyo ya wale wenyi kukuimbia*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Katika uwanja mbele ya baraza ya hukumu ya makafiri, Mashahidi Watakatifu wakalalamika kwa furaha*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Zamani, tangu tumbo la tasa sauti ya Neno ikapata njia ya kutukuza Mungu na Neno aliyefichama tumboni mwako, ee Bikira Mtakatifu kamili, na akatangulia kupewa neema wakati ulipomukumbatia Elisabeti; kwa sauti ya Mama yake akatambua ya kuwa ni wewe Mzazi-Mungu Mtakatifu, akatuliza utasa wa mama na unyamavu wa baba uliyosaidia kwa kumtukuza Bwana.

## MU KAZI PILI MANGARIBI KATIKA SAUTI YA SABA

**Wimbo ya Usulubisho.**

Makafiri wakakupigilia Msalabani, lakini katika hii ukashinda mauti: ee Bwana, utukufu kwako.

Ukavumilia makofi, ee Mungu wa mapendo, sababu ya kuokoa wanadamu ku utumwa: Ee Bwana, utukufu kwako.

Kwa muti wa Msalaba unasahihisha uchungu wa tunda la kwanza tena unawafungulia wanadamu Paradizo mara ya pili. Ee Bwana, utukufu kwako.

**Wimbo ya Mzazi-Mungu.**

Tumtolee Bikira salamu ya Malaika na tumulalamikie Mzazi-Mungu: Ee Bikira Safi na mtukufu, utukufu kwako.

Ee Mama wa Bwana tena Bikira usiyolewa, opoa watumishi waaminifu wako ku mishale ya nyoka.

Ee Mtakatifu kamili, uliondoa uchungu wa Adamu wakati ulipozaa furaha yetu, ee Bikira usiyeolewa, salamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Wakati Bikira Mtakatifu kamili alipokuona umesulubiwa Msalabani kwa kutaka kwako, akaimba akilalamika: Utukufu ku uwezo wako,ee Bwana.

### APOSTIKHA

Hata mara moja hatutatengwa ku muti wa uzima sasa hapa tunapotumainia Msalaba wako, ee Bwana, utukufu kwako.

Ee msiyekufa, ulipotundikwa pa muti wa Msalaba, ukapasua nyavu za shetani. Ee Bwana, utukufu kwako.

Ee Mashahidi Watakatifu, mulipozarau vitu vyote vya hapa chini, mukamtangaza na usabiti Kristu katika uwanja; mukapokea kwake tuzo la mateso yenu, na kwa sasa maana munauwezo, muombeni Mungu mwenyezi aokoe roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Neno umesulubiwa Msalabani, unaitika kushuka kuzimuni, ndivyo alivyosema Bikira Mama akilia machozi yake pamoja na mwenyi elimu mpenzi; kwa maombezi yao, ee Kristu, uliyeteswa kwa ajili yetu na uliyeshinda, fezehesha tamaa zangu na fanya ili niweze kushariki ku uzima wako kimungu na uniokoe.

## MU KAZI TATU ASUBUI KATIKA SAUTI YA SABA

### KATHISMA YA KWANZA

Wewe uliyeteswa kwa ajili yangu uliposulubiwa Msalabani, unipe sifa ya milele, ee mpenda-wanadamu tena Bwana Mungu wetu.

Ee Bwana wa majeshi ya mbinguni, wewe unajua uzaifu wa moyo wangu, uniokoe, ee Kristu Mungu wetu, kwa Msalaba wako na wema wako wa pekee.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Bikira, tunapolindwa daima kwa Msalaba wa Mwana wako, tunatoka salama ku mashambulio wa shetani; na tena tunakuimbia na kukutukuza kama inavyopashwa, ee Mzazi-Mungu mwenyi kustahili nyimbo zetu.

**KATHISMA YA PILI**

Uliangazisha muti wa Msalaba wako kushinda moto*:* Inanguza zambi za wagonjwa na inangaza mioyo ya wale wenyi kuimbia kusulubiwa kwako*:* Ee Kristu Mungu wetu, utukufu kwako.

Eklezya yako inaposujudu mbele yako, inakuimbia, ee Kristu Mungu wetu*:* Leta ushindi kwa wakristu na katika Mzazi-Mungu utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Kama viumbe vimekutambua kama Mama, Muumba amekuonyesha kama Bikira, ulizaa Kristu Mungu wetu mwilini, Mwokozi wa roho zetu.

**KATHSMA YA TATU**

Ee Kristu Mungu wetu, wewe uliyeteswa haya Msalabani kwa ajili yetu, pokea wale wenyi kuimbia Mateso yako na okoa roho zetu, ee Bwana.

Wenyi haki wafurahiwe, mbingu zishangilie, kwani Mashahidi duniani wameshinda udanganyifu; Eklezya icheze na furaha ikitukuza ushujaa wa washindaji na imwimbie Bwana wa mashindano, Kristu Mungu wetu mwenyi kuleta neema ya wokovu duniani.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, umwombe daima Kristu Mungu wetu aliyesulubiwa kwa ajili yetu na aliyeharibu nguvu ya mauti aokoe roho zetu.

**APOSTIKHA**

Kama Rabi, ee mpenda-wanadamu tena chemchem ya uzima, kwa Msalaba wako ulikomboa ulimwengu, ee Bwana, utukufu kwako.

Ee Mungu wa mapendo, jua lilipata giza wakati uliposulubiwa Msalabani kwa kutaka kwako kwa ajili ya dunia, ee Bwana, utukufu kwako.

Mashahidi Watakatifu waliyojitukuza kwa ushindi wao katika mashindano wakawa taa kwangaza ulimwengu wote; wanamwaambia Kristu*:* Ee Bwana utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Wakati Bikira Mtakatifu kamili alipokuona umesulubiwa Msalabani kw akutaka kwako, akaimba akilalamika: Utukufu kwa uwezo wako, ee Bwana.

## MU KAZI TATU MANGARIBI KATIKA SAUTI YA SABA

**Wimbo ya Mitume.**

Sauti ya Mitume Watakatifu ilisikilia mpaka ku mipaka ya dunia ya wanadamu. Ee Bwana, utukufu kwako.

Ninyi kweli ni harufu nzuri ya Neno la Mungu, ee Mitume wenyi heri unimwangie manukato ya Roho.

Ninyi ni raia wa inchi ya mbinguni; munifundishe mawazo ya mbinguni na maneno yenyi kufuatanisha mapenzi ya kimungu.

**Wimbo ya Mtakatifu Nikola.**

Ee Baba mtakatifu, kama ulivyookoa wakubwa wa maaskari ku lufu katika maombezi yako, vivyo hivyo utuokoe nasi pia sasa kwa namna ileile.

Ee Mwongozi mwenyi heri, okoa ku mateso yoyote waaminifu wenyi kukuomba na kukutukuza.

Ee Mwongozi mwenyi hekima Nikola, opoa watumishi wako ku njia, ku mtetemeko wa dunia, kumateso na ku uhitaji wowote.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . **THEOTOKION.**

Tunaungama ubikira wako hata kisha kuzaa; bila kujua mume ukapata mimba ya Mwokozi; umuombe ili roho zetu ziokolewe.

**APOSTIKHA**

Enyi Mitume Watukufu, nguzo za maeklezya , watangazaji wa ukweli tena taa za nuru, kwa moto wa Roho Mtakatifu mukateketeza makosa yote mukangaza wanadamu wote; muombeni Mwokozi Mungu wetu alete amani duniani na aokoe roho zetu.

Enyi Mitume wa Kristu, watumishi wa Mwokozi, mulipochukua Msalaba ku mabega yenu kama mashini ya kulima udongo, mulitakasa magugu yetu isiyolimwa ku udanganyifu wa sanamu ya kupandamo neno la imani; tunawatolea ibada kama inavyopashwa, ee Mitume Watakatifu wa Kristu Mungu wetu.

Ee Mashahidi wenyi kustahili sifa yote, sadaka zenyi uzima, zabihu za kiroho, sadaka zenyi kumpendeza Kristu Mungu wetu, dunia haikuwaficha ninyi, ni mbingu iliwapokea ninyi, mukawa wenzao wa Malaika; pamoja nao muombeni amani ya dunia na wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . **THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, utuopoe ku zambi zetu, kwani sisi waaminifu hatuna matumaini ingine ila wewe kisha Mungu uliyezaa mwilini.

## MU KAZI INE ASUBUI KATIKA SAUTI YA SABA

### KATHISMA YA KWANZA

*Sauti ya saba.*

Ee Neno, uliwafanya Mitume wako kuwa watumihsi wa mavuno yako; waliondosha miungu ya uwongo walitangaza Bwana wako; wakakutukuza na mapendo mbele ya mataifa.

Enyi Wafuasi watukufu wa Bwana muliyoangaza dunia kama taa, kwa maombezi yenu enezeni nuru pa giza yangu ya tamaa na aya zambi.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . **THEOTOKION.**

Ee Bikira Mtakatifu kamili, tunda la tumbo lako ni utimizo wa Manabii na wa sheria na tena, tunapokutukuza kama Mzazi-Mungu, sisi waaminifu tunakusifu.

### KATHISMA YA PILI

Enyi Mitume Watakatifu wa Bwana, munapokuwa miangaza mikubwa ya hii dunia, munangaza waaminifu na neno lenu, mukifukuza mbali giza za upotevu; kwa Ubatizo munangaza mataifa, ee watangazaji watukufu, wa Utatu Mtakatifu.

Manabii walitangaza, Mitume walifundisha, mashahidi waliungama, na sisi wenyewe tunasadiki ya kwamba ni wewe, ee Kristu, Mwana wa Mungu tena peke yako mkombozi wa hii dunia.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . **THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, washuhuda wa neema kimungu walikutangaza kama mbingu mpya yenyi kuonekana duniani, wewe ambaye tumbo lako likichukua Mungu wa mbinguni mwenyi kuifanya kuwa ya mbinguni hali ya wanadamu iliyokuwa katika utumwa wa shetani.

**KATHISMA YA TATU**

Ee Mitume watukufu, musipopendelea utukufu hata moja duniani, ni pa kuwahubiri wanadamu neno la Mungu wa mbinguni muliwaongoza watu wote kwa Yeye.

Ee Bwana, walipolindwa kwa uwezo wa Msalaba, mashahidi wako wakakimbiza adui, wakatangaza uwongo wa miungu ya uwongo; sasa wanaimba pamoja na Malaika mbinguni wimbo wwa ushindi kwa kukutukuza, ee Kristu; kwa maombezi yao, ee Bwana, utuokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . **THEOTOKION.**

Ee Mchumba kimungu, tunda la tumbo lako ameonekana kuwa chemchem ya wokovu. na tena, ee Mzazi-Mungu, tunapokutukuza kwa kinywa na kwa moyo, sisi waaminifu tunakusifu.

**APOSTIKHA**

Enyi Mitume wa Kristu, watumishi wa Mwokozi, mulipochukua Msalaba ku mabega yenu kama mashini ya kulima udongo, mulitakasa magugu yetu isiyolimwa ku udanganyifu wa sanamu ya kupandamo neno la imani; tunawatolea ibada kama inavyopashwa, ee Mitume Watakatifu wa Kristu Mungu wetu.

Enyi Mitume Watukufu, nguzo za maeklezya , watangazaji wa ukweli tena taa za nuru, kwa moto wa Roho Mtakatifu mukateketeza makosa yote mukangaza wanadamu wote; muombeni Mwokozi Mungu wetu alete amani duniani na aokoe roho zetu.

Walipokuwa na ukomo moja, na moyo mmoja, mashahidi wakafuata njia moja ya uzima wao*:* Kwa ajili ya Kristu wakachagua kufa, wakashindana kwa bidii sababu ya kufa; mateso ikawasaidia kuwa hazina; ni vizuri sana! Wakaambiana mmoja kwa mwingine*:* Kama sasa tunakimbia kufa, tunapashwa kwa namna yote kulipa haki ku dunia, tufanye mateso yetu kuwa utukufu, kwa lufu yetu tupate uzima wa kweli! Kwa maombezi yao, ee Bwana, utuokoe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . **THEOTOKION.**

Ole wangu! Mimi maskini, tazama nakuwa mchezo wa furaha; adui ananizunguka daima kwa ubishi, na tena, ee Bikira Mtakatifu, nasujudu mbele yako; Ona kufazaika kwnagu, kuja unisaidie, kwa machozi yangu umtakase na uniokoe, nakuamba, ee Bikira Safi kamili, wanyamazishwe wale wenyi kufurahiwa katika mateso yangu.

## MU KAZI INE MANGARIBI KATIKA SAUTI YA SABA

**Wimbo ya Usulubisho.**

Kwa kumfanya mtu kuwa Mungu, ukawa mwenyi kufa na ukajiachilia kusulubiwa, ee Bwana, utukufu kwa wema wako kubwa.

Wakati ulipohukumiwa ku mateso ya Msalaba, ee Neno, inchi ikatetemeka, na jua likaficha mwangaza.

Ee Mungu wa mapendo, jua lilipata giza kwa kusulubiwa kwako, ulimwengu ukatikisika na ukapaza sauti: Ee Bwana, utukufu kwako.

**Wimbo ya Mzazi-Mungu.**

Ee Mtakatifu kamili, kwa wema wako inamisha sikio lako kwangu, ukisikiliza ombi langu; usinitupe mbali ya uso wako, usitenge mbali nami msaada wako; kwa werevu wake mdanganyifu anafikiri kunipoteza, anashauria moyo wangu ku tamaa mbaya; lakini wewe, ee Bikira, unilinde mimi wote salama ku mabaya yake.

katika mwili, ee roho yangu, hautapata faida hata moja; kwa mwili unashurulika na vitu vya bure vya hii uzima, kwa mwili unaungaa katika shuruli; shurulika basi katika Bwana atakayekuja kukuhukumu na umulalamikie kwa machozi. Ee Rabi mpenda-wanadamu, kwa maombezi ya huyu aliyekuzaa, uniokoe.

Ulipomondolea sifa ya ibada yako, mimi ni mchezo wa upotevu na wa majivuno; na kwa uvivu wangu napambana na hii viroga mbili; ndio maana nakuomba, ee Bikira, uniokoe, kwani wewe ni furaha na matumaini ya roho yangu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee mwanangu, zamani nilipokuchukua mimba, nikasikia maneno ya furaha yaliyonipatia matumaini ya furaha yangu na ya roho za wenyi kusumbuka lakini hii yote ikageuka kuwa huzuni katika kufa kwako Msalabani; huzuni imeniunguza, na natumainia kufa, kwani mateso inajaa moyoni mwangu.

**APOSTIKHA**

Hata mara moja hatutatengwa ku muti wa uzima sasa hapa tunapotumainia Msalaba wako, ee Bwana, utukufu kwako.

Ee msiyekufa, ulipotundikwa pa muti wa Msalaba, ukapasua nyavu za shetani. Ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu, matumaini ya Mitume tena furaha ya Mashahidi waliyotangaza Utatu wa asili moja usiyotengana.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote...**THEOTOKION**

Bikira Mtakatifu kamili akalia machozi na akasema: Ninapokuona Msalabani, naumizwa kwa upanga wa huzuni, wewe uliyesabitisha inchi juu ya maji na uliyetandaza mbingu kama hema, kwani ninapokuona bila mavazi, umetundikwa na umetolewa sadaka, nataka kufa, ee Mwanangu mpenzi, ee dunia, ogopa na tetemeka.

## MU KAZI TANO ASUBUI KATIKA SAUTI YA SABA

### KATHISMA YA KWANZA

Wewe uliyeteswa kwa ajili yangu uliposulubiwa Msalabani, unipe sifa ya milele, ee mpenda-wanadamu tena Bwana Mungu wetu.

Ee Bwana wa majeshi ya mbinguni, wewe unajua uzaifu wa moyo wangu, uniokoe, ee Kristu Mungu wetu, kwa Msalaba wako na wema wako wa pekee.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu na Bikira daima, wakati ulimuona Mwana wako ametundikwa Msalabani, kwa uchungu wako wa umama ukasifu mapendo yake ya milele, ee Bibi msiyeolewa.

### KATHISMA YA PILI

Uliangazisha muti wa Msalaba wako kushinda moto*:* Inanguza zambi za wagonjwa na inangaza mioyo ya wale wenyi kuimbia kusulubiwa kwako*:* Ee Kristu Mungu wetu, utukufu kwako.

Wewe uliyevumilia kusulubiwa kwako kwa kutaka kwa ajili yetu, kusanya maadui zetu pampeni yako na wajuwe ya kama wewe ni Mungu wetu kweli.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Wakati ulipotobolewa misumari na kuwekwa Msalabani kwa kutaka kwako, mbele yako Mzazi-Mungu akalalamika: Bwana, Bwana, mwanamuke hata mmoja hajapataka uchungu wa huu namna; kwa miujiza yako najua ya kama wewe ni Mungu, sasa nakuona umekufa Msalabani; lakini fufuka kama ulivyosema, ili nikuimbie na furaha: Utukufu kwako.

**KATHISMA YA TATU**

Ee Bwana, wewe uliyetuokoa Msalabani ku hukumu ya maadui zetu, utuokoe pia ukiponyesha vidonda vya mioyo yetu.

Ee Mashahidi Watakatifu, ombeni kwa ajili ya maondoleo ya zambi zetu ili tuokolewe ku uchungu wa mauti na ku hatari yoyote.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Bikira, bila mbegu ulipata mimba tumboni mwako ya huyu uliyeona amesulubiwa Msalabani; umuombe daima ili roho zetu ziokolewe.

**APOSTIKHA**

Unapokuwa Rabi, ee mpenda-wanadamu tena chemchem ya uzima, kwa Msalaba wako ulikomboa ulimwengu, ee Bwana, utukufu kwako.

Mzabibu wa kweli ulipigiliwa Msalabani, mataifa ya Mnyanganyi wakapata Paradizo; hii ni utukufu wa Eklezya, hii ni hazina ya ufalme! Wewe uliyeteswa kwa ajili yetu, ee Bwana, utukufu kwako.

Ee Kristu, tunaposhangilia makumbusho ya Mashahidi wako Watakatifu tunakuimbia tukisema*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Bwana mvumilivu, uliitika kutolewa katika sadaka na ukasulubiwa na machukizo kama muovu sababu ya kutukuza kwa mti wa Msalaba wanadamu waliyoanguka ku mti uliyokatiziwa, lakini Bikira Mama yako akapata woga wakati alipokuona umekufa, akapaza sauti akilia: Namna gani makafiri wanamuua Mwenyi Haki?

## MU KAZI TANO MANGARIBI KATIKA SAUTI YA SABA

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.**

Ewe Mwokozi, usiwe na haya juu yangu sababu ya matendo yangu mabaya wakati utakapokuja kuhukumu dunia yote.

Kwa ajili ya zambi zangu nyingi naongojea azabu nyingi. Unihurumie,ee Mungu wangu na uniokoe.

Ewe Bwana, pokea marehemu waaminifu katika uwanja wako wa utakatifu na uwastahilishe ku ufalme wa mbinguni.

**Wimbo ya Mashahidi.**

Enyi Mashahidi Watakatifu mulioshindana bora na kutukuzwa mbinguni muombeni Bwana aokoe roho zetu.

Ewe Mashahidi Watakatifu, mulipozarau vitu vyote vya hapa chini, mukamtangaza na usabiti Kristu katika uwanja; mukapokea kwake tuzo la mateso yenu, na kwa sasa maana munauwezo, muombeni Mungu mwenyezi aokoe roho zetu.

Ee Mashahidi wenyi kustahili sifa yote, sadaka zenyi uzima, zabihu za kiroho, sadaka zenyi kumpendeza Kristu Mungu wetu, dunia haikuwaficha ninyi, ni mbingu iliwapokea ninyi, mukawa wenzao wa Malaika; pamoja nao muombeni amani ya dunia na wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ulijulishwa kama mama kuliko asili, ee Mzazi-Mungu; ulibaki Bikira usiyosikilikwa kwa neno na mawazo; na ajabu ya uzazi toka kwako, usiyoweza kufasiriwa katika lugha; kwani uchukuo wa mimba yako, ewe uliye safi, ni wa ajabu, na namna ya mimba ni isiyosikilikwa*:* Kwani popote Mungu anataka, usawa wa hali unashindwa; kwa hii sisi wote tukikujuwa sawa mama wa Mungu, tunakusihi bila kuchoka*:* Umupatanishe kwa wokovu wa nafsi yetu.

**APOSTIKHA**

Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu, matumaini ya Mitume tena furaha ya Mashahidi waliyotangaza Utatu wa asili moja usiyotengana.

*Shairi*: heri wale uliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe, ee Bwana.

Ee Bwana, zamani ulipamuumba mtu wa kwanza kwa sura na mfano wako, ukamuweka katika Paradizo, ili awe mfalme wa viumbe vyote; lakini shetani kwa wivu wake alipomudanganya, akavunja kanuni zako wakati alipoonja tunda lililokataziwa; na tena, ee Bwana, ukamurudisha ku udongo kwenye ulimutosha zamani, katika matumaini ya kama utamupa mapumziko.

*Shairi*: Na makumbusho yao ni ya milele.

Ee Mungu Mwokozi, pumzisha marehemu ndugu zetu wenyi kukulalamikia*:* Ee Chemchem ta uzima, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

**N**abii Danieli alikuona kama mlima takatifu, mwenyi hekima Isaya akatangaza kuzaa kwako kwa ubikira, ewe Bikira Safi kamili uliyechunga salama mwilini mwako Mungu aliyeumba zamani mtu wa kwanza, huyu Wakeruvu walitetemeka pakuona amejifanya mtu, wakati walimuimbia na kumutukuza daima kwa sauti zao kama Mungu mara tatu; muombe alete wokovu ku roho zetu.

## MU POSHO ASUBUI KATIKA SAUTI YA SABA.

### KATHISMA YA KWANZA

Ee Bwana, walipolindwa kwa uwezo wa Msalaba, mashahidi wako wakakimbiza adui, wakatangaza uwongo wa miungu ya uwongo; sasa wanaimba pamoja na Malaika mbinguni wimbo wwa ushindi kwa kukutukuza, ee Kristu; kwa maombezi yao, ee Bwana, utuokoe.

Ee Bwana, Mashahidi wako walishindana duniani wakashinda adui tena wakaharibu uwongo wa miungu ya uongo; wakapokea mkononi mwako taji la washindaji, ewe Bwana na Mungu mwema mwenyi kutupatia neema.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Wewe uliyechunga hazina ya ufufuo wetu, ee Mtukufu kamili, okoa kuzimuni ya zambi wale ambao wenyi kukutumainia wewe: Ulipozaa wokovu wetu, ukatuokoa ku nguvu ya zambi, wewe ambaye ulipokuwa bikira mbele ya kuzaa, umekaa Bikira katika kuzaa kwako, na hata tena Bikira kisha kuzaa.

**KATHISMA YA PILI**

Ee Mashahidi Watakatifu, ombeni kwa ajili ya maondoleo ya zambi zetu ili tuokolewe ku uchungu wa mauti na ku hatari yoyote.

**Nyimbo ya wafu.**

Ewe Bwana, lufu yako ilistawisha uzima wa milele wa wafu; uliondoa Hadeze wakati uliwaita kwako wale waliyolala katika giza za Gehena; ee chemchem ya uzima, tunakuomba, ee Mungu wetu: Kwa wale uliyochukuwa kati yetu uwapumzishe kati, ya wenyi haki ili ku wakati wa hukumu iwasamehe.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Salamu wewe uliyekuwa fasi ya huyu hata mbingu haikuweza kuchunga; salamu, chombo cha mafundisho ya manabii, ee Bikira uliyezaa Emmanueli, Mama wa Kristu Mungu wetu.

**EKSAPOSTILARION YA SIKU**

*(Angalia ku mwisho ya hii Kitabu)*

## MASIFU

Katika uwanja mbele ya baraza ya hukumu ya makafiri, Mashahidi Watakatifu wakalalamika kwa furaha*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

Mashahidi Watakatifu waliyojitukuza kwa ushindi wao katika mashindano wakawa taa kwangaza ulimwengu wote; wanamwaambia Kristu*:* Ee Bwana utukufu kwako.

Walipokuwa na ukomo moja, na moyo mmoja, mashahidi wakafuata njia moja ya uzima wao*:* Kwa ajili ya Kristu wakachagua kufa, wakashindana kwa bidii sababu ya kufa; mateso ikawasaidia kuwa hazina; ni vizuri sana! Wakaambiana mmoja kwa mwingine*:* Kama sasa tunakimbia kufa, tunapashwa kwa namna yote kulipa haki ku dunia, tufanye mateso yetu kuwa utukufu, kwa lufu yetu tupate uzima wa kweli! Kwa maombezi yao, ee Bwana, utuokoe.

Ee Kristu, tunaposhangilia makumbusho ya Mashahidi wako Watakatifu tunakuimbia tukisema*:* Ee Bwana, utukufu kwako.

**Nyimbo ya wafu.**

Ee Bwana, kwa huruma yako weka waaminifu uliyochukua pamoja nawe wa hii dunia ya kupita katika inchi ya wenyi haki, ee Mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira, omba pamoja na Mitume na Mashahidi ili ku wakati wa hukumu marehemu wapate neema ya wokovu.

Elezo: *Kama kuna Alliluya, tunaimba ku masifu nyimbo za mashahidi zenyi kutangulia hapa juu, na kama Apostikha tunaimba Mifano (Prosomia) yafwatayo:*

**APOSTIKHA**

**Wimbo ya wafu.** *Sauti ya saba..*

Ulikufa Msalabani, ee Bwana msiyekufa, ukawekwa kaburini kama mufu, ukakomboa kuzimuni na ku mauti wanadamu wenyi kuharibika na zambi; Ee bahari ya wema usiyoweza kuisha, chemchem ya huruma ya milele, uwape marehemu wetu mapumziko.

*Shairi:* Heri wale waliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe, ee Bwana.

Kwa mapendezi ya milele ya uzuri wako na miangaza ya nuru yako kimungu, angaza marehemu watumishi wako katika nuru ya kiroho yenyi kutokea kwako ili pamoja na Malaika watukuze uBwana wa ufalme wako.

*Shairi:* Na makumbusho yao ni ya milele.

Ee Hazina ya wema isiyokwisha yenyi kugawanya zawadi zako nyingi, uwape marehemu watumishi wako fasi ya mapumziko na makao ya wateule wako, nyumba ya utukufu wako na nyumba ya mabikira, na kwa wema wako uwape furaha za Paradizo.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Ee Mama, unazaa ukamilifu wa Sheria, Mkombozi aliyejifanya mtu kwa ajili yetu; hakuwa wa kweli kwa wale waliyoishi zamani chini ya Sheria, lakini Kristu alitimiza haki yote wakati alisulubiwa Msalabani kwa kutaka kwake kwa ajili yetu. Umuombe Bwana wako wa huruma apumzishe roho za marehemu waliyokufa na ibada, ee Bikira mwenyi kustahili nyimbo zetu.



# KIPANDE CHA SAUTI YA MUNANE

## MU POSHO MANGARIBI

**Wimbo ya ufufuo.**

Tunakutolea, ee Kristu, wimbo wa mangaribi, na ibada yenye maana; kwani ulipendezwa kutuhurumia kwa ufufuo.

Ee, Bwana, Bwana, usitutupe mbali ya uso wakol; lakini upendezwe kutuhurumia, kwa ufufuo.

Furahi, ee Sayuni takatifu, Mama wa Makanisa, nyumba ya Mungu; kwani wewe ulipokea kwanza usamehe wa zambi, kwa ufufuo.

Neno aliyezaliwa toka Mungu Baba, mbele ya milele na yeye mwenyewe aliyetwaa mwili kwa Bikira asiyeolewa, katika miaka ya mwisho, alivumilia usulubisho wa lufu kutaka kwake, na aliokoa mutu aliyekufa tangu zamani, kwa ufufuo wake.

Tunatukuza, ee Kristu, ufufuo wako katika wafu; kwa hii uliopoa uzao wa Adamu, toka uzulumu wa Hadeze; sawa na Mungu ulileta duniani, uzima wa milele na rehema kubwa.

Utukufu kwako, ee Kristu Mwokozi, Mwana wa pekee wa Mungu, uliyepigiliwa Msalabani, na uliyefufuka toka kaburi siku ya tatu.

Tunakutukza, ee Bwana, uliyevumilia Msalaba kwa kutaka kwako kwa ajili yetu na tunakuabudu, ee Mwokozi na mwenyezi; usitutupe mbali ya uso wako, lakini utusikie na utuokoe, ewe Mpenda-wanadamu, kwa ufufuo wako.

Utukufu kwa Baba...Sasa na siku zote... **THEOTOKION**.

*Sauti ya mnane*

Mufalme wa mbinguni, kwa kupenda-wanadamu, alionekana juu ya inchi akazoea kati ya watu; kwani alipotwaa mwili kwa Bikira safi, na alipotokea kwa huyu, pamoja na hali ya umutu, huyu ni Mwana moja, kwa hali mbili, lakini hana uso mbili; kwa hii tukihubiri ya kama huyu kweli ni Mungu mkamilifu na Mtu mkamilifu, tunaungama Kristu Mungu wetu; umusihi ewe Mama usiyeolewa, kwa huruma wa nafsi yetu.

**APOSTIKHA**

Ulipanda juu ya Msalaba, ee Yesu, uliyeshuka toka mbingu; ulikuja kwa lufu, ee Uzima usiyokufa. Wewe ni Nuru ya kweli kwa wale waliokaa gizani, ni ufufuo wa wote kwa wale walioanguka. Angazo na Mwokozi wetu, utukufu kwako.

Tutukuze Kristu, mwenye kufufuka katika wafu; kwani alipotwaa nafsi na mwili, kwa mateso alitenganisha yote mbili; nafsi yake isiyo na doa, ilishuka ku Hadeze, na ilimunyanganya; mwili wake takatifu haukujua uharibifu kaburini; yeye ni Mukombozi wa nafsi yetu.

Kwa zaburi na kwa nyimbo tutukuze, ewe Kristu, Ufufuo wako katika wafu; kwa hii ulituopoa sisi toka uzulumu wa Hadeze, na sawasawa na Mungu ulileta uzima wa milele na rehema kubwa.

Rabi wa wote, Muumba usiyosikilikwa wa mbingu na inchi, kwa mateso ya Musalaba, ulinichirizikia uzima usiyo na tamaa; ulipokubali maziko, na ulipofufuka na utukufu, ulifufua pamoja nawe Adamu, ku mkono wako wa uwezo. Utukufu kwa ufufuo wako wa siku tatu; kwa hii umetupatia uzima wa milele, na usamehe wa zambi, kwani wewe peke ni mwema.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote... **THEOTOKION**

*Sauti ya sita.*

Wewe uliyezaliwa kwa Bikira kwa ajili yetu, na uliyevumilia usulubisho, ee Mwema, uliyenyanganya mauti kwa lufu, na uliyeonyesha usimamao sawasawa na Mungu, usikengue walioumbwa kwa mikono wako; onyesha mapendo yako kwa wanadamu, murehemu; pokea Mzazi-Mungu aliyekuzaa, aliyepatanisha juu yetu, na okoa, ee Mwokozi wetu, taifa isiyotumainia.

**APOLITIKION YA UFUFUO**

Toka juu ulishuka, ee Mwema, na ulikubali maziko ya siku tatu, kusudi utuokoe toka tamaa, Uzima na Ufufuo wetu, Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote... **THEOTOKION**

Wewe uliyezaliwa kwa Bikira kwa ajili yetu, na uliyevumilia usulubisho, ee Mwema, uliyenyanganya mauti kwa lufu, na uliyeonyesha usimamao sawasawa na Mungu, usikengue walioumbwa kwa mukono wako; onyesha mapendo yako kwa wanadamu. Murehemu; pokea Mzazi Mungu aliyekuzaa, aliyepatanisha juu yetu, na okoa, ee Mwokozi wetu, taifa isiyotumainia.

## SIKU YA MUNGU ASUBUI KATIKA SAUTI YA MNANE

### KATHISMA YA KWANZA

Ulifufuka katika wafu, ee Uzima wa milele, Malaika wa nuru akawaambia wanawake watakatifu: Musilie, nendeni mbio kuwapasha Mitume habari ya wokovu; imbeni mukipaza sauti, kwani Kristu Bwana amefufuka, kama Mungu alipenda kuokoa wanadamu wote.

Utukufu kwa Baba...*Tin sofian ke Logon.*

Ulipofufuka kweli kaburini, ukawaamuru wanawake watakatifu, kama inavyoandikwa, kuwapasha Mitume habari ya Ufufuo wako, na Petro akaenda mbio kaburini alipoona nuru kaburini akaogopa, kwani aliona paka sanda bila mwili takatifu; akasadiki na akalalamika: Utukufu kwako, ee Kristu, kwani unaokoa watu wote, ee Mungu Mwokozi, wewe uliye kweli Baba wa nuru.

Sasa na siku zote...**THEOTOKION.**

Tuimbie Safina mpya tena mlanga wa mbinguni, mlima takatifu, wingu la nuru, mungaza wa mbingu, wokovu wa Eva, Paradizo ya siri tena hazina kubwa ya ulimwengu wote; kwani katika yeye wokovu umetimizika dunia imesamehewa deni yake ya zamani; ndio maana

tunamulalamikia: Umsihi Kristu Mungu wetu awaondolee zambi zao wale wenyi kumuabudu Mwana wako na kusujudu mbele yake.

**KATHISMA YA MBILI**

Ee Mwokozi, wenyi mauti walifunga kaburi yako, lakini Malaika akaondoa jiwe ku mulango wa kaburi; Wanawake walikuona ukifufuka katika wafu na wakapasha Wafuasi wako habari katika Siyoni: Tazama, amefufuka Uzima wa milele akivunja vifungo vya mauti. Ee Bwana, utukufu kwako.

Utukufu kwa Baba...

Walipoleta manukato kwa maziko yako, wanawake wakasikia kaburini sauti ya Malaika ikawaambia: Musilie, pahali pa kuomboleza, furahini, pazeni sauti mukiimba ya kama Bwana Kristu amefufuka; kama Mungu ilimupendeza kuokoa wanadamu.

Sasa na siku zote...

Ee Mjaliwa neema, katika wewe viumbe vyote vinafurahiwa: Malaika mbinguni na mataifa duniani; Ee Hekalu Takatifu la Bwana, shamba la ajabu la Paradizo tena utukufu wa ubikira, ambaye kwako Mungu mkuu alipata mwili na akawa mtoto mchanga, Yeye Mungu wa mbele ya nyakati Mungu wetu aliye juu mbinguni. Bwana aliweka kiti chake tumboni mwako, akalifanya kuwa pana kuliko mbingu. Ee Mjaliwa neema, katika wewe viumbe vyote vinafurahiwa: Utukufu kwako.

Elezo: *Sasa tunaimba Mahimidi (Evlogitaria) ya Ufufuo ya Kristu.*

**IPAKOI**

Mirofori walipokuja kaburini ya chemchem ya uzima wakatafuta katika wafu Rabi msiyekufa; lakini walipopokea kwa Malaika habari ya furaha, wakawaambia Mitume ya kama Bwana alifufuka kuleta duniani neema kubwa.

## ANAVATHMI

**ANTIFONON YA KWANZA**

Adui ananijaribu tangu ujana wangu, ananiunguza na tamaa ya furaja, laikini natumainia wewe, ee Mwokozi wangu, na juu yako naonekana.

Ma adui ya sayuni wawe kama ubua wenye kukatwa ku mavuno. Chini ya muti kuna shoka; Kristu atakuja kuwakata.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote... **THEOTOKION**

Roho yote inaishi kwa neema ya roho Mtakatifu, pamoja na Baba na neno tunamuimba nuru toka nuru na Mungu wa ufalme.

**ANTIFONON YA PILI**

Moyo wangu unapojinyenyekeza ulindwe na woga wako, usianguke katika majivuno mbali yako, ee Mungu wa huruma.

Anayetumainia Bwana yataogopa wakati atakapokuja pa moto kuhukumu na kuazibu dunia.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote... **THEOTOKION**

Katika Roho Mtakatifu mtu wote mwenyi ibada anatabiri na anafanya maajabu, akiimba Mungu mmoja katika watu tatu ambaye nuru inangaa na miangaza tatu.

## ANTIFONON YA TATU

Nilipaza sauti kwako, ee Bwana, tega sikio ku mlio wangu; unitakase mimi wote mbele ya kuniondoa hapa dunia.

Anaposhuka chini ya udongo, mtu wote atarudi sababu ya kupata tuzo kadiri ya matendo ya uzima wake.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote... **THEOTOKION**

Katika Roho Mtakatifu anajulikana kwetu Mungu mmoja na mara tatu mtakatifu: Baba wa milele na Mwana asiye wa wakati, Roho wa asili moja anayotoka kwa Baba.

## ANTIFONON YA INE

Tazameni ginsi alivyo mwema, ginsi alivyo mpole wa kuvaa katika ndugu wote pamoja: Bwana analeta furaha ya uzima wa milele aliyoahidi.

Huyu mwenye kuwaza mmea wa shamba wa mapendo yake mengi anatualika kuacha shuruli yote ya dunia.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote... **THEOTOKION**

Kama ulimwengu unakaa mu amani, ni Roho Mtakatifu aliye asili: Pamoja na Baba na Neno ana hali ileile ya umungu.

## PROKIMENON

Bwana anatawala milele, Mungu wako, ee sayuni, kizazi hata kizazi.*(mara tatu).*

*Shairi:* Tukuza Bwana, ee Roho yangu; nataka kumutukuza Bwana ningali mzima.

## KANUNI YA UFUFUO YA KRISTU

## WIMBO YA KWANZA

*Armatilatin farao.*

**IRMOS:** Zamani, farao alipotangulia jeshi lake akaangamizwa kwa fimbo ya Musa wakati, kwa alama ya Msalaba, akapiga juu ya bahari na kuigawanya, akaokoa Israeli aliyeweza kukimbia na kuvuka pakavu, akamwimbia Bwana wimbo.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Namna gani hatutashangaa uwezo kamili kimungu wa Kristu ambaye kwa m,ateso yake alituenezea sisi wote uzima takatifu na wa milele wasipo mateso wala kuharibika uliyotiririka ku ubavu wake na ambao kaburi yake yenyi kuleta uzima inachemusha.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Na utukufu gani Malaika ameonekana sasa kwa wanawake watakatifu! Mwenyi alama za kuangaa za usafi wake wa kiroho na akiwatangazia kwa kuonekana kwake nuru ya utukufu, anapaza sauti: Bwana amefufuka.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.**THEOTOKION.**

Ni tukufu, hii iliyoambiwa kizazi hata kizazi kwa ajili yako, ee Maria Mzazi-Mungu, wewe uliyepokea Neno la Mungu tumboni mwako, umebaki kweli Bikira; kisha Mungu peke yako ni msaada, ndio maana tunakuimbia kwa moyo mmoja

*Kanuni ongine. Igran diodefsas.*

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Milango ya mateso yakainuka, wachungaji wa hadeze walitetemeka wakati walimuona chini kuzimuni huyu aliye mkuu wa hali ya milele.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Malaika wakashangaa pakuona hali ya wanadamu iliyopashwa kufungua katika giza za kuzimuni imewekwa imara pa kiti cha Baba.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.**THEOTOKION.**

Makundi ya Malaika na ya wanadamu wanakuimbia daima, ee Mama usiyeolewa, kwani ulibeba Muumba wa ulimwengu mikononi mwako kama mtoto.

## KANUNI YA MZAZI-MUNGU

*Asomen to Kirio.*

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Ee Mtakatifu Mzazi-Mungu, tunakuimbia wewe uliyezaa kwa namna ya ajabu Neno la milele na takatifu aliyepata mwili tumboni mwako.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Ee Kristu, Bikira alikuzaa wewe mzabibu ubebaji uzima mwenyi kumwanga duniani huruma ya wokovu.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.

Ee Mzazi-Mungu, okoo wa Adamu wenyi kuongozwa kwa ajili yako katika heri yenyi kupita wazo lolote unakutukuza kama inavyopashwa.

## WIMBO YA TATU

*O stereosas katarkas.*

**IRMOS:** Ku mwanzo kwa akili yako, ulisabitisha mbingu na ukaumba inchi juu ya maji, ee Kristu, unisabitishe juu ya mwamba wa mari zako, kwani hakuna aliye Mtakatifu ila wewe peke yako Mpenda-wanadamu.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Ee Kristu, mateso ya wokovu ya mwili wako ilihakikisha Adamu aliyehukumiwa zamani alipoonja uchungu wa zambi, kwani uliteswa bila kosa ku majaribu ya mauti, ee Bwana usiye na zambi.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

Nuru ya Ufufuo iliangazia wale waliyolala katika giza na kuvuli cha mauti; kwani kwa umungu wake, Yesu Mungu wangu alifunga mfalme wa uovu na akamunyanganya mateko yake.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.**THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, ulionekana juu kabisa kuwapita Wakeruvi na Waserafi, kwani peke yako, ee Bikira Mtakatifu kamili, ulipokea tumboni mwako Mungu ambaye kitu hata moja hakiwezi kumuzunguka tena sisi waaminifu kwa nyimbo zetu daima tunakutaja mwenyi heri.

*Kanuni ingine. Uranias apsidos.*

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.

E Bwana, wakati nilivunja zamani amri ya Muumba, ukanifukuza paradizoni, lakini ulipotwaa hali ya mtumwa ukanifundisha kutii na Msalaba wako ukanirudisha ku mapendo yako.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.
Ee Bwana, wewe uliyefanya yote kwa hekima, kwa uelekevu wako ukaumba ulimwengu, kwa akili yako makao ya moto wa milele, kwa ukuu wako, ee Neno, ukakubali kumufufua huyu uliyeumba kwa mfano wako.

Utukufu kwa Ufufuo wako takatifu, ee Bwana.
Ee Bwana, ulipokaa mwilini tumboni mwa Bikira, ukaonekana kwa wanadamu kama ilivyofaa kuonekana; ee Mpenda-wanadamu, ukamtaja kama Mzazi-Mungu tena msaada wa waaminifu.

### KANUNI YA MZAZI-MUNGU

*Si i to stereoma.*

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.
Kwa maombi yako, ee Bikira Mtakatifu kamili, kuja utusaidie ukitukinga ku hatari zenyi kutuzunguka.

Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, utuokoe.
Ee Mzazi-Mungu, ulimuinua Eva mama ya wazima, kwani Muumba wa Uzima.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote... **THEOTOKION**
Unizungushe na uwezo, ee Mtakatifu kamili uliyezaa Mungu kweli katika mwili, yeye uwezo wa baba wa nafsi mbalimbali.

### KONTAKION

Ulipofufuka kaburini, ukaamusha wafu na ukamufufua Adamu, kwa Ufufuo wako Eva anacheza kwa furaha, mipaka ya dunia inashangilia kufufuka kwako katika wafu, ee Mungu wa huruma.

### NYUMBA (IKOS)

Ee Bwana wa huruma, ulipoondoa ufalme wa Hadeze na kuwafufua wafu, ukawatangulia wanawake Wabebaji-manukato, pahali pa machozi ukawaletea furaha, ee Mwokozi, kwa Mitume wako ukawaonyesha ushindi wako, ee Bwana chemchem ya uzima; ee Mpenda-wanadamu, uliangaza viumbe vyote; ndio maana dunia pia inafurahi kwa kufufuka kwako katika wafu, ee Mungu wa huruma.

## MASIFU

Ee Bwana, japo ulisimama mbele ya baraza ya hukumu, ukihukumiwa kwa Pilato, lakini haukuache kiti cha ufalme pahali unapokaa pamoja na Baba; na ukifufuka katika wafu, uliopoa dunia toka utumwa wa adui, kama Mwema na Mpenda-wanadamu.

Ee Bwana, japo Wayuda walikuweka Kaburini kama mwenye kufa, lakini askari walikuchunga sawa Mfalme anayelala, na walikufunga kwa mhuri kama hazina ya uzima; lakini ulifufuka na ulileta uzima usiyoharibika kwa nafsi yetu.

Ee Bwana, ulitupatia Msalaba wako, kama silaha juu ya shetani; kwani yeye anaitetemekea na anaifazaikia kwa woga, bila kuweza kuona nguvu Yake; kwa kuwa Msalaba unafufua wafu, na uliharibu mauti; kwa hii tunaabudu, maziko na ufufuo wako.

Ee Bwana, Malaika wako, aliyehubiri ufufuko, aliogopesha wachungaji; tena aliita kwa wanawake, akiwaambia: Kwa nini munatafuta yeye aliye hai katika wafu? Alifufuka, kwa kuwa Yeye ni Mungu na alileta uzima kwa ulimwengu.

**Wimbo Anatolika.**

Uliteswa kwa Msalaba, ewe usiyeteswa katika umungu; ulikubali maziko ya siku tatu, kusudi utuopoe toka utumwa wa adui; na utufanye wasiokufa, na utupatiye uzima, ee Kristu Mungu mpenda-wanadamu, kwa Ufufuo wako.

Ninaabudu na ninatukuza na ninaimba, ee Kristu, Ufufuko wako toka kaburi; kwa njia ya hii ulituopoa toka minyororo isiyofunguliwa ya Hadeze, na sawasawa na Mungu unaleta duniani uzima wa milele na rehema kubwa.

Wavunja-sheria wakichunga kaburi yako iliyopokea uzima waliifunga kwa muhuri pamoja na askari walinzi; lakini wewe sawasawa na Mungu msiyekufa na mwenyezi, ulifufuka kisha siku tatu.

Bwana, wakati ulipoenda kwa milango ya Hadeze, na ulipoivunja Hadeze aliyefungwa alipaza sauti sawa: Nani huyu, asiyehukumiwa kukaa katika vilindini, laqini aliharibu kifungo cha mauti, kama hema? Nilimupokea kama mwenye kufa, na ninamutetemekea sawasawa na Mungu. Lakini wewe, Mwokozi na Mwenyezi, utuhurumie.

## SIKU YA MUNGU MANGARIBI KATIKA SAUTI YA MNANE

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.** *O tu paradoksu thavmatos.*

Namna gani nitatembea bila kushurulika na kuishi maisha yangu mu hii ukosefu wa utaratibu bila kutazama zambi zangu nyingi ku makumio ya ajabu ya mauti na ku mashindano kali siku ya hukumu! Nani atakayeniopoa ku moto ya milele kama wewe kwa wema wako kubwa haunihurumie, ee Bwana.

Ole wako, ee roho maskini, mara ngapi utakapolia kule mbinguni ukifiri matendo yako wakati wenyi haki watakapoitwa ku ufalme wa milele na wewe utakapohukumiwa ku moto ya milele sababu ya matendo yako! Lalamika tena lia na kimbilia sasa kwa Kristu Mukombozi wako tena safisha uovu wa zambi zako.

Ee roho yangu, katika muda wa hii uzima, tubu fanya nguvu yako tangu hapa chini sababu ya zambi zako ili upate mapumziko kule juu mbinguni na ukingwe ku azabu ya milele. Ee Bwana, Bwana, Mungu wa mapendo na wa wema, unistahilishe nipate bahati ya wateule wako.

**Wimbo ya Malaika.** *Kirie i ke kritirio.*

Ee Bwana, Malaika wengi wabila-mwili wanakutukuza bila kupumzika, wakifurahiwa kwa nuru yako isiyokadirika na kwa uzuri wako tena wakipokea mwanga wa jua lako tatu; kwa maombezi na ulindi wao, ee Mwokozi, okoa roho zetu.

Ee Bwana, uliweka makundi ya Malaika wako wenyi kujaa na umoja kwa sababu ya Neno lako mwenyezi na Roho Mtakatifu, ukiwapa bila kosa nuru ya miangaza yako; kwa maombezi na ulinzi wao, ee Mwokozi, okoa roho zetu.

Ee Bwana, Waserafi wanakuimbia, Malaika na Malaika Wakuu pamoja na Wakuu, wenye vitu vya Ezi, Watawala, Wenye uwezo na Wakeruvi wa ajabu wanakutolea sifa kwa nyimbo zao; kwa maombezi na ulinzi wao, ee Mwokozi, okoa roho zetu.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote... **THEOTOKION**

Salamu wewe mwenye kutenga mashetani mbali, salamu, ewe Binti ya Adamu uliyestawisha kweli ua lisilofifia; salamu, ewe utukufu wa watumishi wako, wokovu wa hatari, salamu, Bikira Mtakatifu kamili. Salamu, zawadi Mungu aliyofanyia dunia. Wokovu wa yeyote mwenyi kukuomba, salamu, Malkia Mtakatifu tena utukufu wa yoyote mwenyi kukutukuza.

**APOSTIKHA**

Malaika wanakuimba daima kama Rabi na Mfalme wao, na mimi nasujudu mbele yako kama Mtoza-kodi na nakulalamika*:* Unihurumie, ee Bwana na uniokoe.

Ee roho yangu, wewe ni mwenyi kufa, usijiachilie kuangamizwa na mawimbi ya hii uzima, amka na umulalamikie Mungu mfazili wako*:* Unihurumie, ee Bwana, na uniokoe.

Enyi Mashahidi wa Bwana, ombeni kwa Mungu ili kwa wema wake atusamehe zambi zetu nyingi.

Utukufu kwa Baba... Sasa na siku zote... **THEOTOKION**

Salamu, njiwa wa kiroho tena makao ya Mfalme Mkuu, salamu, muji wa Muumba, slaamu, boma tena makimbilio ya waaminifu, mlinzi wa wale wenyi kukutumainia wewe, ukombozi na wokovu wao, salamu, kilalo chenyi kupeleka mutu wowote mbinguni, salamu, Bibi Mtakatifu na Mbarikiwa wakati wote.

## MU KAZI MOJA ASUBUI KATIKA SAUTI YA MNANE

### KATHISMA YA KWANZA

Ee Bwana, tazama mateso yangu na unihurumie, kwani uzima wangu ni karibu kuungua, sina na mateso yenyi kuniongoza ku wokovu*:* Ndio maana nakuomba, ee Bwana, kwa mapendo yako ona mateso yangu na uniokoe.

Ee roho yangu, uwe macho ukiwaza hii siku ya ajabu, tayarisha mafuta yako tena shika taa yako yenyi kuwaka, kwa sababu haujui wakati gani itafika sauti itakayokuambia*:* Tazama Bwana Arusi wako! Kesho basi, ee roho yangu, usilale, ili mulango usifungwe kwako kama zamani kwa mabikira wapumbafu, lakini uwe imara na mwenyi kuangalia kusudi upatane katika nuru yote na Kristu Mungu wetu, ili akuingize katika chumba cha arusi cha utukufu wake kimungu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Rabi na Muumba wa ulimwengu alipopata mwili tumboni mwako, akakufanya wewe Mtakatifu kamili kuwa mlinzi wa wanadamu; na sisi tunakimbilia kwako, ee Bibi wetu, tukikuomba maondoleo ya zambi zetu, na tunakuomba tuokolewa kule juu mbinguni ku mateso ya milele na ku azabu yoyote ili tukulalamikie na imani yetu. Ee Bikira umuombe Kristu Mungu wetu amusamehe mwaminifu wote mwenyi kukimbilia ku ulinzi wako.

### KATHISMA YA PILI

Ee roho, tazama hali ya hukumu, ujitayarishe ku majilio ya hii siku ya woga*:* Kwa mioyo mbaya hana huruma; na tena lalamika mbele ya mwisho*:* Unisamehe, ee Mwokozi mpenda-wanadamu.

Nasujudu kwako kama kahaba, sababu ya kupata maondoleo ya zambi zangu, pahali pa manemane nakutolea machozi ya moyo wangu; ee Kristu Mungu wetu, unizungushe na rehema ileile tena unisamehe makosa yangu; kama yeye basi nakulalamikia, ee Mungu Mwokozi*:* Uniokoe ku matope ya zambi zangu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira Mtukufu tena Mjaliwa neema ya Mungu, umuombe daima pamoja na Malaika, Malaika Wakuu na Majeshi yote ya mbinguni kwa ajili yetu huyu ambaye kwa kutaka mwake akawa mwana wako. Fanya ili mbele ya mwisho atusamehe na atuondolee zambi zetu tena ageuze maisha yetu, ili tuwe wenyi kustahili huruma yake.

**KATHISMA YA TATU**

Ee roho yangu mpaka wakati gani utaishi bila shuruli? Mpaka wakati gani hii uvivu wa maisha yako? Ee maskini! Amka ku usingizi wako wa uzaifu, waza matendo yako na lalamika, ogopa hukumu ya mwamuzi wa haki. Utajibu nini wakati wa hukumu? namna gani utakimbia ku hii moto kama haugeuze maisha yako? Lakini mbele ya mwisho umulalamikie mwamuzi: Unisamehe makosa yangu, ee Mwokozi mvumilivu.

Leo hema ya mbinguni imeangaziwa katika hii majeshi ya mbinguni yanafurahiwa tena makundi ya Watakatifu yanaungana ku furaha yao kwa ukumbosho wa Mashahidi washindaji; kwa maombezi yao, ee Kristu, tuma amani duniani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Matengeneo ya fumbo ilipojulikana kwa Malaika, akaenda mpaka ku mlango wa Yosefu; akamwambia Bikira: Huyu ambaye kwa kushuka kwake aliinamisha mbingu duniani kote anakaa katika wewe bila kugeuza. Ninapomwona tumboni mwako akichukua hali ya mtumwa, nashangaa tena nakulalamikia: Salamu, ee Bibi usiyeolewa.

**APOSTIKHA**

Wakati ninapotazama wingi wa matendo yangu mbaya, wakati ninapowaza hukumu ya ajabu, ninapoogopa, nakimbilia kwako*:* Ee Bwana mpenda-wanadamu, usinizarau, peke yako ndiwe usiye na zambi; mbele ya mwisho unipe toba tena uniokoe.

Unipe machozi, ee Bwana, kama zamani kwa Mwanamuke mwenyi zambi tena unihurusu niyamwangia pa miguu yako, kwani yameniondoa ku njia ya uovu; kama manukato ya harufu nzuri nitakutolea toba ya moyo wangu na usafi wa maisha yangu sababu ya kusikia tena sauti yako pole*:* Wende na amani, imani yako imekuokoa.

Namna gani tutawaita ninyi, ee Mashahidi Watakatifu? Wakheruvi? Maana ninyi ni kiti cha ezi cha Kristu; Waserafi? Maana munamutukuza daima; Malaika? Kwani mumekataa mwili wenu; Majeshi? Kwa ajili ya miujiza ombeni kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Bingu zinaimba neema yako, ee Mzazi-Mungu usiyeolewa, na tunatukuza kuzaa kwako kusiyokadirika; ee Mzazi-Mungu, omba kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

## MU KAZI MOJA MANGARIBI KATIKA SAUTI YA MNANE

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.** *O tu paradoksu thavmatos.*

Ee roho yangu, nitakufananisha na nani,wewe mwenyi kuishi na uzaifu katika maisha yako mu usingizi wa uzembe? Ujiharikishe kukimbia mbio wangukie ku miguu ya mwenyi kujaa yote, umuombe na machozi wakati wa kutubu mbele ya kuwa mateka ya moto ya milele.

Ee Kristu, unajua uzaifu wa mwili wetu, ukosefu wa imara wa hali yetu unaujua, ee Rabi, wewe Mungu wetu uliyetuumba; tuliza zoruba ya moyo wangu, tuliza roho yangu, kwa mapendo yako sahihisha ubaya wa matendo yangu yena uniokoe ku moto ya milele.

Ee mpenda-wanadamu, nilitumia vibaya uzima wangu katika haya na katika upotevu, bila kuwaza azabu ya kule juu mbinguni; lakini kama mwana mupotevu unipokee mimi ninayerudi kwako, ee Mwokozi na Mungu wangu; kwa maombezi ya Mtangulizi wako na ya watakatifu wako wote kama ya huyu aliyekuzaa, ee Kristu, uniokoe.

**Wimbo ya Mtangulizi Yoane.**

Chipukizi la tasa tena mmea wa usafi, pambo la wenyi mauti tena Mtangulizi wa Bwana, ee Mtakatifu Yoane mwenyi kujaa na sifa tukufu, mlinzi takatifu wa roho yangu maskini, unipe sala yako na msaada wako ukiniopoa ku mitego ya nyoka, ku mashambulio yake na ku ,mabaya yake yote.

Ili niimbe, niheshimu na nitukuza, ili nisifu na nishangilie na imani jina lako takatifu, ewe mjaliwa neema na nuru, usiondoke mbali nami, usijitenge mbali ya mtumishi wako, ee Mtangulizi, unilinde daima ku uovu wote.

Ee Mtangulizi mtukufu, wewe wote umejaa na uzuri takatifu na wema, unawafurahisha waaminifu wote wenyi kukujongea, ukituliza mahasa ya roho na ya mwili, ukituopoa daima ku huzuni, ku magonjwa, ku hatari, ku mateso, ku uchungu na ku furaha huko roho yetu inakufa.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Salamu, Malkia Mzazi-Mungu, salamu, makao takatifu ya aliye-Juu, salamu, gari kimungu ya Neno, uliyejaliwa neema kwa Mungu; Salamu, nyumba ya umwilisho kimungu, salamu hazina takatifu, meza takatifu tena chumba cha arusi cha Mungu, safina ya agano tena makao ya Roho Mtakatifu.

### APOSTIKHA

Malaika wanakuimba daima kama Rabi na Mfalme wao, na mimi nasujudu mbele yako kama Mtoza-kodi na nakulalamika*:* Unihurumie, ee Bwana na uniokoe.

Ee roho yangu, wewe ni mwenyi kufa, usijiachilie kuangamizwa na mawimbi ya hii uzima, amka na umulalamikie Mungu mfazili wako*:* Unihurumie, ee Bwana, na uniokoe.

Enyi mashahidi wa Bwana, muombeni Mungu kwa ajili ya roho zetu na kwa wema wake atuondolee zambi zetu nyingi mno.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira Mzazi-Mungu, ulinzi wako ni dawa ya kiroho kwa sisi yenyi kuopoa roho zetu ku magonjwa.

## MU KAZI PILI ASUBUI KATIKA SAUTI YA MNANE

### KATHISMA YA KWANZA

Ee Bwana, tazama mateso yangu na unihurumie, kwani uzima wangu ni karibu kuungua, sina na mateso yenyi kuniongoza ku wokovu: Ndio maana nakuomba, ee Bwana, kwa mapendo yako ona mateso yangu na uniokoe.

Nasujudu kwako kama kahaba, sababu ya kupata maondoleo ya zambi zangu, pahali pa manemane nakutolea machozi ya moyo wangu; ee Kristu Mungu wetyu, unizungushe na rehema ileile tena unisamehe makosa yangu; kama yeye basi nakulalamikia, ee Mungu Mwokozi: Uniokoe ku matope ya zambi zangu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Ee boma imara la imani tena hazina bora ya roho zetu, tunakutukuza kwa nyimbo zetu, ee Mzazi-Mungu; Salamu, kwani ulichukua tumboni mwako chemchem ya uzima, salamu, matumaini ya mipaka ya ulimwengu tena mlinzi wa wenyi kuhuzunika, salamu, ewe Bibi usiyeolewa.

## KATHISMA YA PILI

Ee roho, tazama hali ya hukumu, ujitayarishe ku majilio ya hii siku ya woga: Kwa mioyo mbaya hana huruma; na tena lalamika mbele ya mwisho: Unisamehe, ee Mwokozi mpenda-wanadamu.

*Tin sofian ke Logon.*

Ee roho yangu, tazama furaha ya mabikira wenyi akili na uzaifu wa wapumbafu; furahisha wenyi njaa na ingiza wageni, angazisha taa yako na mafuta yako ya matendo mema, usijitukuze kwa mema yako madogo; kwani anakubali rehema apana sadaka, anatuza wema mara mia zaidi, yeye Rabi wa mapendo, kwani kwa wale wenyi kugawanya duniani mali yao kwa ukarimu anawapa karamu ya arusi ya utukufu wake mbinguni.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Nilipozama katika bahari ya kukata kitumaini kabisa sababu ya matendo yangu mabaya na ya uovu, nafazaika, tena sasa mimi ni mateka ya kutotumaini. Ee Mzazi-Mungu tena Bibi wetu, kwa rehema yako uniokoe; wewe ni msaada, utakaso na wokovu wa wakosefu.

## KATHISMA YA TATU

Ee roho yangu, ulitumia vibaya uzima wako bila kushurulika, amka, utubu, lia kwa uchugvu moyoni mwako ili usimwange bure machozi kule juu mbinguni; tetemeka ukiwaza majilio ya Rabi, ujitambue wewe mwenyewe mbele ya hukumu, hivi utaepuka hukumu ya kweli.

Enyi mashahidi Watakatifu, mumeonekana kama taa za siri, kwa imani yenu muliondoa giza za uovu, muliangaza taa ya mioyo yetu katika utukufu wa mbinguni mulifikilia chumba cha Bwana Arusi: Muombeni kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira, kama sadaka ndogo ya mjane zamani nakutolea sifa yenye kukuelekea na ushukuru sababu ya mema yako. Kwani ndiwe msaada na ulinzi wa ulinzi wangu, unanuopoa daima ku vishawishi na ku mateso; kama katika tanuru ya moto unaniokoa kwa wazulumu wangu, nakulalamikia kwa moyo wangu wote. Ee Mzazi-Mungu, unisaidie tena umuombe Kristu Mungu wetu ili aniondolee zambi zangu, kwani ndiwe matumaini ya mtumishi wako.

## APOSTIKHA

Wakati ninapotazama wingi wa matendo yangu mbaya, wakati ninapowaza hukumu ya ajabu, ninapoogopa, nakimbilia kwako*:* Ee Bwana mpenda-wanadamu, usinizarau, peke yako ndiwe usiye na zambi; mbele ya mwisho unipe toba tena uniokoe.

Unipe machozi, ee Bwana, kama zamani kwa Mwanamuke mwenyi zambi tena unihurusu niyamwangia pa miguu yako, kwani yameniondoa ku njia ya uovu; kama manukato ya harufu nzuri nitakutolea toba ya moyo wangu na usafi wa maisha yangu sababu ya kusikia tena sauti yako pole*:* Wende na amani, imani yako imekuokoa.

Ee Mashahidi, mulishindana ushujaa, muliteswa vema na mateso ya makafiri na mukaungama Kristu mbele ya wafalme; kisha kuondoka mu hii uzima, uwezo wenu unatendeka duniani, munaponyesha mateso yote na ugonjwa wote. Ombeni kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira Mtakatifu Mzazi-Mungu, nakimbilia ku uoinzi wako na hakika yakupata wokovu. Ee Bikira Safi, una uwezo wa kunisaidia.

## MU KAZI PILI MANGARIBI KATIKA SAUTI YA MNANE

**Wimbo ya Usulubisho.** *O tu paradoksu thavmatos*

Ee Neno la Mungu, wemakubwa, wewe ambaye uliyesulibiwa Msalabani kwa ajili yetu kama muovu, kwa maombezi ya Mzazi-Mungu utuokoe ku hukumu ya ajabu, ku moto ya Gehena, na ku mateso yote; kwani sisi wote kila siku, ee mpenda-wanadamu, kwa mawazo yetu ya uzaifu tunakasirisha wema wako kubwa.

Ee Yesu Jua liliogopa wakati lilikuona umetundikwa Msalabani, inchi ikatetemeka na mawe yakapasuka, makafiri yakafunguka kwa woga, nguvu za mbinguni zikaogopa, na Bikira alipokuona Msalabani, akalalamika, ee Bwana. Ole wangu, ni ndoto gani inaona macho yangu!

Ee Mzazi-Mungu mstahili kalimi wa nyimbo zetu, wema wa Mwana wako aliyecxhukua mwili tumboni mwako ni kubwa! Alikufa kwa kutaka kwake Msalabani sababu ya kuokoa ulimwengu aliyoumba. Umuombe aniokoe mimi mwenyi mateso ku azabu tena aniweke kule kunaangaa.

**Wimbo ya Mzazi-Mungu.**

Salamu, ee Bibi Bikira wa Mungu, salamu, ee maytumaini ya waaminifu, utakaso wa dunia, salamu, unaokoa watumishi wako ku mateso yote unawaopoa ku mauti; salamu, Paradizo yenyi kutuletea uzima, msaada wa yoyote mwenyi kukuomba, salamu, makao takatifu ya Mungu tena mlima takatifu.

Salamu, ee Mtakatifu Mzazi-Mungu, chemchem ya uzima, mungazi wa mbinguni, Bibi Malkia wa viumbe vyote; salamu, ee Bikira Mtakatifu kamili na mtukufu, usiye na aibu tena mjaliwa neema, mstahili wa nyimbo zetu, hema takatifu; salamu, ee Bikira Mama, Bibi usiyeolewa.

Salamu, Malkia Mzazi-Mungu, salamu, peke yako matumaini ya wenyi kufa, salamu, msaada wao tena makimbilio yao; salamu kinara cha Nuru, salamu, makao nzuri sana, utukufu

safi wa ubikira tena taa yenyi kuangaa, chemchem humo munatiririka kupona kwa yoyote mwenyi kukujongea.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ni ajabu kweli! Ni fumbo ya ajabu tena mpya! Ndivyo alivyosema Bikira alipoona ametundikwa Msalabani katikati ya Wanyanganyi huyu aliyezaa bila uchungu, na alipolalamika, akalia akisema: Ole wangu! Ee mwanangu mpenzi, namna gani watu hawa wabaya wasiyo na shukrani wamekusulubisha Msalabani?

### APOSTIKHA

Unainuliwa Msalabani, ee Kristu Mungu wetu, na unaokoa wanadamu: ee Bwana, tunatukuza Mateso yako ya wokovu.

Unasulubiwa Msalabani, ee Kristu Mungu wetu, na unafungua milango ya paradizo. Katika wewe tunatukuza mkombozi wa wanadamu.

Ee Bwana, Mashahidi wako waliposahau hii uzima tena walipozarau pia mateso sababu ya uzima wa milele, wakariti mbingu na wanafurahiwa pamoja na Malaika*:* Kwa maombezi yao uwape watu wako neema ya wokovu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Bwana mvumilivu, wakati Mama yako alipokuona umepigiliwa Msalabani, akalia machozi kwa ajili yako, lakini kwa wema wako mkuu na kwa huruma yako kwa wanadamu, akaimba uwezo wako wa milele.

## MU KAZI TATU ASUBUI KATIKA SAUTI YA MNANE

### KATHISMA YA KWANZA

Alipomuona Mfalme wa Uzima ametundikwa Msalabani, Munyanganyi akalalamika na imani*:* Kama huyu anayesulubiwa pamoja nasi hakuna Mungu aliyejifanya mtu, jua halikupashwa kuficha miangaza yake wala dunia haikupashwa kutetemeka na woga; na wewe mwenyi kuvumilia hii yote, unikumbuke mimi, ee Bwana, katika ufalme wako.

Msalaba wako ilisimikwa kule Kalvario, mizazi ya haki kati ya Wanyanganyi wawili ambao mmoja akakokotwa kwa uzito wa kufuru yake mpaka mu Gehena, na mwingine aliposamehewa makosa yake, akapanda ku maarifa ya Mungu. Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Alipokuona wewe Mwana kondoo Msalabani, Mchungaji tena Mwokozi wa dunia, huyu aliyekuzaa akalia machozi na akasema: Dunia inafurahi kwa kupokea ukombozi na tumbo langu linaungua kwa kuona kusulubiwa uliyosulubiwa kwa ajili yetu kwa mapendo ya moyo wako, ee wema kubwa tena Bwana usiye na zambi. Ndiyo maana tunamulalamikia kwa imani: Ee Bikira, utuhurumie na uwaondolee zambi zao waaminifu wenyi kusujudu mbele ya Mateso ya Mwana wako.

### KATHISMA YA PILI

Katikati ya shamba la Edeni muti ilizaa mauti, katikati ya dunia muti ikachanua uzima; tulipoonja ya kwanza tukufe, ku wa pili tukapata furaha ya milele, kwa sababu Msalabani, ee Mungu, uliokoa wanadamu.

Zamani adui aliniondoa ku Paradizo, akanipa kuonja tunda la muti akaingiza mauti; lakini muti wa Msalaba ukasimikwa duniani, ikamuvika mtu vazi la uzima tena dunia yote inajaa na furaha: Tunapoona Msalaba umetukuzwa, sisi wote tumulalamikie Bwana kwa sauti moja: Hekalu yako imejaa na utukufu wako!

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Aliposimama karibu na Msalaba, Mzazi-Mungu akalia machozi, akalalamika akijaa na huruma: Ee Mwanangu, Mateso yako ni isiyosikilika; siwezi kuvumilia maumivu ya moyo wangu tena siwezi kuteswa kukuona Msalabani; usimzarau mjakazi wako, fufuka katika wafu sababu ya kunitukuza mimi mwenyi kukulalamikia: Ee Mungu wa mapendo, utukufu kwako.

**KATHSIMA YA TATU**

Zamani mti ya shamba la Edeni ulileta uchungu, mti ya Msalaba ukachamusha furaha ya uzima; kwani, alipoonja ya kwanza, Adamu akaanguka mu zambi; lakini sisi tunapokula mwili wa Kristu, tunapata uzima mpya na kwa fumbo tunakuwa miungu, tunapokea ufalme wa Mungu; ndio maana tunalalamika na imani yetu: Ee Bwana, utukufu ku Mateso yako.

Walipoteshwa kwa kukataa ukali na woga na mateso yao, Mashahidi wa Kristu wakapokea uwezo wa kufukuza uzaifu wote na ugonjwa wote na wa kufanya miujiza ya uzima hata kisha kufa kwao. Ni ajabu ya kushangaa! Mifupa ya bure imekuwa chemchem ya kuponyesha. Tutukuzeni hekima ya pekee ya Mungu Muumba.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Mwana kondoo jike alipomuona Mwana kondoo tena Mchungaji ametundikwa Msalabani, akalalamika: Ee Mwanangu, ni ndoto gani hii ya ajabu yenyi kudanganya matumaini yote? Tazama wewe uzima wa milele umehukumiwa wa kama mufu! Lakini, ee Neno fufuka katika wafu siku ya tatu kama ulivyosema.

**APOSTIKHA**

Ee Mwokozi, bakora ya Musa ilikuwa ni mfano wa Msalaba wako. Katika hii, ee Mpenda-wanadamu, unaokoa watu wako chini ya bahari.

Paradizo iliyosimikwa zamani katika shamba la Edeni ilistawisha mti ya maarifa katikati yake; na Eklezya yako, ee Kristu, iliotesha Msalaba wako takatifu wenyi kutirikiza uzima duniani, lakini ya kwanza ilimuua Adamu aliyeikula, alafu ya pili ilimupa Mnyanganyi uzima yeye aliyeokolewa kwa imani yake; uturuhusu, ee Kristu Mungu wetu, tushariki ku ukombozi uleule, wewe ambaye mateso yako ilituokoa ku hasira ya Adui tena utufanye tustahili ufalme wako wa mbinguni.

Enyi Mashahidi wa Kristu wasiyoweza kushindwa muliyoshinda upotevu kwa uwezo kwa Msalaba, mulipokea neema ya uzima wa milele; bila woga muliteswa ku makamio ya wazulumu, sasa munafurahiwa tena roho zetu zinaponyeshwa kwa damu yenu; ombeni kwa ajili ya wokovu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Bwana, wakati Bikira Kondoo jike aliyekuzaa alipokuona umepigiliwa Msalabani, akapasua uso wake, akalalamika akilia: Ee Mwanangu, namna gani unateswa hii sadaka isiyo ya haki? Ewe Msiyekuda namna gani unakufa lufu ya wanadamu? Unijibu, ee Nuru ya furaha, tazama Mama yako mwenyi kulia; umtukuze, ee Neno, kwa Ufufuo wako takatifu.

## MU KAZI TATU MANGARIBI KATIKA SAUTI YA MNANE

**Wimbo ya Mitume.** *Kirie i ke kritirio.*

Ee Bwana uliangaza Mitume wako na nuru ya Roho Mtakatifu, ukawaweka kama nyota zenyi kuangaza ulimwengu na mwanga wa kiroho wa maarifa ya Mungu; ndio maana tunasujudu mbele ya wema wako kubwa.

Ee Bwana, unapozungusha zizi lako na maombezi ya Mitume wako watakatifu, unalilinda kwa amani juu ya mashambulio ya maadui; ulipolikomboa kwa bei ya damu yako, uliiopoa hivi ku utumwa wa Adui, ee Mwokozi, kwa mapendo ya moyo wako.

Mumeonekana pa taji ya Eklezya ya Kristu kama alimasi, mukiangaza ulimwengu na nuru yenu ambayo katika ninyi iliangaa na maarifa ya Mungu, enyi Mitume wenyi heri wenyi kuuzunguka Utatu Mtakatifu, na ombeni kwa hii kwa ajili ya roho zetu.

**Wimbo ya Mtakatifu Nikola.**

Ee Bwana, kwa maombezi takatifu Mtakatifu Nikola anakutolea, opoa ee Mpenda-wanadamu ku hatari yote na ku bahati yote mbaya vilevile na ku matusi ya waovu, watumishi wako wenyi kusujudu na imani yao ku ukuu wako usiyoweza kufananishwa.

Ee Bwana, duniani humu ulimufanya Hierarki wako kuwa manukato ya harufu nzuri, kwani kwa miujiza yake anapakaa mafuta mioyo ya waaminifu wote na kwa neema yako anaondoa mateso na magonjwa ya roho zao; ee Mungu wa mapendo, kwa maombezi yake okoa waimbaji wa jina lako.

Ee Bwana, ulimtukuza Askofu wako mtakatifu, ukamupa neema ya kufanya miujiza na ukamufanya kuwa msimamizi wa wale wenyi kuwa katika hatari na wa wale wenyi kushamuliwa ngambo yote kwa mateso na huzuni, na wenyi kuomba daima ulinzi wake.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Ee Bibi usiyeolewa, sikiliza kulia kwa moyo wangu wenyi kuhuzunika na kuzarauliwa, ee Bikira Maria, Mama Mtakatifu kamili, usikatae, lakini pokea kuinua kwa mikono yangu, ee Bikira Safi kamili tena mchumba wa mema, ili niimbie na nimusifu huyu mwenyi kutukuza wanadamu.

**APOSTIKHA**

Ee Bwana, Mitume wako walipokupenda kuliko yote, wakazania kitu chochote kuwa kama majivu na takataka, kwa kuwa nawe kama hazina ya pekee na kwa ajili yako, wakatoa miili yao ku mateso; ndio maana, wanapotukuzwa mbinguni, wanaombea roho zetu.

Ee Bwana, duniani ulitukuza makumbusho ya Mitume wako watakatifu; unapotukusanya wote pamoja tunakutukuza leo, kwani katika wao unatuponyesha, na kwa maombezi yao dunia inapokea amani na neema ya wokovu.

Utukufu wote na sifa yote ni kwa Mashahidi walikufa ku upanga kwa ajili yako wewe uliyeshuka ukiinamisha mbingu; walimwanga damu yao kwa ajili yako wewe uliyejishusha wakati ulitwaa hali ya mtumwa; na walipojinyenyekeza mpaka kufa, wakafwa umaskini wako*:* Ee Bwana, kwa maombezi yao na kwa rehema yako, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Wale Mungu alistahilisha kumuona akijifanya mtu wakakutangaza kama Bibi Bikira wa ukubwa wa Baba na wa umungu wake, ee Mama Mzazi wa Neno Takatifu, makao ya Roho Mtakatifu, kwani akakaa mwilini ndani yako, ee Mjaliwa neema, ukamilifu wa umungu.

## MU KAZI INE ASUBUI KATIKA SAUTI YA MNANE

### KATHISMA YA KWANZA

Tunawatukuza Mitume Watakatifu wa Mungu wetu kama waongozi, taa za ulimwengu na malimbuko ya wokovu wetu, kwani walishushe nuru juu ya giza zetu tena walituonyesha Jua la Haki; walifukuza uwongo wa miungu ya uwongo, wakitangaza Utatu Mtakatifu mu umungu moja; Ndio maana tunawaomba, enyi Mitume Watakatifu wa Kristu Mungu wetu, muwasamehe zambi zao wale wenyi kutukuza na mapendo makumbusho yenu takatifu.

Enyi Mitume watukudu wa Bwana, sauti yenu ya hekima ilipozunguka kweli duniani mpaka ku mipaka yake, ikatangaza waziwazi maarifa kimungu na ikageuza ujinga wa wapagano kuwa maarifa, wakiangazisha nuru pa giza za udanganyifu. Ndio maana, tunawaomba ninyi. Ombeni kwa Kristu Mungu wetu ili awasamehe zambi zao wale wenyi kutukuza na mapendo makumbusho yenu takatifu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira Mtakatifu kamili, utuokoe ku uovu wowote na ku hatari yoyote, kwani wewe ni boma na ulinzi wetu, na kwa matumaini tunayokutumainia wewe tunasujudu kwa huyu aliyetoka tumboni mwako; umuombe atuokoe ku hatari yoyote.

### KATHISMA YA PILI

*To prostakthen.*

Mumeonekana kama taa za kwangaa, enyi washuhuda wa Neno wenyi kueneza daima nuru yenu duniani kote na wenyi kuondoa giza nyingi za miungu ya uongo kwa mwangaza wa mafundisho yenu juu ya imani; na mimi mwenyi kutembea bila woga katika giza ya furaha muniangaze kwa mwangaza wa maombezi yenu takatifu, ee Mitume watakatifu wabebaji-Mungu.

Walipookea na ibada ahadi za Bwana kama hazina nyingi rohoni mwao, Mitume wakawa wafazili wa ulimwengu, wakafukuza umaskini shetani anatupatia kwa kuwatajirisha wanadamu wote na uzuri wa Mungu; sisi wote pamoja tunawalalamikia: Kwa maana kwa matendo mema tumekuwa maskini, tunawaomba ninyi kututajirisha sisi pia.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira Mtakatifu kamili, tazama roho yangu ya mateso ya yenyi kuangamizwa, yasipo usukani ku zoruba ya uzima na ku hasira ya majaribu, yenyi kuzamishwa waziwazi kwa mzigo wa zambi zake na ikihatirishwa kuzama mpaka chini ya Gehena; ujiharikishe, ee Mzazi-Mungu, kwa maombezi yako ya motomoto, uiokoe, wewe mwenyi kuleta bandari ya amani, ili kwa imani nikulalamikie: Umuombe Kristu Mungu wetu anisamehe zambi zangu, kwani wewe ni matumaini yangu na mimi ni mtumishi wako.

### KATHISMA YA TATU

*Tin Sofian ke Logon.*

Mulipovua wanadamu kama samaki nyingi katika wavu wa mafundisho yenu takatifu mukawatolea kwa malimbuko kwa Mungu; mulipotaka kufunika alama ya vidonda vya Kristu, mukafananisha Mateso yake. Tunapokusanyika leo, tunatukuza kama inavyofaa, ee Mitume watukufu, ibada yenu kubwa tena tunalalamika kwa sauti moja. Ombeni kwa Kristu Mungu wetu awasamehe zambi zao wale wenyi kutukuza na mapendo makumbusho yenu takatifu.

Kwa imani ya ushuhuda mumefunuliwa kama taa za ulimwengu, wenyi kuangaa daima; mulipomtumainia Kristu, mukawakisha taa ya mioyo yenu na mafuta ya fumbo ya Roho Mtakatifu; na kama vikombe vya kiroho munamwanga maponyesho mengi kwa ajili ya Kristu. Ee Mashahidi Takatifu wenyi kustahili sifa yote, ombeni kwa Kristu Mungu wetu awaondolee zambi zao wale wenyi kutukuza na mapendo makumbusho yenu takatifu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Ee lango wa siri wa uzima wetu, Mzazi-Mungu tena Bikira Mtakatifu kamili, okoa ku hatari yote waaminifu wenyi kukukimbilia ili tutukuze kuzaa kwako takatifu kamili kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

**APOSTIKHA**

*Kirtie, i ke kritirio.*

Ee Bwana, Mitume wako walipokupenda duniani kuliko yote, wakazania kitu chochote kuwa kama majivu na takataka, kwa kuwa nawe kama hazina ya pekee na kwa ajili yako wakatoa miili yao ku mateso; ndio maana, wanapotukuzwa mbinguni, wanaombea roho zetu.

Ee Bwana, duniani ulitukuza makumbusho ya Mitume wako wataaktifu; unapotukusanya wote pamoja tunakutukuza leo, kwani katika wao unatuponyesha, na kwa maombezi yao dunia inapokea amani na neema ya wokovu.

Mulipovaa silaha ya imani, muliposhika alama ya Msalaba kama silaha mumeonekana kuwa maaskari washujaa; mukashindana vema na wazulumu, mukaondoa uongo wa shetani, mukastahili taji la Washindaji*:* Ombeni kwa Kristu kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Ee Bibi wetu, pokea ombi la watumishi wako, utuokoe ku hatari yote na ku mateso yote.

## MU KAZI INE MANGARIBI KATIKA SAUTI YA MNANE

**Wimbo ya Usulubisho.** *O agelos su Kirie.*

Ee Yesu, watu wasiyo na haki wakakusulubisha katikati ya wanyanganyi wawili, wewe Bwana tena Muumba ulimwengu wote; ilipoona uhodari wa hawa watu inchi yote ikatetemeka sababu ya kuonyesha ya kama ndiwe, ee Rabi, Muumba wa ulimwengu.

Wote tumeopolewa ku zambi zetu na ku laana ya sheria, kwani Rabi wa sheria ametukuzwa Msalabani, akitutirikizia daima baraka, neema na rehema sisi wenyi kuimbia Mateso yake.

Ee Mpenda-wanadamu, na vidonda vyetu unaponyesha wakati mikono yako ilitobolewa; ee Bwana, unaongoza hatua zetu ku njia ya wokovu wako, wakati miguu yako ilitobolewa Msalabani, hii miguu zamani ilipokanyanga paradizo, ikamufichamisha mtu wa kwanza kuumba.

**Wimbo ya Mzazi-Mungu.**

Salamu, ee Malkia Mzazi-Mungu, fimbo ya Daudi tena Mlango wa mbinguni, kichaka isiyoteketezwa tena mlima wa kivuli; Salamu, kinara cha Nuru, Salamu, ee Bikira Mtakatifu kamili, salamu, kikombe munamolindwa manemane, salamu, makao ya Mfalme mkuu, salamu, Mama Mtakatifu kamili wa Mungu wetu, Koleo ya moto tena meza palipokea Mkate wetu, salamu, matumaini ya dunia yote.

Nilipotiliwa giza kwa tamaa za uovu, mimi mwenyi mateso, najiharikisha kuanguka katika shimo la kutotumaini, ee Mjaliwa-neema tena Bikira Mtakatifu, nakuomba uniangaze na mwangaza wa rehema yako na uniongoze ku njia sawa usikose kunitazama, ee Mtakatifu kamili.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Kristu Mtakatifu kamili alipokuona umetundikwa Msalabani kwa kutaka kwako, alipojua uwezo wako, akahuzunika, na kwa uchungu wake akakulalamikia: Usimuache Mama yako, ee mwanangu, usinyamaze kwangu, ee Mwanangu, lakini umujibu mjakazi wako, ee Neno la Mungu.

### APOSTIKHA

Unainuliwa Msalabani, ee Kristu Mungu wetu, na unaokoa wanadamu: ee Bwana, tunatukuza Mateso yako ya wokovu.

Unasulubiwa Msalabani, ee Kristu Mungu wetu, na unafungua milango ya paradizo: katika wewe tunatukuza Mkombozi wa wanadamu.

Ee Mashahidi wa Bwana wenyi kutakasa ulimwengu na kuponyesha ugonjwa wowote, mutuombee sasa kwa ajili ya kuokoa roho zetu ku wavu wa adui.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Alipokuona umesulubiwa Msalabani, Mzazi-Mungu akalalamika: Ole wangu! Ee Mwanangu mpole kabisa, namna gani unateswa hii mateso? Moyo wangu umechomwa kwa mkuki wako, tumbo langu limeteketezwa kwa Mateso yako; lakini nakuimbia wewe uliyetaka kuteswa yote hii kwa kuwaokoa wanadamu.

## MU KAZI TANO ASUBUI KATIKA SAUTI YA MNANE

### KATHISMA YA KWANZA

Alipomuona Mfalme wa Uzima ametundikwa Msalabani, Munyanganyi akalalamika na imani*:* Kama huyu anayesulubiwa pamoja nasi hakuna Mungu aliyejifanya mtu, jua halikupashwa kuficha miangaza yake wala dunia haikupashwa kutetemeka na woga; na wewe mwenyi kuvumilia hii yote, unikumbuke mimi, ee Bwana, katika ufalme wako.

Msalaba wako ilisimikwa kule Kalvario, mizazi ya haki kati ya Wanyanganyi wawili ambao mmoja akakokotwa kwa uzito wa kufuru yake mpaka mu Gehena, na mwingine aliposamehewa makosa yake, akapanda ku maarifa ya Mungu. Utukufu kwako, ee Kristu Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ee Bikira Mtakatifu kamili, ulipomuona huyu aliyejifanya mtu tumboni mwako kwa namna ya ajabu ametundikwa Msalabani katikati ya wanyanganyi, moyo wako ukahuzunika na kama mama ukalia ukilalamika: Ole wangu, ee Mwanangu, hii ni fumbo gani isiyokadirika na takatifu ambayo unaokoa nayo viumbe vyako ukiwapatia uzima? Naimba mapendo yako na rehema yako.

### KATHISMA YA PILI

*Tin Sofian ke Logon.*

Ee Mungu wa wema uliyeteswa Msalabani kwa ajili yetu, ulipochukua umaskini wa Adamu, ee Bwana usiye na zambi, peka yako wema mkuu kwa mapendo yako ukaharibu nguvu ya mauti na ukaokoa dunia katika Mateso yako takatifu; nakuomba, ee Rabi mwenyi kutupatia

uzima, huruma roho yangu yenyi kuanguka, ee mpenda-wanadamu tena mwamuzi wa haki wakati utakapokuja kuhukumu matendo yangu; kwa huruma yako kubwa samehe zambi zangu, ee Mungu wa mapendo, peke yako Mutimilifu.

Katikati ya shamba la Edeni muti ilizaa mauti, katikati ya dunia muti ikachanua uzima; tulipoonja ya kwanza tukufe, ku wa pili tukapata furaha ya milele, kwa sababu Msalabani, ee Mungu, uliokoa wanadamu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Zamani, Bikira Mtakatifu kamili alipomwonma Kristu amesulubiwa Msalabani akalalamika akilia: Kwa damu ya tumbo langu ulikufa, kwa damu yako iliyomwangika ukawafanya wanadamu kuwa miungu; kwa wema wako kubwa ulishuka kuwatafuta wale waliyoonja mauti juu ya mti uliyokataziwa! Na kwa lufu yake akalia machozi mengi, akaparua uso wake na akamusifu Mwana wake kama Mungu.

**KATHISMA YA TATU**

*Anestis ek nekron.*

Alipodanganyikia akitumainia kuwa kama Mungu, mkubwa yetu wa kwanza akawa kisa ya uharibu wa milele kwa wazai wake wote; lakini kwa wema wako kubwa ukapenda kutirikiza Msalabani chemchem ya uzima, ukapigiliwa misumari sababu ya kutuokoa ku hukumu ya kwanza; ndio maana, ee Kristu, tunaimbia Mateso yako ya kutaka.

Leo hema ya mbinguni imeangaziwa katika hii majeshi ya mbinguni pamoja na makundi ya watakatifu wanafurahiwa kwa makumbusho ya Mashahidi watukufu; kwa maombezi yao, ee Kristu, tuma amani duniani na neema ya wokovu rohoni mwetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Hii ni habari ya ajabu tena ni fumbo ya kushangaa! Ndivyo alivyolalamika Bikira Kondoo jike alipoona Mwana wake amepigiliwa katika mti wa Msalaba; Ee Neno msiyekufa tena Mtakatifu, hii maana yake ni nini? Namna gani nakuona unakufa, wewe mwenyi kuitikisa dunia kama Bwana mwenyezi? Naimbia mapendo yako ya ajabu tena takatifu.

**APOSTIKHA**

Ee Mwokozi, bakora ya Musa ilikuwa ni mfano wa Msalaba wako. Katika hii, ee Mpenda-wanadamu, unaokoa watu wako chini ya bahari.

Paradizo iliyosimikwa zamani katika shamba la Edeni ilistawisha mti ya maarifa katikati yake; na Eklezya yako, ee Kristu, iliotesha Msalaba wako takatifu wenyi kutirikiza uzima duniani, lakini ya kwanza ilimuua Adamu aliyeikula, alafu ya pili ilimupa Mnyanganyi uzima yeye aliyeokolewa kwa imani yake; uturuhusu, ee Kristu Mungu wetu, tushariki ku ukombozi uleule, wewe ambaye Mateso yako ilituokoa ku hasira ya Adui tena utufanye tustahili ufalme wako wa mbinguni.

Namna gani tutawaita ninyi, ee Mashahidi Watakatifu? Wakheruvi? Maana ninyi ni kiti cha ezi cha Kristu; Waserafi? Maana munamutukuza daima; Malaika? Kwani mumekataa mwili wenu; Majeshi? Kwa ajili ya miujiza ombeni kwa ajili ya roho zetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **STAVROTHEOTOKION.**

Ni ajabu kweli! Ni fumbo ya ajabu yenyi kuleta woga! Namna gani msiyekufa ametundikwa Msalabani? Namna gani anaonja sasa mauti namna gani asiye na zambi anahukumiwa? Ee Jua, ficha nuru yako na tetemeka, pakuona uhodari wa makafiri! Ndivyo alivyosema Bikira akilia wakati alipomwona Kristu Mwana wake amesulubiwa.

# MU KAZI TANO MANGARIBI KATIKA SAUTI YA MNANE

**Wimbo ya Rabi wetu Yesu Kristu.**

Nafanana na mtini usiyozaa matunda wakati nilipovaa vazi la utakatifu kama majani isiyofunika tunda hata moja; ee Bwana naogopa shoka. Usinikate sababu ya kunitupa katika moto ya milele; unipe wakati nitubu ili nikutolee tunda nzuri ya matendo yangu mema tena nistahili ufalme wako kule mbinguni.

Ee Bwana wa mapendo, ee Bwana, usinitupa mbali ya uso wako mimi mtumihsi wako ambaye kila siku nasirikisha mapendo yako na wema usiniazibu kwa hasira yako nimekosa, nainguma kwako kama mtu wowote; kwa maombezi ya Mzazi-Mungu, unihurumie tena uniokoe.

Wakati utakapokaa na utukufu wako katika kiti cha hukumu, wakati Malaika watakatifu watakaokuzunguka na woga na wakati wanadamu wote watakatifu mbele yako kwa kuhukumiwa, hapo, ee Bwana, kwa maombezi ya Mama yako, uwaokoe ku azabu yote watumishi wako waliolala katika imani.

**Wimbo ya Mashahidi.**

Ee Mashahidi wa Bwana wenyi kutakasa ulimwengu na kuponyesha ugonjwa wowote, mutuombee sasa kwa ajili ya kuokoa roho zetu ku wavu wa adui.

Ee Bwana, mashahidi wako waliposahau hii uzima tena walipozarau pia mateso sababu ya uzima wa milele, wakariti mbingu na wanafurahiwa pamoja na Malaika*:* Kwa maombezi yao uwape watu wako neema ya wokovu.

Utukufu wote na sifa yote ni kwa Mashahidi walikufa ku upanga kwa ajili yako wewe uliyeshuka ukiinamisha mbingu; walimwanga damu yao kwa ajili yako wewe uliyejishusha wakati ulitwaa hali ya mtumwa; na walipojinyenyekeza mpaka kufa, wakafwa umaskini wako*:* Ee Bwana, kwa maombezi yao na kwa rehema yako, utuhurumie.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Mfalme wa mbinguni, kwa kupenda-wanadamu, alionekana juu ya inchi akazoea kati ya watu; kwani alipotwaa mwili kwa Bikira safi, na alipotokea kwa huyu, pamoja na hali ya umutu, huyu ni Mwana moja, kwa hali mbili, lakini hana uso mbili; kwa hii tukihubiri ya kama huyu kweli ni Mungu Mukamilifu na Mutu mukamilifu, tunaungama Kristu Mungu wetu; umusihi ewe Mama usiyeolewa, kwa huruma wa nafsi yetu.

## APOSTIKHA

Ee Mashahidi wa Bwana wenyi kutakasa ulimwengu na kuponyesha ugonjwa wowote, mutuombee sasa kwa ajili ya kuokoa roho zetu ku wavu wa adui.

*Shairi:* Heri wale waliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe, ee Bwana.

Nalia tena naomboleza nikiwaza lufu, wakati ninapoona imelala kaburini bila hali, bila utukufu na bila mapendo, neema tuliyopewa kwa mfano wa Mungu*:* Ni fumbo ya ajabu! Namna gani tutaweza kushuka kaburini? Namna gani tutaunganishwa ku mauti? Kama ilivyo Maandiko Takatifu ni kwa amri ya Mungu mwenyi kuwapa marehemu mapumziko.

*Shairi:* Na makumbusho yao ni ya milele.

Ee Bwana, lufu yako inatupatia uzima wa milele na kwa kushuka Kwako kaburini unatufungulia Paradizo*:* Uwape marehemu mapumziko na amani.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Ee Mlango wa Neno, Bikira Mtakatifu, wewe Mama wa Mungu wetu, utuombee wokovu wetu.

## MU POSHO ASUBUI KATIKA SAUTI YA MNANE

### KATHISMA YA KWANZA

Enyi mashahidi Watakatifu, mumeonekana kama taa za siri, kwa imani yenu muliondoa giza za uovu, muliangaza taa ya mioyo yetu katika utukufu wa mbinguni mulifikilia chumba cha Bwana Arusi*:* Muombeni kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Walipoteshwa kwa kukataa ukali na woga na mateso yao, Mashahidi wa Kristu wakapokea uwezo wa kufukuza uzaifu wote na ugonjwa wote na wa kufanya miujiza ya uzima hata kisha kufa kwao. Ni ajabu ya kushangaa! Mifupa ya bure imekuwa chemchem ya kuponyesha. Tutukuzeni hekima ya pekee ya Mungu Muumba.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Wewe uliyezaliwa kwa Bikira kwa ajili yetu, na uliyevumilia usulubisho, ee Mwema, uliyenyanganya mauti kwa lufu, na uliyeonyesha usimamao sawasawa na Mungu, usikengue walioumbwa kwa mukono wako; onyesha mapendo yako kwa wanadamu. Murehemu; pokea Mzazi Mungu aliyekuzaa, aliyepatanisha juu yetu, na okoa, ee Mwokozi wetu, taifa isiyotumainia.

### KATHISMA YA PILI

Ee Manabii, Mashahidi wa Kristu tena wakubwa watakatifu muliyoshindana mashindano bora kufwatana na kanuni tena na imani, na muliyopokea kwa Mungu taji isiyofifia, Mutuombee kwa wema wake atusamehe zambi zetu.

Ee Bwana, waaminifu waliyotoka hii uzima na waliyokuja kwako uwahesabie katika kundi la wenyi haki katika uwanja wa wateule wako, uwapumzisho kule kunasikilika sauti ya shangwe, katika furaha ya milele ya paradizo, kwa wema wako kubwa uwasamehe makosa yao waliyotenda, yakutaka na yasiyokutaka, ee Mpenda-wanadamu.

Ee Kisima cha hekima mwenyi kuwapenda wanadamu tnea mwenyi kuongoza vitu vyote ku wokovu, peke yako Muumba ambaye kila mmoja anapokea ile yenyi kumfaa, ee Bwana, pumzisha roho za watumishi wako, kwani wamekutumainia wewe asili yetu, Muumba wetu na Mungu wetu.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Ee Mzazi-Mungu, wewe ni boma letu na bandari yetu ya wokovu, msimamizi wa kweli kwa Mungu uliyezaa, ee Bikira Mzazi-Mungu, ndiwe wokovu wa wakristu.

## MASIFU

Ee Mashahidi, mulishindana kwa ushujaa, mukateswa vema na mateso ya makafiri tena mukamuungama Kristu kwa  wafalme; kisha kuacha hii uzima uwezo wenu unatendeka duniani, munaponyesha mateso yote na ugonjwa wote. Ombeni kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Ee Mashahidi, mulishindana kwa ushujaa, mukateswa vema na mateso ya makafiri tena mukamuungama Kristu kwa wafalme; kisha kuacha hii uzima, uwezo wenu unatendeka duniani, munaponyesha mateso yote na ugonjwa wote. Ombeni kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

Enyi Mashahidi wa Kristu wasiyoweza kushindwa muliyoshinda upotevu kwa uwezo wa Msalaba, mulipokea neema ya uzima wa milele; bila woga muliteswa ku makamio ya wazulumu, sasa munafurahiwa tena roho zetu zinaponyeshwa kwa damu yenu; ombeni kwa ajili ya wokovu wetu.

Lufu ya wale wenyi kuishi katika uovu haina kipimo: Kusaga meno, kilio isiyoweza kutulizwa, giza za inje na usiku wasipo nuru, nyungunyungu mwenyi kuguguna bila mwisho, vilio vyasipo mafaa na mwamzi wasipo huruma. Tulalamike tena mbele ya mwisho: Ee Kristu Rabi wetu, uwapumzishe marehemu pamoja na wateule wako.

Utukufu kwa Baba. . . Sasa na siku zote. . . . **THEOTOKION.**

Ee Bikira Mtakatifu Mzazi-Mungu, nakimbilia ku ulinzi wako na hakika ya kupata wokovu. Ee Bikira Mtakatifu, una uwezo wa kunisaidia.

Elezo: *Kama kuna Alliluya, tunaimba ku masifu nyimbo za mashahidi zenyi kutangulia hapa juu, na kama Apostikha tunaimba Mifano (Prosomia) yafwatayo:*

**APOSTIKHA**

**Wimbo ya wafu.** *O tu paradoksu thavmatos.*

Ee Bwana, kama Mfalme ulisahihisa uhuru wangu kwa damu yako, sasa nakuomba kwa wema wako, andika marehemu waaminifu ku kitabu cha wazaliwa wa kwanza; ukiwapa furaha ya wateule wako.

*Shairi:* Heri wale waliyochagua, wale uliyochukua pamoja nawe, ee Bwana.

Ulipoteswa kama kohani na kutolewa sadaka kama Mwana-kondoo, ulitolea kwa baba yako wanadamu waliyokombolewa ku mauti; ee Mpenda-wanadamu, weka marehemu waaminifu katika inchi ya wenyi hai, huko kunamwangika heri nyingi na chemchem ya uzima wa milele.


*Shairi:* Na makumbusho yao ni ya milele.

Ee Kisima cha hekima ya milele, iliweka mpaka wa uzima, na uliweka tayari ukomo wetu utakaokuja*:* Unawaita watumishi wako ku uzima ingine, ee Bwana uwapeleke ku maji ya mapumziko, katika nuru ya watakatifu, kule kunasikilika sifa na furaha.

Ee Neno la Mungu msiyeonekana, wa hali moja na Baba na mwenyi utukufu uleule na Roho Mtakatifu, ulijifanya mtu kwa ajili ya sisi wanadamu; kwa rehema na mapendo yako, uwape waaminifu waliyoondoka hii uzima wangae na nuru yako, na ukuu wako tena na uzuri wako.

Utukufu kwa Baba. . .Sasa na siku zote. . . **THEOTOKION.**

Ee Mama uliyezaa Neno la Mungu, kwa deni unayo kwake umuombe aweke watumishi wake katika makao ya furaha ya milele pamoja na wale wenyi kutukuza jina lako, kule kunangaa nuru ya milele na kunasikilika sauti ya furaha, ee Mzazi-Mungu.


Ἡ ϹΤΑΥ
ΡΩϹΙϹ
IϹ
XϹ
ΜΡ ΘΥ
+ ΙΩ Ο ΘΕΟΛΟΓΟϹ

# EKSAPOSTILARI NA EOTHINA YA MA SIKU YA MUNGU

*Maelezo: Ma Eksapostilario yoyote yanaimbwa katika sauti ya pili.*

## EKSAPOSTILARIO WA KWANZA

Tuwafikie Wafuasi mlimani wa Galilea, enyi waaminifu, kwa kumutazama Kristu aliyewaambia: «Nimepewa uwezo wote mbinguni na duniani»; tujuwe ginsi anayewafundisha kubatiza kwa jina la Baba mataifa yote, kwa jina la Mwana na la Roho Mtakatifu, kwa wafuasi wote akiwaahidi kuwa pamoja nao mpaka mwisho wa nyakati.

## THEOTOKION

Ulifurahi pamoja na wafuasi, ewe Bikira Mzazi-Mungu kwani ulimwona Kristu akifufuka kaburini siku ya tatu alivyosema; akajionyesha kwao, akiwafundisha na kuwafunulia ukweli kubwa, akiwaamuru kubatiza wenye kuamini katika Baba, Mwana na Roho, ili katika Ufufuo wake tuwe na imani na tunakutukuza kama Mzazi-Mungu.

## EOTHINON YA KWANZA

*Sauti ya kwanza*

Mlimani Bwana akaonekana kwa Wafuasi waliokuja mbio sababu ya kunyanyuliwa kwake hapa chini na wakasujudu mbele yake. Walipofundishwa juu ya uwezo wake wa milele, wakatumwa ku mataifa yote iliyo chini ya mbingu kutangaza ufufuo wake katika wafu na kurudi kwake mbinguni toka duniani.

## EKSAPOSTILARIO WA PILI

Walipoona jiwe limefingirishwa inje ya kaburi, Myrofor Wakashangilia na furaha, wakaona kijana amekaapo aliyewaambia: «Tazameni, Kristu amefufuka; ambieni Petro na Wafuasi wa Bwana: Endeni upesi mlimani wa galilea; huko mtamuona, kama alivyowaambia marafiki zote.

## THEOTOKION

Ku siku ya kupata kwako mwili, Bwana, Malaika akamwambia Bikira: «Salamu». Ku siku ya ufufuo wako Malaika alikuja kufingirisha jiwe la kaburi yako tukufu; pahali pa sikitiko na mauti mumoja akachukua alama za furaha, mwingine akakutangaza kama chemchem ya uzima, akitukuza Ufufuo wako mbele ya Wanawake na Wafuasi.

## EOTHINON YA PILI

*Sauti ya pili.*

Wabebaji, manukato, wenzi wa maria wakaulizana ginsi gani watafanya kwa kufikia ukomo wao; Lakini wakaona jiwe limeondoshwa tena Malaika mtakatifu akaonekana kwao aliyerudisha amani ku roho yao yenye kufazaika: «Kwani, alivyosema, Bwana Yesu amefufuka; muwapashe Wafuasi habari, Mitume wake, ili waende upesi ku Galilea huko watamuona amefufuka katika wafu, yeye Bwana na chemchem ya uzima.

## EKSAPOSTILARIO WA TATU

Hata mumoja asisite! Kristu amefufuka, kwani ameonekana kwa maria; kisha akaonekana mara ingine tena kwa wale walioenda mashambani; vivyo hivyo Wafuasi kumi na mmoja wakamuona wakati walipokua mezani; na wote akawatuma kubatiza dunia yote, kisha akapanda mbinguni huko alishuka, akihakikisha na miujiza mingi mafundisho yake kimungu.

## THEOTOKION

Leo umetoka kaburini kama Jua, kama Bwana Arusi anavyotoka nyumbani mwa Arusi, ewe Mshindi wa Hadeze na muvunjifu wa mauti kwa maombi ya Mama yako ututumie mwangaza wako, nuru ya kwangaza roho na mioyo yetu, nuru ya kuvuta kila mtu kwa kutembea katika njiaza amri zako na katika njia za amani.

## EOTHINON YA TATU

*Sauti ya tatu.*

Wakati Maria Magdalena alipotangaza na furaha kuonekana kwa Bwana aliyefufuka katika wafu, Mitume wenye shaka wakapatilizwa sababu ya ugumu wa moyo wao; lakini walipojaliwa na alama za nuru, wakatumwa duniani kuhubiri; na wakati, ee Bwana, ulipanda kwa Baba aliye chemchem ya nuru yote, wakatangaza neno lako pahali pote, kwa miujiza yao iliyozaa imani; na sisi wenye kuangazwa kwa sababu yao, tunaimba ufufuo wako katika wafu: Mpenda wanadamu, Bwana, utukufu kwako.

## EKSAPOSTILARIO W A INNE

Tukinarika na fazila, tutaona kaburini yenye kuleta uzima watu hawa wenye vazi la kuangaa ambao Myrofori wakainua macho; kwa Rabi wa mbingu tutafundishwa kuamka; pamoja na Petro twende mbio ku kaburi ya uzima tena mbele ya Ufufuo wake wa ajabu tutazame maajabu ya Kristu.

## THEOTOKION

Ulipowaamuru Myrofori wafurahiwe, ukaachisha huzuni ya wazazi wetu wa kwanza; duniani, ee Bwana, ukaweka furaha ya ufufuo wako takatifu. Kwa maombi ya huyu aliyekuzaa, ewe chemchem ya uzima, angaza mioyo yetu, tuma nuru ya mapendo yako, ili tuweze kukulalamikia: Utukufu ku ufufuo wako, ewe Mpenda-wanadamu na Mungu wetu.

## EOTHINON YA INNE

*Sauti ya inne.*

Asubui na mapema Wanawake walikuja ku kaburi yako, ee Bwana, lakini hawakupata kamwe mwili wako tukufu; mbele ya mshangao wao, watu wenye mavazi ya kuangaa wakawaambia: «Kwa nini munatafuta kati ya wafu yele aliyemzima»? Kama alivyosema amefufuka! Kumbukeni namna alivyowaambia ninyi: kwa maneno haya, wakatangaza ndoto yao, lakini habari njema ikaonekana kuwa madanganyo, hata akili ya Wafuasi ikawa zito; lakini Petro akajiharikisha kwenda kuona na akatukuza maajabu yako, ee Bwana.

## EKSAPOSTILARIO W A TANO

Kristu, uzima wetu, njia yetu, alipofufuka katika wafu akasafiri pamoja na Luka na Kleopa; hawa wakamutambua ku Emau wakati alipomega mkate mbele yao; roho yao na moyo wao zikawaka ndani yao wakati aliposimulia nao njiani, akawaeleza katika Maandiko yote mambo yaliyomwelekea yeye. Tutangaze pamoja nao: Amefufuka, ameonekana kwa Simoni.

## THEOTOKION

Ninaimba mapendo yako bila mipaka, ee Muumba ambaye kwa kuokoa hali ya unaji ya wanadamu ukajishisha kabisa chini na sawa ulivyokuwa Mungu ukateswa kwa kuzaliwa na Bikira mu hali yangu ya dunia na ukashuka hata ku Hadeze kwa kuniokoa sababu ya maombi ya mama yako asiye na doa, ewe Neno la Mungu na Bwana wa huruma.

**EOTHINON**

*Sauti ya tano*

Hekima gani katika maamzi yako, ee Kristu! Namna gani ulimupa Petro kwa kushika katika vitambaa Ufufuo wako wenyi kuleta uzima? na namna gani katika njia ya Emau ulisemezana na Luka na Kleopa bila maneno yako kukufunuliwa pale? Tena ukakemewa kuwa wewe peke yako mgeni katika Yerusalema usiyejua mambo yaliyotendeka humo siku hizi.

**EOTHINON INGINE**

*Sauti ya tano*

Ee Bwana mwenye kulinganisha mambo yote juu ya mema ya kila mumoja, ukawaeleza unabii wenye kukuelekea na wakakutambua ku baraka ya mkate, kwani moyo wao umekuishawaka na hamu ya kukutambua ee Bwana, na mbele ya Wafuasi wenye kukusanyika wakapasha waziwazi jabari ya Ugufuo wako kimungu. Katika hii utufazilie na utuhurumie.

**EKSAPOSTILARIO W A SITA**

Ulipofunua hali yako ya ubinadamu ee Mwokozi, kisha Ufufuo wako kaburini, ukakula pamoja na Wafuasi wako na ukasimama katikati yao, ukawafundisha kuhubiri toba; kisha ukapanda kwa Baba yako mbinguni na ukawaahidi Mitume wako kuwatumia Mfariji. Utukufu ku Ufufuo wako, mpenda-wanadamu na Mungu wa Juu.

**THEOTOKION**

Muumba wa kiumbe, Mungu wa ulimwengu akachukuwa mwili wa mauti tumboni mwako, ee Mzazi-Mungu; yote nzima, akafanya mpya hali yangu ya kuoza, akakuacha Bikira kisha kama mbeleya kuzaa; tena tunakuimba na ibada: Salamu, Malkia wa kiumbe**.**

**EOTHINON**

*Sauti ya sita*

Kwa wanadamu ndiwe kweli, ee Kristu, amani ya Mungu, wewe uliyeleta amani yako kwa Wafuasi kisha Ufufuo wako, ukawajaza na woga kwani walizani ya kama wameona mzimu; lakini ukafuta mashaka ya moyo wao, ukawaonyesha mikono yako na miguu yako na, kama walivyosita na macho yao, ukakula chakula pamoja nao; ukawafunulia ile Baba aliyeahidi, na ulipowabariki, ukawacha ukaenda mbinguni; tena tunasujudu mbele yako, kama walivyoifanya, na tunakulalamikia: Bwana, utukufu kwako.

**EKSAPOSTILARIO WA SABA**

Wakati maria Magdalena alipokuja kupasha habari ya kwamba wamemuondoa Bwana, Simoni Petro na yule mfuasi mwingine wa Kristu aliyependelewa naye wakaenda mbio kaburini; wote wawili wakajiharikisha na wakaona ndani vitambaa vimeweka udongoni; na ile sanda imewekwa pembeni; Wafuasi wakanyamaza mpaka walipomwona Kristu.

**THEOTOKION**

Ee Kristu mwenye kujaa na mapendo, kwa ajili yangu ulitenda mambo ya ajabu na ya juu: Ukazaliwa kwa Bikira namna isiyokadirika na ukata Msalabani; ukafufuka kaburini katika utukufu na ukaokoa hali yetu ku lufu. Utukufu ku uwezo wako, Bwana wa utukufu, Yesu Kristu.

**EOTHINON**

*Sauti ya saba*

Huu ni mwisho wa usiku na ni mapambazuko ya mchana, kwa nini, ee Maria, umesimama mbele ya kaburi? Kwa nini giza inajaa roho yako inayotafuta kujua wapi wamemuweka Yesu? Tazama ginsi Wafuasi walioenda mbio kaburini waliona katika sanda na

vitambaa alama ya ufufuo wa kweli, wakikumbuka maneno ya Maandiko yenye kwelekea hii fumbo kimungu. na sisi wenye kuamini pamoja nao, tunakuimba, ee Kristu, kama chemchem ya Uzima.

## EKSAPOSTILARIO WA MNANE

Alipoona Malaika wawili kaburini, Maria akashangaa; Hakumutambua Kristu na akamuuliza kama huyo ni mlinda shamba: Bwana, umweweka wapi mwili wa Yesu? Lakini kwa mwito wake akamtambua Mwokozi aliyemuambia: Usiniguse, ninapanda kwenda kwa baba, uwapashe ndugu zangu habari.

## THEOTOKION

Ee Bikira, ulizaa Mumoja wa Utatu mwenye hali na mapenzi mbili, bila kuacha umuombe kwa ajili ya waaminifu wenye kusujudu mbele yako ili waokoe ku mtego wote wa adui: Tunakimbilia kwako, Malkia Mzazi-Mungu.

## EOTHINON

*Sauti ya mnane*

Machozi ya uchungu ya maria hayakumuangika bure, kwani amestahili kupokea habari kwa Malaika na ndoto yako, ee Yesu; lakini sawa ni mwanamuke zaifu mwenye kuwa tena na mawazo ya dunia, ee Kristu, akapata agizo ya kutokukugusa; mtume wa habari njema, lakini akatumwa kwa Wafuasi kuwapasha habari ya kupanda kwako ku uriti wa Baba, pamoja naye, Rabi na Bwana, utupe kukuona mwenye kuonekana waziwazi.

## EKSAPOSTILARIO WA TISA

Ee Rabi, wakati ulipoingia, milango yenye kufungwa, ukawajaza Mitume na Roho Mtakatifu; ulipowapulizia, ukawapa amani na ukawaambia kwa kufunga na kufungua zambi; kisha siku nane, ukamuonyesha Tomas mikono yako na ubavu wako. pamoja naye tunakulalamikia: Bwana wangu na Mungu wangu!

## THEOTOKION

Wakati uliona Mwana wako akifufuka kaburini siku ya tatu, ee Bikira takatifu na Mchumba wa Mungu, ukasahau huzuni uliyokuwa nayo, kama Mama, wakati ulipomuona akiteswa na Mateso yake, na ulipojaa na roho ya furaha pamoja na Wafuasi wake ukamutukuza kwa nyimbo. Okoa sasa hawa wanaokutangaza Mzazi-Mungu.

## EOTHINON

*Sauti ya tano*

Kwa nyakati hizi za mwisho, ee Kristu, mangaribi moja ya Sabato, unaonekana mbele ya marafiki zako na miujiza mpya: Kuingia kwako milango yenye kufungwa. Ukawajaza Wafuasi wako na furaha, ukawaeneza Roho Mtakatifu na ukawapa uwezo wa kusamehe zambi; tena haukumuacha Tomas kuzama katika shimo ya ukosefu wa imani. Kwa sisi pia utupe maarifa ya kweli na usamehe wa makosa yetu; Bwana wa huruma.

## EKSAPOSTILARIO WA KUMI

Zamani bahari ya Tiberia ikawashauria Simoni Petro na Tomas. Nathanaeli na Wana wa wili wa Zebedeo pamoja na Wafuasi wengine wawili kwenda kuvua samaki; kwa amri ya Kristu, walipotupa wavu wao upande wa kuume, hawakuweza kuukokota sababu ya wingi wa samaki; Petro alipomtambua Bwana akajitupa baharini mpaka kwa yeye; Hii ndiyo mara ya tatu alionekana, na pa moto wa makaa akawaonyesha samaki na mkate.

## THEOTOKION

Ee Bikira, umsihi Bwana aliyefufuka kaburini siku ya tatu, kwa ajili ya waimbaji wa jina lako wenye kukuambia na moyo: Mwenye heri. Sisi wote, tuna ndani yako makimbilio ya wokovu, na mpatanishi kwa yeye; tuko urisi wako, watu wa nyumba yako, Mzazi-Mungu, tunatumaini pa ulinzi wako wema.

## EOTHINON

*Sauti ya sita*

Kisha kushuka kwako ku hadeze na Ufufuo wako katika wafu, Mitume waliyokatwa kitumaini kwa kwenda kwako, ee Kristu, wakarudi ku kazi yao na wakakamata vyombo vya na wavu wao, lakini hawakupata samaki, hapo Mwokozi, ukaonekana kama Rabi wa ulimengu, ukawaambia kutupa wavu upande wa kuume wa chombo, na neno lako likafanyika palepale: Wakavua samaki mingi na pale pwani chakula kimewaongoja. Siku ile Wafuasi wako wakapata sehemu yao, na sasa utufanye sisi pia wastahili, ee Bwana mpenda-wanadamu, wakiuonja katika roho.

## EKSAPOSTILARIO WA KUMI NA MOJA

Kisha Ufufuo wake kimungu, Bwana alipomuuliza Petro mara tatu: «Unanipenda kuliko hawa?» Akamuweka kama mchungaji mkuu wa wana-kondoo wa zizi lake; na Petro alipoona wamefuatwa na yule mfuasi aliyependelewa na Yesu, akamuuliza Rabi: «Na kwa huyu itakuwa je?». Bwana akamujibu: «Ee Petro nikitaka yeye akae mpaka nitakapokuja, ni neno lako?».

## THEOTOKION

Fumbo ya kuogopesha sana, jambo la ajabu! Lufu imevunjwa kwa lufu. Nani basi atakataa kuimba, ee Neno, Ufufuo wako kimungu na kusujudu mbele ya hii na mbele ya mama Bikira aliyekuzaa katika mwili? Kwa maombi yake utuokoe ku ulimi wa moto wasipo mwisho.

## EOTHINON

*Sauti ya mnane*

Wakati ulipoonekana kwa Wafuasi wako, ee Mwokozi; kisha Ufufuo wako, ukamupa Petro kazi ya kuchunga kondoo, kwa tuzo ya mapendo yake, na ukamuomba awalishe kwa taratibu, ndiyo maana unamwambia kuwa mchungaji wa kondoo zangu. Na Petro palepale akauliza juu ya Mfuasi mwingine, akitaja mpendelevu. Kwa maombi yao, ee Bwana linda kondoo zako juu ya mbwaa-mwitu wanyanganyi.



# THEOTOKIA YA KUIMBA MWAKA NZIMA KISHA APOLITIKiON YA WATAKATIFU

## SAUTI YA KWANZA

### Siku ya Mungu ku Esperinos na siku ya kwanza ku mwanzo wa Orthros.

Muujiza wa ajabu, ee Mjaliwa neema, kiumbe kilishangilia na furaha pakukuona, bila mbegu ukapata mimba na ukamzaa namna isiyokadirika huyu ambaye Malaika mwenyewe kutazama ee Bikira Mzazi-Mungu, umuombe kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

### Siku ya kwanza ku mwisho wa Orthros

Bikira Safi, mbarikiwa mbinguni na msifiwa duniani, salamu, ee Bibi msiyeolewa.

### Siku ya kwanza ku Esperinos na siku ya pili ku mwanzo ya Orthros.

Ulipopata mimba bila kuteketezwa na moto kimungu, na bila mbegu ulipochirikizisha Bwana chemchem ya uzima, ee Bikira mjaliwa neema na Mzazi-Mungu, utuokoe sisi tunaotukuza.

### Siku ya pili ku mwisho wa Orthros

Kwa namna isiyokadirika ukamzaa bila baba hapa chini huyu asiye na Mama mbinguni; karibu yake, ee Mzazi-Mungu, umuombe kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

### Siku ya pili ku Esperinos na siku ya tatu ku mwanzo wa Orthros.

Ee Bikira, tunasabitisha na ulinzi wako, na kwa maombi yako tunaokolewa ku hatari yote na kulindwa kila wakati na Msalaba wa Mwana wako, sisi waaminifu, tunakutukuza.

### Siku ya tatu ku mwisho wa Orthros

Bikira safi mbarikiwa mbinguni na  msifiwa duniani, salamu, ee Bibi msiyeolewa.

### Siku ya tatu ku Espesrinos na siku ya Ine ku mwanzo wa Orthros.

Ulipopata mimba bila kuteketezwa na moto kimungu, na bila mbegu ulipochirikizisha Bwana chemchem ya uzima, ee Bikira Mjaliwa neema tena Mzazi-Mungu, utuokoe sisi tunaokutukuza.

### Siku ya Ine ku mwisho wa Orthros

Kwa namna isiyokadirika ukamzaa bila baba hapa chini huyu asiye na mama mbinguni; karibu yake, ee Mzazi-Mungu, umuombe kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

### Siku ya ine ku Esperinos na siku ya tano ku mwanzo ya Orthros

Ee Bikira, tunasabitishwa na ulinzi wako, na kwa maombi yako tunaokolewa ku hatari yote na kulindwa kila wakati na Msalaba wa Mwana wako, sisi waaminfiu, tunakutukuza.

### Siku ya tano ku mwisho wa Orthros

Bikira Safi, mbarikiwa mbinguni na msifiwa duniani, Salamu, ee Bibi msiyeolewa.

### Siku ya tano ku Esperinos na siku ya sita ku mwanzo ya Orthros.

Wakati Gabrieli alisema kwako Bikira, salamu, kwa sauti; Rabi wa wote alichukua mwili, ndani yako safina takatifu, sawa mwenye haki Daudi alivyosema. Ulionekana kuwa munene sana kuliko mbingu, kwa sababu ulichukuwa Muumbaji wako. Utukufu kwa yule alikaa ndani yako; utukufu kwa yule alitoka kwako; utukufu kwa yule alitupatia uhuru, juu ya uzazi wako.

### Siku ya sita ku mwisho wa Orthros

Kwa namna isiyokadirika ukamzaa bila baba hapa chini huyu asiye na Mama mbinguni; karibu yake, ee Mzazi-Mungu, umuombe kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

## SAUTI YA PILI

### Siku ya Mungu ku Esperinos na siku ya kwanza ku mwanzo ya Orthros.

Chemchem ya huruma, ee mzazi-Mungu, utustahilishe ku huruma yako; tazama watu wenye zambi, onyesha nguvu yako ya siku zote; tunweka matumaini yetu kwako na tunakulalamikia: Salamu, kama alivyoifanya zamani Malaika mkuu Gabrieli.

### Siku ya kwanza ku mwisho wa Orthros

Mama wa Nuru isiyokadirika, kama Malaika mbinguni tunakuimba kwa kukutukuza.

### Siku ya kwanza ku Esperinos na siku ya pili ku mwanzo ya Orthros.

Kwa msaada wako, ee Mzazi-Mungu na Bikira Maria daima, tuliweza kushariki ku hali ya Mungu; kwa ajili yetu, lakini ukamzaa Mungu aliyevaa mwili wetu, na sawa alivyo mwenye haki, sisi wote tunakutukuza na ibada.

### Siku ya pili ku mwisho wa Orthros

Mzazi-Mungu, tunakutukuza tukiimba: salamu, wingu la Nuru yasipo mwisho, Bwana wa utukufu uliyechukua tumboni mwako.

### Siku ya pili ku Esperinos na siku ya tatu ku mwanzo ya Orthros.

Uliyejazwa na utukufu kuliko wote, tunakuimba, ee Mzazi-Mungu; Lufu ilivunjwa kwa lufu na hadeze ilishindwa kwa Msalaba wa Mwana wako, akatufufua ku lufu, akatupatia uzima wa milele; Paradizo ilipewa kwa sisi mara ingine sababu ya kufurahimo kama zamani; tena katika ushukuru tunatukuza mapendo na uwezo wa Kristu Mungu wetu.

### Siku ya tatu ku mwisho wa Orthros

Mzazi-Mungu, tunakutukuza tukiimba: salamu, tawi lenye kuzaa ambapo bila mbegu pa kasitawi Mungu aliyeshinda mauti pa muti.

### Siku ya tatu ku Esperinos na siku ya ine ku mwanzo ya Orthros.

Kwa msaada wako, ee Mzazi-Mungu na Bikira maria daima, tuliweza kushariki ku hali ya Mungu; kwa ajili yetu, lakini, ukamzaa Mungu aliyevaa mwili wetu, na sawa alivyo mwenye haki, sisi wote, tunakutukuza na ibada.

### Siku ya ine ku mwisho wa Orthros

Mzazi-Mungu, tunakutukuza tukiimba: salamu, wingu la Nuru yasipo mwisho, Bwana wa utukufu uliyechukua tumboni mwako.

### Siku ya ine ku Esperinos na siku ya tano ku mwanzo ya Orthros.

Uliyejazwa na utukufu kuliko wote, tunakuimba, ee Mzazi-Mungu; Lufu ilivunjwa kwa lufu na hadeze ilishindwa kwa Msalaba wa Mwana wako, akatufufua ku lufu, akatupatia uzima wa milele; Paradizo ilipewa kwa sisi mara ingine sababu ya kufurahimo kama zamani; tena katika ushukuru tunatukuza mapendo na uwezo wa Kristu Mungu wetu.

### Siku ya tano ku mwisho wa Orthros

Mzazi-Mungu, tunakutukuza tukiimba: salamu, tawi lenye kuzaa ambapo bila mbegu pa kasitawi Mungu aliyeshinda mauti pa muti.

### Siku ya tano ku Esperinos na siku ya sita ku mwanzo ya Orthros.

Siri zako zote zinapita ufahamu, na zote ni tukufu, ee Mzazi-Mungu, ulikaa Bikira na Mtakatifu bila kosa, na ulikuwa kweli Mama wakati ulipomzaa Mungu wa kweli. Umuombe ili aokoe roho zetu.

### Siku ya sita ku mwisho wa Orthros

Mama wa Nuru isiyokadirika, kama Malaika mbinguni tunakuimba kwa kukutukuza.

### Siku ya tano ku Esperinos na siku ya sita ku Orthros, kama kuna Alliluya, ikiwa sauti ya nafasi: Wimbo na Theotokion ya sauti ya pili:

Mitume, Manabii na Mashahidi, wakuu Watakatifu na wenye haki wote, ninyi mulioshindana vema na kulinda imani, kwa deni mulionayo kwa Mwokozi; mutukamatie kwa wema wake neema ya wokovu na roho zetu.

### Utukufu kwa Baba...

Bwana, kwa wema wako uwakumbuke watumishi wako, uwasamehe zambi zao zote walizotenda mu uzima hii. Hakuna mtru asiye na zambi ila wewe peke unayeweza kuwapa marehemu mapumziko.

### Sasa na siku zote...

Mama wa Nuru isiyokadirika, kama Malaika mbinguni tunakuimba kwa kukutukuza.

## SAUTI YA TATU

### Siku ya Mungu ku Esperinos na siku ya kwanza ku mwanzo ya Orthros

Mbele ya neema isiyofananishwa ya ubikira wako, mbele ya Nuru ya mapenzi na ya kimungu ya utakatifu wako, Gabrieli alipoogopa akalalamika, ee Mzazi-Mungu. Sifa gani yenye kustahili utakatifu wako ninaweza kukuonyesha? Kwa Jina gani kubwa nitakuita? Sijui na ninakatazwa. Tena nikishika amri niliyopewa, nakuimba: Salamu, ewe Mjalizwa-neema.

### Siku ya kwanza ku mwisho wa Orthros

Kila mwanadamu anakimbilia kule anakopata wokovu; katika wewe peke tunapata kimbilio, ee Mzazi-Mungu, mulinzi wa roho zetu.

### Siku ya kwanza ku Esperinos na siku ya pili ku mwanzo wa Orthros.

Mzazi-Mungu, nguvu yetu na boma yetu, msaada wa nguvu wa ulimwengu, ee Bikira mbarikiwa katika wote, kwa maombi yako okoa watumishi wako ku hatari yote.

### Siku ya pili ku mwisho wa Orthros

Kila mwanadamu anakimbilia kule anakopata wokovu; katika wewe peke tunapata kimbilio, ee Mzazi-Mungu, mulinzi wa roho zetu.

### Siku ya pili ku Esperinos na siku ya tatu ku mwanzo wa Orthros.

Tuna Msalaba wa Mwana wako kama fimbo ya nguvu, ee Mzazi-Mungu, katika hii tunashusha majivuno ya adui, sisi tunaokutukuza na moyo wote bila kuacha.

### Siku ya tatu ku mwisho wa Orthros

Mzazi-Mungu, nguvu yetu na boma yetu, msaada wa nguvu wa ulimwengu, ee Bikira mbarikiwa katika wote, kwa maombi yako okoa watumishi wako ku hatari yote.

### Siku ya tatu ku Esperinos na siku ya inne ku mwanzo wa Orthros.

Manabii walipasha habari, Mitume walifundisha, Mashahidi waliungama na sisi wenyewe tunasadiki ya kwamba ndiwe kweli Mzazi-Mungu na tunatukuza uzazi wako usiyokadirika.

### Siku ya inne ku mwisho wa Orthros

Kila mwanadamu anakimbilia kule anakopata wokovu; katika wewe peke tunapata kimbilio, ee Mzazi-Mungu, mulinzi wa roho zetu.

### Siku ya inne ku Esperinos na siku ya tano ku mwanzo wa Orthros.

Tuna Msalaba wa Mwana wako kama fimbo ya nguvu, ee Mzazi-Mungu, katika hii tunashusha majivuno ya adui, sisi tunaokutukuza na moyo wote bila kuacha.

### Siku ya tano ku mwisho wa Orthros

Mzazi-Mungu, nguvu yetu na boma yetu, msaada wa nguvu wa ulimwengu, ee Bikira mbarikiwa katika wote, kwa maombi yako okoa watumishi wako ku hatari yote.

### Siku ya tano ku Esperinos na siku ya sita ku mwanzo wa Orthros.

Bikira Mzazi-Mungu tunakuimbia, wewe mupatanishi wa wokovu juu ya ukoo wetu; katika mwili alipata Kwako, Mwana wako na Mungu wetu, alitaka kuteswa Msalabani, juu ya kutukomboa ku lufu, sawa Mpenda-wanadamu.

### Siku ya sita ku mwisho wa Orthros

Manabii walipasha habari, Mitume walifundisha, Mashahidi waliungama na sisi wenyewe tunasadiki ya kwamba ndiwe kweli Mzazi-Mungu na tunatukuza uzazi wako usiyokadirika.

## SAUTI YA INNE

### Siku ya Mungu ku Esperinos na siku ya kwanza ku mwanzo ya Orthros

Kwa huyu aliyeishwa katika hekalu, katika Patakatifu wa Watakatifu, mwenye kupambwa na hekima na imani na ubikira safi, Malaika Mkuu Gabrieli akaleta habari ya mbinguni: «Salamu, Bikira Mbarikiwa na Mjaliwa na utukufu, Bwana yupo pamoja nawe».

### Siku ya kwanza ku mwisho wa Orthros

Kwa maana unakaa juu ya kiumbe yote, tunapashwa kukuimba kama inavyofaa: Ndiyo naana, ee Mzazi-Mungu, tunakuomba, utufanyie hii zawadi, ya kutuhurumia.

## Siku ya kwanza ku Esperinos na siku ya pili ku mwanzo wa Orthros.

Tukimbilie sasa kwa Muzazi-Mungu, sisi wenye zambi na kupondwa na tusujudu, tukiita kwa kutubu toka roho: Bibi Malkia saidia, utuhurumie, fanya mbio tunapotea, kwa wingi wa makosa. Usifukuze watumishi wako kwa mikono mitupu. Kwani tulikupata, wewe peke yako matumaini.

## Siku ya pili ku mwisho wa Orthros

Mzazi-Mungu, tunakutukuza tukiimba: Ndiwe kichaka kisichoteketea ambako Musa alitazama Umungu kama ulimi wa moto.

## Siku ya pili ku Esperinos na siku ya tatu ku mwanzo wa Orthros.

Bikira Safi na Mama ya Kristu Mungu wetu, upanga ulichoma moyo wako wakati uliona Mwana wako wa Mungu wako Msalabani: Umuombe bila kuacha kwa ajili ya maondoleo ya zambi zetu.

## Siku ya tatu ku mwisho wa Orthros

Mzazi-Mungu, tunakutukuza tukiimba: Ndiwe mulima haramu ambako jiwe isiyokadirika likajifungua na likavunja milango ya Hadeze.

## Siku ya tatu ku Esperinos na siku ya inne ku mwanzo wa Orthros.

Neno la Baba, Kristu Mungu wetu, tunajuwa hya kama alitwa mwili tumboni mwako, ee Mzazi Mungu na Bikira Safi mbarikiwa katika wote, na bila kuacha tunakuimba kwa kukutukuza.

## Siku ya inne ku mwisho wa Orthros

Kwa maana unakaa juu ya kiumbe yote, tunapashwa kukuimba kama inavyofaa: Ndiyo naana, ee Mzazi-Mungu, tunakuomba, utufanyie hii zawadi, ya kutuhurumia.

## Siku ya inne ku Esperinos na siku ya tano ku mwanzo wa Orthros.

Bikira Safi na Mama ya Kristu Mungu wetu, upanga ulichoma moyo wako wakati uliona Mwana wako wa Mungu wako Msalabani: Umuombe bila kuacha kwa ajili ya maondoleo ya zambi zetu.

## Siku ya tano ku mwisho wa Orthros

Mzazi-Mungu, tunakutukuza tukiimba: Ndiwe mulima haramu ambako jiwe isiyokadirika likajifungua na likavunja milango ya Hadeze.

## Siku ya tano ku Esperinos na siku ya sita ku mwanzo wa Orthros.

Siri ya kificho tangu milele iliyokuwa isijulikane na Malaika, imeonekana duniani katika wewe, ee Mzazi-Mungu; maana Mungu alitwaa mwili kwa ushirika, bila muchanganyo, na alikubali Msalaba kwa kutaka kwake kwa ajili yetu; juu ya hii akifufua Muumbwa wa kwanza, akaokoa toka lufu nafsi yetu.

## Siku ya sita ku mwisho wa Orthros

Mzazi-Mungu, tunakutukuza tukiimba: Ndiwe kichaka kisichoteketea ambako Musa alitazama Umungu kama ulimi wa moto.

# SAUTI YA TANO

## Siku ya Mungu ku Esperinos na siku ya kwanza ku mwanzo ya Orthros

Pamoja na Malaika mbinguni, pamoja na wanadamu duniani, tunakuimba katika shangwe, ee Mzazi-Mungu: salamu, mlango pana kuliko mbingu, salamu, msaada wa pekee wa wenye mauti, salamu, Mjaliwa neema ambaye katika mwili ukamzaa Mungu.

## Siku ya kwanza ku mwisho wa Orthros

Ee Kristu Mugu wetu uliyetoka kwa Bikira sababu ya kuangaza ulimwengu, kwa maombi yake utufanye sisi kuwa waana wa Nuru, ee Bwana, utuhurumie.

## Siku ya kwanza ku Esperinos na siku ya pili ku mwanzo wa Orthros.

Ujiharikishe kutusaidia na kutulinda, onyesha huruma yako kwa watumishi wako, ee Bikira Mtaakatifu, tuliza mawimbi ya mawazo yetu ya upumbafu, ee Mzazi-Mungu, inua roho yangu yenye kuanguka; ee Bikira, najua lakini ya kama unaweza kufanya yote ile inataka.

## Siku ya pili ku mwisho wa Orthros

Mtakatifu kamili Mzazi-Mungu, mulinzi wa wakristu, okoa taifa lako lenye kukwita na matumaini naibada: Fukuza haya ya mawazo yetu ya kutangatanga ili tukulalamikie: Mama Bikira daima, salamu.

## Siku ya pili ku Esperinos na siku ya tatu ku mwanzo wa Orthros.

Mjaliwa neema, kwa Msalaba wa Mwana wako uongo wa miungu ya uongo ukaondolewa, na nguvu ya mashetani ikashindwa; ndiyo maana sisi waaminifu kama inavyopashwa, tunakuimba, tunakushukuru na tunakutukuza kweli kama Mzazi-Mungu.

## Siku ya tatu ku mwisho wa Orthros

Ee Kristu Mugu wetu uliyetoka kwa Bikira sababu ya kuangaza ulimwengu, kwa maombi yake utufanye sisi kuwa waana wa Nuru, ee Bwana, utuhurumie.

## Siku ya tatu ku Esperinos na siku ya inne ku mwanzo wa Orthros.

Toka kwa Bikira Fumbo ya ajabu ilifunuliwa mubebaji wa wokovu duniani; bila mbegu furaha ya wote ikazaliwa kwake na ikaonekana takatifu katika mwili. Bwana, utukufu kwako.

## Siku ya inne ku mwisho wa Orthros

Mtakatifu kamili Mzazi-Mungu, mulinzi wa wakristu, okoa taifa lako lenye kukwita na matumaini naibada: Fukuza haya ya mawazo yetu ya kutangatanga ili tukulalamikie: Mama Bikira daima, salamu.

## Siku ya inne ku Esperinos na siku ya tano ku mwanzo wa Orthros.

Mjaliwa neema, kwa Msalaba wa Mwana wako uongo wa miungu ya uongo ukaondolewa, na nguvu ya mashetani ikashindwa; ndiyo maana sisi waaminifu kama inavyopashwa, tunakuimba, tunakushukuru na tunakutukuza kweli kama Mzazi-Mungu.

## Siku ya tano ku mwisho wa Orthros

Ee Kristu Mugu wetu uliyetoka kwa Bikira sababu ya kuangaza ulimwengu, kwa maombi yake utufanye sisi kuwa waana wa Nuru, ee Bwana, utuhurumie.

### Siku ya tano ku Esperinos na siku ya sita ku mwanzo wa Orthros.

Salamu, mulango wa Bwana usioweza kupitwa; Salamu, ukuta na kivuli cha wale waliokimbilia kwako; salamu, kivuko bila kutikisika, na musiyeolewa, uliyezaa katika mwili Muumba na Mungu wako; usiache kupatanisha kwa ajili ya wale walikuimbia, na walioabudu Mwana wako.

### Siku ya sita ku mwisho wa Orthros

Ee Kristu Mugu wetu uliyetoka kwa Bikira sababu ya kuangaza ulimwengu, kwa maombi yake utufanye sisi kuwa waana wa Nuru, ee Bwana, utuhurumie.

## SAUTI YA SITA

### Siku ya Mungu ku Esperinos na siku ya kwanza ku mwanzo ya Orthros

Habari njema ya Gabrieli kwa Maria ikawa mwanzo wa wokovu wetu, wakati Malaika alitokea, hakukataa salamu; hakuwa na shaka kama alivyofanya Sara chini ya hema, lakini akasema: Mimi ni mtumishi wa Bwana, nitendewe vile ulivyosema!

### Siku ya kwanza ku mwisho wa Orthros

Kwa Neno la Malaika mkuu, ukawa kiti cha Wakeruvi, na ukachukua mikononi mwako, ee Mzazi-Mungu, matumaini ya roho zetu.

### Siku ya kwanza ku Esperinos na siku ya pili ku mwanzo wa Orthros.

Matumaini ya ulimwengu, Bikira Mzazi-Mungu, naomba ulinzi wako wa pekee wenye kuongoza heshima; hurumia taifa lenye kusongana ku upande wako, umusihi Mungu ili atuonyesha mapendo yake akiokoa roho zetu ku azabu zote, ee Bikira mbarikiwa katika wote.

### Siku ya pili ku mwisho wa Orthros

Hata mmoja wa hawa wenye kukimbilia kwako harudi na haya, ee Bikira Safi na mzazi-Mungu, lakini anayeomba neema yako anapokea kadiri ya ombi lake neema yenye kumufaa.

### Siku ya pili ku Esperinos na siku ya tatu ku mwanzo wa Orthros.

Mzazi-Mungu na Bikira mbarikiwa, umuombe Mwana wako, Kristu Mungu wetu, aliyejiachilia kupigiliwa Msalabani sababu ya kuokoa ulimwengu ku udanganyifu, ahurumie roho zetu.

### Siku ya tatu ku mwisho wa Orthros

Mwana na Neno la Mungu aliyezaliwa kwa Baba mbele ya nyakati bila msaada wa Mama, kwa nyakati hizi za mwisho akazaliwa katika mwili tumboni mwako mwa ubikira, ee Mzazi-Mungu, umuombe atupe sisi mbele ya mwisho maondoleo ya zambi zetu.

### Siku ya tatu ku Esperinos na siku ya inne ku mwanzo wa Orthros.

Bibi Mtakatifu tena Mzazi-Mungu safi uliyezaa kwa namna isiyokadirika Muumba wa ulimwengu, pamoja na Mitume Watakatifu umuombe kila siku kwa wema wake atuokoe ku mateso na atupe maondoleo ya zambi zetu.

### Siku ya inne ku mwisho wa Orthros

Umejaliwa na zawadi za umungu Bikira safi na mzazi-Mungu, kwani ni mmoja wa Utatu Mtakatifu, Kristu, chemchem ya uzima, ulizaa mwilini sababu ya wokovu wa roho zetu.

### Siku ya inne ku Esperinos na siku ya tano ku mwanzo wa Orthros.

Mzazi-Mungu na Bikira mbarikiwa, umuombe Mwana wako, Kristu Mungu wetu, aliyejiachilia kupigiliwa Msalabani sababu ya kuokoa ulimwengu ku udanganyifu, ahurumie roho zetu.

### Siku ya tano ku mwisho wa Orthros

Mwana na Neno la Mungu aliyezaliwa kwa Baba mbele ya nyakati bila msaada wa Mama, kwa nyakati hizi za mwisho akazaliwa katika mwili tumboni mwako mwa ubikira, ee Mzazi-Mungu, umuombe atupe sisi mbele ya mwisho maondoleo ya zambi zetu.

### Siku ya tano ku Esperinos na siku ya sita ku mwanzo wa Orthros.

Gideoni aligua kupata kwako mimba, Daudi akaangaza uzazi wako, kwani alishuka kama mvua pa manyoya, ee Mzazi-Mungu ukachipukiza Neno tumboni mwako bila mbegu, Inchi takatifu, Mjaliwa neema, wokovu wa ulimwengu, Kristu Mungu wetu.

### Siku ya sita ku mwisho wa Orthros

Mwana na Neno la Mungu aliyezaliwa kwa Baba mbele ya nyakati bila msaada wa Mama, kwa nyakati hizi za mwisho akazaliwa katika mwili tumboni mwako mwa ubikira, ee Mzazi-Mungu, umuombe atupe sisi mbele ya mwisho maondoleo ya zambi zetu.

## SAUTI YA SABA

### Siku ya Mungu ku Esperinos na siku ya kwanza ku mwanzo ya Orthros

Mzazi-Mungu na Bikira bila aibu, umuombe Mwana wako pamoja na Majeshi ya juu-mbinguni ili awape waaminifu wenye kukutukuza maondoleo ya zambi zao.

### Siku ya kwanza ku mwisho wa Orthros

Uliye mtukufu kuliko majeshi ya mbinguni, umekuwa hekalu kimungu, ee Mzazi-Mungu na Bikira mbarikiwa, kwani ulizaa Kristu, Mwokozi wa roho zetu.

### Siku ya kwanza ku Esperinos na siku ya pili ku mwanzo wa Orthros.

Mzazi-Mungu, tunakutolea wokovu wa gabrieli; kwani umewapita Malaika ulipomzaa Mungu wetu.

### Siku ya pili ku mwisho wa Orthros

Kwa maombi ya mzazi-Mungu, patanisha uzima wetu wakati tunakulalamikia: Bwana wa mapendo utukufu kwako.

### Siku ya pili ku Esperinos na siku ya tatu ku mwanzo wa Orthros.

Ee Mzazi-Mungu, umsihi Kristu Mungu wetu aliyesulubiwa kwa ajili yetu na aliyevunja nguvu ya mauti, aokoe roho zetu.

### Siku ya tatu ku mwisho wa Orthros

Utuokoe ku zambi zetu, ee Mzazi-Mungu, kwani sisi waaminifu, kisha Mungu uliyezaa mwilini, tunatumaini paka wewe.

### Siku ya tatu ku Esperinos na siku ya inne ku mwanzo wa Orthros.

Tunda la tumbo lako, ee Bikira safi, ni utimizo wa Manabii na wa sheria, tena, tunapokutukuza Mzazi-Mungu, sisi waaminifu, tunakusifu.

### Siku ya inne ku mwisho wa Orthros

Tunda la tumbo lako, ee Mzazi-Mchumba wa Mungu, anaonekana kwa wanadamu chemchem ya wokovu; tena Mzazi-Mungu, tunapokutukuza kwa kinywa na kwa roho, sisi waaminifu, tunakusifu.

### Siku ya inne ku Esperinos na siku ya tano ku mwanzo wa Orthros.

Ee Mzazi-Mungu, umsihi Kristu Mungu wetu aliyesulubiwa kwa ajili yetu na aliyevunja nguvu ya mauti, aokoe roho zetu.

### Siku ya tano ku mwisho wa Orthros

Utuokoe ku zambi zetu, ee Mzazi-Mungu, kwani sisi waaminifu, kisha Mungu uliyezaa mwilini, tunatumaini paka wewe.

### Siku ya tano ku Esperinos na siku ya sita ku mwanzo wa Orthros.

Wewe uliyelinda hazina ya ufufuo wetu, ewe Mtukufu kamili, okoa ku kisima cha zambi hawa wanaokutumainia; ulipozaa wokovu wetu, ulituokoa ku wezo wa zambi, wewe ambaye, ulipokuwa Bikira mbele ya kuzaa, ukakaa Bikira katika uzazi na pia Bikira kisha kuzaa.

### Siku ya sita ku mwisho wa Orthros

Salamu, wewe tumboni mwako mulikuwa fasi ya huyu ambaye hata mbingu hasiwezi kuwa naye; salamu, chombo cha mafundisho ya Manabii, Bikira ambako akazaliwa Emmanueli, ee Mama wa Kristu Mungu wetu.

## SAUTI YA MNANE

### Siku ya Mungu ku Esperinos na siku ya kwanza ku mwanzo ya Orthros

Salamu, wewe uliyepokea furaha ya ulimwengu kwa sauti ya Malaika, salamu, wewe uliyezaa Muumba na Bwana wako. Salamu, wewe uliyestahili kuwa Mama wa Kristu Mungu wetu.

### Siku ya kwanza ku mwisho wa Orthros

Salamu, mlango takatifu wa Mfalme wa utukufu unayekaa mwenye kufunga kisha kupita kwa Bwana, kwani paka peke yake aliye-juu alipitamo kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

### Siku ya kwanza ku Esperinos na siku ya pili ku mwanzo wa Orthros.

Boma imara ya imani, na hazina ya samani ya roho zetu, tunakutukuza kwa nyimbo zetu, ee Mzazi-Mungu; salamu, kwani ulichukua tumboni mwako chemchem ya uzima; salamu, matumaini ya mipaka ya ulimwemgu na mlinzi wa wenye kuteswa; salamu, Bibi usiyeolewa.

### Siku ya pili ku mwisho wa Orthros

Bikira Safi, kwa maombi yako utuokoe, sababu ya uwezo wa umama unao pa Mwana wako na Mungu wetu.

### Siku ya pili ku Esperinos na siku ya tatu ku mwanzo wa Orthros.

Alipoona Mwana-Kondoo, Mchungaji na Mwokozi wa ulimwengu Msalabani, huyu aliyekuzaa, katika machozi yake akasema: Dunia inafurahi kwa kupokea ukombozi na tumbo langu limeungua pakuona usulubisho wako kwa ajili yetu, ee Mwanangu na Mungu wangu.

## Siku ya tatu ku mwisho wa Orthros

Tunda la tumbo lako, ee Bikira safi, ni utimizo wa Manabii na wa sheria, tena, tunapokutukuza kama Mzazi-Mungu, sisi waaminifu, tunakusifu.

## Siku ya tatu ku Esperinos na siku ya inne ku mwanzo wa Orthros.

Mlango wa siri wa uzima wetu, Mzazi-Mungu na Bikira safi, okoa kuhatari yote waaminfu wenye kukukimbilia, ili tutukuze uzazi wako takatifu kamili kwa ajili ya wokovu wa roho zetu.

## Siku ya inne ku mwisho wa Orthros

Bikira Safi, kwa maombi yako utuokoe, sababu ya uwezo wa umama unao pa Mwana wako na Mungu wetu.

## Siku ya inne ku Esperinos na siku ya tano ku mwanzo wa Orthros.

Alipoona Mwana-Kondoo, Mchungaji na Mwokozi wa ulimwengu Msalabani, huyu aliyekuzaa, katika machozi yake akasema: Dunia inafurahi kwa kupokea ukombozi na tumbo langu limeungua pakuona usulubisho wako kwa ajili yetu, ee Mwanangu na Mungu wangu.

## Siku ya tano ku mwisho wa Orthros

Tunda la tumbo lako, ee Bikira safi, ni utimizo wa Manabii na wa sheria, tena, tunapokutukuza kama Mzazi-Mungu, sisi waaminifu, tunakusifu.

## Siku ya tano ku Esperinos na siku ya sita ku mwanzo wa Orthros.

Wewe uliyezaliwa kwa Bikira kwa ajili yetu, na uliyevumilia usulubisho, ee Mwema, uliyenyanganya mauti kwa lufu, na uliyeonyesha usimamao sawasawa na Mungu, usikengue walioumbwa kwa mukono wako; onyesha mapendo yako kwa wanadamu. Murehemu; pokea Mzazi Mungu aliyekuzaa, aliyepatanisha juu yetu, na okoa, ee Mwokozi wetu, taifa isiyotumainia.

## Siku ya sita ku mwisho wa Orthros

Bikira Safi, kwa maombi yako utuokoe, sababu ya uwezo wa umama unao pa Mwana wako na Mungu wetu.


Ἡ ΚΟΙΜΗΣΙΣ ΤΗΣ ΘΕΟΤΟΚΟΥ

# EKSAPOSTILARI ZA SIKU ZA JUMA

## Siku ya kwanza

*Ginekes akutisthite. Sauti ya mbili.*

Malaika na Malaika wakuu, utawala, Nguvu, Majeshi, mamlaka, Ezi kuu na Wakeruvi wenyi macho mengi, Waserafi wa Mabawa sita, mutuombee sisi ili tuokoe ku hatari yote na ku moto yasipo mwisho.

**THEOTOKION**.

Ee Bikira, ndiwe msaada wangu, ulinzi wa ulimwengu, boma lake imara, nasujudu mbele yako nikilalamika: Uniokoe ku azabu yote na ku moto wa milele, maana karika wewe, ee Bikira, munakaa matumaini yangu.

## Siku ya pili

*Sauti ya tatu.O uranon tis astris.*

Tumutukuze Yoane Mutangulizi, Mbatizaji wa Mwokozi, Nabii aliyezaliwa kwa Nabii tena mwana wa jangwa, mtoto wa Elisabeti, na sisi wote tusifu makumbusho yake.

Ee Bikira, unaniombea mimi mbele ya Mungu mwenye kupenda wanadamu, usichongee matendo ya uzima wangu mbele ya Malaika, lakini nakuomba, ujiharikishe kuja kunisaidia.

## Siku ya tatu

*Ginekes akutisthite. Sauti ya mbili.*

Silaha isiyoweza kushindwa, tegemeo ya imani, Msalaba Takatifu, tunakuimba, tukisujudu mbele yako katika imani: Uko kimbilio, utukufu wa wakristu, mulinzi wa Waorthodoksi tena usharifu wa Mashahidi, hakika tunakutukuza.

O *uranon tis astris. Sauti ya tatu.*

Asiye doa kamili alisimama karibu ya Msalaba na alipoona Mwana wake mwenyi kupanuliwa pa muti sababu ya lufu, sawa mama akalia na alipotoa machozi mengi, akasema: Ni kitu gani hiki kisijaonekana bado? Kusulibiwa kwa Muumba wa ulimwengu!

## Siku ya inne

*Sauti ya tatu.O Uranon tis astris.*

Ee utukufu wa Mitume na Kumi na wawili Watakatifu, pamoja na Mtakatifu wa Myre, askofu Nikolao, mutuombee bila kuacha kwa Mwokozi.

Matumaini ya wasiyo-tumaini, Mzazi-Mungu, mstahiliu kamili wa nyimbo zetu, katika machozi yangu nalalamika kweli kwako: Ee Bikira, uniondoe ku mapango ya Hadeze.

## Siku ya Tano

*Sauti ya tatu.O Uranon tis astris.*

Msalaba, mulinzi wa ulimwengu, Msalaba, Kango na uzuri wa Eklezya, uwezo kweli wa ufalme wenyi kulinda nguvu ya imani yetu, Msalaba, oga kuu ya majeshi ya gehena, Msalaba, utukufu wa Malaika mbinguni.

**STAVROTHEOTOKION**

Aliposimama karibu ya Msalaba, huyu ambaye aliyekuzaa bila mbegu katika machozi akalalamika: Ee Mwana mupole kabisa, namna gani Nuru ya macho yangu imelela? Namna gani umehesabiwa kati ya wafu, wewe chemchem ya uzima?

## Siku ya Sita

*O uranon tis astris. Sauti ya tatu.*

Ee Mungu uliyepamba mbingu na nyota na mwenye kuangaza dunia yote katika watakatifu wako, Muumba wa ulimwengu, okoa waimbaji wa Jina lako.

Ee Mungu, uko Rabi wa wazima na wafu: Pumzisha watumishi wako katika hema ya wateule; na hata walitenda zambi, Mungu Mwokozi hawatengwe mbali nawe.

Upole wa Malaika mfariji wa wenye kuhuzunika, mulinzi wa Wakristu, Bikira Mama wa Bwana, uniopoe ku azabu ya milele na uniokoe.

## UTUKUFU KWA UTATU MTAKATIFU

**MONASTERI YA MTAKATIFU GRIGORIO**
**KILIMA TAKATIFU ATHOS**
**GREKIA-HELLAS**
**MWEZI YA SABA 2001**

?? pa??? í?í??? µetaf??s???e st? ???????? t?□ ????? t? 1994 Ap? ,µ?da Ade?f™? Af???a?™? ?a? U?????? ?a? A?t????f???e st?? □p?????st? t?? ’?????? t?□ 2001 Ap? µ??. ?aµas???? G???????t?.

